# Kiswahili

## Shule za Sekondari

### Kitabu cha Mwanafunzi Kidato cha Tano na Sita

# Lugha na Sarufi




Taasisi ya Elimu Tanzania

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Kiswahili

## Shule za Sekondari

### Kitabu cha Mwanafunzi

### Kidato cha Tano na Sita

## Lugha na Sarufi


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

*Cheti cha Ithibati*

Na.172

Jina la Chapisho: Kiswahili Shule za Sekondari Kitabu cha Mwanafunzi Kidato cha Tano na Sita - Lugha na Sarufi

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Taasisi ya Elimu Tanzania

ISBN: 978-9987-09-025-9

Kitabu hiki kimeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 18 Agosti, 2019 kuwa Kitabu cha Kiada kwa ajili ya Mwanafunzi wa Kidato cha Tano na Sita katika ngazi ya elimu ya Sekondari nchini Tanzania kulingana na Muhtasari wa Mwaka 2009.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kaimu Kamishna wa Elimu

**Taasisi ya Elimu Tanzania**

For Online Only

PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 1 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

© Taasisi ya Elimu Tanzania, 2019

Toleo la Kwanza 2019

ISBN 978-9987-09-025-9

Taasisi ya Elimu Tanzania
S.L.P. 35094
Dar-es-Salaam

Simu: +255-22-2773005 / +255 22 2771358
Faksi: +255-22-2774420
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

For Online Use Only

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri wala kukitoa kitabu hiki kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi ya Taasisi ya Elimu Tanzania.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 2 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



# Dibaji

Kitabu hiki cha *Kiswahili Sekondari Kidato cha Tano na Sita - Lugha na Sarufi* kina jumla ya sura tisa. Sura hizo ni Matumizi ya lugha, Maendeleo ya Kiswahili, Kukua na kuenea kwa Kiswahili, Sarufi ya Kiswahili, Tungo za Kiswahili, Utungaji, Ufahamu na ufupisho, Tafsiri na ukalimani, na Makosa katika matumizi ya lugha.

Kitabu hiki kimezingatia Muhtasari wa Somo la Kiswahili kidato cha Tano na Sita wa mwaka 2009. Mada zote zimefafanuliwa kwa kina na zinamshirikisha mwanafunzi kikamilifu. Kuna mazoezi ya kutosha kila mwisho wa mada ndogo, na kila mwisho wa mada kuu kuna tamrini kwa ajili ya marudio. Maswali ya mazoezi na tamrini yameandaliwa kwa lengo la kumfikirisha na kumjengea mwanafunzi umahiri katika somo. Hali kadhalika, lugha iliyotumika katika kitabu hiki ni rahisi, na itakayomwezesha mwanafunzi kujifunza somo la Kiswahili vizuri.

**Taasisi ya Elimu Tanzania**

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 3 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Shukurani

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini mchango muhimu wa washiriki waliofanikisha uandishi wa kitabu hiki cha mwanafunzi.

TET inatoa shukurani za dhati kwa mchango uliotolewa na wataalamu wote walioshiriki kutayarisha kitabu hiki:

**Waandishi:** Dkt. Janeth Barongo, Dkt. Rehema Stephano, Dkt. Michael A. Mashauri, Mwl. Monica W. Manyanga, Mwl. Pius Kiraka, Mwl. Amani Mgheni & Mwl. Saul S. Bichwa

**Wahariri:** Prof. Kulikoyela Kahigi, Prof. David Massamba, Dkt. Pendo Salu Malangwa, Mwl. Modesta Mboya & Dkt. Adventina Buberwa (Mwenyekiti wa jopo)

**Msanifu:** Bi. Rehema H. Maganga

**Wachoraji:** Alama Art and Media Production Co. Ltd.

**Mratibu:** Mwl. Monica W. Manyanga

Pia, TET inatoa shukurani kwa shule zote zilizoshiriki katika ujaribishaji wa kitabu hiki.

Aidha, TET inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kuwezesha uandishi wa kitabu hiki.



Dkt. Aneth A. Komba
Mkurugenzi Mkuu
Taasisi ya Elimu Tanzania

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 4 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



## Yaliyomo

**Dibaji ....................................................................................... iii**
**Shukurani ....................................................................................... iv**
**Orodha ya vielelezo ....................................................................................... vii**
**Orodha ya majedwali ....................................................................................... viii**
**Maelezo ya vifupisho ....................................................................................... x**

**Sura ya Kwanza: Matumizi ya lugha ....................................... 1**
Dhana ya lugha ....................................................................................... 1
Tabia za lugha ....................................................................................... 3
Istilahi za lugha ....................................................................................... 4
Rejesta ....................................................................................... 8
Mambo ya kuzingatia katika kutumia lugha ....................................... 10
Mitindo ya matumizi ya lugha ....................................................................................... 13
Misimu ....................................................................................... 16
Umahiri wa lugha ....................................................................................... 19
Utata katika matumizi ya lugha ....................................................................................... 22

**Sura ya Pili: Maendeleo ya Kiswahili ....................................... 26**
Asili ya Kiswahili ....................................................................................... 26
Chimbuko la Kiswahili ....................................................................................... 42
Usanifishaji wa Kiswahili ....................................................................................... 47

**Sura ya Tatu: Kukua na kuenea kwa Kiswahili ....................... 59**
Kukua na kuenea kwa Kiswahili Afrika Mashariki ....................................... 59
Kukua na kuenea kwa Kiswahili duniani ....................................................... 98

**Sura ya Nne: Sarufi ya Kiswahili ....................................... 110**
Dhana ya sarufi ....................................................................................... 110
Matawi ya sarufi ....................................................................................... 110
Mofimu ....................................................................................... 132
Uundaji wa maneno ....................................................................................... 140



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 5 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kauli za vitenzi vya Kiswahili ........................................ 144
Ngeli za nomino ........................................ 148

**Sura ya Tano: Tungo za Kiswahili ........................................ 154**
Dhana ya tungo ........................................ 154
Urejeshi katika Kiswahili ........................................ 186

**Sura ya Sita: Utungaji ........................................ 190**
Dhana ya insha ........................................ 190
Uandishi wa barua ........................................ 196
Uandishi wa risala ........................................ 213
Uandishi wa hotuba ........................................ 217
Uandishi wa matangazo ........................................ 223
Wasifukazi ........................................ 228

**Sura ya Saba: Ufahamu na ufupisho ........................................ 234**
Dhana ya ufahamu ........................................ 234
Ufupisho ........................................ 237

**Sura ya Nane: Tafsiri na ukalimani ........................................ 241**
Dhana ya tafsiri ........................................ 241
Ukalimani ........................................ 250

**Sura ya Tisa: Makosa katika matumizi ya lugha ........................................ 257**
Makosa ya kisarufi ........................................ 257
Makosa ya kimantiki ........................................ 261
Makosa ya kiuakifishaji ........................................ 262

**Faharasa ........................................ 266**
**Marejeleo teule ........................................ 268**

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 6 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



# Orodha ya vielelezo

1.1 Mtindo wa lugha ya gazetini ............................................................15
2.1 Ramani ya Afrika kuonesha msambao wa Wabantu kwa mujibu wa Greenberg (1955) ..........................................................43
2.2 Ramani ya Pwani ya Afrika Mashariki kuonesha mzagao wa lahaja za Kiswahili ..........................................................46
3.1 Ramani ya Afrika Mashariki ikionesha misafara ya biashara na utawala ..........................................................................70
4.1 Matawi ya sarufi.........................................................................115
5.1 Aina za tungo ..........................................................................155
8.1 Mkalimani akiwa katika kitituri cha ukalimani ...............................253

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 7 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Orodha ya majedwali


2.1a Muundo wa mzizi wa Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu .........36

2.1b Muundo wa mashina ya Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu.......36

2.2 Kufanana kwa baadhi ya maneno ya lugha ya Kiswahili na lugha ......... nyingine za Kibantu .....................................................................37

2.3 Muundo wa tungo za Kiswahili na lugha nyinyine za Kibantu ...........37

2.4 Upatanisho wa kisarufi wa tungo za Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu ....................................................................................37

2.5 Mwanzo wa vitenzi vya Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu.......38

2.6 Miisho ya vitenzi vya Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu ..........38

2.7 Miisho ya vitenzi vya Kiswahili vyenye asili ya Kiarabu....................39

2.8 Mnyambuliko wa vitenzi vya Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu ....................................................................................39

2.9 Uambishaji wa vitenzi vya Kibantu ....................................................40

2.10a Ngeli za nomino za Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu kwa kigezo cha maumbo ya majina ....................................................41

2.10b Ngeli za nomino za Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu kwa kigezo cha upatanisho wa kisarufi ...............................................41

2.11 Lahaja za Kiswahili.............................................................................45

2.12 Tofauti kati ya maandishi na matamshi...............................................55

4.1 Viwakilishi vya nafsi...........................................................................119

4.2 Maumbo ya viwakilishi vioneshi ........................................................120

4.3 Maumbo ya mofimu huru na shina katika Kiswahili .........................137

4.4 Ngeli za nomino kwa mtazamo wa kimapokeo (kimaumbo) (Guthrie, 1948; Polomé 1967).........................................................148


For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 8 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



4.5 Ngeli za nomino kwa mtazamo wa kimapokeo (Broomfield, 1935)… ....149
4.6 Ngeli za nomino kwa mtazamo wa kisasa ....151
5.1 Maumbo ya urejeshi kwa kila ngeli ....163
5.2 Urejeshi wa ngeli… ....188

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 9 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Maelezo ya vifupisho

| | |
|---|---|
| **A** | Kiarifu |
| **B** | Kibainishi |
| **BAKITA** | Baraza la Kiswahili la Taifa |
| **BAKIZA** | Baraza la Kiswahili la Zanzibar |
| **BAMITA** | Baraza la Mitihani la Taifa |
| **CH** | Chagizo |
| **CHAKA** | Chama cha Kiswahili cha Afrika |
| **CHAKAMA** | Chama cha Kiswahili Afrika Mashariki |
| **CHAKITA** | Chama cha Kiswahili cha Taifa Kenya |
| **CHAUKIDU** | Chama cha Ukuzaji Kiswahili Duniani |
| **CMS** | Church Missionary Society |
| **E** | Kielezi |
| **EALB** | East African Literature Bureau |
| **EATV** | East Africa Television |
| **EWW** | Elimu ya Watu Wazima |
| **H** | Kihusishi |
| **I** | Kiingizi, Irabu |
| **IFAMU** | Idara ya Fasihi, Mawasiliano na Uchapishaji |
| **ILUKII** | Idara ya Lugha ya Kiswahili na Isimu |
| **ITV** | Independent Television |
| **JKK** | Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo |
| **K** | Konsonanti / Kiima |
| **KAKULU** | Kamati ya Kusanifu Lugha |
| **KAR** | King's African Rifles |
| **KBC** | Kenya Broadcasting Corporation |
| **KE** | Kirai kielezi |
| **KKK** | Kamusi Kuu ya Kiswahili |
| **KN** | Kirai Nomino |



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

For Online Use Only

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 10 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


| | |
|---|---|
| **KR** | Kishazi rejeshi |
| **KT** | Kirai kitenzi |
| **KV** | Kirai kivumishi |
| **L1** | Lugha ya kwanza |
| **L2** | Lugha ya pili |
| **LC** | Lugha chanzi |
| **LL** | Lugha lengwa |
| **MC** | Matini chanzi |
| **ML** | Matini lengwa |
| **N** | Nomino |
| **S** | Sentensi |
| $\mathbf{S_1}$ | Sentensi ya kwanza |
| $\mathbf{S_2}$ | Sentensi ya pili |
| **SH** | Shamirisho |
| **SKILUKI** | Skuli ya Kiswahili na Lugha za Kigeni |
| **S.P.C.K.** | Society for Promoting Christian Knowledge |
| **t** | Kitenzi kishirikishi |
| **T** | Kitenzi |
| **TAMISEMI** | Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| **TAKILUKI** | Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni Zanzibar |
| **TATAKI** | Taasisi ya Taaluma za Kiswahili |
| **TBC** | Tanzania Broadcasting Corporation |
| **TET** | Taasisi ya Elimu Tanzania |
| **TFDA** | Tanzania Food and Drugs Authority |
| **Tk** | Kitenzi kikuu |
| **TOT** | Tanzania One Theatre |
| **TPH** | Tanzania Publishing House |
| **TTCL** | Tanzania Telecommunications Company Limited |
| **TUKI** | Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili |
| **TUMI** | Taasisi ya Ukuzaji Mitaala |


PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 11 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

| | |
|---|---|
| **TYL** | TANU Youth League |
| **U** | Kiunganishi |
| **UKUTA** | Chama cha Usanifu wa Kiswahili na Ushairi Tanzania |
| **UMCA** | University Mission to Central Africa |
| **UMISAVETA** | Umoja wa Michezo na Sanaa Vyuo vya Elimu Tanzania |
| **UMISETA** | Umoja wa Michezo Sekondari Tanzania |
| **UMITASHUMTA** | Umoja wa Michezo na Taaluma kwa Shule za Msingi Tanzania |
| **UPC** | Uganda People's Congress |
| **UWAVITA** | Umoja wa Waandishi wa Vitabu Tanzania |
| **V** | Kivumishi |
| **W** | Kiwakilishi |

For Online Use Only


PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 12 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



# Sura ya Kwanza
# Matumizi ya lugha

## Utangulizi

Sura hii inahusu matumizi ya lugha. Kwa hiyo, utajifunza dhana ya lugha (maana, sifa, na tabia), dhana ya pijini, krioli, lugha ya kwanza, lugha ya pili, lugha ya taifa, lugha ya kimataifa, na lugha rasmi. Vilevile, utajifunza dhana ya rejesta katika lugha, mambo ya kuzingatia katika kutumia lugha, misimu, umahiri wa lugha, na utata katika matumizi ya lugha. Lengo la kujifunza mada hizi ni kukuwezesha kutambua na kutumia mitindo anuwai ya lugha katika kuzungumza na kuandika. Baada ya kujifunza sura hii, utapata maarifa na ujuzi wa kuzungumza na kuandika kwa Kiswahili sanifu katika miktadha mbalimbali.

### Dhana ya lugha

Wataalamu mbalimbali wamefasili dhana ya lugha kwa mitazamo tofauti. Mathalani, TUKI (1990:35) wanasema kuwa lugha ni "mfumo wa sauti nasibu zinazotumiwa na watu wa jamii fulani wenye utamaduni unaofanana ili kuwasiliana." Naye Crystal (1992) anaifasili lugha kuwa ni "mfumo wa sauti nasibu, ishara au maandishi kwa ajili ya mawasiliano na kujielezea katika jamii ya watu." Aidha, Massamba (2004:45) anasema kuwa lugha ni "mfumo wa sauti nasibu ambazo zimebuniwa na jamii kwa madhumuni ya mawasiliano kati yao." Hivyo basi, kwa kuangalia fasili hizo tunaona kwamba, wataalamu hawa wanaonekana kukubaliana kwamba lugha ni mfumo wa sauti nasibu pamoja na mfumo wa ishara (alama), ambazo hutumiwa na jamii ya watu kwa madhumuni ya mawasiliano baina yao. Kwa ujumla, fasili hizi zinahusisha mambo ya msingi yafuatayo:

1. ***Mfumo***
   Lugha yoyote ile huundwa kwa mfuatano wa sauti ambazo huungana kuunda silabi. Silabi hizo huungana kuunda neno ambapo maneno nayo huwekwa pamoja kwa utaratibu maalumu ili kuunda sentensi zenye maana. Vilevile, sentensi hizo zikiunganishwa huunda kifungu cha habari. Mifumo ya miundo hii ndiyo hutofautisha lugha moja na nyingine na ndiyo huunda



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 1 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

mfumo mzima wa lugha. Hata hivyo, kuna baadhi ya vipengele vya miundo hiyo ambavyo ni vya jumla, yaani vinapatikana katika lugha zote duniani.

**2. *Unasibu***

Sauti za lugha ni sauti ambazo uteuzi wake haufanywi kwa kufuata utaratibu maalumu, bali unatokana na makubaliano ya kimazoea tu ya watumiaji wa lugha inayohusika. Kwa hiyo, hakuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya kitaja na kitajwa. Hii inamaanisha kuwa hakuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya dhana au kitu kinachorejelewa (kitajwa) na neno linalotaja (kitaja). Kwa mfano, kitaja *meza* hakina uhusiano wa moja kwa moja na *kitu kilichotengenezwa kwa mbao, chuma, madini, au kioo chenye uvungu na ubapa juu, kinachotumiwa kulia chakula, kuandikia, au kwa ajili ya michezo.*

**3. *Sauti***

Sauti ndiyo msingi wa lugha. Kila lugha huunganisha sauti ili kuunda silabi na silabi kuunda neno na maneno kuunda tungo kubwa zaidi. Sauti hizo huunganishwa pamoja kwa utaratibu maalumu kulingana na lugha inayohusika.

**4. *Jamii ya wanadamu***

Lugha ni chombo cha mawasiliano baina ya jamii ya wanadamu. Hii ina maana kuwa binadamu tu ndio wanaotumia lugha. Binadamu huteua na kuyapa maneno maana wanazozitaka kulingana na mazingira na tamaduni zao. Kwa msingi huu, tunaona kuwa mifumo ya mawasiliano ya viumbe wengine wasio binadamu haina sifa ya kuitwa lugha.

**5. *Mawasiliano***

Lugha ni chombo cha mawasiliano miongoni mwa wanajamii. Kwa maana hiyo, lugha huwawezesha wanajamii fulani kuwasiliana baina yao na kuwasiliana na jamii nyingine. Kwa hiyo, lugha ni kiungo muhimu kati ya mtu na mtu, mtu na jamii, au taifa na taifa lingine.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 2 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



**Tabia za lugha**

Lugha ya binadamu huwa na tabia zifuatazo:

***1 Hukua***

Lugha ya binadamu ina tabia ya kukua kadiri inavyotumiwa na jamii. Kukua kwa lugha hujumuisha kuongezeka kwa msamiati, na kupanuka kwa maana za maneno. Kukua huko kunatokana na mahitaji na mabadiliko ya jamii. Mathalani, maendeleo ya sayansi na teknolojia na uvumbuzi wa vitu na mambo mapya husababisha kukua kwa lugha. Vitu vinavyovumbuliwa hupewa majina na kusababisha kuongezeka kwa msamiati katika lugha. Kwa mfano, katika lugha ya Kiswahili, msamiati ambao umetokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia ni kama vile *runinga, king'amuzi, tovuti, simufifi,* na *simumtelezo.*

***2 Kuathiriana***

Lugha ya binadamu ina tabia ya kuathiri au kuathiriwa na lugha nyingine. Lugha mbili au zaidi zinapokaribiana huweza kuathiriana katika vipengele mbalimbali kama vile msamiati, muundo, au maana. Kwa mfano, lugha ya Kiswahili imeathiriwa na Kiarabu, Kiingereza, Kijerumani, Kireno, Kifaransa na Kiajemi, hususani katika kipengele cha msamiati. Vilevile, lugha ya Kiswahili imeathiri lugha nyingine za Kibantu zilizopo Tanzania katika msamiati.

***3 Ubora wa lugha***

Lugha yoyote ile ya binadamu inajitosheleza katika matumizi yake. Hujitosheleza kulingana na mahitaji ya jamii inamotumika katika kipindi husika. Lugha huwawezesha watumiaji wa jamii inayohusika kuwasiliana na kushiriki katika majukumu mbalimbali. Kwa hiyo, tunaweza kusema kuwa hakuna lugha bora kuliko nyingine. Kila lugha ni bora katika muktadha wa matumizi yake.

***4 Kitambulisho cha utamaduni***

Kila lugha huwa ni kitambulisho cha utamaduni wa jamii fulani inayotumia lugha hiyo. Lugha hubeba dhana za shughuli, majina ya watu na vitu vilivyopo katika jamii inayohusika. Dhana hizi hubeba utamaduni wa jamii hiyo. Kwa mfano, majina ya Kiswahili kama vile Uhuru, Azimio, Amani, Chausiku, Chiriku, au Mwanaheri yanadokeza dhana zinazobeba matukio fulani katika jamii ya Waswahili.

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 3 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### 6 *Lugha hufa*

Lugha huwa na tabia ya kufa. Lugha yoyote duniani isipotumiwa kwa muda mrefu hufa. Hali hii inajitokeza pale ambapo wazungumzaji wa lugha inayohusika watatoweka au kuacha kuitumia lugha hiyo na kuanza kutumia lugha nyingine. Uhai wa lugha hutokana na kutumiwa katika nyanja mbalimbali za kijamii. Kwa mfano, baadhi ya lugha za Kibantu, mathalani Kividunda (Morogoro) na Kikahe (Moshi), zinasemekana kuwa ziko hatarini kutoweka kwa sababu ya kupungua kwa wazungumzaji wake.

## Istilahi za lugha

Kuna istilahi mbalimbali ambazo zinatumika katika kujifunza na kuelezea dhana mbalimbali kuhusu lugha. Dhana hizo ni pijini, krioli, lugha ya kwanza (L1), lugha ya pili (L2), lugha ya taifa, lugha ya kimataifa na lugha rasmi.

### 1 *Pijini*

Pijini ni lugha ya mawasiliano inayozaliwa kutokana na makundi mawili ya watu wanaotumia lugha tofauti kukutana na kushirikiana katika shughuli za kijamii au kiuchumi. Kwa kuwa watu wanaokutana huwa hawana lugha moja inayowaunganisha kimawasiliano katika shughuli mbalimbali, huamua kuunda lugha moja itakayokidhi mawasiliano yao kwa kipindi fulani. Pijini huwa ina tabia ambazo ni tofauti na lugha zinazozungumzwa na makundi yanayohusika.

#### Sifa za pijini

Pijini ina sifa zifuatazo:

(i) Huwa na mchanganyiko wa lugha mbili tofauti zinazojitosheleza;

(ii) Hutumiwa katika mawasiliano ya muda mfupi, hususani katika shughuli inayowakutanisha na hatimaye kila mtu akirudi kwake anaendelea na lugha yake ya awali;

(iii) Haina wazungumzaji wa kudumu;

(iv) Huzungumzwa aghalabu na watu wazima katika shughuli zao kwa sababu siyo lugha ya jamii nzima;

(v) Huwa na msamiati mchache wenye mchanganyiko wa maneno;

(vi) Inapokomaa huitwa krioli; na

(vii) Huwa si lugha mama kwa mtu yeyote katika kundi la watumiaji.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 4 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



**2** ***Krioli***

Krioli ni pijini iliyokomaa. Hivyo, krioli huzaliwa kutokana na pijini. Watu wanaozungumza pijini wanapooana na kuzaa watoto, watoto hao huzungumza lugha ambayo si ya mama wala ya baba, bali huzungumza lugha hiyo mpya ambayo ndiyo huitwa krioli. Lugha hii inaweza kuwa na msamiati mwingi zaidi kutoka lugha moja, au msamiati sawa kutoka lugha zinazotumiwa na wazazi wa watoto hao.

**Sifa za krioli**

Krioli ni lugha yenye sifa zifuatazo:

(i) Huzaliwa na kuchipuka kutokana na pijini;

(ii) Huwa na wazungumzaji wa kudumu;

(iii) Hutumika katika mawasiliano kwa muda mrefu;

(iv) Huzungumzwa na watoto na watu wazima, hivyo kuwa lugha ya jamii;

(v) Huwa na sauti zake na msamiati wa kutosha, hivyo, kuweza kusanifishwa; na

(vi) Ni lugha mama inayotumiwa na wazungumzaji wazawa ambao, kihistoria wametokana na jamiilugha ya pijini.

**3** ***Lugha ya kwanza (L1)***

Hii ni lugha ambayo mtu huiamili kwa mara ya kwanza kutoka kwa wazazi au walezi au jamii inayomzunguka baada ya kuzaliwa. Mtu huamili lugha ya kwanza kwa urahisi na kuwa mahiri kutokana na kukulia katika jamii inayotumia lugha hiyo. Lugha ya kwanza hujulikana pia kama lugha mama kwa sababu ni lugha ambayo hutumika katika kumlea na kumkuza mtu hadi pale anapopata ufahamu wa kuamili au kujifunza lugha nyingine. Lugha ya kwanza ina sifa zifuatazo:

(i) Maneno yake huendana na mazingira alimokulia mtu, yaani huelezea vitu vinavyomzunguka;

(ii) Huamiliwa kwa kusikiliza, kuongea na kuona vitendo vinavyohusiana na maneno yanayotamkwa;

(iii) Hufungamana na utamaduni wa jamii ambayo inatumia lugha hiyo;

(iv) Huwa na uwezo mkubwa wa kufafanua dhana mbalimbali zinazotumika katika jamii au taifa linalotumia lugha hiyo kuliko lugha nyingine; na



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 5 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(v) Huathiri uzungumzaji wa mtu kwa kiwango kikubwa kwa kuwa huwa ndiyo lugha ya kwanza kujifunza na mtu huitumia kwa muda mrefu kabla ya kujifunza lugha nyingine.

Lugha ya kwanza hutumika katika kufanikisha mawasiliano kati ya mtoto na wazazi na jamii inayomzunguka. Kwa mfano, katika mazingira ya Tanzania, wale waliozaliwa vijijini hujikuta wakiamili lugha za jamii zao kama lugha ya kwanza. Kwa upande wa wale waliozaliwa mijini huwa na nafasi kubwa ya kuamili Kiswahili kama lugha yao ya kwanza.

### *4 Lugha ya pili (L2)*

Hii ni lugha ambayo mtu hujifunza baada ya kuamili lugha ya kwanza. Kwa mfano, Kiswahili katika jamii ya Watanzania ni lugha ya pili kwa baadhi ya watu, hususani waliokulia vijijini. Aidha, watu wengi waliozaliwa mijini hujifunza lugha ya Kiingereza kama lugha ya pili. Mtu hujifunza lugha ya pili akiwa na malengo ya kufanya jambo fulani kama vile kufanya mawasiliano na watu wa jamii nyingine katika shughuli za kijamii, kibiashara, kielimu, na kadhalika. Lugha ya pili ina sifa zifuatazo:

(i) Hufundishwa katika mazingira maalumu kama vile darasani ingawa mtu anaweza pia kujifunza katika mazingira asilia; na

(ii) Ni lugha ambayo mtu huiamili akiwa tayari amekwishaamili lugha ya kwanza.

Lugha ya pili hutumika katika kuwaunganisha watu wenye lugha tofauti. Vilevile, lugha hii hutumika kama nyenzo ya kufundishia na kujifunzia. Kwa mfano, nchini Tanzania lugha ya Kiswahili, ambayo ni lugha ya pili kwa baadhi ya Watanzania, hutumika kufundishia katika elimu ya msingi, hususani katika shule za serikali.

### *5 Lugha ya taifa*

Hii ni lugha ambayo huteuliwa na taifa fulani kuwa utambulisho wa taifa hilo, na kutumika katika mawasiliano baina ya watu wake. Kwa upande wa Tanzania, lugha ya Kiswahili ndiyo lugha ya taifa tangu mwaka 1963. Aidha, lugha ya Kiswahili ni lugha ya taifa katika nchi za Kenya, Uganda na Rwanda. Hivyo, Kiswahili ni utambulisho wa utamaduni wa jamiilugha ya Waswahili mbele ya jamii nyingine duniani. Lugha ya taifa ina sifa zifuatazo:

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 6 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



(i) Hutosheleza mahitaji ya kimawasiliano baina ya jamii za taifa linalo husika;
(ii) Hutumika kwa namna moja katika jamii mbalimbali za taifa moja;
(iii) Hutumika katika shughuli za biashara ndani ya taifa linalohusika;
(iv) Hutumika katika shughuli za kiserikali katika taifa linalohusika;
(v) Hutumika katika shughuli mbalimbali za kitaifa;
(vi) Hutumika katika vyombo mbalimbali vya habari ndani ya taifa linalohusika; na
(vii) Huwa ni lugha sanifu.

Hata hivyo, ifahamike kwamba lugha ya taifa huweza kuwa zaidi ya moja. Kwa mfano, lugha za taifa katika nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (JKK) ni nne; Kituba, Chiluba, Lingala, na Kiswahili.

***6 Lugha ya kimataifa***

Lugha ya kimataifa ni lugha inayotumiwa na idadi kubwa ya watu katika mataifa mbalimbali. Hii ni lugha ambayo matumizi yake yamevuka mipaka ya taifa moja; yaani hutumika katika mataifa zaidi ya moja. Husaidia katika kukidhi mahitaji ya mawasiliano ya watu wenye lugha tofauti tofauti kutoka mataifa mbalimbali. Mifano ya lugha za kimataifa ni kama vile Kiswahili, Kiingereza, na Kifaransa. Lugha ya kimataifa huwa na sifa zifuatazo:

(i) Hutumiwa na idadi kubwa ya watu katika nchi mbalimbali;
(ii) Hutumiwa kama lugha rasmi na lugha ya taifa katika mataifa mbalimbali;
(iii) Huweza kutumika kama lugha ya kutolea elimu katika nchi mbalimbali;
(iv) Hutumika katika biashara za kimataifa;
(v) Huwa na machapisho mengi;
(vi) Hutumika katika vyombo vya habari;
(vii) Huweza kutumika katika shughuli za kimataifa kama imeamuliwa hivyo; au
(viii) Hutumika kwenye shughuli za kidiplomasia;



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 7 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### *7 Lugha rasmi*

Lugha rasmi ni lugha ambayo huteuliwa na serikali ili itumike katika shughuli za kiserikali. Lugha ya Kiswahili ni lugha rasmi nchini Tanzania, na inatumika katika nchi za kigeni. Pia, inaweza kuwa zaidi ya moja kama ilivyo nchini Tanzania ambapo lugha rasmi ni Kiswahili na Kiingereza. Lugha hizi ziliteuliwa kuwa lugha rasmi mwaka 1963. Kimsingi, lugha rasmi hutumika katika mawasiliano, hususani katika shughuli rasmi za kijamii, ofisini, shuleni na katika mihimili ya serikali kama vile bunge, mahakama na katika baraza la mawaziri. Lugha rasmi ina sifa zifuatazo:

(i) Hutumika katika shughuli za kiserikali zinazofanyika katika maeneo kama vile bungeni, mahakamani, katika dhifa mbalimbali za kitaifa na kadhalika;

(ii) Huweza pia kuwa lugha ya taifa; na

(iii) Hujitosheleza katika mawasiliano.

Tofauti na ilivyo katika nchi ya Tanzania ambapo Kiswahili kina hadhi ya kuwa lugha ya taifa na lugha rasmi, lugha rasmi na lugha ya taifa zinaweza kuwa lugha mbili tofauti katika nchi moja.

## Rejesta

Lugha hutumika katika mazingira mbalimbali ambako kuna watu wanaofanya shughuli tofauti tofauti. Kutokana na kuwa na mazingira yanayotofautiana kishughuli, kimahusiano na kiutamaduni, matumizi ya lugha moja hutofautiana. Mitindo ya matumizi ya lugha fulani katika mazingira mahususi ndiyo huitwa rejesta. Kwa mfano, lugha inayotumika katika makundi ya wavuvi, wawindaji, wafanyabiashara, na wanamichezo inatofautiana kwa kiasi fulani.

## Mambo yanayosababisha kuzuka kwa rejesta

Rejesta huzuka kutokana na mambo mbalimbali. Miongoni mwa mambo hayo ni haya yafuatayo:

### *1. Upekee*

Hii ni hali waliyonayo kikundi fulani cha watu katika namna ya kusoma au kuzungumza. Hali hii hutofautisha kikundi kimoja na kingine katika utumiaji wa lugha. Upekee huu huweza kujitokeza katika matamshi na msamiati. Hivyo, watu wanakuwa na mtindo wao wa kuzungumza ambao haubadiliki kila wanapozungumza katika muktadha mahususi.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 8 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



2. ***Shughuli iliyopo***

Shughuli inayotendeka katika mazingira mahususi hutupatia rejesta za mahali kama vile, kanisani au msikitini, sehemu za biashara, mahakamani na bandarini. Kwa mfano, katika shughuli ya harusi kuna rejesta yake inayoweza kuoneshwa na maneno kama vile, *hongera kwa kupata jiko, anameremeta, tumpambe maua*, na kadhalika.

3. ***Mahitaji ya kuficha jambo***

Matumizi ya lugha kwa lengo la kuficha mambo husababisha kuzuka kwa rejesta miongoni mwa wazungumzaji wa lugha moja. Kwa mfano, vijana wakiwa vijiweni wanaweza kutumia mtindo wa lugha ambao watu wenye umri tofauti wanaweza wasielewe kinachosemwa. Wanapotumia maneno kama vile *oya mwanangu, tujikate* wakimaanisha *tuondoke*, mtu wa rika lingine anaweza asielewe.

**Dhima za rejesta**

Rejesta zina dhima zifuatazo katika matumizi ya lugha:

(i) Kuwatambulisha wazungumzaji kwa kikundi au jamii yenye utamaduni, uga, au ujuzi unaolingana. Wazungumzaji hao wanaweza kuwa wahunzi, wanasheria, matabibu, wahudumu wa hotelini, mafundimchundo, wavuvi, makasisi, mashehe, na kadhalika.

(ii) Kuficha maana ya dhana au maneno yanayotumika kwa hadhira isiyotoka katika kundi au jamii inayohusika.

(iii) Hutumika ili kurahisisha mawasiliano katika muktadha unaohusika. Kwa mfano, kutumia maneno ya mkato katika kuandika historia ya matatizo ya mgonjwa, matibabu, dawa, na matumizi yake hurahisisha mawasiliano katika muktadha wa hospitalini.

(iv) Kukuza lugha kwa kuongeza msamiati mpya na kukidhi mahitaji ya kimawasiliano ya wanaotumia mtindo wa lugha unaohusika.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 9 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Mambo ya kuzingatia katika kutumia lugha**

Matumizi ya lugha yoyote hutawaliwa na mazingira ya watumiaji wa lugha hiyo. Kwa hiyo, watumiaji wa lugha huongozwa na mambo ya msingi yafuatayo katika mitindo mbalimbali ya lugha wanayotumia.

1. ***Uhusiano wa wazungumzaji***

Uhusiano wa wazungumzaji huamua aina ya lugha ya kutumia, uteuzi wa maneno, na utamkaji. Kwa mfano, mtu mwenye cheo cha chini ataonesha tofauti ya jinsi atakavyotumia lugha anapoongea na mkuu wake wa kazi tofauti na anapoongea na mtu mwenye cheo kama chake. Uhusiano huu unaweza kuwa wa rika, madaraka, au familia. Chunguza mazungumzo yafuatayo ya marafiki wawili:

**Mazungumzo 1**

**Kibude:** Oya wangu, vipi mambo?
**Kwezu:** Poa mwanangu. Inakuwaje?
**Kibude:** Baridi mshikaji. Mambo leo siyo shwari wangu!
**Kwezu:** Vipi, maji shingoni siyo! Usikonde. Kuna ishu ikienda poa basi …
**Kibude:** Basi taim, taim … nistue. Nipo maskani.
**Kwezu:** Poa!

**Mazungumzo 2**

**Nduke:** Vipi mshikaji, mbona unamisi skuli siku hizi? Niaje?
**Ndosi:** Ah! Si yule ticha Mbwetu … ananimaindi saana!
**Nduke:** Niaje kwani?
**Ndosi:** Si juzi kati dogo, nilikuwa viwanja kwenye anga zangu basi ndo …
**Nduke:** (*Anamuona baba yake anakuja*). Kausha basi dogo, dingi huyooo.
**Ndosi:** Haina mbaya braza. Samtaim basi, tujikate mshikaji. (*Wanatawanyika kila mmoja anaelekea upande wake*)

Mazungumzo haya yanaonesha jinsi kuzoeana kwa vijana kunavyowapa uhuru wa kutumia maneno. Unaposoma mazungumzo haya unaona jinsi vijana hawa wa rika moja wanavyozungumza lugha ya Kiswahili ambapo si



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 10 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



rahisi kwa mzungumzaji wa Kiswahili wa rika lingine kuelewa kwa urahisi kile kinachozungumzwa.

2. ***Mada inayozungumzwa***

Mada inawafanya wanaozungumza kuchagua maneno yanayohusiana na jambo linalozungumziwa na kuhakikisha kuwa maneno hayo yanawasilisha dhana na ujumbe uliokusudiwa. Hii inawafanya wazungumzaji kuelekeza fikira zao kwenye jambo linalozungumziwa. Kwa mfano, wazungumzaji wanaozungumzia mambo ya ufundi wa magari watatumia maneno kama vile *injini, giaboksi, breki padi, rejeta,* na *klachi*. Wazungumzaji wa mambo ya utabibu wa hospitalini watatumia maneno kama vile *vipimo vya malaria, vidonge* na *sindano*. Iwapo tiba hiyo inahusiana na uganga wa kijadi, wazungumzaji watatumia maneno kama vile *tunguli, ramli, mavumba, ubani, kifungua mkoba,* na kadhalika.

3. ***Muktadha***

Muktadha ni mazingira au mahali ambapo tukio au jambo hutendeka. Muktadha ni kitu cha kuzingatia katika matumizi ya lugha kwa sababu humsaidia mtumiaji wa lugha kutumia lugha inayotakiwa katika mazingira ya tukio linalohusika. Lugha inayotumika katika miktadha mbalimbali hujibainisha kwa shughuli za mazingira ambamo lugha hiyo inatumika. Mazingira yanaweza kuwa ya kidini, kisheria, kisiasa, kibiashara, au yale ya migodini, bandarini, hotelini, sokoni, ofisini, na kadhalika. Katika matumizi ya lugha, mazingira kama hayo ndiyo yanayowafanya wazungumzaji kuibua maneno maalumu yanayotumika katika mazungumzo yao. Chunguza mazungumzo yafuatayo:

**Hakimu:** Ninakuuliza, jaribio la kuvunja nyumba kwa kutumia silaha na kukusudia kuiba lilitendeka?

**Mbiche:** Hapana mheshimiwa hakimu. Mimi sikuwa na kusudio hilo bali nilipopita na kuusogelea mlango sikujitambua kwani nilikuwa nimelewa.

**Hakimu:** Ulikuwa na silaha gani ulipousogelea mlango?

**Mbiche:** Sikuwa na silaha yoyote, bali kulikuwa na shoka nje ya nyumba ambalo lilisahaulika wakati wenye nyumba walipokwenda kulala.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 11 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Hakimu:** Umewezaje kukumbuka shoka ulililoliona usiku, ilhali wewe ulikuwa umelewa kiasi cha kukosa kujitambua?

**Mbiche:** Kwa neema tu mheshimiwa hakimu.

**Hakimu:** Shauri lako linaahirishwa hadi tarehe 03.04.2016 litakaposomwa tena. Dhamana yako imekataliwa na utarudi tena rumande.

Mazungumzo haya ni mazungumzo ya mahakamani kwa sababu kuna msamiati wa mahakamani kama vile *hakimu, shauri, dhamana,* na *rumande,* pamoja na matumizi ya lugha rasmi. Mara nyingi mahojiano katika mahakama hayaendi haraka haraka. Kwa mfano, kila mtu anayehusika hususani hakimu, mwendesha mashtaka, wakili, mshtakiwa, na shahidi hujieleza kwa uwazi bila kujali urefu wa maelezo yake. Hivyo, tunaweza kusema kuwa hii ni rejesta ya mahakamani.

Kwa upande mwingine, rejesta ya mahakamani ni tofauti na rejesta ya hotelini, mahali ambapo watu hupata huduma ya chakula. Lugha ya hotelini ina mtindo wake ambao, katika hali ya kawaida, huenda isieleweke kwa mtu asiyehusika katika mazungumzo hayo. Chunguza mazungumzo yafuatayo:

**Mhudumu:** Nani mbuzi?

**Mteja:** Mimi!

**Mhudumu:** Kuku?

**Mteja:** Hapa!

**Mhudumu:** Biriani?

**Mteja:** Mimi!

Mzungumzaji anapouliza, *"Nani mbuzi?"* haimaanishi kuwa anamuulizia mtu anayeitwa *Mbuzi*, bali anaulizia mteja aliyeagiza nyama ya mbuzi. Pia, anaposema *kuku* anamaanisha mteja aliyeagiza kuku. Aidha, anaposema *biriani* hakuna mteja anayeitwa *biriani*, bali mteja aliitikia akiwa na maana angehitaji kula *biriani*.

### 4. *Leng l a mazung mzo*

Lengo la mazungumzo humwezesha mtumiaji wa lugha kuteua mtindo wa lugha ya kutumia. Mtu mwenye lengo la kuomba hela atatumia lugha ya unyenyekevu na upole. Mtu huyo huyo akiwa na lengo la kuelimisha

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 12 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



kuhusu athari za matumizi ya simu, atatumia lugha ya kuonya, kusisitiza, na kushauri.

**Mitindo ya matumizi ya lugha**

Dhana ya mitindo ya lugha inakwenda sambamba na dhana ya rejesta katika lugha. Mitindo ya lugha, katika mazungumzo au maandishi, hurejelea namna au jinsi lugha inavyotumika katika mazingira na shughuli maalumu. Kwa hiyo, mitindo ya lugha husaidia pia kubaini aina za rejesta. Kuna mitindo mbalimbali ya lugha ambayo inaweza kuwa katika makundi yafuatayo:

***1. Mtindo wa lugha ya kiofisi***

Mtindo huu hutumika katika mawasiliano rasmi ambayo hufanyika katika ofisi au mahali popote pa kazi. Mtindo huu huweza pia kujulikana kama mtindo wa lugha ya kikazi. Mtindo huu hutumika katika mikataba, sera, kanuni za kazi, matini za kisheria, matangazo ya vikao, ripoti za mikutano, na kadhalika.

**Sifa za mtindo wa lugha ya kiofisi**

(i) Huwa na usahihi wa mambo yanayojadiliwa;
(ii) Hutumia istilahi maalumu kulingana na shughuli za kiofisi zinazohusika;
(iii) Hakuna matumizi ya misimu, mafumbo wala tafsida; na
(iv) Hutumia vifupisho rasmi kama vile TUKI, TAKILUKI, TAKUKURU, MKURABITA, BAKIZA, BAMITA, na kadhalika.

Chunguza mfano wa lugha yenye mtindo wa kiofisi:

*Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu inakuhukumu kufungwa jela miaka ishirini na mitano ili iwe fundisho kwa watu wengine wanaofanya ubadhirifu wa mali ya umma. Hukumu hii inaanza mara moja kuanzia sasa.*

***2 Mtindo wa lugha ya kitaaluma***

Huu ni mtindo unaopatikana katika vitabu na majarida ya kitaaluma na katika utoaji wa mafunzo yanayohusu elimu. Mtindo huu hutumika shuleni, vyuoni, kwenye semina, warsha, makongamano, na ripoti mbalimbali za kitaaluma.

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 13 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Sifa za mtindo wa lugha ya kitaaluma**

(i) Mada inayozungumzwa au kuandikwa ni ya kitaaluma.

(ii) Kuna usahihi na ukweli wa mambo yanayojadiliwa.

(iii) Hutumia kauli ya kutendwa na kutendeka kwa wingi zaidi.

(iv) Hutumia lugha sanifu ya wazi na inayoeleweka.

(v) Hakuna matumizi ya tamathali za semi au mafumbo isipokuwa kwa kazi za kifasihi.

(vi) Kuna ufupishaji maalumu wa maneno.

(vii) Hutumia wakati uliopita hasa katika uandishi wa ripoti.

(viii) Mara nyingi, hutumia nafsi ya kwanza wingi na nafsi ya tatu au mtindo usiorejelea nafsi yoyote ili kuficha ubinafsi wa mwandishi. Kwa mfano, *… imekubaliwa kuwa ujumbe uliotolewa na …* au *…imeshauriwa kuwa matumizi ya madawa ya kulevya…*

(ix) Hutumia istilahi maalumu kulingana na uwanja husika.

***3 Mtindo wa lugha ya magazetini***

Mtindo huu hutumika katika uandishi wa habari katika magazeti.

**Sifa za mtindo wa lugha ya magazetini**

(i) Huonesha hisia za mwandishi.

(ii) Hutumia sana chuku, yaani maneno yanayolikuza jambo hata kama ni dogo. Kwa mfano, *Bungeni kwafukuta moto!*

(iii) Huwa na matumizi mapana ya visawe. Kwa mfano, matumizi ya msamiati wa michezo huweza kuwa na visawe kama vile kushinda mchezo (kuibuka kidedea) na nunge (sifuri).

(iv) Huwa na matumizi mengi zaidi ya nafsi ya tatu kama vile *alikuwa* au *walikuwa*.

(v) Mara chache hutumia nafsi ya kwanza, hasa kwenye barua za mhariri.

(vi) Vichwa vya habari havizingatii nyakati. Kwa mfano, *Yanga Yafa Kiume*, *Mafuriko Yalaza Mamia Nje*, *Acacia Yafungasha Virago*, *Mtanzania Aula UN*, na *Simbu Ang'aa Jumuiya ya Madola*.

(vii) Huwa na matumizi ya vifupisho rasmi kama vile TRA, TBC, UDOM na TTCL.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 14 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Chunguza mfano ufuatao wa uandishi wa magazetini.



**Taifa Stars Yairarua Malawi**

**Samatta atupia mawili**

**Msuva akihitimisha karamu ya magoli matatu**

*Chanzo: Gazeti la Mtanzania 7/10/2017*

Dar es Salam. Timu ya Taifa ya Tanzania "Taifa Stars" imefanikiwa kuibuka na ushindi wa magoli matatu kwa sifuri katika pambano la kukata na shoka dhidi ya timu ya Taifa ya Malawi. Katika mchezo uliopigwa katika Uwanja wa Taifa. Mshambuliaji hatari wa Tanzania na timu ya Genk, Mbwana Samatta alifunga magoli mawili kabla Simon Msuva hajapigilia msumari wa mwisho katika dakika ya 89. Mchezo huo ulishuhudiwa pia na Rais Mstaafu wa Tanzania Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete…

**Kielelezo 1.1** Mtindo wa lugha ya gazetini

***4 Mtindo wa lugha ya mazungumzo na maandishi ya kawaida***

Haya ni maongezi au maandishi ya kawaida yanayotumika kila siku nyumbani, katika sehemu za starehe, kwenye misiba, na mahali pengine popote pasipohusika na shughuli za kiofisi, kikazi, au kitaaluma.

**Sifa za mtindo wa lugha ya mazungumzo na maandishi ya kawaida**

(i) Kutokuwepo kwa maandalizi ya awali, hususani katika mazungumzo;
(ii) Huwa na matumizi ya viungo vya mwili na ishara, hususani katika mazungumzo;
(iii) Huwa na matumizi ya tamathali za semi, misimu na mafumbo;
(iv) Huwa na matumizi ya nafsi zote katika mazungumzo;
(v) Huwa na matumizi ya vifupisho vya maneno visivyo rasmi;

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 15 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(vi) Huruhusu matumizi ya lugha zaidi ya moja; na

(vii) Huwa na matumizi makubwa ya lugha isiyo sanifu.

## Zoezi la 1.1

1. Kwa kutumia mifano, fafanua mambo ya kuzingatia katika kutumia lugha.
2. Jadili mitindo mbalimbali ya lugha kulingana na muktadha wa matumizi.
3. Bainisha matumizi ya rejesta katika jamii.
4. Eleza tofauti zilizopo kati ya lugha ya taifa, na lugha rasmi.

**Misimu**

BAKITA (2015) wanafasili msimu (simo) kuwa ni neno au maneno yanayozuka na kutumiwa na watu kwa muda fulani na baadaye kupotea. Aidha, misimu inaweza kufasiliwa kama maneno yasiyo sanifu ambayo huzushwa na kikundi cha watu wenye utamaduni mmoja ili kuelezea uhusiano wao. Hata hivyo, kuna baadhi ya misimu ambayo huweza kudumu na hata kusanifishwa kuwa msamiati sanifu kama vile *kasheshe*, *vuvuzela*, na *chakachua*.

**Aina za misimu**

Kwa kuzingatia muktadha wa utumiaji wa misimu, tunaweza kupanga misimu katika makundi makuu matatu kama ifuatavyo:

***1M isimu ya p kee***

Hii ni misimu ambayo hueleza uhusiano wa jamii yenye utamaduni mmoja, yaani kundi dogo la watu. Eneo la matumizi ya misimu hii ni dogo ukilinganisha na makundi mengine na huwa haijulikani kwa watu wengi. Makundi hayo huweza kuwa ya wanafunzi, wafanyabiashara au wafanyakazi wa ofisi moja na kadhalika. Kwa mfano, msimu *bumu* (pesa za kujikimu) hutumika katika vyuo vikuu nchini Tanzania na haujulikani katika jamii nyingine.

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 16 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



***2M isimu ya kieneo***

Hii ni misimu ambayo inatumika katika eneo kubwa au pana kidogo kimatumizi. Misimu ya aina hii inaweza kupatikana kwenye kata, tarafa, au wilaya. Mifano ya misimu hii ni pamoja na *sekido* (pikipiki ya abiria - Bukoba), *toyo* (pikipiki ya abiria - Kanda ya Kaskazini mwa Tanzania).

***3M isimu zago***

Hii ni misimu ambayo inatumika katika eneo kubwa kimatumizi. Ni misimu ambayo inafahamika kwa watu wengi katika nchi na huweza kuvuka hata mipaka ya nchi. Misimu ya aina hii hutumika katika magazeti, vitabu, na vipindi vya redio. Aghalabu, misimu hii huweza kuota mizizi na kusanifiwa kisha kutumika kama msamiati sanifu. Mifano ya misimu hii ni kama vile *bodaboda* (pikipiki inayosafirisha abiria), *chakachua* (kuharibu ubora au uhalisi wa kitu) *daladala* (mabasi madogo yanayosafirisha abiria mijini) na kadhalika. Misimu hii imezagaa na inaeleweka katika nchi nzima ya Tanzania. Aidha, imedumu katika matumizi kiasi kwamba imefikia hatua ya kusanifishwa na kuingizwa katika kamusi.

**Sifa za misimu**

Misimu ina sifa mbalimbali. Baadhi ya sifa hizo ni kama zifuatazo:

(i) Misimu mingi ni semi zinazozuka na kutoweka. Hii ina maana kwamba misimu haina uhai mrefu katika matumizi. Misimu huzaliwa na kufa kulingana na mabadiliko yanayotokea katika jamii. Mfano wa msimu uliotoweka katika matumizi ni kuiita Sh. 500 *pajero*. Siku hizi msimu huu umefupishwa na badala ya *pajero* unaitwa *jero*.

(ii) Misimu si sanifu. Hii ni kwa sababu hutumika kwa muda mfupi. Hata hivyo, misimu inayodumu huweza kusanifishwa.

(iii) Baadhi ya misimu hutumia lugha ya mafumbo, hususani misimu inayotumiwa na kikundi kidogo cha watu. Misimu hii hulenga kuficha dhana inayowakilishwa na msimu unaohusika.

(iv) Msimu mmoja unaweza kuwakilisha dhana moja au zaidi. Maana ya msimu hutegemea mahali ambapo msimu huo unatumika. Mfano mzuri ni matumizi ya msimu *kula kichwa*. Msimu huu kwa dereva na kondakta wa daladala humaanisha *kuchukua abiria* lakini katika mazingira ya vyuo vikuu wanafunzi wanaposema *Profesa amekula kichwa*, wanamaanisha kuna *mtu hajafaulu somo la Profesa huyo*.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 17 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Umuhimu wa misimu**

(i) Misimu hukuza lugha. Baadhi ya misimu hutumika kwa muda mrefu na kuota mizizi. Aina hii ya misimu husanifishwa na kutumika kama lugha sanifu. Hivyo, huongeza msamiati.

(ii) Misimu husaidia kuziba pengo la kueleza dhana fulani katika mazingira maalumu ya watu wa kikundi maalumu.

(iii) Kimatumizi, misimu huongeza uhusishaji wa hisia katika mazungumzo kwa sababu matumizi ya misimu hutiwa chumvi sana. Aidha, misimu hubeba kebehi na kejeli.

**Changamoto za kutumia misimu katika lugha**

Misimu ina changamoto mbalimbali katika matumizi ya lugha endapo haitatumika vizuri. Zifuatazo ni changamoto zinazoweza kujitokeza katika kutumia misimu:

(i) Misimu ni lugha maalumu na hutumiwa na kikundi cha watu maalumu katika mazingira maalumu. Hivyo, mara nyingi inapotumika mahali pasipostahili inaweza kusababisha kutoelewana katika mawasiliano kati ya watumiaji wa lugha.

(ii) Misimu ina sifa ya kuwa na maana zaidi ya moja. Msimu unaotumiwa na kundi moja unaweza kuwa tofauti na ule unaotumiwa na kundi lingine. Kwa mfano, matumizi ya msimu *daladala* hujitokeza zaidi katika mkoa wa Dar es Salaam na baadhi ya mikoa kama vile Morogoro na Pwani lakini mikoa ya Mwanza, Moshi na Arusha wanatumia *vifodi* au *haisi* (hiace). Wakati mwingine, hali hii huweza kusababisha kukosekana kwa mawasiliano kwa watumiaji wa misimu wa makundi tofauti kwa sababu maana inayotarajiwa kwa kila kundi huwa tofauti na ile iliyozoeleka.

(iii) Mara nyingi, misimu huongeza chumvi inapotumika katika mawasiliano. Misimu hiyo hubeba kebehi, kejeli, au chuki. Tabia hii inaweza kuleta uhusiano mbaya kati ya watumiaji. Hivyo, ni vizuri kutumia misimu kwa kuzingatia wakati, mazingira, mada, na hadhira.


PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 18 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



## Zoezi la 1.2

1. Jadili aina, sifa, na umuhimu wa kutumia misimu katika lugha.
2. Eleza jinsi unavyoweza kukabili changamoto za kutumia misimu katika lugha.

### Umahiri wa lugha

Umahiri wa lugha ni uwezo wa mtu kumudu stadi nne za lugha, ambazo ni: kusikiliza, kuzungumza, kuandika, na kusoma, katika mawasiliano yake ya kila siku pamoja na kuuelewa utamaduni wa lugha inayohusika. Umahiri katika stadi hizo unatokana na kumudu vizuri vipengele vya lugha kama vile msamiati, miundo, matamshi, maana, na mbinu za utumiaji wa lugha katika miktadha mbalimbali. Watumiaji wa lugha ambao bado hawajamudu stadi hizo za lugha huwa si mahiri wa lugha.

### Mambo yanayomwezesha mtu kuwa mahiri wa lugha

Yafuatayo ni mambo ya msingi yanayoweza kumsaidia mtumiaji wa lugha kupata umahiri wa lugha:

1. ***Matumizi ya lugha katika shughuli mbalimbali***

   Shughuli mbalimbali anazofanya mzungumzaji wa lugha humwezesha kumudu stadi za lugha hiyo. Kwa mfano, shughuli zinazohusiana na elimu, kusoma vitabu na magazeti, kusikiliza redio na televisheni, kuhudhuria mikutano mbalimbali, kuhudhuria na kushiriki katika shughuli mbalimbali katika maeneo kama vile mahakamani, kanisani, misikitini, na kadhalika. Kadiri mtu anavyozidi kushiriki katika shughuli kama hizi ndivyo anavyozidi kukuza umahiri wake wa lugha.

2. ***Kusomea lugha kwa kiwango cha juu***

   Umahiri pia hupatikana kwa kujifunza lugha inayohusika kwa kiwango cha juu. Jambo hili humpa mtu uwezo wa kubainisha na kutumia mitindo mbalimbali ya lugha katika mazingira mbalimbali. Kwa mfano, kuna wataalamu mbalimbali wa lugha ya Kiswahili ambao wamesomea lugha

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

hiyo katika ngazi mbalimbali za elimu kama vile, stashahada, shahada ya kwanza, shahada ya umahiri, na shahada ya uzamivu. Umahiri wa lugha kwa watu hawa ni mkubwa. Wengine wamekuwa mahiri kwa kuwa wamekuwa wakiitumia lugha hiyo katika miktadha na taaluma mbalimbali.

3. ***Kuwa karibu na watumiaji mahiri wa lugha***

Kuwa karibu na wazungumzaji wa lugha inayohusika husaidia kuongeza kiwango cha umahiri. Kwa mfano, mtu akikaa karibu na wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili humwezesha kumudu zaidi lugha hiyo kwa kusikiliza na kujirekebisha, au kurekebishwa na watumiaji hao mahiri.

**Athari za utovu wa umahiri wa lugha zaidi ya moja**

Utovu wa umahiri wa lugha zaidi ya moja unaweza kusababisha athari mbalimbali zifuatazo:

1 ***Athari katika matamshi***

Mtumiaji wa lugha zaidi ya moja asipokuwa makini anaweza kuathiri utamkaji wa maneno katika lugha ya pili. Kwa mfano, Mkurya hutamka neno *chakura* badala ya kusema *chakula*. Hii inatokana na athari ya lugha yake ya kwanza ambayo ni Kikurya.

2 ***Athari katika msamiati***

Utovu wa umahiri wa lugha zaidi ya moja husababisha mzungumzaji kuchanganya maneno ya lugha mbili wakati wa mazungumzo. Kwa mfano, mzungumzaji anaweza kuchanganya lugha ya Kiswahili na Kiingereza kwa kusema *nitakuinform* badala ya kusema *nitakujulisha*.

3 ***Athari za kimuundo***

Muundo wa tungo huweza kutofautiana kati ya lugha moja na nyingine. Tofauti hizo huweza kujitokeza katika mpangilio wa maneno au upatanisho wa kisarufi katika tungo. Mathalani, mzungumzaji wa kabila la Kihehe hutumia wingi anapozungumza na mtu ambaye anamheshimu. Kwa mfano, anapozungumza Kiswahili kama lugha ya pili anaweza kuuliza *Baba mmekuja?* Akimaanisha *Baba umekuja*? Hii hutokana na athari ya lugha ya Kihehe katika kipengele cha upatanisho wa kisarufi.


PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 20 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



**4** ***Athari katika maana***

Hii hujitokeza wakati kunapokuwa na maneno ya lugha mbili yanayoeleza dhana moja. Neno la lugha moja linaweza kuwa na maana pana zaidi kuliko lugha nyingine. Kwa mfano, maneno katika tungo, *Wash your hand* yanaweza kufasiliwa kama *Osha mikono yako* wakati kiuhalisia katika Kiswahili tunasema *Nawa mikono yako*.

**Mambo yanayopoteza umahiri wa lugha**

Kuendelea kuwa na umahiri wa lugha hutegemea ni kwa kiasi gani mtu anaendelea kutumia lugha hiyo. Umahiri wa lugha unaweza kuathiriwa na mambo yafuatayo:

**1** ***Matumizi madogo ya lugha inayohusika***

Umahiri wa lugha kwa mzungumzaji hudumaa ikiwa mzungumzaji haitumii lugha hiyo mara kwa mara. Kwa hiyo, kadiri mtumiaji anavyoendelea kuitumia lugha, ndivyo anavyokuza umahiri wake katika lugha hiyo lakini asipoitumia, hudumaza umahiri wake.

**2** ***Kupunguza kusoma machapisho na kusikiliza vyombo vya habari***

Mtumiaji wa lugha anapopunguza kusoma machapisho kama vile vitabu, majarida, magazeti, vipeperushi, na kusikiliza vipindi mbalimbali vya redio na televisheni huweza kufifisha umahiri wake katika lugha inayohusika. Kufanya hivyo kunasaidia kuongeza msamiati na kuzidi kujua miundo na mitindo mbalimbali ya lugha na matumizi yake katika miktadha sahihi.

**3** ***Kuishi katika jamii isiyotumia lugha inayohusika***

Umahiri wa lugha hukuzwa iwapo mtumiaji wa lugha ataishi katika jamii inayotumia lugha hiyo. Iwapo ataishi katika jamii ambayo haitumii kabisa lugha hiyo, basi umahiri wake unaweza kupungua.

**4** ***Kuchanganya lugha katika matumizi***

Kuchanganya lugha mbili au zaidi katika matumizi hufifisha umahiri wa lugha. Kila lugha ina muundo na mtindo wake kimatumizi. Kuchanganya lugha mbili au zaidi katika matumizi kunaharibu sarufi na utaratibu wote wa matumizi ya lugha inayohusika. Kwa mfano, baadhi ya watu waliosoma, hasa nchini Tanzania, huchanganya lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Tabia hii hupoteza umahiri katika lugha zote mbili.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 21 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

***5 Kukosa ari na umuhimu wa kutumia lugha inayohusika***

Baadhi ya watu hukosa ari ya kutumia lugha yao kwa sababu mbalimbali kama vile kuinasibisha na jamii fulani, uduni, kundi fulani la kisiasa, au kundi la dini fulani. Hali hii hupunguza umahiri wao katika lugha hiyo.

***6 Kubadili mfumo wa maisha***

Wakati mwingine mtumiaji wa lugha anapobadili mfumo wa maisha hupunguza au hupoteza umahiri wa lugha. Kwa mfano, mtu anapoingia na kuishi katika jamii ambamo kiwango na ujuzi wa lugha alionao hauhitajiki sana hujikuta akitumia kiwango cha chini cha lugha; jambo ambalo hupunguza umahiri wake katika lugha.

### Zoezi 1.3

1. Unafikiri kwa nini Watanzania wengi wana umahiri wa kuzungumza lugha ya Kiswahili?
2. Kwa kutumia mifano, eleza mambo yanayosababisha kupoteza au kupunguza umahiri miongoni mwa watumiaji wa lugha.

**Utata katika matumizi ya lugha**

Utata ni hali ya tungo kuwa na maana zaidi ya moja. Kiswahili, kama zilivyo lugha nyingine, kina sentensi na maneno yenye maana zaidi ya moja. Chunguza mifano ifuatayo:

(i) Kombo anapaa.

Tungo hii inaweza kutoa maana hizi: *Kombo anaruka juu (anaelekea angani)* au *Kombo anatoa magamba ya samaki.*

(ii) Kimindi amenunua mbuzi.

Tungo hii inaweza kuwa na maana zifuatazo: *Kimindi amenunua mnyama anayefugwa* au *Kimindi amenunua kifaa cha kukunia* nazi.

(iii) Ameshauriwa na baba

Tungo hii itakuwa na maana zifuatazo: *Baba amemshauri mtu fulani* au *baba na mtu mwingine wameshauriwa.*

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 22 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



(iv) Ana amenunua kata.

Neno *kata* katika muktadha wa sentesi hii, linaweza kuibua maana hizi: *Ana amenunua chombo kinachotengenezwa kwa kutumia kibuyu, au kifuu cha nazi kwa ajili ya kutekea maji, au kunywea mvinyo* au *Ana amenunua kitambaa, au pamba inayofunika jeraha linalotoa damu.*

(v) Juma ana ua nyumbani kwake.

Neno ua linaweza kuwa na maana ya *uzio uliojengwa kwa mabua, tofali, au matete kuzunguka nyumba* au *sehemu ya mmea inayochanua.*

**Chanzo cha utata katika lugha**

Utata katika lugha husababishwa na mambo anuwai yafuatayo:

***(a)*** ***Neno kuwa na maana zaidi ya moja.*** Kwa kawaida, katika kila lugha kuna maneno yenye maana zaidi ya moja. Kwa mfano, neno *paa* lina maana zifuatazo:

(i) Kitendo cha kuruka kwenda juu;

(ii) Sehemu ya juu ya nyumba;

(iii) Mnyama wa porini anayefanana na mbawala;

(iv) Kutoa magamba ya samaki kwa kuyakwangua; na

(v) Kutoa kiasi cha mkaa wa moto kwenye jiko ili kuukoleza sehemu nyingine au kumpatia mtu mwingine.

***(b)*** ***Utumiaji wa maneno yenye taswira au maana ya kisanaa iliyofichika.*** Kwa mfano, neno *ua* lina maana za msingi zaidi ya moja ambazo ni *sehemu ya mmea, kitendo cha kutoa uhai wa mtu au kiumbe kingine na uzio uliojengwa kuizunguka nyumba.* Vilevile, lina maana ya kitaswira ambayo ni *msichana mrembo.*

***(c)*** ***Kutozingatia alama za kiuakifishaji.*** Kwa mfano, tungo: *Baba Farida amekuja* inatoa taarifa ambayo ni *kuja kwa baba mzazi wa Farida.* Ikiwa mzungumzaji anakusudia kuja kwa Farida, atatumia alama ya mkato baada ya neno *baba.* Kwa mfano: *Baba, Farida amekuja.* Mzungumzaji asipozingatia alama za kiuakifishaji katika tungo kama hizi anaweza kutoa ujumbe usiokusudiwa.

***(d)*** ***Matumizi ya viamb shi vya utendea katika tung.*** Kwa mfano, tungo *Alimpigia mpira* inadokeza: *sababu, uelekeo, kwa niaba ya, na kifaa kilichotumika.*



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 23 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kuondoa utata katika matumizi ya lugha**

Mawasiliano ni muhimu sana katika jamii. Ili mawasiliano yaweze kufanikiwa ni lazima lugha iwe fasaha bila ya kuwa na utata wowote. Kuna njia mbalimbali za kuondoa utata katika matumizi ya lugha. Njia hizo ni pamoja na:

**(i)** ***Kufafanua maneno au tung zenye maana zaidi ya moja.*** Kwa mfano, tungo *Levota amenunua mbuzi* ina utata. Ili kuondoa utata katika tungo hii mtumiaji wa lugha anatakiwa kuongeza maelezo. Kwa hivyo, tungo inaweza kuwa *Levota amenunua mbuzi ya kukunia nazi*.

**(ii)** ***Kutumia alama za kiuakifishaji kwa usahihi.*** Kwa mfano, sentensi *Baba Esta amekuja* ina utata iwapo mzungumzaji amekusudia kuja kwa Esta. Mkato unapaswa kuwekwa baada ya neno *baba* ili kuonesha kuwa aliyekuja ni *Esta* na si baba mzazi wa Esta. Kwa hiyo, sentensi hiyo inatakiwa isomeke: *Baba, Esta amekuja*.

**(iii)** ***Kutumia maneno kwa kuzingt ia muktadha na hadhira.*** Hali hii huwezesha maana iliyokusudiwa ya maneno tata kujitokeza.

**(iv)** ***Kuzingatia upatanisho wa kisarufi.*** Matumizi sahihi ya upatanisho wa kisarufi huondoa utata katika matumizi ya lugha. Kwa mfano, tungo *Nimenunua mbuzi wawili* na *Nimenunua mbuzi mbili* zinaonesha kuwa vitu vilivyonunuliwa katika tungo ya kwanza ni wanyama na katika tungo ya pili ni vifaa vya kukunia nazi.

## Zoezi la 1.4

1. Jadili chanzo cha utata katika lugha.
2. Kwa kutumia mifano, eleza ni kwa namna gani utata unaweza kuondolewa katika matumizi ya lugha.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 24 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



## Tamrini

1. Bainisha tofauti zilizopo kati ya lugha ya taifa na lugha rasmi.
2. Jadili dhana ya rejesta na onesha kwa mifano umuhimu wa rejesta katika jamii.
3. Wataalamu wengi wametoa fasili ya dhana ya lugha kwa mitazamo yao. Fasili hizo zinafananaje?
4. Kwa kutumia mifano jadili changamoto ya matumizi ya misimu katika lugha.
5. Je, utachukua hatua zipi kutunza na kuongeza umahiri wako katika lugha unazozijua? Eleza huku ukitoa mifano dhahiri.
6. Eleza kwa mifano tofauti kati ya misimu na rejesta.
7. (a) Tunga sentensi tano zenye utata kisha bainisha maana mbalimbali zinazotokana na sentensi hizo.
   (b) Eleza njia za kuondoa utata katika sentensi za kipengele (a).

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 25 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Pili Maendeleo ya Kiswahili

## Utangulizi

Sura hii inahusu maendeleo ya Kiswahili. Katika sura hii utajifunza asili ya lugha ya Kiswahili, uhusiano wa Kibantu na lugha ya Kiswahili, chimbuko la Kiswahili, na usanifishaji wa Kiswahili. Lengo la sura hii ni kukuwezesha kupata maarifa na ujuzi ambao utakusaidia kufafanua na kueleza maendeleo ya lugha ya Kiswahili.

**Asili ya Kiswahili**

Lugha yoyote katika jamii huwa na asili yake. Asili ya Kiswahili ni mada ambayo imejadiliwa na wataalamu kwa mitazamo mbalimbali kulingana na tafiti walizozifanya. Neno *asili* lina maana ya mwanzo wa kitu fulani. Kwa hiyo, tunaposema asili ya Kiswahili tunamaanisha namna lugha hii ilivyoanza. Katika kujaribu kufafanua asili ya Kiswahili, kuna mitazamo mikuu minne: Kiswahili ni Kiarabu, Kiswahili ni lugha chotara, Kiswahili ni pijini au krioli, na Kiswahili ni Kibantu. Mitazamo hiyo inaelezwa kwa mapana yake kama ifuatavyo:

***1 Asili ya Kiswahili ni Kiarabu***

Wafuasi wa mtazamo huu wanadai kuwa asili ya Kiswahili ni lugha ya Kiarabu. Kwa mujibu wao, Kiswahili kilianza kuwapo mara baada ya Waarabu kufika katika Pwani ya Afrika Mashariki. Katika kutetea mtazamo wao, wafuasi hawa wanajenga hoja ambazo ni hoja ya maneno mengi ya mkopo yaliyomo katika Kiswahili ambayo, yana asili ya Kiarabu pamoja na hoja ya dini ya Kiislamu.

Kwanza, wanadai kuwa lugha ya Kiswahili ina msamiati mwingi wenye asili ya lugha ya Kiarabu. Watu hawa wanadai kuwa msamiati mwingi wa maneno yanayohusu biashara na uchumi una asili ya Kiarabu. Baadhi ya maneno hayo ni *fedha, biashara, ushuru, bei,* na kadhalika. Aidha, wanadai kuwa msamiati unaohusu sehemu ya kitu kama vile *theluthi, thumni, sudusi,* na kadhalika, una asili ya lugha ya Kiarabu.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 26 25/09/2019 13:57

For Online Use Only

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Vilevile, inadaiwa kuwa kwa kiasi kikubwa msamiati wa hesabu kama vile *ishirini, thelathini, arobaini, hamsini, na kadhalika* una asili ya lugha ya Kiarabu. Aidha, wanaendelea kudai kuwa neno "Kiswahili" linatokana na neno la Kiarabu *sahil*, likiwa kwenye umoja, na *sawahil* likiwa kwenye wingi. Maneno haya yana maana ya *upwa* au *pwani*, huku neno *Waswahili* likiwa na maana ya *Wapwani*. Kwa hiyo, wanaona kuwa huo ni uthibitisho kwamba asili ya Kiswahili ni Kiarabu.

Hata hivyo, hoja hii imekosolewa na wanaisimu wanaodai kuwa wafuasi wa mtazamo huo wanashindwa kuelewa kuwa kila lugha ina maneno ya mkopo. Massamba (2017:19) anadai kuwa hata maneno hayo, ambayo wanadai kuwa ni ya Kiarabu, kuna mengine kietimolojia hayana asili ya Kiarabu, bali asili yake ni lugha nyingine kama vile Kiajemi na Kihindi. Vilevile, ni ukweli ulio wazi kuwa lugha ya Kiswahili haijakopa maneno kutoka katika lugha ya Kiarabu pekee. Kuna maneno mengi yenye asili ya lugha nyingine kama vile Kiingereza, Kijerumani, Kireno, Kiajemi, Kifaransa, na nyinginezo. Kwa kawaida, lugha yoyote ina tabia ya kuathiriana na lugha nyingine. Lugha ya Kiswahili imeingiliana na lugha nyingine kwa sababu ya mwingiliano wa watumiaji wa lugha hizo katika shughuli za kiuchumi, kiutamaduni, na kisiasa.

Sambamba na hayo, inadaiwa kuwa lugha hukopa maneno ambayo hayahusu msamiati wa msingi wa lugha hiyo. Msamiati wa msingi ni ule unaoweza kuhimili mwingiliano wa lugha moja na nyingine bila kuathiriwa. Mfano wa maneno yanayohusu msamiati wa msingi ni pamoja na msamiati unaohusu maumbo ya kijiografia, viungo vya mwili, na kadhalika. Kwa mfano, ni vigumu kukuta msamiati unaohusu viungo vya mwili wa binadamu kama vile *jicho, mkono, mguu, pua, mdomo, sikio, kidole, paja,* na kadhalika ukiwa umekopwa kutoka lugha nyingine. Hali kadhalika, ni vizuri ikaeleweka wazi kuwa lugha haiwezi kufafanuliwa kwa kipengele kimoja tu cha msamiati. Lugha inapaswa kufafanuliwa kwa kutumia pia kigezo cha matamshi, maumbo, na miundo ya tungo. Vipengele vyote hivi vinaonesha kuwa Kiswahili kina mnasaba wa wazi kabisa na lugha nyingine za Kibantu.

Aidha, madai kwamba maneno mengi ya Kiswahili yametoka katika lugha ya Kiarabu hayana ushahidi yakinifu wa kitakwimu. Kuna baadhi ya watafiti waliojaribu kutoa takwimu ambazo bado zina dosari za wazi. Mathalani, Krumm (1940) anatoa makadirio kuwa kuna asilimia 20 ya



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 27 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

maneno ya mkopo katika Kiswahili cha mazungumzo, asilimia 30 katika Kiswahili cha maandishi na takribani asilimia 50 ya Kiswahili cha ushairi wa kale. Katika takwimu hizo, Massamba (2007) anayaona mambo mawili ambayo yanaibua dosari. Kwanza, Krumm haoneshi kama maneno yote ya mkopo yaliyomo katika Kiswahili yametoka katika lugha ya Kiarabu. Kwa hiyo, ni rahisi kugundua kuwa siyo maneno yote ya mkopo yametoka katika lugha ya Kiarabu. Pili, makadirio ya asilimia hizo hayakutolewa kwa kutafiti lahaja zote za Kiswahili. Krumm alitafiti kutoka kwenye vitabu vya sarufi vilivyoandikwa, kamusi na magazeti ya Mambo Leo yaliyochapishwa mwaka 1931 tu. Kwa hiyo, kisayansi sampuli hii haitoshi kujumuisha lugha ya Kiswahili kwa mapana yake na lahaja zote.

Mfano mwingine unaotolewa na Massamba (2007), unaohusu takwimu za msamiati wa Kiswahili, ni ule uliotolewa na Sassoon (1980). Yeye anadai kuwa asilimia 80 ya msamiati wa Kiswahili unashabihiana na msamiati wa lugha za Kibantu na asilimia 20 ni msamiati wa Kiarabu. Takwimu za Sassoon zinaonesha kwamba msamiati wa Kiarabu katika Kiswahili si mwingi kama inavyodhaniwa. Hata hizo asilimia 20 zinazotajwa si za msamiati wa Kiarabu pekee bali kuna maneno yenye asili ya Kijerumani kama vile *shule* na *hela*, lugha ya Kiingereza kama vile *shati*, *sketi* na *soksi*, na lugha ya Kireno kama vile *meza*, *gereza*, *kanisa*, na kadhalika. Kwa hiyo, tunaweza kusema kuwa takwimu zilizotolewa na Sassoon zinatia wasiwasi.

Hoja nyingine inayotumiwa na wafuasi wa mtazamo unaodai kuwa asili ya Kiswahili ni Kiarabu ni ile inayoegemea katika dini ya Kiislamu. Wafuasi wa mtazamo huu wanadai kuwa lugha ya Kiswahili imeletwa na Waarabu. Kwa kuwa lugha ya Kiswahili imeanzia Pwani ya Afrika Mashariki na wakaazi wengi wa Pwani ni Waislamu, na Uislamu uliletwa na Waarabu, basi inatosha kusema kuwa Kiswahili nacho kililetwa na Waarabu. Aidha, wanasisitiza kuwa hata dini ya Kiislamu ilisambazwa na kuenezwa kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Hivyo basi, Kiswahili kinatokana na Kiarabu.

Hoja hii inakosolewa na wanazuoni mbalimbali kwa madai kuwa huwezi kuchanganya lugha na dini.Wanazuoni wanaodai kuwa huwezi kuchanganya lugha na dini wanaeleza kwamba Kiswahili ni tofauti na Uislamu. Kwa maelezo yao wanasema kuwa Uislamu ni ule utamaduni unaofuatwa na waumini wake ambao haufungamani na lugha yoyote. Kuna Waislamu wengi duniani ambao hawawezi kuzungumza Kiswahili na kuna Waswahili

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 28 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


wengi ambao sio Waislamu. Lugha siyo dini, na utamaduni wa Kiswahili unatofautiana na wa Kiarabu (Chiraghdin na Mnyampala, 1977; Mazrui na Shariff 1994; na Massamba, 2017).

*2 Kiswahili ni lugha chotara*

Mtazamo huu unadai kuwa lugha ya Kiswahili ni lugha ambayo imetokana na mwingiliano kati ya lugha ya Kiarabu na lugha za Kiafrika. Madai haya yaliibuka na kupata umaarufu mkubwa kwa wanaakiolojia wa miaka ya 1950 hadi 1960. Mtazamo huo unadai kuwa Waarabu walipofika katika upwa wa pwani ya Afika Mashariki waliwaoa wanawake wa Kiafrika, na kuzaa nao watoto. Watoto hao walikuwa chotara wa Kiarabu na Kiafrika. Lugha ya Kiarabu (ya baba) iliingiliana na lugha za Kiafrika (upande wa mama), na mwingiliano huo ndio ulizaa lugha ya Kiswahili. Kwa hiyo, lugha ya Kiswahili ni chotara ya lugha ya Kiarabu na lugha za Kiafrika.

Hata hivyo, mtazamo huu umekosolewa kwa kukosa ushahidi thabiti. Kwanza, madai kuwa Kiswahili ni mchanganyiko wa Kiarabu na lugha nyingine za Kiafrika yana kasoro kubwa. Kwa mfano, haikuelezwa wazi ni lugha zipi za Kiafrika ambazo zimechanganyikana na Kiarabu na kuzaa Kiswahili. Pia, haikuelezwa wenyeji walioolewa na Waarabu walikuwa watu gani kwa mfano ni Wabantu, Wanailoti, Wakushiti, na kadhalika. Aidha, kuwapo kwa lahaja mbalimbali za Kiswahili katika upwa wa Afrika ya Mashariki kunatoa nafasi ya kupinga madai haya. Haiwezekani kila mahali Waarabu wanapochanganyikana na Waafrika ipatikane lahaja ya Kiswahili. Ingelikuwa hivyo, kungelikuwa na lahaja nyingi za Kiswahili katika sehemu mbalimbali za Afrika Magharibi ambapo kulikuwa na mwingiliano mkubwa kati ya Waarabu na Waafrika katika himaya za Ghana, Mali, Taghaza, Songhai, na kadhalika. Kwa hiyo, tunaona kuwa mtazamo huu una kasoro kubwa katika kueleza asili ya Kiswahili (Chiraghdin na Mnyampala 1977; Massamba 2017).

*3 Asili ya Kiswahili ni pijini au krioli*

Mtazamo huu unadai kuwa lugha ya Kiswahili ilianza kama pijini ambayo baadaye ilikuwa krioli. Inaelezwa kuwa Kiswahili ni lugha iliyopatikana wakati Waarabu walipoingiliana na Waafrika. Kwa kuwa walikuwa hawaelewani, basi kila mtu alizungumza lugha yake hali iliyosababisha


PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 29 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kuzaliwa kwa pijini. Kisha watoto waliozaliwa hawakuzungumza lugha ya Kiarabu wala lugha ya Kiafrika, bali waliongea mchanganyiko wa lugha hizo ambao ndiyo krioli.

Mazrui na Shariff (1994) wanadai kuwa Kiswahili kilianza kama pijini ambayo ilikuwa ni mchanganyiko wa lugha ya Kiarabu kwa kiasi kikubwa na lugha nyingine za Kiafrika. Baadaye, pijini hiyo ilikomaa na kuwa krioli. Kwa hiyo, lugha ya Kiswahili ikaonekana kuwa ni krioli ya Waarabu waliokuwa Afrika. Wanaendelea kudai kuwa baadaye krioli hiyo ilianza kubadilika kufanana na lugha zilizokuwa jirani yake ambazo zimetajwa kuwa ni Kipokomo na Kimijikenda.

Ukiyachunguza madai haya unaona kwamba hakuna uthibitisho wowote walioutoa kuonesha muundo wa pijini hiyo ulivyokuwa kabla ya kubadilika na kuwa krioli. Aidha, hawakuonesha mfumo wa krioli hiyo kifonolojia, kimofolojia na kisintaksia ulikuwaje. Sambamba na hayo, wafuasi wa mtazamo huo hawaoneshi huo msamiati mwingi wanaosema ulikuwa wa Kiarabu. Vilevile, hawasemi kuwa msamiati huo umechukua asilimia ngapi ya msamiati wote wala hatuambiwi hiyo sehemu ndogo ya msamiati ambao ulikuwa wa lugha ya Kiafrika ulichukua asilimia ngapi.

Upungufu mwingine unajitokeza wanapodai kuwa krioli hiyo ilibadilika na kufanana na lugha za Kibantu zilizokuwa jirani yake. Kwa hali ya kawaida, lugha huweza kubadilika na kuchukua sifa za lugha nyingine pale inapotokea lugha hiyo nyingine inazungumzwa na watu wa tabaka tawala, tabaka la juu kiuchumi (matajiri), watu mashuhuri, wasomi, au watu wenye maendeleo makubwa. Katika kipindi hicho, Waarabu ndiyo waliokuwa watu wenye sifa hizo za tabaka la juu. Kwa minajili hiyo, tunatarajia krioli hiyo ingebadilika na kufanana na Kiarabu kabisa kuliko kufanana na lugha za wenyeji ambazo ziliitwa za kishenzi na zisizo na ustaarabu wowote. Hivyo, tunaona kuwa mtazamo huu nao hauna ushahidi mujarabu wa kufanikisha kuweka bayana asili ya lugha ya Kiswahili.

### 4 *Asili ya Kiswahili ni Kibantu*

Mtazamo huu ndio unaoonekana kuwa na mashiko kwa wanaisimu wengi na wachambuzi mbalimbali wa masuala ya lugha. Mtazamo huu unasisitiza kuwa Kiswahili ni lugha yenye asili ya Kibantu, na unaweza kuthibitishwa kwa ushahidi wa kihistoria na kiisimu.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 30 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



**Ushahidi wa kihistoria kuwa Kiswahili ni Kibantu**

Ushahidi wa kihistoria ni matokeo ya kuchunguza mfumo mzima wa maisha katika maeneo ya pwani ya Afrika Mashariki kabla na baada ya ujio wa wageni. Ushahidi huu unadhihirisha kuwa kabla ya kuja kwa wageni katika Pwani ya Afrika Mashariki kulikuwa na wenyeji ambao walikuwa wakiishi hapo. Bila shaka, wenyeji hao walikuwa na lugha yao. Kuna ushahidi unaodhihirisha kwamba wenyeji wa Pwani ya Afrika Mashariki walikuwa na lugha zao ambazo baadaye ndizo zilikuja kujulikana kama lahaja za Kiswahili. Hivyo, ushahidi huu unathibitisha kuwa Kiswahili kilikuwapo hata kabla ya ujio wa wageni. Hoja zifuatazo, zinathibitisha madai hayo.

**1 *Kitabu cha Periplus of the Erythrean Sea***

Inaelezwa kwamba kitabu cha Periplus of the Erythrean Sea kiliandikwa na nahodha wa meli ya Alexandria ambaye hakutajwa jina lake. Kitabu hiki kinatoa maelezo ambayo ni mwongozo kuhusu bahari ya Hindi. Katika kitabu hicho kuna majadiliano na maelezo mengi yanayohusu historia ya eneo la pwani ya Afrika Mashariki. Massamba (2002) anaeleza kuwa maneno *periplus* na *erythrean* ni ya Kiyunani ambayo tunaelezwa kuwa asili yake hasa ni Kilatini. Neno *periplus* humaanisha *safari ya kuzunguka* na neno *erythrean* linamaanisha *ekundu*. Hivyo, Erythrean Sea inamaanisha *Bahari ekundu* (*Bahari ya Shamu)*. Haijulikani hasa kitabu hicho kiliandikwa mwaka gani ila inadhaniwa kuwa kiliandikwa huko Alexandria karne ya kwanza ya Majilio ya Masihi. Kitabu hicho kinataja na kusimulia habari za bandari mbalimbali za *Azania* (Afrika Mashariki) na habari za vyombo kama vile *ngalawa*, *madema*, na *mitepe*. Kuwapo kwa maneno kama hayo, ambayo yamo katika Kiswahili cha leo, kunadhihirisha kuwa lugha hii ilikuwapo kabla ya ujio wa wageni.

**2 *Ushahidi wa Al-Masudi (karne ya 10)***

Al-Masudi alifika Pwani ya Afrika Mashariki kati ya mwaka 915 na 945 B.K. Yeye alisema kuwa wenyeji wa Pwani ya Afrika Mashariki waliitwa *Wazanji* na watawala wao waliitwa *Wakilimi*. Watawala hao waliaminika kuwa walitawala kwa nguvu za Mungu, na kwamba *Kiazania* ndiyo lugha yao iliyotumika katika mawasiliano. Al-Masudi anadai kuwa neno *Zanzibar* linatokana na *Zenjibar*, yaani Pwani ya Zanji. Ushahidi huu unaonesha kuwa wenyeji wa Pwani ya Afrika Mashariki walikuwa na lugha yao hata kabla ya wageni.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 31 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### 3 *Ushahidi wa Al-Idrisi (karne ya 12*

Huyu alikuwa mfanyakazi katika mahakama ya Mfalme Rogers II kutoka kisiwa cha Sicily. Ugunduzi wake ulijikita juu ya jina la Zanzibar. Yeye anasema jina la zamani la Zanzibar ni Unguja. Vilevile, aliandika kitabu ambacho kilikuwa na majina ya ndizi kama vile *mkono wa tembo*, *muriani*, na *sukari*, ambayo ni maneno ya Kiswahili. Kwa kuwa maneno haya ni ya Kiswahili cha leo, basi hatuna shaka kusema kuwa lugha hii ilikuwapo kabla ya ujio wa wageni.

### 4 *Ushahidi wa Marco Polo*

Marco Polo alikuwa ni mgeni aliyeandika kitabu kikiwa na maelezo kuwa Zanzibar (Zanguabar) iliitwa *Ungudya* kutokana na lugha ya wakazi hao. Vilevile, anadai kuwa chakula cha wenyeji wa Zanzibar kilikuwa ni ndizi aina ya *muriyani*, *mkono wa tembo* na vyakula vingine kama *kundi* (*kunde*) na *fili* (aina ya maharage). Maneno haya yanadhihirisha kuwa lugha ya Kiswahili ilikuwapo hata kabla ya wageni kufika katika upwa wa Afrika Mashariki.

### 5 *Historia ya Kilwa*

Historia ya Kilwa inahusu historia ya zamani ya Kilwa Kisiwani na Kilwa Kivinje katika karne ya 10-16 B.K. Historia hii inahusisha majina ya utani ya masultani wa kwanza Ali Ibn Husein, ambaye aliitwa *Nguo nyingi*, na mwanae Mohamed Ibn Ali wa Kilwa aliyeitwa *Mkoma watu*. Kutokana na habari hizi, inasemekana kuwa Kiswahili kiliwahi kusemwa katika karne ya 10 au ya 11 B.K. Pia, kuna maelezo ya Talt Ibn al- Husein ambaye aliitwa *Hasha Hazifiki* kama jina la utani. Majina haya ya utani yanathibitisha kuwepo kwa lugha ya Kiswahili hata kabla ya ujio wa wageni.

### 6 *Ushahidi wa Ibn Batuta (karne ya 14*

Ibn Batuta alifika Pwani ya Afrika Mashariki mwaka 1331 B.K. Alisafiri kutoka Mogadishu kwenda Kilwa kupitia Mombasa. Katika maelezo yake, anaeleza maisha ya watu wa nchi hii ya Afrika Mashariki ingawa yeye aliita nchi ya *Sahel*. Katika maelezo yake anadai kuwa alianza safari baharini kutoka Mogadishu kwenda nchi ya Sahel na mji wa Kilwa ambao umo katika nchi za Zanj. Pia anaeleza kuwa safari kutoka Mombasa, katika nchi ya Sahel ilichukua siku mbili… Vilevile watu wa Mombasa huagiza nafaka kutoka Uswahilini.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 32 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Ushahidi mwingine unaoonesha kuwa Kiswahili kilikuwapo kabla ya ujio wa Waarabu ni kwamba, inasemekana kuwa Ibn Batuta alipofika Kilwa alikutana na washairi wenyeji walioandika mashairi na tenzi katika lugha ya Kiswahili.

7. ***Ushairi wa Kiswahili***

Ushahidi wa ushairi wa Kiswahili umejitokeza katika tendi na tenzi ambazo ziliandikwa kwa vipindi tofauti. Utendi wa *Fumo Liyongo* ambao mtunzi wake ni Mohamed bin Abubakar katika miaka ya 1160 – 1204 ni mfano wa ushahidi wa ushairi wa Kiswahili. Utendi huu wenye beti 234 ulitungwa kwa lahaja za Kiamu na Kimvita ambazo zinafanana na Kiswahili. Ufuatao ni mfano wa beti za Utendi wa Fumo Liyongo:

1. Hadithi niwandikiye,
   Ya ajabu musikiye,
   Yalojiri amriye,
   Mupate kufahamiya.

2. Niweleze kwa utungo,
   Hadithi yake Liyongo,
   Niweleze na mazingo,
   Mambo yalomzingiya.

*(Mulokozi, 1999), Tenzi Tatu za Kale*

Vilevile, kuna utenzi wa Tambuka ulioandikwa katika miaka 1700. Utenzi huu uligunduliwa na Dkt. E. A. Alpers wa Goa ambaye pia aligundua barua 14. Ushahidi huu unaonesha kuwa barua hizo ziliandikwa kwa lahaja ya Kimvita ambayo ni moja ya lahaja za Kiswahili. Mfano wa ubeti wa utenzi wa Tambuka ni:

450. Kwa mau mema mekundu,
     Yali mivazi ya ngandu,
     Na ukundufu ya tundu,
     Haiba yakwe ya pua.

Utenzi mwingine unaothibitisha Ubantu wa Kiswahili ni utenzi wa Mwanakupona. Utenzi huu umeandikwa kwa Kiswahili cha lahaja ya Pate na Mwanakupona (Nana) kwenye miaka ya 1850 akimuusia bintiye aliyejulikana kwa jina la Hashima binti Sheikh Mataka. Zifuatazo ni baadhi ya beti za utenzi huo:



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 33 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

28. Keti naye kwa adabu,
Simtie ghadhabu,
Akinena simjibu,
Jitahidi kunyamaa.

31. Kilala siikukuse,
Mwegeme umpapase,
Na upepo asikose,
Mtu wa kumpepea.

34. Mnyoe mpalilize,
Sharafu umtengeneze,
Na udi umfukize,
Bukurata wa ashia.

Tenzi hizi za kale ambazo zinafanana sana na Kiswahili, hasa kimsamiati, ni uthibitisho kuwa Kiswahili ni lugha ya Kibantu kwa kuwa kilitumika hata kabla ya ujio wa wageni.

**Ushahidi wa kiisimu kuwa Kiswahili ni Kibantu**

Ushahidi wa kiisimu ni matokeo ya uchunguzi wa lugha ya Kiswahili kwa kuangalia misingi ya kisayansi ya lugha inayohusu orodha ya msamiati, vipengele vya kifonolojia, vipengele vya kimofolojia, pamoja na vipengele vya kisintaksia. Ushahidi wa kiisimu unathibitishwa na tafiti za wataalamu wa isimu wafuatao:

***1. Ushahidi wa msamiati***

Kuna tafiti mbalimbali ambazo zimefanywa kuhusu kufanana kwa msamiati wa lugha za Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu. Kwa mfano, Clement Maganga (1997) alifanya utafiti kwa kukusanya na kuchunguza jumla ya maneno 9179 ya Kiswahili. Katika utafiti wake, aligundua asilimia 60 ya maneno yote yanayoweza kuandikwa na kutamkika katika lugha ya Kiswahili yana asili ya lugha za Kibantu; asilimia 30 ni lugha ya Kiarabu na asilimia 10 ni lugha nyingine za kigeni kama vile Kiingereza, Kirejumani, Kireno, Kihindi, Kiajemi, na Kifaransa. Kwa hiyo, kutokana na idadi kubwa ya maneno hayo kuwa ni ya Kibantu ni dhahiri kuwa Kiswahili ni Kibantu.


PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
For Online Use Only

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Mtafiti mwingine ni Malcom Guthrie ambaye alifanya utafiti kuhusu uhusiano uliopo baina ya lugha za Kibantu zilizoko eneo ambalo Wabantu wanaishi. Guthrie alichunguza maneno 22,000 kutoka lugha 200 za Kibantu. Katika uchunguzi wake, aligundua kuwa maneno 2300 yamo katika lugha mbalimbali za Kibantu na Kiswahili kikiwemo. Pia, mashina ya maneno yapatayo 500 ya lugha ya Kiswahili yamo katika lugha mbalimbali za Kibantu kama ifuatavyo:

51% Kiluba kutoka Katanga Zaire (Kwa sasa ni Jamhuri ya Kidemokrasia ya watu wa Kongo)
54% Kiwemba (Zambia)
44% Kikongo (Zaire Mashariki)
44 % Kiswahili (Pwani ya Afrika Mashariki)
41% Kisukuma (Tanzania)
35% Kiyao (Tanzania /Msumbiji)
20% Kisotho (Botswana)
43% Kirundi (Burundi)
37% Kinyoro (Uganda)
29% Kizulu (Afrika ya Kusini)

Uchunguzi wa Guthrie unathibitisha kuwa Kiswahili ni Kibantu kwa kuwa kinafanana kimsamiati na lugha nyingine za Kibantu (Guthrie, 1971).

Hali kadhalika, kuna ushahidi unaonesha kuwa lugha ya Kiswahili na zile za Kibantu zinafanana katika mpangilio wa mofimu na mashina ya maneno. Batibo (2001) alifanya uchunguzi wa Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu na kugundua kuwa:

(i) Kuna mfanano wa muundo wa mofu kwa kuangalia mzizi, vitenzi na mashina ya vitenzi katika Kiswahili. Mzizi wa vitenzi katika lugha ya Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu una muundo wa konsonanti, irabu na konsonanti (KIK). Angalia mifano ifuatayo:



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 35 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Jedwali 2.1 (a)** Muundo wa mzizi wa Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu

| Lugha | Kitenzi | Mzizi | Muundo wa mzizi wa kitenzi |
|---|---|---|---|
| Kiswahili | pika | -pik- | -KIK- |
| Kilingala/Zaire | bila | -bil- | -KIK- |
| Kiluguru | kana (kata) | -kan- | -KIK- |

(ii) Mashina ya maneno ya lugha ya Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu yana mfanano katika muundo wake ambapo huwa na muundo wa KIKI. Chunguza mifano ifuatayo:

**Jedwali 2.1 (b)** Muundo wa mashina ya Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu

| Lugha | Kitenzi | Shina | Muundo wa shina la kitenzi |
|---|---|---|---|
| Kiswahili | kucheka | cheka | KIKI |
| Kihaya | okusheka | sheka | KIKI |
| Kinyaturu | uheka | heka | KIKI |
| Kipare | kuseka | seka | KIKI |

Mifano ya mizizi na mashina ya vitenzi katika majedwali hapo juu ni uthibitisho wa mfanano wa mashina ya maneno ya Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu.

Wataalamu wengine waliochunguza kufanana kwa msamiati wa msingi kunakojitokeza baina ya lugha ya Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu ni Massamba *na wenzie* (1999), na Massamba (2017). Msamiati wa msingi ni ule unaohusu mambo ambayo hayabadiliki kutokana na mabadiliko ya kiutamaduni kama vile msamiati wa sehemu za mwili na vitu vya asili. Kufanana huko hujitokeza zaidi katika mzizi. Jedwali lifuatalo linaonesha kufanana kwa baadhi ya maneno ya lugha ya Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 36 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



**Jedwali 2.2** Kufanana kwa baadhi ya maneno ya lugha ya Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu

| Kiswahili | Kindali | Kizigua | Kijita | Kikurya | Kindendeule |
|---|---|---|---|---|---|
| Mtu | umu-ndu | m-ntu | omu-nu | omu-ntu | mu-ndu |
| Maji | a-mashi | manzi | o-manji | a-manche | maache |
| Mwana | umw-ana | mwa-ana | o-mw-ana | omo-na | mwa-ana |

**2 *Muundo wa tungo***

Muundo wa tungo za lugha nyingine za Kibantu hufanana sana na ule wa lugha ya Kiswahili katika kirai nomino (KN) na kirai kitenzi (KT) kwa kuzingatia mfuatano na uhusiano wa maneno katika tungo. Tazama mifano ifuatayo:

**Jedwali 2.3** Muundo wa tungo za Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu

| **Lugha** | **KN** | | | **KT** | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **N** | **V** | **V** | **T** | **N** |
| **Kiswahili** | mtoto | wangu | mdogo | anacheza | ngoma |
| **Kisukuma** | ng'wana | wane | ndo | alebina | ng'oma |
| **Kikonongo** | mwana | nane | mdo | akusapa | ngoma |

Pia nomino au kiwakilishi cha Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu hutawala upatanisho wa kisarufi kati yake na maneno mengine yanayoandamana nayo katika tungo. Upatanisho huo hujidhihirisha katika viambishi vya upatanisho wa kisarufi vya maneno hayo. Mfano ufuatao unathibitisha hoja hii:

**Jedwali 2.4** Upatanisho wa kisarufi wa tungo za Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu

| **Lugha** | **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|---|
| Kiswahili: | *m*toto *m*zuri *a*nacheza | *wa*toto *wa*zuri *wa*nacheza |
| Kijita: | o-*mw*-ana *w*ekisi keenya | *a*-*bh*-ana *bh*ekisi *abhee*nya |
| Kilugulu: | i-mw-ana i*m*notzi *k*ofvina | i-*w*-ana i*w*anotzi *w*ofvina |
| Kihaya: | o-*mw*-ana o*m*uruungi *na*zana | a-*b*-ana *b*aruungi ni*ba*zana |
| Kinyaturu: | *mw*-ana *m*ʊja ʊgisa | *v*-ana *a*ja *vi*gisa |
| Kipare: | *mw*-ana *w*edi *e*shinjiga | *v*-ana *v*edi *ve*shinjiga |



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 37 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Viambishi vilivyoandikwa kwa hatimlalo katika jedwali vinaonesha upatanisho wa kisarufi kati ya nomino, vivumishi, na vitenzi. Huu ni uthibitisho kwamba Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu hufanana katika utaratibu wa upatanisho wa kisarufi.

### *3 V itenzi*

Kuna mfanano mkubwa kati ya vitenzi vya lugha ya Kiswahili na vya lugha nyingine za Kibantu. Mfanano huo hujidhihirisha katika vipengele vifuatavyo:

**(i) Mwanzo wa vitenzi**

Vitenzi vyote vya Kiswahili na vile vya lugha nyingine za Kibantu huanza na viambishi awali vipatanishi vya nafsi. Viambishi vilivyoandikwa kwa hatimlalo katika vitenzi ni viambishi awali vya nafsi ya kwanza umoja. Chunguza mifano ifuatayo:

**Jedwali 2.5** Mwanzo wa vitenzi vya Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu

| Lugha | Vitenzi |
|---|---|
| Kiswahili | *ni*-nakwenda |
| Kihaya | *ni*-ngenda |
| Kiyao | *n*-gwenda |
| Kindendeule | *ni*-yenda |

**(ii) Miisho ya vitenzi**

Vitenzi vingi vya Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu huishia na irabu **a** katika hali ya uyakinishi. Chunguza mifano ifuatayo ya vitenzi vya Kiswahili, lugha nyingine za Kibantu, na vitenzi vyenye asili ya Kiarabu.

**Jedwali 2.6** Miisho ya vitenzi vya Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu

| Kiswahili | Kihaya | Kijita | Kinyaturu | Kinyakyusa |
|---|---|---|---|---|
| kulal*a* | okuniam*a* | okumaam*a* | ura*a* | ukulambalal*a* |
| kuva*a* | okujwal*a* | okufwaal*a* | uri*a* | ukufwal*a* |
| kulet*a* | okulet*a* | okuleet*a* | get*a* | get*a* |
| kwend*a* | okugend*a* | okugend*a* | gend*a* | ukubhuk*a* |
| kuzik*a* | okuziik*a* | okusiik*a* | uvïk*a* | ukusyil*a* |



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 38 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Kwa upande mwingine, vitenzi vya Kiswahili vyenye asili ya Kiarabu vina miisho yenye irabu tofauti na zile zinazopatikana katika vitenzi vya lugha za Kibantu.

**Jedwali 2.7** Miisho ya vitenzi vya Kiswahili vyenye asili ya Kiarabu

| Vitenzi vinavyoishia na irabu *i* | Vitenzi vinavyoishia na irabu *u* |
|---|---|
| adil*i* | abud*u* |
| ajir*i* | adhib*u* |
| ahid*i* | dhulum*u* |
| da*i* | dhur*u* |
| dahil*i* | kufur*u* |
| farij*i* | hesab*u* |
| rubun*i* | nusur*u* |

Ukichunguza mifano hiyo hapo juu unabaini kwamba vitenzi vya Kiswahili na vile vya lugha nyingine za Kibantu vinaishia na irabu -*a*. Kwa upande mwingine, vitenzi vya Kiarabu huishia na irabu -*i* au -*u* badala ya –*a*.

**(iii) Mnyambuliko wa vitenzi**

Vitenzi vya lugha nyingine za Kibantu huweza kunyambuliwa kama ilivyo katika vitenzi vya lugha ya Kiswahili. Tazama mifano ifuatayo katika jedwali:

**Jedwali 2.8** Mnyambuliko wa vitenzi vya Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu

| Lugha | Kitenzi | Mnyambuliko |
|---|---|---|
| Kiswahili | kulima | m-lim-aj-i, ki-lim-o, u-lim-aj-i na m-ku-lim-a |
| Kihaya | okulima | o-mu-lim-i (mkulima) |
| Kiha | ukurima | indimo (kilimo) |
| Kinyaturu | urima | mu-rimi (mkulima) i-rima (kilimo) |

Mfano huu unaonesha jinsi vitenzi vya Kiswahili na vile vya lugha nyingine za Kibantu vinavyokubali utaratibu wa unyambulishaji. Aidha, hali hii hujitokeza pia katika uambishaji wa viambishi mbalimbali kwenye mzizi wa vitenzi.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 39 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**(iv) Uambishaji wa vitenzi**

Vitenzi vya lugha nyingine za Kibantu vinaweza kupokea viambishi katika mzizi kama ilivyo katika vitenzi vya lugha ya Kiswahili. Tazama mifano ifuatayo:

**Jedwali 2.9** Uambishaji wa vitenzi vya Kibantu

| Lugha | Kitenzi | Uambishaji |
|---|---|---|
| Kiswahili | anacheza | a-na-chez-a |
| Kihaya | nazaana | na-zaan-a |
| Kinyaturu | uguina | u-gu-in-a |
| Kichaga (Kivunjo) | naitema | na-i-tem-a |

Mifano katika jedwali hapo juu inaonesha uambishaji unavyojitokeza katika vitenzi vya Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu. Tazama uchanganuzi ufuatao wa vitenzi hivyo:

Kiswahili: *anacheza*:

a- ni kiambishi cha nafsi ya tatu umoja.
-na- ni kiambishi cha wakati uliopo.
-chez- ni mzizi.
-a ni kiambishi tamati, uyakinishi.

Kihaya: *nazana*:

na- ni kiambishi nafsi ya tatu umoja.
-ø- ni kiambishi cha wakati uliopo.
-zan- ni mzizi wa neno.
-a ni kiambishi tamati, uyakinishi.

Kinyaturu: *uguina*,

ʋ- ni kiambishi nafsi ya tatu umoja.
-gʋ- ni kiambishi wakati uliopo.
-in- ni mzizi wa neno.
-a ni kiambishi tamati, uyakinishi.

Kichaga (Kivunjo): *naitema*

na- ni kiambishi cha nafsi ya tatu umoja.
-i- ni kiambishi cha wakati uliopo.

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 40 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



-tem- ni mzizi wa neno.

- a ni kiambishi tamati, uyakinishi.

**4 *Ngeli za nomino***

Katika lugha ya Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu nomino hupangwa katika makundi yaitwayo *ngeli za nomino* kwa kuzingatia kigezo cha maumbo ya umoja na wingi wa nomino hizo au upatanisho wa kisarufi kama ifuatavyo:

**(i) Maumbo ya nomino**

Maumbo ya umoja na wingi wa majina hutumika kupanga makundi maalumu ya majina yenye sifa zinazofanana katika lugha ya Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu. Chunguza mifano ifuatayo:

**Jedwali 2.10 (a)** Ngeli za nomino za Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu kwa kigezo cha maumbo ya majina.

| Lugha | Umoja | Wingi | Ngeli za nomino |
|---|---|---|---|
| Kiswahili | mti | miti | m(u)-/mi- |
| Kinyamwezi | (u)mti | imiti | mu-/mi- |
| Kihehe | umubiki | imibiki | mu-/mi- |
| Kirangi | muti | miti | mu-/mi |

**(ii) Upatanisho wa kisarufi**

Utaratibu wa kubainisha makundi ya majina kwa kutumia upatanisho wa kisarufi unaotumika katika Kiswahili, unatumika pia katika lugha nyingine za Kibantu. Chunguza mifano ifuatayo:

**Jedwali 2.10 (b)** Ngeli za nomino za Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu kwa kigezo cha upatanisho wa kisarufi

| Lugha | Umoja | Wingi | Ngeli za nomino |
|---|---|---|---|
| Kiswahili | mtoto *a*-nacheza | watoto *wa*-nacheza | a - wa |
| Kingoni | mwana *i*-kina | vana *vi*-kina | i - vi |
| Kichaga | mona *a*-itema | wana *wa*-itema | a - wa |
| Kisambaa | Ng'wana *a*-shezigha | wana *wa*-shezigha | a - wa |



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 41 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 2.1

1. Tumia vitenzi vya lugha mbalimbali za Kibantu kuthibitisha ubantu wa Kiswahili.

2. Tathmini hoja zinazotolewa na wanaisimu wanaodai kuwa asili ya lugha ya Kiswahili ni Kiarabu.

3. Baada ya kusoma hoja mbalimbali zinazohusu asili ya Kiswahili, una msimamo gani kuhusu asili ya Kiswahili? Toa hoja kutetea msimamo wako.

**Chimbuko la Kiswahili**

Neno chimbuko lina maana ya mahali ambapo kitu fulani huanzia. Kumekuwa na mitazamo mbalimbali kuhusu chimbuko la Kiswahili kulingana na tafiti zilizofanywa. Katika kiwango hiki tutapitia kwa juujuu tu mitazamo mitatu, ambayo ni: (i) wa Johnston (1919) unaodai kwamba Wabantu Azali walitokea maeneo ya magharibi ya Afrika wakaelekea mashariki hadi maeneo ya kaskazini-magharibi ya Uganda na kusini-magharibi ya Sudani, eneo la Nyanza-Albert-Nile; hapo wakaibukia mame-Bantu; (ii) wa Greenberg (1955) unaodai kwamba Wabantu waliinukia katika maeneo ya mpakani mwa Kameruni na kaskazini-mashariki ya Nijeria na (iii) wa Guthrie unaodai kwamba Wabantu chimbuko lao ni mpakani mwa Zambezia-Kongo, maeneo karibu na msitu wa Ikweta. Wataalamu wote hawa wanadai kwamba wabantu hawa walisambaa kusini mwa jangwa la Sahara huku wengine wakibaki kaskazini, na wengine wakaelekea mashariki hadi pwani ya Afrika Mashariki ambako ndiko kulikoibuka lugha ya Kiswahili.

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology




**Kielelezo 2.1** Ramani ya Afrika kuonesha msambao wa Wabantu kwa mujibu wa Greenberg (1955)



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 43 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kwa mujibu wa Turton (1975), hadi kufikia karne ya 10 Wabantu walikwishafika maeneo ya mto Tana. Wabantu walikuwa wamesambaa katika upwa wote wa Afrika Mashariki. Katika maisha yao walianza kuwa na uhusiano wa kibiashara na kijamii kama vile kuoleana. Katika kufanya hivyo, lugha zao zikaanza kuingiliana. Kwa kuwa lugha zao zote zilikuwa zimetoka katika asili moja zikaanza kufanana, zilizokaribiana zaidi zikafanana zaidi kuliko zile zilizokuwa mbali. Huu ndio ulikuwa mwanzo wa lahaja za Kiswahili.

**Lahaja**

TUKI (2013) wanasema kuwa lahaja inatokana na tofauti katika matamshi, maumbo, na matumizi ya maneno katika maeneo mbalimbali kwa lugha yenye asili moja. Hata hivyo, tofauti hizo haziwezi kukwamisha maelewano miongoni mwa watumiaji wa lahaja hizo. Lugha ya Kiswahili ina lahaja mbalimbali, ingawa wanazuoni wanatofautiana kuhusu majina na hata idadi. Jedwali lifuatalo linaorodhesha baadhi ya lahaja za Kiswahili kwa mujibu wa wataalamu mbalimbali.

For Online Use Only


PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 44 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



**Jedwali 2.11** Lahaja za Kiswahili

| Lahaja | Eneo | Mifano ya maneno |
|---|---|---|
| Chimiini | Kusini mwa Somalia | moyi (moja), muti (mti), mamba (mamba) |
| Kitikuu | Mpakani mwa Kenya na Somalia | nke (mke), imi (mimi), mbe (mbele) |
| Kisiu | Kisiwa cha Pate | mbeu (mbegu), saa (zaa), Sawahili (Swahili) |
| Kipate | Kisiwa cha Pate, Kusini Magharibi | vumi (vumbi), kija (kiza), lele (lala) |
| Kiamu | Kisiwa cha Amu Kaskazini | muhi (mji), mbee (mbele), mlulu (mdudu) |
| Kimvita | Mombasa na Kilifi | leso (kanga), misu (panga), mivu (mishale) |
| Kijomvu | Mombasa | hali (ghafi), luha (lugha), tangi (tangu) |
| Chichifundi (Shirazi) | Mombasa na Rasi ya Funzi | jenje (genge), mosi (moshi), fuvi (fupi) |
| Kimtang'ata (Kimrima) | Tanga | sabaa (saba), mabwe (mawe), winza (winda) |
| Kipemba | Kisiwa cha Pemba | gino (jino), dade (dada), sizia (sinzia), mfereji (bomba) |
| Kiunguja (Kimji) | Zanzibar Mjini | mfereji (bomba), mwamu (shemeji), teleka (pika) |
| Kitumbatu | Kisiwa cha Tumbatu | kazu (kanzu), zi (nzi), kolo (koo) |
| Kimakunduchi (Kikae au Kikale) na Kihadimu | Zanzibar Kusini | bui (buibui), bwe (jiwe), ndo (ndiyo) |
| Kimwani | Kaskazini mwa Msumbiji | julu (juu), kuli (kuni), mnu (mtu). |



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 45 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE




**Kielelezo 2.2** Ramani ya Pwani ya Afrika Mashariki kuonesha mzagao wa lahaja za Kiswahili



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

**Sababu za kuibuka kwa lahaja za Kiswahili**

Kuna sababu mbalimbali za kuzuka kwa lahaja za Kiswahili. Sababu hizo zinaweza kuwa ni kuhamahama kwa watu, uwezo wa kiuchumi, umbali wa kijiografia, mwingiliano wa kijamii, elimu, dini, na kupita kwa wakati. Kuna sababu mbalimbali za kutokea kwa lahaja kama zinavyofafanuliwa hapa chini:

1. ***Mwingiliano wa kijamii***
   Kutokana na kuingiliana kwa tamaduni mbalimbali kama vile kuoleana, kushiriki katika masuala ya dini, vita, na mengineyo huweza kusababisha watu kuathiriana kimatamshi, kimsamiati, na kimuundo. Hivyo, athari hizo zinaweza kusababisha kuzuka kwa lahaja mpya.

2. ***Umbali wa kijiografia***
   Wazungumzaji wa lugha moja huweza kutawanyika katika maeneo tofauti kutokana na sababu mbalimbali. Sababu hizo zinaweza kuwa ni matakwa yao binafsi, au ya lazima kama vile kutenganishwa na maumbile ya kijiografia. Maumbile hayo yanaweza kuwa kisiwa, mipaka ya kisiasa na uharibifu mkubwa wa mazingira unaotokana na majanga ya asili kama vile tetemeko la ardhi, mlipuko wa volkano, na mafuriko. Mtawanyiko huo unapotokea huweza kuathiri lugha kwa namna moja ama nyingine. Huweza kusababisha kuwapo kwa tofauti za kimatamshi, kimuundo, na hata msamiati. Ifahamike kuwa mabadiliko yanayosababisha kutokea kwa tofauti hizo hayatokei ghafla bali hutokea taratibu kadiri muda unavyozidi kupita. Matokeo ya tofauti hizo huweza kuibua lahaja.

## Zoezi la 2.2

1. Eleza sababu za kutokea kwa lahaja za Kiswahili.
2. Jadili mitazamo mbalimbali kuhusu chimbuko la Kiswahili.

**Usanifishaji wa Kiswahili**

Usanifishaji ni uamuzi wa makusudi wa kuteua lugha moja au mojawapo ya lahaja za lugha na kuifanyia marekebisho ya kimatamshi, kimaana, kimuundo na kimaandishi, ili iweze kutumika katika mawasiliano rasmi (Msanjila *na wenzie*, 2009:129). Mawazo haya yanaonekana kufanana na yale ya King'ei (2010)


PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 47 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

ambaye anasema usanifishaji wa lugha ni utaratibu wa kukuza na kuendeleza lahaja moja ya lugha iliyoteuliwa kuwa msingi wa lugha sanifu.

**Uteuzi wa lahaja ya kusanifisha**

Yafuatayo ni mambo ya kuzingatia katika uteuzi wa lahaja ya kusanifisha:

(i) Lahaja kutonasibishwa na watu au jamii maalumu. Uteuzi huu husaidia watu wasiokuwa wazawa wa lahaja hiyo kupenda kuitumia.

(ii) Idadi ya watumiaji wa lahaja hiyo. Lahaja inatakiwa kuwa na watumiaji wengi. Hii inamaanisha kwamba lahaja hiyo lazima iwe imeenea katika maeneo mbalimbali ya jamii inayohusika.

(iii) Urahisi au wepesi wa kujifunza lahaja hiyo. Lahaja inayoteuliwa lazima iwe na mlandano na lugha au lahaja za makundi mengine katika jamii. Hii inasaidia watu kujifunza lugha itakayotolewa na lahaja hiyo kwa urahisi.

(iv) Kuwepo kwa machapisho yaliyoandikwa kwa lahaja hiyo. Lahaja inayoteuliwa inatakiwa kuwa na machapisho katika nyanja mbalimbali kama vile dini, elimu, uchumi, na siasa.

**Historia ya usanifishaji wa Kiswahili**

Usanifishaji wa Kiswahili ulitokana na uamuzi uliofanywa na Tume ya Phelps-Stokes iliyokuwa inashughulika na masuala ya elimu. Tume hiyo ilipotembelea Tanganyika mwaka 1924, ilibaini kuwa hakukuwa na ushirikiano kati ya serikali za kikoloni na misheni. Baada ya ziara hiyo, tume iliamua kuwa Waafrika wawe na haki ya kutumia lugha zao za kwanza katika elimu, ili kuhifadhi utamaduni wao. Mnamo mwaka 1925, mkutano wa elimu ulifanyika Dar es Salaam. Katika mkutano huo, iliamriwa kuwe na lugha moja ya kutumika kutolea elimu katika eneo lote la Tanganyika ili kupunguza gharama za elimu. Kiswahili kilichaguliwa bila kupingwa kwa sababu kilikuwa kimekwisha enea kote nchini na kutumiwa katika mawasiliano ya nyanja zote.

Baada ya mkutano wa Dar es Salaam wa mwaka 1925, mkutano mwingine uliojumuisha nchi zote za Afrika Mashariki uliitishwa Mombasa Juni 5, 1928. Mkutano huu ulihudhuriwa na wajumbe wa nchi zote za Afrika Mashariki pamoja na mwanaisimu mashuhuri Carl Meinhof. Miongoni mwa mambo yaliyojadiliwa katika mkutano huo ni ripoti ya mkutano wa Dar es Salaam wa mwaka 1925. Maafikiano ya mkutano wa mwaka 1925 yalikubaliwa na nchi zote baada ya



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 48 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



kuboreshwa ikizingatiwa kwamba mapendekezo ya kutumia Kiswahili katika elimu yaliihusu Tanganyika peke yake. Uamuzi mwingine muhimu uliofanyika ni kuteua lahaja ya Kiunguja kwa ajili ya kusanifishwa.

Pia, katika mkutano huo wa mwaka 1928 iliamriwa kuwepo ushirikiano wa kimataifa katika uandishi wa machapisho kama vile kamusi na vitabu vya sarufi. Aidha, iliamuriwa kuwa iundwe kamati ambayo ingeshughulikia uandishi wa vitabu na tafsiri ya vitabu kwa ajili ya kufundishia katika shule za nchi zote za Afrika Mashariki. Hali kadhalika, iliamuriwa kuwa nchi zote za Afrika Mashariki ziwe na wajumbe katika kamati hiyo. Baada ya mkutano huo, nchi za Afrika Mashariki ziliendelea kuwasiliana, ambapo mwaka 1929 zilifikia uamuzi wa kuanzisha Kamati ya Lugha (Kiswahili) ya Afrika Mashariki (Inter–Territorial Language (Swahili) Committee). Uamuzi huo ulifanyika katika mkutano wa Wakurugenzi wa elimu wa nchi za Afrika Mashariki na Kati uliofanyika Dar es Salaam.

Kamati hii ndiyo iliyobeba dhamana ya kusanifisha na kukuza Kiswahili. Mwanzoni, kamati hii ilikuwa na wajumbe 17 wote walikuwa Wazungu. Kufikia mwaka 1939, kamati ilikuwa na wajumbe wanne Waafrika kutoka kila nchi ya Afrika Mashariki. Pamoja na mambo mengine, wakati wa kuunda kamati ilikubaliwa kwamba makao makuu ya Kamati hii yangekuwa mahali ambapo pamekubaliwa na nchi zote.

Kamati ilipitia katika vipindi muhimu vinne, ambapo majina ya kamati hiyo yalikuwa yakibadilika kama ifuatavyo:

(i) 1930 – 1947 Kamati ilikuwa chini ya himaya ya magavana wa nchi za Afrika Mashariki ikijulikana kwa jina la Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki (Inter-territorial Language (Swahili) Committee).

(ii) 1948 – 1952 Kamati ilikuwa chini ya kamati kuu ya Kiswahili ya Afrika Mashariki ikijulikana kama Kamati ya Kiswahili ya Afrika Mashariki (East African Swahili Committee).

(iii) 1952 – 1962 Kamati ilikuwa chini ya Chuo Kikuu cha Makerere ikijulikana kwa jina la Chuo cha Uchunguzi wa Lugha ya Kiswahili.

(iv) 1962 na kuendelea kamati ilikuwa chini ya Chuo Kikuu Kishiriki cha Dar es Salaam (baadaye Chuo Kikuu cha Dar es Salaam) kuanzia mwaka 1970 ikajulikana kama Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI) ambayo



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 49 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

mwaka 2009 TUKI iliungana na iliyokuwa Idara ya Kiswahili na kuunda Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI).

**Kazi za kamati**

Kamati ya lugha ya Kiswahili ya Afrika Mashariki iliundwa na kukabidhiwa majukumu yafuatayo:

(i) Kusanifu mtindo wa maandishi ili uwe wa aina moja katika nchi zote;

(ii) Kuhakikisha kuwa kuna aina moja ya msamiati na sarufi;

(iii) Kutoa ushauri kwa waandishi wanaotaka kuandika vitabu;

(iv) Kuwatia moyo waandishi na kuwasaidia wanapoandika;

(v) Kuwashauri waandishi chipukizi katika uandishi wa makala wanazoziandika.

(vi) Kuandaa na kutoa orodha ya vitabu vya kiada na ziada shuleni;

(vii) Kuweka mpango wa kutafsiri vitabu katika lugha ya Kiswahili kwa ajili ya kutumika shuleni au kuviandika upya kwa Kiswahili sanifu;

(viii) Kusanifu maandishi ya vitabu kabla ya kuchapishwa;

(ix) Kusahihisha na kuboresha vitabu vilivyoshughulikiwa na kamati;

(x) Kuwapa waandishi wa vitabu taarifa kuhusu mitindo ya ufundishaji iliyokuwa inatumiwa na nchi zote nne;

(xi) Kuwa tayari kuibua na kujibu hoja zote zinazohusiana na lugha ya Kiswahili na maandishi yake;

(xii) Kufanya jambo lolote ambalo lingesaidia kuyatimiza madhumuni yaliyoainishwa na kamati; na

(xiii) Kuwa na mhuri wa ithibati kwa ajili ya kuidhinisha vitabu.

**Sababu za Kiunguja kuteuliwa kuwa msingi wa Kiswahili sanifu**

Tume ya Elimu ya Phelps-Stokes ilitoa mapendekezo kuwa kulikuwa na haja ya kuwa na lugha moja sanifu inayofahamika kwa wengi, na itakayotumika katika mawasiliano katika nchi nne ambazo ni Zanzibar, Tanganyika, Uganda, na Kenya. Ilikubaliwa kuwa Kiswahili ndicho kingefaa kuwa chombo cha mawasiliano kwa nchi hizo nne chini ya udhibiti wa dola ya Waingereza. Uteuzi wa lahaja mojawapo kati ya lahaja nyingi zilizokuwa zinapatikana Afrika Mashariki ulifuata hatua kadhaa. Kwanza ziliteuliwa lahaja tatu ambazo zilikuwa katika nafasi ya kuteuliwa kuwa msingi wa Kiswahili Sanifu. Lahaja hizo ni Kiunguja, Kimvita (ilichanganywa na Kijomvu na Kingare), na Kiamu. Lahaja ya Kiunguja ilipata hadhi ya kuwa msingi wa kusanifu Kiswahili tofauti na lahaja nyingine.


PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 50 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


Mapendekezo kadhaa yaliwekwa kwenye kikao cha Kamati ya Lugha ya Kiswahili mwaka 1930 chini ya Mkurugenzi wa Elimu wa Kenya ili kukiteua Kiunguja na kukifanya kuwa msingi wa Kiswahili sanifu. Mapendekezo hayo yalikuwa kama ifuatavyo:

(i) Kuanzia mwaka 1932 Kiunguja kingetumika katika shughuli zote za kielimu.
(ii) Pamoja na marekebisho yaliyofanyika, lahaja ya Kiunguja ikubalike kuwa ni lugha sanifu.
(iii) Maneno ya Kibantu, Kiarabu na lugha nyingine yasipuuzwe bali yatumike kila inapotakiwa.
(iv) Kitabu cha Steere cha *A Handbook of the Swahili Language, as Spoken at Zanzibar* (1870), pamoja na sehemu ya sarufi na kamusi ya Madan vikubalike kuwa sanifu.

Hata hivyo, kulikuwa na sababu kadhaa ambazo zilisababisha kuteuliwa kwa Kiunguja kuwa msingi wa Kiswahili Sanifu. Miongoni mwa sababu hizo ni kuwa:

(i) Kiunguja kilikwishaenea sehemu kubwa na kueleweka vizuri katika nchi za Zanzibar, Tanganyika, Uganda na Kenya hadi Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (JKK), kandokando ya Ziwa Tanganyika, Umanyema, Kivu, Katanga na Bujumbura (Burundi).
(ii) Lahaja ya Kiunguja ilikwishatumika katika taaluma na dini hasa Tanganyika na sehemu nyingine katika kipindi cha Wajerumani ambapo ilienezwa na wahubiri wa dini.
(iii) Kiunguja kilikuwa na machapisho mengi. Hivyo, kikapata hadhi ya kuwa msingi wa usanifishaji wa lugha ya Kiswahili.
(iv) Aidha, ilidaiwa kuwa Kiunguja kilikuwa chepesi zaidi kimatamshi.
(v) Kiunguja kilikuwa na utajiri wa msamiati ambao ulikifanya kiweze kukidhi haja ya watumiaji katika mawasiliano kikilinganishwa na lahaja nyingine.

**Hatua za usanifishaji wa Kiswahili**

Usanifishaji wa Kiswahili ulipitia hatua kadhaa kama ifuatavyo:

(i) **Uteuzi wa lahaja ya kusanifisha**

Hatua ya kwanza ilikuwa ni kuteua lahaja. Uteuzi wa lahaja ulifanyika mwaka 1928 huko Mombasa. Lahaja ya Kiunguja iliteuliwa kuwa lahaja ya usanifishaji na wajumbe kutoka nchi zote za Afrika Mashariki. Lahaja hii iliteuliwa miongoni mwa lahaja tatu zilizopambanishwa. Lahaja nyingine mbili ni Kiamu na Kimvita.


PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(ii) **Kuunda kamati ya usanifishaji**

Kamati ya usanifishaji iliundwa mnamo Januari 1, 1930. Kamati hiyo iliitwa *The Inter-territorial Language (Swahili) Committee* ikiwa na lengo la kusanifisha na kuendeleza lugha ya Kiswahili katika maeneo yote ya Afrika Mashariki yaliyokuwa chini ya utawala wa Mwingereza. Makao yake makuu yalikuwa Dar es Salaam na Katibu wake wa kwanza ni Fredrick Johnson. Hata hivyo, makao makuu yalikuwa yakihamahama kulingana na uamuzi wa kamati.

(iii) **Kukubaliana kuhusu mfumo wa kisarufi utakaotumika**

Makubaliano kuhusu mfumo wa kisarufi yalijumuisha othografia, mfumo wa matamshi ya lugha, alama za kialfabeti, na msamiati. Othografia iliyokubalika ni kutumia fonimu zinazotumika katika Kiswahili cha sasa. Katika kipengele cha msamiati, kamati ilikubaliana kuhusu msamiati mwafaka wa kutumika miongoni mwa maneno kadhaa yaliyokuwa yanatumika kuwasilisha dhana moja. Miongoni mwa istilahi zilizoshughulikiwa ni *konsonanti* na *irabu* ambazo ziliafikiwa kutumika badala ya *herufi* ili *herufi* ibaki kuwa dhana inayowakilisha hati yoyote; *shule* badala *schule* (ya Kijerumani); *herufi* badala ya *harufu* ili neno *harufu* libaki kumaanisha dhana ya mnuko au mnukio wa kitu. Msamiati mwingine uliokubaliwa na kamati ya usanifishaji ni *kimo* na *kina*. Awali, neno *kina* lilikuwa linatumika kumaanisha urefu kwenda juu na chini. Baada ya usanifishaji, neno *kina* linamaanisha urefu kwenda chini na *kimo* linamaanisha urefu kwenda juu. Vilevile, ilikubalika kwamba *senti hamsini* itumike badala ya *nusu shilingi* (deka) na *senti tano* badala ya *nusu peni* (pente). *Deka* na *pente* ni majina ya pesa kwa Kiyunani.

Orodha ya msamiati ilipelekwa kwa mhariri wa kamati pamoja na kuchapishwa katika jarida la *ILC Bulletin* ili kuwapa wahariri na raia nafasi ya kujadili kabla ya kuchapishwa kama msamiati sanifu. Kamati pia ilijadili na kukubali kuchukua maneno ya Kibantu kama vile *shamba* na *kizibau* na kuyasanifisha. Katika jarida hilo, Fredrick Johnson alijadili chanzo cha baadhi ya maneno na Kasisi Hellier alitoa orodha ya msamiati wa vipimo na mzani. Juzuu za majarida hayo zilikuwa zinatolewa kila mwaka. Hali hii iliwezesha Kiswahili sanifu kukua na kuenea ndani na nje ya Afrika Mashariki.

(iv) **Kutoa machapisho**

Sambamba na kusanifisha lugha, kamati ilichapisha machapisho mbalimbali kama vile kamusi, majarida, na vitabu vya sarufi ya Kiswahili sanifu. Mnamo



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 52 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



mwaka 1930 - 1942, kamati ilishughulika na Kamusi ya Madan (Kiswahili – Kiingereza). Vilevile, kamati iliboresha kamusi iliyotayarishwa na Fredrick Johnson. Kazi hiyo ilianza mwaka 1933 na kumalizika mwaka 1939.

(v) **Kuandaa wataalamu wa usanifishaji**

Ikumbukwe kwamba kabla ya uhuru wataalamu wa kigeni ndio walioongoza mchakato wa usanifishaji wa Kiswahili. Baada ya uhuru shughuli za usanifishaji zilifanywa na wataalamu wa Kiafrika ambao, wengi wao walikuwa wanafanya kazi TUKI (ambayo kwa sasa inajulikana kwa jina la TATAKI), Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), na vyombo vingine vya ukuzaji wa lugha. Usanifishaji unaendelea mpaka sasa ambapo unafanywa na vyombo vyenye mamlaka ya kuratibu na kusimamia shughuli za ukuzaji na usanifishaji wa Kiswahili katika nchi inayohusika. Kamusi za Kiswahili zimeendelea kutungwa katika kipindi chote baada ya uhuru. Mathalani, mwaka 2015 BAKITA lilichapisha Kamusi Kuu ya Kiswahili (KKK).

Vilevile, BAKITA, kupitia Kamati ya Kusanifu Lugha (KAKULU) ambayo hujumuisha wajumbe wa bara na visiwani, liliandaa istilahi za masomo mbalimbali. Istilahi hizo zilisanifishwa kwa ajili ya kutayarisha kamusi mbalimbali za kitaaluma. Aidha, TUKI nao wamekuwa wakichapisha kamusi mbalimbali kama vile *Kamusi ya Fizikia, Kemia na Biolojia*, *Kamusi ya Lugha na Isimu*, *Kamusi ya Historia*, *Kamusi ya Tiba*, *Kamusi ya Sheria*, na *Kamusi ya Biashara na Uchumi.*

BAKITA na TUKI wanaunda istilahi za Kiswahili kwa njia ya kutafuta visawe vya maneno ya Kiingereza katika Kiswahili, lahaja za Kiswahili, lugha za Kibantu, na zile zisizo za Kibantu. Mifano ifuatayo inaonesha baadhi ya istilahi hizo:



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 53 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

| **Kiingereza** | **Kiswahili** |
|---|---|
| crop | zao |
| policy | sera |
| skills | stadi |
| industry | tasnia |

| **Kiingereza** | **Lahaja** |
|---|---|
| Hob | Kiangata (Kisiu na Kiamu) |
| Breakfast dish | Kisabeho (Kipemba) |

| **Kiingereza** | **Kibantu** |
|---|---|
| Bone marrow | Uloto (Kizaramo) |
| Jetstream | Upepo nyiri (Kipare) |
| Virgin land | Lweya (Kihaya) |

| **Kiingereza** | **Lugha zisizokuwa za Kibantu** |
|---|---|
| Diodenum | Mbuti (Kimasai) |
| Carving knife | Ngalemu (Kimasai) |

**Changamoto zilizojitokeza wakati wa usanifishaji**

Mchakato wa usanifishaji wa lugha ya Kiswahili ulikumbwa na changamoto zifuatazo:

(i) Tofauti kati ya maandishi na matamshi

Miongoni mwa changamoto hizo ni kuwapo kwa maneno ambayo yanatamkwa tofauti na jinsi yanavyoandikwa. Wasanifishaji walikiuka utaratibu wa maandishi ya lugha ya Kiswahili ambapo neno hutamkwa jinsi linavyoandikwa. Baadhi ya maneno ya Kiswahili yaliyosanifishwa huwakilishwa kimaandishi na herufi pungufu kuliko ilivyo katika matamshi. Angalia mfano ufuatao:



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

For Online Use Only

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



**Jedwali 2.12** Tofauti kati ya maandishi na matamshi

| Maandishi | Matamshi |
|---|---|
| Nge | nnge |
| Mbwa | mmbwa |
| Mbu | mmbu |
| Nje | nnje |
| Nchi | nnchi |

Katika mifano hiyo matamshi ya [nn] lazima yafungamane na matamshi ya konsonanti inayofuata. [n] ya kwanza lazima iwe na usilabi.

Mifano hapo juu inaonesha kwamba matamshi halisi ya kila neno yanahitaji sauti zaidi ya zile zilizoko kwenye maandishi.

(ii) Uhaba wa vitabu
Kamati ilitoa vitabu vichache, ambavyo havikutosheleza mahitaji ya watumiaji wa lugha ya Kiswahili. Vilevile, vitabu vilivyotafsiriwa vilikuwa na makosa mengi mno ya semi na miundo ya Kiingereza. Kamati ilipata shida ya kupata vitabu vya Kiswahili ambavyo vingewasaidia katika kazi yao ya usanifishaji.

(iii) Uhaba wa fedha
Kuzuka kwa Vita vya Pili vya Dunia kuliathiri shughuli za usanifishaji hususani kwa upande wa fedha. Fedha nyingi zilitumika kugharimia vita. Hivyo, shughuli za kielimu zilififia. Baadhi ya mikutano ya kamati haikuweza kuitishwa kama ilivyokuwa imepangwa. Mathalani, wajumbe wa Kiafrika walioteuliwa mwaka 1939 hawakuweza kuhudhuria mikutano mpaka mikutano ilipoanza kuitishwa tena mwaka 1946. Pia, wakati wa vita kulikuwa na upungufu wa vitendea kazi, hususani karatasi. Hivyo, iliwalazimu kutuma miswada Uingereza ili ikachapishwe. Kitendo cha kutuma miswada Uingereza kilisababisha vitabu na machapisho mengine yasipatikane kwa muda mwafaka.

(iv) Upungufu wa istilahi
Kulikuwa na upungufu mkubwa wa istilahi katika nyanja za elimu, hasa upande wa sayansi na teknolojia. Vifaa vingi vya kisayansi na kiteknolojia vilivumbuliwa katika nchi zilizoendelea. Kwa hiyo, hata vilipoingizwa



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 55 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

katika nchi za Afrika Mashariki viliingia na majina yake kwa lugha za kigeni. Kwa hiyo, ilikuwa vigumu kupata majina yake katika Kiswahili kwa haraka baada ya kuingia.

(v) Kiswahili kutopewa kipaumbele
Baadhi ya nchi za Afrika Mashariki hazikujali Kiswahili kama ilivyo kuwa kwa lugha nyingine. Mathalani, Kenya lugha za jamii ndizo zilipewa hadhi hususani mara baada ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia. Pia, Kiingereza kiliendelea kupewa hadhi ya juu kuliko Kiswahili kwa sababu kilikuwa kinatumika katika shughuli za kiuchumi, hasa katika utalii.

**Changamoto zinazokikabili Kiswahili kwa sasa**

Usanifishaji wa Kiswahili unakabiliwa na changamoto zifuatazo:

(i) Kutokupewa hadhi ya kutumika katika baadhi ya maeneo.
Pamoja na kwamba Kiswahili ni lugha ya taifa, lugha rasmi na lugha ya kimataifa bado hakijapewa hadhi ya kutumika katika nyanja mbalimbali. Kwa mfano, nchini Tanzania, Kiswahili kimekuwa kikitumika kama lugha ya kufundishia shule za msingi za serikali. Shule binafsi na baadhi ya shule za serikali Tanzania bara zimeendelea kutumia Kiingereza kama lugha ya kufundishia isipokuwa somo la Kiswahili. Kwa upande wa Zanzibar shule zote za serikali zinatumia Kiingereza kufundishia masomo ya sayansi, hesabu, TEHAMA, na jiografia kuanzia darasa la tano na kuendelea. Matumizi ya Kiingereza katika elimu yanadunisha Kiswahili. Kwa mantiki hii, msamiati wa Kiswahili hauongezeki kwa kasi kwa sababu ya matumizi yake kujikita katika ngazi za chini za elimu.

(ii) Matumizi ya istilahi za kigeni
Tatizo la istilahi limeendelea kuwa changamoto katika usanifishaji wa Kiswahili kwa sababu ya maendeleo ya sayansi na teknolojia yanayotokea katika jamii. Vitu vipya vinapotokea katika jamii hukosa istilahi za Kiswahili za kuvieleza au kuvitaja. Uundaji wa istilahi za Kiswahili za vitu hivyo hufanyika kwa kuchelewa sana kiasi cha kusababisha istilahi za kigeni kutamalaki katika mazungumzo ya Kiswahili. Istilahi za Kiswahili zinapoundwa, hukosa watumiaji kutokana na kuzoea kutumia istilahi za kigeni. Hata watumiaji wakizikubali istilahi mpya za Kiswahili, hujikuta wakitumia istilahi nyingi kurejelea dhana moja. Chunguza mifano ya istilahi zinazorejelea dhana moja:



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 56 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



(i) Smartphone - simatifoni, simujanja au simumtelezo
(ii) Computer – kompyuta, tarakilishi
(iii) Television – televisheni, runinga
(iv) Decoder – dikoda, king'amuzi au kisimbuzi

(iii) Ufinyu wa bajeti

Vyombo vilivyoundwa kwa ajili ya kuratibu shughuli za ukuzaji na usanifishaji wa Kiswahili vimekuwa vikikabiliwa na bajeti isiyokidhi mahitaji kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kwa hiyo, ni dhahiri kuwa usanifishaji wa Kiswahili hufanyika kwa kusuasua sana. Vilevile, kutokana na ukosefu wa pesa vyombo vingi vya kukuza na kueneza Kiswahili vimeshindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Mfano wa vyombo hivyo ni Chama cha Usanifu wa Kiswahili na Ushairi Tanzania (UKUTA) na Chama cha Kiswahili Afrika (CHAKA).

(iv) Usambazaji wa taarifa na machapisho

Tatizo la usambazaji wa taarifa na machapisho yanayohusu matumizi ya Kiswahili sanifu linaukumba usanifishaji wa Kiswahili. Watumiaji wengi wa Kiswahili hawapati taarifa za usanifishaji unaofanyika. Hali kadhalika, machapisho yanayotolewa na vyombo vya usanifishaji kama vile TATAKI, BAKITA, na BAKIZA huwafikia watu wachache hasa ambao wako katika taasisi za kitaaluma. Kwa hiyo, machapisho mengi yanayohusu istilahi zilizosanifishwa hutumika katika taasisi za elimu ya juu tu. Shule za Msingi na Sekondari, ambazo ndizo nyingi, hazina machapisho hayo wala taarifa ya kuwepo kwa machapisho hayo. Pamoja na kuwapo kwa vyombo vingi vya habari bado vipindi vinavyohusiana na lugha ya Kiswahili ni vichache. Kwa mfano, BAKITA imekuwa ikiendesha vipindi vilivyorushwa katika redio na televisheni. Majina ya vipindi hivyo ni *Kumepambazuka Kiswahili* (Redio One Stereo), *Kiswahili Lugha ya Taifa* (TBC - Taifa) na *Ulimwengu wa Kiswahili* (TBC1). Aidha, TBC1 huandaa na kurusha kipindi kinachohusu Kiswahili kinachoitwa *Lulu za Kiswahili.*

**Kudumaa kwa lahaja nyingine za Kiswahili**

Lahaja yoyote inapotumika kama chanzo cha kusanifu lugha huzifanya lahaja nyingine kutotambulika vizuri au kutojulikana kabisa. Kiunguja kilipata hadhi ya juu na kujulikana zaidi bara na pwani kwa sababu kilitumika katika shughuli nyingi za mawasiliano kama vile katika dini, utawala, na biashara. Hata hivyo, baada ya Kiunguja kusanifishwa, kilipatikana Kiswahili sanifu ambacho ndicho



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

sasa kimeenea mahali pengi na kuhatarisha lahaja mbalimbali za Kiswahili. Kwa hiyo, baada ya Kiswahili sanifu kushamiri kwa kiwango kikubwa lahaja nyingine zilibaki katika maeneo ya wazungumzaji wake wazawa.

Miongoni mwa sababu zilizosababisha lahaja nyingine kudumaa ilhali Kiswahili sanifu kikishamiri ni :

(i) Kutumika katika machapisho mbalimbali ya kielimu, kidini, kisiasa na kijamii;

(ii) Kutumika katika shughuli mbalimbali za kiserikali na za umma;

(iii) Kufundishwa shuleni kama somo;

(iv) Kuwa na machapisho mengi yanayohusu nyanja mbalimbali kuhusu lugha hiyo zikiwamo kamusi, vitabu vya hadithi, vitabu vya nyimbo, vitabu vya sarufi, na kadhalika;

(v) Kutumika katika mikutano na makongamano ya kimataifa kama vile mikutano ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Umoja wa Afrika;

(vi) Kufundishwa katika nchi mbalimbali duniani kama lugha ya kigeni; na

(vii) Kukua kwa matumizi yake katika sayansi, teknolojia na TEHAMA.

## Zoezi la 2.3

1. Fafanua namna mchakato wa usanifishaji wa lugha ya Kiswahili ulivyokuwa wakati wa ukoloni.
2. Usanifishaji wa Kiswahili haukuishia kipindi cha ukoloni tu bali unaendelea mpaka sasa. Thibitisha kauli hii kwa kutumia hoja na mifano.

## Tamrini

1. Kwa nini Kiswahili kinadhaniwa kuwa ni Kiarabu?
2. Huku ukijikita katika kamusi za Kiswahili, eleza mchango wa kimsamiati wa lugha za kigeni (tofauti na Kiarabu) katika Kiswahili.
3. Eleza sababu za kusanifisha Kiswahili.
4. Jadili madai kuwa chimbuko la Kiswahili ni Kongo.
5. Thibitisha ubantu wa Kiswahili kwa kutumia kigezo cha kihistoria.

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 58 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



# Sura ya Tatu
# Kukua na kuenea kwa Kiswahili

## Utangulizi

Sura hii inahusu kukua na kuenea kwa Kiswahili. Katika sura hii utajifunza kukua na kuenea kwa Kiswahili Afrika Mashariki kabla na baada ya uhuru. Aidha, utajifunza kuhusu kuenea kwa Kiswahili duniani. Lengo la sura hii ni kukuwezesha kupata maarifa na ujuzi ambao utakusaidia kufafanua na kueleza jinsi lugha ya Kiswahili ilivyokua na kuenea katika vipindi mbalimbali.

**Kukua na kuenea kwa Kiswahili Afrika Mashariki kabla ya uhuru**

Kabla ya kuanza kuelezea kukua na kuenea kwa Kiswahili Afrika Mashariki, inafaa dhana hizi zifafanuliwe. Kukua kwa lugha ni kuongezeka kwa msamiati na miundo ya lugha fulani. Aidha, kuenea kwa lugha ni kuongezeka kwa matumizi ya lugha katika maeneo ambayo hapo awali yalikuwa hayatumii lugha hiyo.

**Kukua na kuenea kwa Kiswahili Tanganyika na Zanzibar kabla ya uhuru**

Kuna sababu mbalimbali zilizochangia kukua na kuenea kwa Kiswahili maeneo ya Tanganyika na Zanzibar kabla ya uhuru. Miongoni mwa sababu hizo ni harakati za kueneza dini, biashara, utawala, harakati za kisiasa, na vyombo vya habari. Sababu hizo zimebainishwa katika vipindi vitatu vya utawala kama zinavyofafanuliwa katika sehemu zinazofuata:

**Utawala wa Waarabu**

Katika utawala wa Waarabu, Sultani wa Unguja alitawala visiwa vya Pemba na Unguja. Baadaye alipewa eneo la maili kumi kutoka ufukwe wa bahari ya Hindi, Tanganyika, na Kenya. Matumizi ya Kiswahili yalihimizwa katika maeneo yote ya utawala wa Sultani huyo. Kwa mfano, katika utawala huo Sultani wa Zanzibar aliandaa mfumo wa utawala katika baadhi ya sehemu za Tanganyika kwa kuwatumia maakida na maliwali. Watu hao walikuwa wametoka pwani na



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

For Online Use Only

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 59 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

walikuwa wanakijua Kiswahili vema. Maakida hao walipelekwa hasa sehemu za Kilwa, Bagamoyo, Tanga, Pangani, Kigoma Ujiji, na Mpwapwa. Katika maeneo hayo walitumia lugha ya Kiswahili; jambo ambalo lilichangia katika kuikuza na kuieneza lugha hii.

***1 Harakati za kueneza dini***

Harakati za kueneza dini katika maeneo ya Tanganyika na Zanzibar kabla ya uhuru ziliendeshwa na maimamu wa Kiislamu na Wamisionari wa Kikristo.

(i) *Dini ya Kiislamu*

Dini ya Kiislamu ilienezwa na Waarabu ambao walifika Pwani ya Afrika Mashariki yapata karne ya nane na kuwakuta wenyeji wakizungumza lugha zao za Kibantu kikiwemo Kiswahili. Waarabu walilazimika kujifunza lugha ya Kiswahili, ili waweze kuhubiri na kutafsiri Kurani katika lugha iliyoeleweka kwa watu wengi. Waarabu walisafiri kutoka pwani hadi bara kueneza dini kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Kwa njia hiyo, walisaidia kueneza lugha ya Kiswahili. Aidha, mashehe na maulamaa walianza kuandika Kiswahili kwa kutumia alfabeti za Kiarabu. Pia, katika kueneza dini waliwafundisha waumini kasida kwa lugha ya Kiswahili.

(ii) *Dini ya Kikristo*

Wamisionari wa Kikristo walifika Afrika Mashariki kabla ya utawala wa Wajerumani. Wamisionari hao walikuja chini ya mashirika mbalimbali ya dini kwa lengo la kueneza dini ya Kikristo. Miongoni mwa mashirika hayo ni Shirika la Roho Mtakatifu, White Fathers kutoka Ufaransa, University Mission to Central Africa (UMCA), na Church Missionary Society (CMS) kutoka Uingereza. Katika harakati za kueneza dini ya Kikristo, mashirika hayo yalisaidia kueneza lugha ya Kiswahili. Mbali na mahubiri na kutafsiri maandiko yaliyohusu dini ya Kikristo kama vile Biblia na vitabu vya nyimbo, mashirika haya yaliandika machapisho mengine kuhusu lugha ya Kiswahili kwa Kiswahili. Mwaka 1905, Misheni ya Magila ilitoa kitabu cha Habari za Wakilindi kilichoelezea historia ya Wasambaa. Shirika la UMCA kutoka Uingereza lilijishughulisha na uandishi wa machapisho mbalimbali kwa kutumia lahaja ya Kiunguja. Mwaka 1870, shirika la S.P.C.K. lilichapisha toleo la kwanza la sarufi ya Kiswahili cha Kiunguja lililoitwa *A Handbook*



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

For Online Use Only

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



*of the Swahili Language as Spoken in Zanzibar* iliyoandikwa na Askofu Edward Steere. Shirika hili liliendelea kuchapisha vitabu mbalimbali kama vile *Kamusi za Kiswahili – Kiingereza* na *Kiingereza – Kiswahili*. Kamusi hizo zilianza kuandikwa na Askofu Edward Steere na kukamilishwa na A. Madan na baadaye kurudiwa na F. Johnson. Kamusi zilizoandikwa na F. Johnson zilijulikana kama *A Standard English – Swahili Dictionary* na *Swahili –English Dictionary*.

Aidha, shirika la UMCA lilichapisha magazeti mbalimbali. Miongoni mwa magazeti hayo ni *Habari za Mwezi* (1888) na *Pwani na Bara* (1910). Magazeti haya yalichapishwa na Waluteri. Magazeti ya Wakatoliki yalikuwa ni *Barazani* na *Rafiki Yangu* (1910). Aidha, Wamisionari hawa walikuwa na vituo katika maeneo mbalimbali kama vile Bagamoyo (1868), Magila (1864), Mpwapwa (1876), Ujiji (1877), Masasi (1876), Zanzibar (1860), na Ziwa Nyasa (1881). Katika mchakato wa kutimiza malengo yao, walijikuta wakieneza na kukuza lugha ya Kiswahili katika sehemu hizo. Kwa ujumla, Wamisionari walijikuta wakieneza lugha ya Kiswahili kwa sababu waliihitaji sana katika shughuli zao za kidini.

### *2 B iashara*

Waarabu walifanya biashara ya watumwa Pwani ya Afrika Mashariki. Misafara ya biashara ya watumwa iliyokuwa ikiendeshwa na Waarabu ilikuwa ikitoka pwani kwenda bara na bara kwenda pwani. Mji wa Unguja ulikuwa ni soko kuu la watumwa. Mbali na biashara ya watumwa, bidhaa nyingine kutoka bara zilikuwa pembe za ndovu na vifaru, meno ya viboko, nta ya nyuki, gundi ya sandarusi, ngozi za chui, malele za kutengenezea rangi nyekundu, na magamba ya kobe ya kutengenezea chanuo. Baadhi ya bidhaa zilizokuwa zinapelekwa bara ni nguo, shanga, nyaya za chuma na za shaba za kutengenezea vito vya thamani na silaha.

Miji mingine iliyokuwa maarufu katika kufanya biashara hizo ni Bagamoyo, Kilwa, Tabora, na Kigoma, hasa sehemu za Ujiji. Katika harakati hizo za biashara, Kiswahili kilitumika. Hali hii ilichochea kukua na kuenea kwa lugha hii katika maeneo ya pwani na bara.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 61 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Utawala wa Wajerumani

Tanganyika ilitangazwa kuwa koloni la Kijerumani mnamo mwaka 1885. Wajerumani walipoingia Tanganyika walikuta tayari kuna misingi ya lugha ya Kiswahili iliyojengwa na Waarabu na Wamisionari. Lengo la Wajerumani lilikuwa ni kutumia lugha ya Kijerumani ili kujenga dola imara la Kijerumani katika misingi yote ya kisiasa, kiuchumi, na kiutamaduni. Hata hivyo, lengo lao halikutimia kwa sababu walihofia kwamba wenyeji wasingeweza kujifunza Kijerumani na kukitumia vizuri katika mawasiliano. Hivyo, walilazimika kusisitiza matumizi ya Kiswahili. Kwa msingi huo, ujuzi wa Kiswahili ulikuwa ni sifa muhimu ili mtu aajiriwe kama akida, tarishi, karani, au afisa yeyote wa ngazi za chini. Sharti hili liliwalazimu watu kujifunza Kiswahili. Kwa njia hiyo, Kiswahili kilikua na kuenea kwa haraka. Mambo mengine yaliyosaidia kukua na kuenea kwa Kiswahili ni elimu na shughuli za kilimo.

### *1 Elimu*

Wajerumani walianzisha shule ya kwanza nchini Tanganyika mnamo miaka ya 1890 huko Tanga. Shule zingine zilianzishwa huko Tabora, Ujiji, Kilimatinde, Kasanga, Mwanza, Tukuyu, na Moshi. Vilevile, walijenga vyuo vya ualimu huko Tabora na Bukoba. Pia, walianzisha shule kwa ajili ya wafanyakazi wa ngazi za chini. Hadi kufikia miaka ya 1890, Wajerumani walikuwa na shule zipatazo 83 za serikali (Iliffe, 1979). Lugha ya Kiswahili ndiyo ilikuwa lugha ya mawasiliano na ya kufundishia katika shule hizo. Walisisitiza lugha ya Kiswahili kutumika shuleni kutokana na umuhimu wake. Kijerumani kilifundishwa kama somo. Hivyo, elimu ilisaidia kuenea kwa lugha ya Kiswahili.

### *2 Shughuli za kilimo*

Shughuli za kilimo, hususani kilimo cha mkonge, zilihusisha kuchukua vibarua waliojulikana kama *manamba* kutoka katika baadhi ya maeneo ya Tanganyika. Maeneo hayo ni kama vile Kigoma, Tabora, na Singida. Mawasiliano baina ya manamba, na kati ya wanyapara na manamba yalifanyika kwa Kiswahili. Aidha, manamba waliporudi kwao waliwafundisha ndugu zao Kiswahili. Kwa njia hiyo, Kiswahili kilikua na kuenea.

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 62 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


**Utawala wa Waingereza**

Utawala wa Waingereza ulianza mwaka 1919 mara tu baada ya Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia. Serikali ya Waingereza ilisisitiza matumizi ya Kiswahili, hususani kwa wafanyakazi wa ngazi za chini kama vile makarani, matarishi, machifu na wahudumu wengine wa ofisi. Wafanyakazi hao walilazimishwa kufahamu Kiswahili ili waweze kukitumia katika shughuli za utawala.Wakati wa utawala huo, mambo mengine yaliyosaidia kukua na kuenea kwa Kiswahili ni elimu, harakati za kisiasa, na shughuli za kijeshi.

***1 E limu***

Sera za Waingereza hazikuruhusu Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia katika shule za viwango vya juu tofauti na shule za msingi, hususani darasa la I–IV. Kiswahili kilichukuliwa kama lugha duni kikilinganishwa na Kiingereza. Hata hivyo, Waingereza walifanya kazi kubwa katika ukuzaji wa Kiswahili kupitia elimu. Katika utawala wao waliona ni vyema kuwa na lugha moja ya kufundishia katika shule za msingi katika makoloni yao ya Afrika Mashariki. Lugha iliyoteuliwa ni Kiswahili ambayo ilitokana na kusanifishwa kwa lahaja ya Kiunguja. Matumizi ya lugha ya Kiswahili katika shule za msingi nchini Tanganyika yalisaidia kukuza na kueneza lugha hiyo.

***2. Mchango wa jeshi la King's African Rifles (KAR)***

Jeshi hili liliundwa na Waingereza mara baada ya Vita Vikuu vya Kwanza vya Dunia (1918). Waingereza walikabidhiwa nchi ya Tanganyika na Baraza la Udhamini (The League of Nations) lililokuwa chini ya Umoja wa Mataifa. Waingereza walipanua mfumo wa KAR na kuwa na vikosi sita ambapo vikosi viwili vilikuwa Kenya, vitatu vilikuwa Tanganyika na kimoja kilikuwa Uganda. Jeshi liliundwa na vikosi vya askari wa miguu, wataalamu wa medani, mawasiliano, mizinga, na vikosi vya huduma. Jeshi hili liliundwa na watu kutoka makabila mbalimbali na lugha iliyokuwa ikitumika jeshini ilikuwa Kiswahili. Askari hawa walisaidia kueneza Kiswahili ndani na nje ya nchi hizo kwa sababu kila walipokwenda walikuwa wakizungumza Kiswahili. Jeshi la vikosi vya usalama kama vile KAR na jeshi la polisi vilitumia Kiswahili katika mawasiliano yao. Maafisa wa jeshi na askari wote walitumia Kiswahili katika masuala yao ya kijeshi. Kwa kufanya hivyo, Kiswahili kilikua na kuenea zaidi.


PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 63 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

***3 Harakati za kisiasa***

Baada ya Vita Vikuu vya Pili vya Dunia vya 1939 – 1945, mataifa mengi ya Afrika yalianzisha harakati za kudai uhuru. Katika harakati za kudai uhuru nchini Tanganyika, vyama vya siasa kama vile TAA baadaye TANU pamoja na Umoja wa Vijana wa TANU (TANU Youth League - TYL) viliundwa. Lugha ya Kiswahili ilikuwa ni nguzo na chombo muhimu sana. Kiswahili kilitumika kuwaunganisha Watanganyika ambao walikuwa na lugha tofautitofauti kushiriki katika harakati za kudai uhuru kutoka kwa wakoloni. Viongozi wa TANU wakiongozwa na Baba wa taifa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere walitumia Kiswahili katika mikutano yao ya kuhamasisha watu kujiunga na TANU. Lugha ya Kiswahili iliweza kuunganisha mawazo, fikira, na mambo mbalimbali yaliyokuwa yakifanywa na chama cha TANU. Lugha ya Kiswahili ndiyo ilikuwa alama ya umoja, uzalendo, utanganyika, na uhuru, hata wito wa chama ukawa UHURU NA UMOJA.

***4 Shirika la uchapishaji na usambazaji wa vitabu***

Shirika hili la Uchapishaji na usambazaji wa vitabu East African Literature Bureau (EALB), lilikuwa na jukumu la kuvichapa vitabu vyote vilivyokuwa vimeidhinishwa na kamati ya lugha ya Afrika Mashariki (East African Language (Kiswahili) Committee).

**Changamoto za kukua na kuenea kwa Kiswahili Tanganyika**

Pamoja na ukweli kwamba Kiswahili kilikua na kuenea nchini Tanganyika, zipo changamoto zilizoathiri matumizi ya Kiswahili. Wamisionari walitumia lugha za kikabila katika kueneza dini, hasa katika maeneo ya bara. Vitabu vya nyimbo, Liturujia na Biblia, hasa Agano Jipya, vilitafsiriwa katika lugha za kikabila. Karibu makabila yote ya Tanganyika yalikuwa yanaendesha ibada katika lugha zao za makabila. Hali hii ilidumaza matumizi ya Kiswahili katika maeneo hayo.

Pia, wamisionari walianzisha vyombo vya habari vilivyokuwa vinatumia lugha za kikabila. Mfano mzuri ni Bukoba ambako kulikuwa na magazeti mawili yaliyokuwa yanamilikiwa na makanisa ya Kikatoliki na Kiluteri. Magazeti hayo ni *Rumuli* na *Ija Webonere*. Magazeti hayo yaliandikwa kwa Kihaya. Magazeti hayo yapo mpaka leo ingawa siku hizi yanaandikwa kwa Kiswahili na Kihaya.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 64 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Vilevile, baadhi ya wananchi hawakupendelea kutumia Kiswahili kwa kuwa walikihusisha na vibaraka wa wakoloni (maakida, wajumbe na maliwali). Walikiona Kiswahili kama lugha ya wadhalimu, wakatili, na watoza kodi. Aidha, watu wengine waliamini kuwa Kiswahili ni lugha ya Waislamu. Kwa hiyo, waliendelea kutumia lugha zao za asili.

Katika utawala wa Waingereza, Kiingereza kilitiliwa mkazo, hususani katika utawala na elimu. Kiswahili kilikuwa ni lugha ya pili hapa nchini, na hakikupewa hadhi yake inayostahili. Ripoti za mashauri yaliyoendeshwa katika mahakama za Waafrika ziliandikwa kwa Kiingereza. Kiingereza ndiyo ilikuwa lugha ya mawasiliano kwa maafisa wa ngazi za juu. Katika elimu, Kiingereza kilitumika kama lugha ya kufundishia katika shule za sekondari; sera ambayo ipo mpaka sasa. Ushindi katika mitihani ya taifa kama vile *Standard X Territorial Examination* ulitegemea ufaulu mzuri wa Kiingereza.

**Kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Kenya kabla ya uhuru**

Kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Kenya kunaweza kutazamwa kwa kuzingatia sababu tatu ambazo ni biashara, dini, na elimu.

***1 B iashara***

Kiswahili kilienea katika eneo la bara ya Kenya kabla ya ujio wa wakoloni. Uenezaji wa Kiswahili wakati huo ulifanywa na wafanyabiashara wa Kikuyu na Waswahili. Wakikuyu na Wakamba walikuwa wakiuza bidhaa zao Mombasa. Bidhaa maarufu zilikuwa ni pembe za ndovu na watumwa. Miji mingine iliyohusika katika biashara ni Takaungu, Malindi na Lamu. Biashara nyingine zilizofanyika Mombasa ni mboga na matunda ambayo yalikuwa yakizalishwa katika maeneo ya Kisauni, Changamwe, Mtongwe, na Likoni. Wafanyabiashara hawa walitumia Kiswahili kama lugha yao ya mawasiliano. Kufanya hivyo, kulisaidia kuenea kwa lugha ya Kiswahili.

***2 D ini***

Ujio wa Wamisionari uliendeleza na kukuza Kiswahili. Kwa mfano, Dkt. J. Krapf na Rebmann walianzisha makazi katika eneo la Raban mwaka 1846. Walijifunza lugha, fasihi, na utamaduni wa Waswahili. Shughuli za uenezaji na ukuzaji wa Kiswahili zilishika kasi baada ya kuanzishwa kwa shirika la



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 65 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Church Missionary Society (CMS) lililoongozwa na Dkt. J.C. Krapf. Shirika hili lilikuwa na makao yake makuu Mombasa. Mwaka 1876, shirika hili liliandika kitabu cha kwanza cha Sarufi ya Kiswahili kwa lahaja ya Kimvita. Kitabu hiki kiliitwa *Outline of the Elements of the Kisuaheli Language with Special Reference to the Kinika Dialect*. Shughuli zote hizi zilisaidia kukuza na kueneza Kiswahili nchini Kenya.

***3 E limu***

Nchini Kenya, Kiswahili kilitumika katika shule za msingi kama lugha ya kufundishia kwa darasa la IV na V katika shule za Waafrika za kipindi hicho. Ingawa tume mbalimbali za elimu, ikiwemo Tume ya Phelps – Stokes, zilipendekeza matumizi ya lugha za jamii katika kutoa elimu, ilikuwa vigumu kupata walimu na machapisho katika lugha hizo. Hivyo, Kiswahili kiliendelea kutumika kama lugha ya kufundishia na ya mawasiliano. Hali hii ilisaidia kukua na kuenea kwa Kiswahili.

Mbali na biashara, dini na elimu, Kiswahili nchini Kenya kilienezwa pia na Jeshi la KAR. Wanajeshi na wafanyakazi wengine waliokuwa chini ya KAR walilazimishwa kufanya mitihani ya Kiswahili. Ili waweze kufaulu mitihani hiyo, walilazimika kujua sarufi ya Kiswahili vizuri. Jitihada za kutaka kufaulu mitihani zilichochea uimarishaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili kwa ufasaha.

Kwa ujumla, Waingereza ndio waliofanya kazi kubwa ya kukuza lugha ya Kiswahili ukilinganisha na Wajerumani. Katika kipindi hicho matumizi ya Kiswahili yalipanuka sana.

**Changamoto za kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Kenya**

Kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Kenya kulikumbwa na changamoto anuwai. Kwanza, kulikuwa na upinzani wa lugha za kikabila na Kiingereza katika elimu. Kwa mfano, Tume ya Elimu ya Afrika Mashariki ya mwaka 1925, kupitia Sera ya Lugha, ilipendekeza kuwa madarasa ya chini yafundishwe kwa lugha za kikabila na baadaye Kiingereza kitumike kama lugha ya kufundishia katika madarasa ya juu. Tume nyingine iliyopendekeza matumizi ya lugha za kikabila zitumike katika kufundishia ni ile iliyoongozwa na Kasisi Mkuu L.J. Beecher,

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



mwaka 1942. Tume hii ilipendekeza lugha za jamii zitumike katika madarasa ya juu. Hali hii, kwa kiasi fulani, ilidumaza lugha ya Kiswahili, hasa katika maeneo ya vijijini.

Pili, kuzuiwa kwa misafara ya biashara iliyokuwa inatoka pwani kwenda bara. Misafara hii ilizuiwa na makabila ya Wamasai na Wakamba. Kwa hiyo, misafara hiyo ilishindwa kupita katika maeneo ya Kenya badala yake ilipita Tanganyika katika maeneo ya Kilimanjaro na Pangani. Pia, kuwapo kwa wanyama wakali katika mbuga ya Tsavo kulisababisha baadhi ya misafara kushindwa kupenya kutoka pwani kwenda bara. Mbali na changamoto za matumizi ya Kiswahili katika elimu na kuzuiliwa kwa misafara, baadhi ya Wakenya hawakukipenda Kiswahili. Hii ni kwa sababu walikihusisha Kiswahili na Uislamu. Kwa hiyo, waliamini kuwa kujifunza Kiswahili ni sawa na kujifunza Uislamu.

**Kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Uganda kabla ya uhuru**

Nchini Uganda, Kiswahili kilianza kukua na kuenea katika karne ya 19. Waarabu ndio walioeneza lugha hiyo kwa kuanzisha shughuli za biashara na kueneza dini ya Kiislamu. Pia, Waarabu walikuwa wakitembelea ikulu ya Kabaka wa Buganda mara kwa mara. Baada ya ujio wa Waarabu, Kiswahili kilianza kutumika katika mabaraza ya kifalme katika himaya za Buganda na Bunyoro. Aidha, Wamisionari wa Church Misionary Society na White Fathers walitumia Kiswahili kuwasiliana na serikali pamoja na kueneza dini ya Kikristo. Walitumia Kiswahili kwa vile walikuta tayari kinatumika katika shughuli mbalimbali. Aidha, lugha ya Kiswahili ilienea sana Kaskazini mwa Uganda, kwa sababu ilikuwa inatumiwa na wanajeshi wengi katika mawasiliano yao.

Serikali ya kikoloni kupitia idara ya elimu mnamo mwaka 1925 – 1926, ilipitisha uamuzi kuhusu lugha ya kufundishia katika madarasa ya mwanzo ya shule za msingi. Iliamuliwa kuwa, Kiganda kitumike eneo lote lililokuwa likitumia lugha za Kibantu. Kwa upande mwingine, Kiacholi kitumike katika mkoa wa Kaskazini, ambako lugha kuu ni Kinailoti halafu Kiateso kitumike katika mkoa wa Kati.

Matumizi ya lugha hizi yalileta changamoto ya upatikanaji wa vitabu vya kufundishia, hali ambayo ilisababisha Kiswahili kipendekezwe kutumika kwa sababu vitabu vilikuwa vinapatikana nchi jirani za Kenya na Tanganyika. Hivyo,



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 67 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

walipendekeza Kiswahili kitumike kama lugha ya kufundishia na kufundishwa kama somo katika shule za msingi. Aidha, ilipendekezwa kuwa, vitabu vya masomo kama afya, jiografia na kilimo viandikwe kwa Kiswahili. Hata hivyo, ifahamike kwamba miaka miwili ya mwanzo wanafunzi walifundishwa kwa lugha zao za kwanza, na baada ya miaka hiyo ndipo Kiswahili kilitumika. Vituo vya elimu viliunga mkono sera mpya kuhusu Kiswahili. Kwa mfano, Shule ya Ufundi Kampala iliamua kufundishia Kiswahili badala ya Kiingereza.

Juhudi za kukuza Kiswahili zilianzishwa mwaka 1927 katika nchi ya Uganda. Gavana Gowers wa Uganda alishauri kwamba Kiswahili kikuzwe katika jimbo la Mashariki isipokuwa Busoga, ambako lugha ya Kiganda ilitumika katika madarasa yote ya shule za msingi. Sehemu zingine ambazo Kiswahili hakikufundishwa ni Bunyoro, Toro, Ankole, na Buganda. Mwaka 1928 Serikali ilianzisha chuo cha ualimu wa shule za msingi. Katika chuo hiki Kiswahili kilitumiwa kama lugha ya kufundishia. Matumizi ya Kiswahili yalikuwa yakienea vizuri nchini kote isipokuwa Buganda ambako Kiswahili kilikuwa kikipingwa kwa kuhusianishwa na dini ya Kiislamu. Vilevile, Kiswahili kilifundishwa kwa mafanikio katika Chuo cha Ualimu cha Misheni ya CMS kilichoitwa *Mukono,* na Chuo cha Ualimu cha *White Fathers* kilichoitwa *Bikira*.

Mnamo mwaka 1930, mradi mahususi wa kufundisha walimu wa vijijini kwa miaka miwili ulianzishwa. Katika kipindi hicho vituo ishirini na tisa (29) vilianzishwa katika mikoa ya Mashariki, Kaskazini, na Magharibi. Vituo hivi vilifundisha masomo ya dini, kilimo, mbinu za ufundishaji, afya, na Kiswahili. Lengo kuu la kufundisha Kiswahili lilikuwa ni kuhakikisha walimu wa ngazi ya cheti watakaofaulu wawe wameandaliwa vya kutosha kufundisha Kiswahili katika shule zao.

Juhudi za kukuza Kiswahili ziliendelea mwaka hadi mwaka. Mathalani, mwaka 1934 Kamati Kuu ya CMS ya Dayosisi ya Elgon iliamua masomo yote katika chuo cha kidini na cha walimu cha Bawanasi yafundishwe kwa Kiswahili. Aidha, uamuzi huo wa Kamati Kuu ulizihusu shule za msingi za misheni zilizokuwa katika maeneo yenye mchanganyiko wa lugha. Kwa hiyo, masomo yote katika shule hizo yalifundishwa kwa Kiswahili.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 68 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Mnamo mwaka 1936, mkutano wa Wakurugenzi wa Elimu wa Kenya, Uganda, Tanganyika, na Zanzibar ulifanyika Makerere. Jambo muhimu lililojitokeza katika mkutano huo ni kuongeza nguvu katika matumizi ya Kiswahili nchini Uganda. Shule za kati zilizokuwa zinapokea ruzuku ya serikali zilianza kufundisha masomo yote kwa kutumia Kiswahili, isipokuwa Buganda na Busoga. Walimu Waganda wapatao hamsini walikuwa wakifundisha wanafunzi zaidi ya mia saba kwa kutumia Kiswahili. Mashindano ya uandishi wa Kiswahili yalifanyika mwaka 1937. Katika mashindano hayo, Waganda kumi na wanne walishiriki, na saba kati yao walipata zawadi. Wanne kati ya waliopewa zawadi walikuwa Wabaganda. Hii inaonesha kuwa, pamoja na mkoa wa Buganda kutokutumia Kiswahili kufundishia katika shule zake, bado Wabaganda walikuwa wanatumia Kiswahili kwa kiwango cha kushiriki mashindano na kushinda.

Kufikia mwaka 1944, sera ya lugha ilikuwa ikihimiza matumizi ya Kiswahili na lugha za kwanza. Lugha zilizokubaliwa kuwa lugha za kufundishia katika shule za msingi ni Kiganda, Kiswahili, Kinyoro, Kitooro, Kijaluo, Kiateso, na Kilugbara. Kiswahili kilienea sana Kaskazini mwa Uganda kwa sababu kilikuwa kikitumiwa na wanajeshi wengi katika mawasiliano. Shule za serikali mbili (za pekee) ambako walikuwa wanasoma watoto wa askari polisi na magereza, zilitumia Kiswahili kufundisha masomo yote. Juhudi za kukuza Kiswahili zilikwama kabisa mwaka 1952, pale ambapo serikali ilitangaza kutotumia Kiswahili katika shule zote za Uganda, isipokuwa shule za polisi na magereza na shule za watoto wao.

**Changamoto za kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Uganda**

Kabla ya tangazo la kutokutambua Kiswahili kama somo, Kiswahili kilikuwa kimepitia changamoto mbalimbali. Changamoto hizo ni kuhusishwa na dini ya Kiislamu, kufikiriwa kuwa ni lugha ya wanajeshi, ambao hawakuwa wastarabu na kutokuungwa mkono na Waganda, kwa lengo la kulinda lugha yao ya Kiganda. Mfalme Kabaka Mutesa alipiga marufuku matumizi ya Kiswahili na kuhimiza matumizi ya Kiingereza. Uhimizaji wa matumizi ya Kiingereza uliathiri kukua na kuenea kwa Kiswahili Uganda.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 69 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE




**Kielelezo 3.1** Ramani ya Afrika Mashariki ikionesha misafara ya biashara na utawala



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 70 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



## Zoezi la 3.1

1. Unafikiri ni kwa nini kukua na kuenea kwa lugha ya Kiswahili katika nchi za Afrika Mashariki kulikuwa na tofauti kubwa? Tumia mifano katika kuthibitisha hoja zako.
2. Tathmini mchango wa dini katika kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Uganda.
3. Kwa jinsi gani lugha za kijamii ziliathiri kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Kenya na Uganda?
4. Kwa nini lugha za kijamii hazikuathiri kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Tanzania?

**Kukua na kuenea kwa Kiswahili Afrika Mashariki baada ya Uhuru**
Katika sehemu hii tutajadili kukua na kuenea kwa Kiswahili katika nchi tatu za Afrika Mashariki, ambazo ni Tanzania, Kenya, na Uganda.

**Kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Tanzania**
Baada ya kupata uhuru mwaka 1961, Tanganyika ilihitaji kujenga utaifa kwa kuimarisha mawasiliano baina ya serikali na wananchi wake. Lugha ya Kiswahili ilihitajika zaidi ili kukidhi haja hii kwa sababu lugha za jamii hazikukidhi haja ya kujenga utaifa na maendeleo ya nchi nzima. Pia, lugha za kigeni kama vile Kiingereza na Kijerumani hazikuweza kutumika kutokana na wananchi wengi kushindwa kuzitumia. Kwa hiyo, serikali ya Tanganyika ilichukua hatua mbalimbali zilizoongeza kasi ya kukua na kuenea kwa Kiswahili. Miongoni mwa hatua hizo ni kufanya Kiswahili kuwa lugha ya taifa na lugha rasmi, kutumia Kiswahili katika utawala, elimu, vyombo vya habari, vikundi vya sanaa, shughuli za biashara, na kuunda vyombo vya kukuza na kueneza Kiswahili.

***1 Kiswahili kuwa lugha ya taifa na lugha rasmi***

Baada ya Tanganyika kupata uhuru, Rais Julius K. Nyerere alihutubia bunge kwa mara ya kwanza kwa lugha ya Kiswahili tarehe 10/12/1962. Tukio hili liliamsha ari ya kutumia lugha ya Kiswahili na kusababisha viongozi wa serikali kutoa matamko mbalimbali kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili. Mnamo Februari, 1963, serikali ya Tanganyika kupitia gazeti la



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 71 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

serikali ilitangaza kuwa, Kiswahili kitakuwa lugha ya taifa na lugha rasmi itakayotumika katika shughuli zote za kiserikali. Jukumu la kusimamia maendeleo ya Kiswahili liliwekwa chini ya Wizara ya Utamaduni wa Taifa na Vijana.

Visiwani Zanzibar, serikali ilichukua hatua madhubuti za kukuza na kueneza Kiswahili siku tisa tu baada ya Mapinduzi ya mwaka 1964, ambapo ilikitangaza Kiswahili kuwa lugha ya taifa na rasmi. Uamuzi huo mkubwa ulitangazwa kupitia gazeti la Serikali lililoitwa *Kweupe*. Serikali iliunda Halmashauri ya Kiswahili iliyopewa jukumu la kuanzisha matumizi ya Kiswahili katika wizara, idara na mashirika ya umma. Vilevile, Serikali ya Mapinduzi ilitoa agizo la kupiga marufuku matumizi ya Kiingereza katika shughuli za kiserikali hivyo, kukipa Kiswahili nafasi.

### 2 K iswahili katika utawala

Baada ya Kiswahili kutangazwa kuwa lugha ya taifa na lugha rasmi, hatua mbalimbali zilichukuliwa kuhakikisha kuwa lugha hii inatumiwa katika shughuli za kiutawala. Kuanzia miaka ya 1960, serikali ilifanya uamuzi kuwa watumishi wa serikali wanaoajiriwa sharti wawe na ujuzi au uwezo wa kutumia lugha ya Kiswahili ili waweze kuwasiliana na wananchi katika kutoa huduma stahiki wawapo kazini. Kwa upande wa Zanzibar, serikali ilifuta sheria ya serikali ya kikoloni iliyokifanya Kiingereza kuwa lugha ya serikali. Aidha, ilipiga marufuku kuandika nyaraka kwa Kiingereza katika ofisi za serikali.

Hatua za kuendeleza Kiswahili ziliungwa mkono na viongozi mbalimbali wa serikali, hasa kwa kutoa matamko yaliyokuwa yanalenga kukuza Kiswahili. Mnamo Februari, 1967, aliyekuwa Waziri Mkuu na Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Awamu ya Kwanza, Rashid Mfaume Kawawa, alitoa tamko lililoelekeza viongozi na watumishi kutumia Kiswahili na kuepuka kuchanganya lugha wakati wa mawasiliano rasmi.

Mwaka 1974, aliyekuwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais (Utumishi),Bw. J.D. Mganga alitoa waraka wa utumishi Na. 1 wa 1974 ulioeleza kuhusu matumizi ya Kiswahili katika ofisi za serikali kwa kutilia mkazo mambo yafuatayo:



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 72 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



(i) Mawasiliano ya barua kati ya wizara na idara yafanywe kwa lugha ya Kiswahili isipokuwa kama barua itaandikwa kwa (na) mtu ambaye si Mtanzania.

(ii) Vibao vyote vya majina ya ofisi au wizara, na matangazo kama ya mahafali na sikukuu za kitaifa viandikwe kwa Kiswahili.

(iii) Madokezo yote baina ya maafisa na fomu zote zijazwe kwa Kiswahili.

Hatua za kukuza Kiswahili hazikuishia katika awamu ya kwanza. Ziliendelea hata katika awamu ya tatu ya serikali, ambapo mnamo Mei, 2005 serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge) iliagiza taarifa za mikutano, semina, na warsha zitolewe kwa lugha ya Kiswahili kwa manufaa ya wananchi. Vilevile, iliagiza kuwa taarifa za miradi inayohusu wananchi, vipeperushi na nyaraka zitolewe kwa Kiswahili.

Aidha, katika awamu ya nne ya serikali, jitihada za kukuza Kiswahili ziliendelea kushika hatamu. Februari, 2010 aliyekuwa Makamu wa Rais, Dkt. Ali Mohamed Shein katika kikao cha Baraza la Mawaziri alisisitiza matumizi ya lugha ya Kiswahili katika shughuli za serikali na kukumbusha watendaji wa serikali kuzingatia waraka wa mwaka 1967 uliotolewa na Waziri Mkuu na Makamu wa Pili wa Rais. Vilevile, Aprili, 2010 serikali, kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, iliagiza Kiswahili kitumike katika dhifa mbalimbali za kitaifa, hotuba, warsha, semina, mikutano ya kitaifa, majina ya barabara, mitaa, na mabango yanayohusu matangazo ya serikali. Katika agizo hilo, maafisa wa serikali na mashirika ya umma walitakiwa pia kutumia Kiswahili katika shughuli za kiutawala.

Pia, agizo hilo lilitaka Kiswahili kitumike katika matangazo na nyaraka zilizobandikwa kwa ajili ya umma. Aidha, sheria ziandikwe kwa Kiswahili na zile zilizoandikwa kwa lugha za kigeni zitafsiriwe. Zaidi ya hayo, jitihada za makusudi zifanyike ili shughuli za mahakama ziendeshwe kwa Kiswahili katika ngazi zote. Mijadala inayohusu shughuli za umma ukiwemo usaili, iendeshwe kwa Kiswahili na kumbukumbu za mijadala hiyo ziandikwe kwa Kiswahili.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 73 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Msukumo mpya wa kutumia Kiswahili katika shughuli zote za kiutawala umejitokeza mara tu baada ya kuanza kwa utawala wa serikali ya awamu ya tano ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika awamu hii, Rais Dkt. John Joseph Pombe Magufuli amejenga desturi ya kuendesha mikutano yote ya kitaifa na kimataifa kwa lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, mnamo tarehe 29.01.2017, Rais Magufuli alihutubia mkutano wa Umoja wa Afrika kwa lugha ya Kiswahili. Mkutano huo uliambatana na hafla ya uzinduzi wa jengo la kituo cha Mwl. Nyerere, Addis – Ababa (Ethiopia). Uamuzi huu umeitikiwa vizuri na viongozi wengine waandamizi wa serikali na mashirika ya umma. Matumizi ya Kiswahili katika shughuli za utawala yamesaidia kukuza na kueneza Kiswahili.

### *3 K iswahili katika elimu*

Baada ya uhuru, mfumo wa elimu uliendelea kama ulivyokuwa wakati wa Mwingereza. Katika mfumo huo, Kiswahili kilitumika kufundishia masomo yote katika Elimu ya Msingi (darasa la I - IV). Mfumo huo ulibadilika mwaka 1967 baada ya kutangazwa kwa Azimio la Arusha lililotangazwa sambamba na sera ya Ujamaa na Kujitegemea. Katika kipindi hiki, mabadiliko makubwa yaliyotokea katika elimu ni kutangazwa rasmi kwa matumizi ya Kiswahili katika kufundishia masomo yote ya elimu ya msingi isipokuwa Kiingereza. Kwa upande wa elimu ya sekondari, Kiswahili kilifanywa somo la lazima kwa kidato cha I – IV na kufundishia somo la siasa.

Vilevile, Kiswahili kilitumika kufundishia katika vyuo vya ualimu, utumishi wa umma, na maendeleo ya jamii. Aidha, serikali ilianzisha Elimu ya Watu Wazima (EWW) ili kupambana na ujinga. Madhumuni ya EWW yalikuwa kuwapa fursa watu wazima ambao hawakupata nafasi ya kwenda shuleni kujifunza kusoma na kuandika. Lugha iliyotumika kufundishia EWW ilikuwa Kiswahili. Aidha, vitabu vyote vilivyotumiwa kufundishia EWW viliandikwa kwa Kiswahili. Hatua hii ilisaidia sana kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili.

Baadaye, Kiswahili kilianza kufundishwa kama moja ya masomo ya kidato cha V na VI. Serikali iliruhusu somo la Kiswahili lifundishwe ngazi ya Chuo Kikuu kuanzia mwaka 1970 ambapo lilianza kufundishwa katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kiswahili kimeendelea kufundishwa kama somo katika vyuo vikuu mbalimbali vilivyoanzishwa baada ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kama vile Chuo Kikuu cha Mt. Yohana cha Tanzania,


PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 74 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Chuo Kikuu cha Waislamu (Morogoro), Chuo Kikuu cha Arusha, na Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino. Pia, programu za shahada za Kiswahili, kuanzia Shahada za Awali hadi Uzamivu zimeanzishwa katika Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, na Chuo kikuu cha Taifa Zanzibar. Matumizi ya Kiswahili katika elimu yamesaidia kukuza na kueneza Kiswahili kwa watu wengi zaidi.

***4. Vyombo vya habari***

Baada ya uhuru, vyombo mbalimbali vya habari vilivyokuwepo kabla ya uhuru vimeendelea kukuza Kiswahili. Vyombo vya habari vilivyokuwepo wakati wa uhuru ni Redio Tanzania (Sauti ya Tanganyika) na magazeti mbalimbali. Aidha, vyombo vipya vya habari vimeendelea kuanzishwa hasa baada ya kuanzisha sera ya soko huria. Redio ya taifa pamoja na magazeti ya *Uhuru* na *Mzalendo* ya chama cha TANU (baadaye CCM), vimekuwa vikifanya kazi kubwa ya kutoa habari, kuelimisha, na kutoa burudani kwa jamii ya Watanzania kwa kutumia Kiswahili. Kwa mfano, Redio ya taifa ambayo imekuwa ikitoa matangazo yake kwa Kiswahili imekuwa ikisikika nchi nzima. Serikali imekuwa ikiitumia kutoa matangazo na taarifa mbalimbali za utendaji wake kwa wananchi. Licha ya kurusha matangazo yake kwa Kiswahili, imekuwa na vipindi maalumu kwa ajili ya lugha ya Kiswahili. Mfano wa vipindi hivyo ni *Kiswahili Lugha Yetu* na *Lugha ya Taifa*. Kupitia vipindi hivi, mijadala mbalimbali inayohusu lugha ya Kiswahili hufanyika. Kuwepo kwa vipindi vya michezo, kampeni za kitaifa kama vile *Mtu ni Afya*, *Chakula ni Uhai*, na *Kupanga ni Kuchagua* zilisaidia kukuza na kueneza Kiswahili. Kwa upande wa Tanzania Visiwani, Sauti ya Tanzania Zanzibar imekuwa ikitangaza matangazo yake kwa lugha ya Kiswahili. Kituo hiki cha Redio husikika katika Visiwa vya Pemba, Unguja, na sehemu ya Tanzania Bara. Idhaa ya Taifa hujiunga na kituo hiki kila siku saa 1:00 jioni kurusha taarifa ya habari.

Baada ya kuanzishwa kwa sera ya soko huria vituo kadhaa vya redio vilianzishwa. Vituo hivyo ni kama vile *Radio One Stereo*, *Radio Free Africa (RFA)*, *Radio Tumaini*, *Radio Clouds*, *Radio Times*, *Radio EFM*, *Radio Praise Power*, *Wapo FM*, *Radio Imani*, *Radio Abood*, *Radio Maria*, *Radio Kwizera*, *Radio Mlimani ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*, *Radio France Internationale* (Kiswahili), na kadhalika. Vituo hivi hutoa matangazo yake kwa Kiswahili na husaidia kukuza Kiswahili. Baadhi ya vituo hivi vina vipindi maalumu vya lugha ya Kiswahili. Mfano wa vituo hivi ni *Radio*



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 75 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*One Stereo*, ambayo hurusha kipindi maalumu cha Kiswahili kinachoitwa *Kumepambazuka Kiswahili*. Aidha, *Radio Clouds* ina utaratibu wa kuteua msamiati wa siku kila siku na kuufafanua (kila baada ya saa kwa siku nzima). Pia, Serikali kupitia Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imekuwa na mkakati wa kuanzisha vituo vya Redio ambavyo hutangaza kwa lugha ya Kiswahili katika kila Halmashauri za Wilaya, miji, na majiji. Mifano ya vituo hivyo ni vile vinavyomilikiwa na Halmashauri ya Jiji la Mbeya na Halmashauri ya Jiji la Tanga.

Vyombo vingine vilivyosaidia kukuza na kueneza Kiswahili ni magazeti. Kama ilivyodokezwa mwanzoni mwa sehemu hii, magazeti ya mwanzo yalimilikiwa na chama cha TANU. Magazeti haya yalisomwa kwa hamasa kubwa sana. Wakati huo, kipimo cha usomi na maendeleo kilikuwa ni kusoma magazeti. Kwa hiyo, kila mtu alijitahidi kujifunza kusoma ili aweze kusoma magazeti kwa lengo la kuonekana msomi. Kwa njia hiyo, watu wengi walijifunza Kiswahili, hivyo, kukifanya kikue na kuenea. Pia, magazeti mengine mengi yalianzishwa kutokana na sera ya soko huria. Magazeti hayo ni *Habari Leo* na *Habari Leo Jumapili* (serikali), *Mwananchi*, *Nipashe*, *Tanzania Daima*, *Majira*, *Jamhuri*, *Zanzibar Leo*, *Rai*, *Raia Mwema*, *Mwanahalisi*, *Kulikoni*, *Spoti Starehe*, *Dimba*, *Mwanaspoti*, *Sayari*, *Tanzania Yetu*, *Simba*, na *Yanga*. Magazeti haya huchapishwa kwa Kiswahili na kusambazwa nchi nzima. Baadhi ya magazeti haya yana makala maalumu kuhusu Kiswahili na maendeleo yake. Magazeti hayo ni pamoja na toleo la Jumatano la gazeti la Mwananchi, ambalo hutoa ukurusa maalumu wa lugha ya Kiswahili. Aidha, toleo la Ijumaa la gazeti la *Habari Leo* hutoa makala yanayohusu lugha ya Kiswahili na toleo la Jumanne hutoa mada inayofundisha Kiswahili kwa wageni.

Aidha, vyombo vingine vya habari ambavyo vimesaidia kukuza na kueneza Kiswahili ni televisheni. Tofauti na redio na magazeti, televisheni zilichelewa kidogo kuanza. Televisheni zimeanza kutumika mwishoni mwa miaka ya 1980 lakini mapinduzi makubwa ya vyombo hivi yametokea miaka ya 1990. Kituo cha mwanzo kilikuwa ni *Televisheni Zanzibar* (*TVZ*) ambacho kinamilikiwa na Shirika la Utangazaji Zanzibar. Kituo hiki kimekuwa kikitangaza kwa lugha ya Kiswahili na hatimaye kimepanua huduma kwa kuanzisha idhaa nyingine ya TVZ-2.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 76 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Vilevile, serikali ilianzisha kituo cha *Televisheni ya Taifa* (TVT) Tanzania Bara ambacho baadaye kilibadilishwa jina na kuwa TBC1 baada ya kuwa chini ya Shirika la Utangazaji Tanzania. Kituo hiki hutangaza kwa Kiswahili. Licha ya kutangaza kwa Kiswahili, kimekuwa na vipindi maalumu vya lugha ya Kiswahili. Vipindi hivyo ni *Lulu za Kiswahili* na *Ulimwengu wa Kiswahili*. Vituo vingine vya televisheni vinavyotoa matangazo kwa Kiswahili vinamilikiwa na watu binafsi na mashirika ya umma. Vituo hivyo ni *Independent Television* (ITV), *Star TV*, *Tumaini TV, Mlimani TV, Channel Ten, East Africa Television* (EATV), *TV1*, *Sibuka TV,* na *Azam TV*.

Kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia kumekuwa na mapinduzi ya hali ya juu katika vyombo vya habari. Suala la mawasiliano na kupashana habari limechukua sura mpya, hasa baada ya kuibuka kwa mitandao ya mawasiliano ya kijamii kama *baruapepe, tovuti, blogu, Facebook, WhatsApp,* na *Tweeter*. Kwa sasa, mitandao hii hutumika kwa kiwango kikubwa kuliko redio, magazeti na televisheni, hususani katika mazingira ya mijini. Matumizi ya mitandao hii, kwa kiwango kikubwa hutumia simumtelezo. Mawasiliano katika mitandao hii hufanyika kwa lugha ya Kiswahili hususani, kwa watumiaji wa lugha ya Kiswahili. Mbali na mawasiliano, katika mitandao hii kuna makala na machapisho yanayohusu lugha ya Kiswahili. Makala na machapisho hayo husaidia watu kupata maarifa yanayohusu lugha ya Kiswahili. Aidha, wajifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni huweza kunufaika kwa kujifunza Kiswahili kwa njia ya mtandao.

### *5 B iashara*

Biashara ni sekta inayogusa karibu watu wote katika jamii. Tanganyika na Zanzibar kabla ya uhuru, zimekuwa zikishirikiana na watu kutoka mataifa mengine ya Kiarabu, Ulaya, Marekani, na Asia katika shughuli za kibiashara. Sekta ya biashara imeendelea kukua siku hadi siku sambamba na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Nchini Tanzania biashara ilianza kushamiri miaka ya 1980 mara baada ya kuanza kwa sera ya soko huria. Shughuli za biashara zimekuwa zikitumia Kiswahili kama lugha kuu ya mawasiliano. Licha ya kuwa lugha ya mawasiliano ya biashara, Kiswahili kimetumika katika kuandika nembo za vifungashio pamoja na maelekezo ya matumizi ya bidhaa. Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA) inasisitiza kutoa maelezo yanayohusu bidhaa za dawa na chakula kwa Kiswahili. Aidha, matangazo mbalimbali ya biashara katika mabango, vipeperushi, na



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 77 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kwenye vyombo vya habari hutolewa kwa Kiswahili. Kwa njia ya biashara, Kiswahili kimepata msamiati mpya kama vile *muamala*, *kitelaoto* na *baba au mama lishe*.

Vilevile, serikali ilifungua milango kwa wawekezaji wa nje kwenye sekta mbalimbali za biashara kama vile kampuni za simu, madini, utalii, na kilimo. Katika sekta hizi watu hutangamana na kuwasiliana kwa kutumia Kiswahili. Kwa njia hii, watu wengi hujifunza Kiswahili ili waweze kuwasiliana. Pia, serikali huratibu maonesho ya biashara ya kimataifa kupitia Bodi ya Biashara za Nje. Maonesho hayo hujumuisha maonesho ya SABASABA, maonesho ya bidhaa za viwandani, maonesho ya viwanda vidogovidogo, maonesho ya bidhaa za kilimo (NANENANE), na maonesho ya nchi za nje kama vile Syria na Uturuki.

***6 K iswahili katika vikundi vya sanaa***

Baada ya uhuru, Kiswahili kimekua na kuenea kwa njia ya vikundi vya sanaa. Kazi hizi zilikuwa zikiratibiwa na chama na serikali, mashirika ya umma, na ofisi za utamaduni. Chama na serikali viliendeleza bendi ya muziki ya NUTA Jazz (JUWATA, OTTU na sasa Msondo Ngoma), na vikundi vingine kama vile vikundi vya Mzee Mwinamila na Tengulabei. Pia, Jumuiya ya Umoja wa Vijana ya chama cha TANU na sasa CCM inamiliki bendi ya *Vijana Jazz*.

Mashirika ya umma na majeshi yalikuwa na bendi za muziki na sanaa ambazo zilitumia lugha ya Kiswahili. Baadhi ya bendi hizo ni *Tancut Almasi Orchestra*, *Bima Lee Orchestr*a, *Washirika Muungano Star*, *UDA Jazz Band*, *Tanzania One Theatre (TOT)*, na *DDC Mlimani Park Orchestra*. Bendi nyingine ni *Polisi Jazz* (Vangavanga), *National Service Jazz Band* (Kimbunga Stereo), *Mwenge Jazz* (Wanapaselepa), na *Magereza Jazz Band* (Super Mnyanyuo).

Baadhi ya nyimbo pamoja na sanaa za maigizo vilitumika kuelezea sera za nchi kama vile *Ujamaa na Kujitegemea* na kuhamasisha utekelezaji wa kampeni mbalimbali za kiserikali kama vile *Usalama Barabarani na Uraia*, *Kilimo cha Kufa na Kupona* na *Mtu ni Afya*.

Vilevile, nyimbo hizo zilitumika na zinaendelea kutumika kuwapongeza viongozi wa kitaifa. Aidha, serikali, kupitia Wizara ya Elimu, ilitoa fursa za



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 78 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



kufundishwa sanaa mbalimbali kama maigizo, nyimbo, ngonjera, na mashairi shuleni. Maonesho ya kazi hizi yalifanyika katika maadhimisho ya kitaifa na katika mashindano yaliyokuwa yakiratibiwa kupitia wataalamu wa sanaa na fasihi pamoja na maafisa utamaduni wa wilaya na mikoa. Miongoni mwa mashindano hayo ni Umoja wa Michezo na Taaluma kwa Shule za Msingi Tanzania (UMITASHUMTA), Umoja wa Michezo Sekondari Tanzania (UMISETA), na Umoja wa Michezo na Sanaa Vyuo vya Elimu Tanzania (UMISAVETA) ambayo yamekuwa yakifanyika hadi ngazi ya taifa. Kwa ujumla, vikundi vya sanaa vimekuwa vikitumia lugha ya Kiswahili katika kuwasilisha kazi zake; hali ambayo imesababisha kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini.

## Zoezi la 3.2

1. Eleza hatua sita zilizochukuliwa na serikali nchini Tanzania za kukuza na kueneza Kiswahili baada ya uhuru.
2. Jadili hatua zilizochukuliwa kukuza na kueneza Kiswahili Tanzania Visiwani baada ya uhuru.
3. Fafanua changamoto zilizojitokeza wakati wa kukuza na kueneza Kiswahili Tanzania baada ya uhuru.
4. Eleza jinsi sekta ya elimu ilivyosaidia kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Tanzania baada ya uhuru.

### 7. Taasisi na vyombo vya kukuza na kueneza Kiswahili Tanzania baada ya uhuru

Baada ya uhuru, hatua ya kuunda taasisi na vyombo mbalimbali kwa madhumuni ya kukuza na kueneza Kiswahili zilichukuliwa na serikali, mashirika ya umma pamoja na wapenzi wa Kiswahili. Taasisi zilizoundwa kwa madhumuni hayo ni Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI) na Idara ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI), Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni Zanzibar (TAKILUKI), Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA), na Umoja wa Waandishi wa Vitabu Tanzania (UWAVITA). Katika sehemu hii tutaangalia madhumuni, mafanikio, na changamoto za taasisi hizo.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

For Online Use Only

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 79 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI)**
Taasisi hii iliundwa Mwaka 1964 kutokana na iliyokuwa Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki ya mwaka 1930, ikiwa sehemu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Hii ilikuwa ni taasisi ya pekee iliyojishughulisha na uchunguzi wa Kiswahili.

**Madhumuni ya TUKI**

TUKI ilikuwa na madhumuni yafuatayo:
(i) Kufanya utafiti kuhusu lugha ya Kiswahili;
(ii) Kuwatia moyo watu wanaojishughulisha na uandishi wa vitabu katika lugha ya Kiswahili;
(iii) Kushughulika na ukuzaji wa istilahi za Kiswahili na uandishi wa kamusi za taaluma mbalimbali;
(iv) Kuhariri vitabu na machapisho mengine;
(v) Kuhifadhi ufasaha wa lugha ya Kiswahili;
(vi) Kutafsiri maandishi yanayohitajika katika matumizi ya lugha ya Kiswahili;
(vii) Kushirikiana na serikali na vikundi vingine vilivyo na lengo la kustawisha lugha ya Kiswahili; na
(viii) Kutoa majarida na machapisho mbalimbali yanayohusiana na Kiswahili.

**Mafanikio ya TUKI**

TUKI ilipata mafanikio yafuatayo:
(i) Kutoa kamusi mbalimbali kama vile Kamusi ya Kiswahili Sanifu, Kamusi ya Kiingereza – Kiswahili na Kamusi ya Kiswahili – Kiingereza;
(ii) Kutoa jarida la *Kiswahili* ambalo huchapisha makala za taaluma ya isimu na fasihi ya Kiswahili linalotolewa mara moja kwa mwaka;
(iii) Kuanzisha na kuchapisha jarida la *Mulika* kwa ajili ya matumizi ya wanafunzi wa shule za sekondari za Tanzania;
(iv) Kutoa kamusi za taaluma maalumu kama vile Kamusi ya Hesabu, Kamusi ya Fizikia, Biolojia na Kemia na Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha;
(v) Kukusanya na kuchapisha mashairi, hadithi, vitendawili, na methali;
(vi) Kuanzisha makavazi ya nyaraka mbalimbali yanayohusiana na lugha;
(vii) Kushirikiana na serikali pamoja na idara nyingine kama vile Idara ya Kiswahili (Chuo Kikuu cha Dar es Salaam), Taasisi ya Elimu na Wizara ya Utamaduni katika kazi mbalimbali kama vile kutafsiri sera na machapisho mbalimbali; na


PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 80 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



(viii) Kuhifadhi baadhi ya mashairi ya zamani yaliyoandikwa kwa lugha ya Kiarabu.

**Changamoto za TUKI**

TUKI ilikabiliwa na changamoto zifuatazo:

(i) Uhaba wa fedha za kutekeleza majukumu yake. Hali hii ilisababisha baadhi ya kazi za taasisi kutofanyika kama ilivyopangwa. Mathalani, TUKI ilirithi miswada ya vitabu zaidi ya 800 kutoka Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki lakini ni miswada michache tu iliyofanyiwa kazi.

(ii) Mwamko mdogo wa watu wanaojishughulisha na uandishi wa vitabu katika lugha ya Kiswahili.

(iii) Ukosefu wa maabara ya lugha na vifaa vya kuchanganulia lugha.

**Idara ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam**

Idara hii ilianzishwa mwaka 1970, kilipoanzishwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Baadaye Idara iliungana na TUKI kuunda TATAKI mwaka 2009. Hii ndiyo idara ya kwanza Afrika kutoa mafunzo ya elimu ya juu kwa lugha ya Kiswahili. Idara hii ilifanya kazi sambamba na TUKI. Madhumuni yake yalikuwa ni haya yafuatayo:

(i) Kutayarisha walimu kwa ajili ya kufundisha somo la Kiswahili katika ngazi ya sekondari na vyuo ndani na nje ya nchi;

(ii) Kuendesha tafiti mbalimbali kuhusu lugha ya Kiswahili na lahaja zake.

(iii) Kutoa msaada wa kitaalamu kuhusu lugha ya Kiswahili ulipohitajika ndani na nje ya nchi;

(iv) Kuandaa wataalamu wa lugha ya Kiswahili kama watafiti, wafasiri, wakalimani na wanaleksikografia; na

(v) Kuanzisha na kuchapisha jarida la *Kioo cha Lugha* kwa ajili ya kuchapisha makala ya kitaaluma.

**Mafanikio ya Idara ya Kiswahili**

Idara ilipata mafanikio mbalimbali kama ifuatavyo:

(i) Kusimamia na kufundisha lugha ya Kiswahili kwa wageni;

(ii) Kutoa walimu wa somo la Kiswahili wa kufundisha katika ngazi mbalimbali za elimu;



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 81 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(iii) Kuandaa wataalamu wa lugha ya Kiswahili kwa ajili ya taasisi mbalimbali kama BAKITA na BAKIZA;

(iv) Kushirikiana na TUKI kuandaa vitabu na machapisho mbalimbali ya lugha ya Kiswahili; na

(v) Kupeleka wahadhiri kufundisha Kiswahili katika vyuo vikuu vya nje ya nchi kwa mfano Rwanda, Nijeria, na Ghana.

**Changamoto za idara**

Katika kutimiza majukumu yake, idara ilikabiliwa na changamoto mbalimbali kama ifuatavyo:

(i) Baadhi ya wataalamu wake kuacha kujishughulisha na lugha ya Kiswahili na kufanya kazi nyingine kama vile kazi za utawala au siasa. Hivyo kupunguza nguvukazi ya kufundisha na kuendeleza lugha ya Kiswahili.

(ii) Ufinyu wa bajeti ya idara ambao ulikwamisha majukumu yake kama vile kufanya tafiti, kuandaa semina, makongamano, na kuandaa miswada kwa ajili ya machapisho mbalimbali.

(iii) Mtazamo hasi kuhusu kusoma Kiswahili. Baadhi ya watu walikuwa na mtazamo hasi na kuona kuwa Kiswahili ni somo lisilokuwa na masilahi. Kwa hiyo, watu wengi walikimbilia taaluma nyingine; hali ambayo ilipunguza wataalamu wa kukiendeleza Kiswahili.

**Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI)**

Taasisi hii iliundwa mwaka 2009 kwa kuunganisha TUKI na Idara ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Lengo la kuunganisha taasisi hizi mbili ni kupanua wigo wa kukuza, kuendeleza na kustawisha lugha ya Kiswahili. Kwa hiyo, kuundwa kwa TATAKI kulipanua wigo wa kushughulikia mambo yote yanayohusiana na lugha ya Kiswahili. TATAKI ina idara kuu mbili za kitaaluma ambazo ni *Idara ya Lugha ya Kiswahili na Isimu (ILUKII)*, na *Idara ya Fasihi, Mawasiliano na Uchapishaji (IFAMU).*

**Madhumuni ya TATAKI**

Ili kutimiza majukumu yake, TATAKI inaongozwa na madhumuni yafuatayo:

(i) Kufanya tafiti mbalimbali kuhusu lugha ya Kiswahili katika taaluma za isimu, fasihi na utamaduni wa Kiswahili;


PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 82 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


(ii) Kufanya tafiti katika taaluma ya leksikografia, kuandaa na kuandika kamusi mbalimbali za lugha ya Kiswahili;

(iii) Kuratibu msamiati na kuunda istilahi anuwai za kitaaluma na kuziingiza katika kamusi;

(iv) Kuratibu na kutafsiri matini mbalimbali katika taasisi za serikali na zile zisizo za serikali;

(v) Kushirikiana na taasisi pamoja na asasi nyingine za kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili;

(vi) Kutoa ushauri wa kitaalamu katika vipengele vya lugha, isimu na fasihi;

(vii) Kuandaa na kuchapisha vitabu na majarida ya Kiswahili kwa matumizi ya watu binafsi na taasisi mbalimbali ndani na nje ya nchi; na

(viii) Kuhakikisha kuwa Kiswahili kinakuwa na msingi imara kama lugha ya kufundishia kuanzia ngazi ya elimu ya awali hadi chuo kikuu.

**Mafanikio ya TATAKI**

Taasisi imefanikiwa katika nyanja mbalimbali kama ifuatavyo:

(i) Taasisi imeweza kudahili na kufundisha wanafunzi wa shahada za awali, umahiri, na uzamivu. Kila mwaka kumekuwa na ongezeko kubwa la wanafunzi na hii husaidia kuongeza wataalamu wa lugha ya Kiswahili.

(ii) Taasisi imefanikiwa kusimamia na kufundisha lugha ya Kiswahili kwa wageni.

(iii) Taasisi imefanya tafiti mbalimbali kuhusu lugha ya Kiswahili na kuchapisha matokeo ya tafiti hizo katika vitabu na majarida ya taasisi na kwingineko.

(iv) Taasisi imefanikiwa kuendelea kuboresha kamusi mbalimbali zilizotolewa hapo awali. Kwa mfano, taasisi ilifanya maboresho ya *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* na *Kamusi ya Kiswahili – Kiingereza.*

(v) Taasisi imetafsiri nyaraka mbalimbali za serikali na taasisi zake na za watu binafsi.

(vi) Taasisi imeandaa semina, warsha na makongamano ya ndani ya taasisi na ya kimataifa.

(vii) Taasisi imepeleka wahadhiri kufundisha Kiswahili katika vyuo vikuu vya nje.

For Online Use Only


PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 83 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Changamoto za TATAKI

Pamoja na mafanikio yaliyotajwa hapo juu, TATAKI inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

(i) Uhaba wa vifaa vya kisasa vya lugha vinavyoendana na kasi ya mabadiliko ya sayansi na teknolojia kama vile vifaa maalumu vya ukalimani na maabara ya lugha.

(ii) Baadhi ya wataalamu kuacha kufanya kazi za Kiswahili na kujihusisha na kazi nyingine; hali ambayo husababisha taasisi kushindwa kufikia malengo yake.

(iii) Taasisi hupata fedha kidogo ambazo hazikidhi mahitaji ya kujiendesha kwa ufanisi.

### Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA)

Baraza la Kiswahili la Taifa liliundwa kwa sheria namba 27 ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1967. Hiki ndicho chombo cha juu kabisa kilichopewa dhamana ya kuratibu, kukuza na kueneza Kiswahili ndani na nje ya nchi. BAKITA limegawanywa katika idara tano (5) ambazo zinahusu ukuzaji na uenezaji wa Kiswahili. Idara hizo ni: Idara ya Uhariri na Uchapishaji, Idara ya Lugha na Fasihi, Idara ya Tafsiri na Ukalimani, Idara ya Istilahi na Kamusi, na Idara ya Mawasiliano na Umma. Pamoja na jukumu la kuratibu shughuli zote za kukuza na kueneza Kiswahili, BAKITA lina madhumuni yafuatayo:

(i) Kusimamia na kuhimiza matumizi ya Kiswahili fasaha na sanifu;

(ii) Kufanya tafiti mbalimbali za lugha ya Kiswahili, kuchapisha matokeo ya tafiti hizo na kutunza kumbukumbu zinazohusiana na Kiswahili;

(iii) Kusanifisha istilahi za Kiswahili zinazohusiana na fani mbalimbali kama vile sheria, sayansi, matibabu, utangazaji na ujenzi;

(iv) Kuweka mazingira mazuri kwa ajili ya maendeleo na matumizi ya Kiswahili nchini;

(v) Kushirikiana na asasi na vyombo vingine vinavyojihusisha na maendeleo ya Kiswahili ili kuinua hadhi ya lugha ya Kiswahili na matumizi yake kwa ujumla;

(vi) Kuchapisha majarida na vitabu vyenye miongozo ya matumizi ya Kiswahili sanifu;

(vii) Kutoa huduma za tafsiri na ukalimani kwa taasisi mbalimbali ndani na nje ya nchi;


PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 84 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


(viii) Kushauri, kuratibu na kufuatilia shughuli zote zinazohusu ukuzaji wa Kiswahili zinazofanywa na asasi, vyombo, au watu binafsi;

(ix) Kuainisha asasi na vyombo anuwai vinavyoratibu tafiti za Kiswahili nchini Tanzania;

(x) Kutoa majibu ya maswali mbalimbali yanayoulizwa kuhusu lugha na fasihi ya Kiswahili; na

(xi) Kupitia kazi za waandishi na wafasiri na kutoa ithibati ya lugha.

**Mafanikio ya BAKITA**

Baraza limekuwa na mafanikio katika vipengele vifuatavyo:

(i) Kuelimisha mambo mbalimbali yanayohusu matumizi ya lugha ya Kiswahili. Baraza limekuwa na vipindi mbalimbali kama vile *Lugha ya Taifa* (TBC – Taifa), *Kumepambazuka Kiswahili* (Radio One Stereo) na *Ulimwengu wa Kiswahili* (TBC1).

(ii) Kutoa ushauri kwa wanafunzi wa Kiswahili wanaoandika miradi na tasnifu mbalimbali kuhusu lugha ya Kiswahili kwa ngazi mbalimbali.

(iii) Kutafsiri kazi mbalimbali za lugha ya Kiswahili na lugha nyingine za kigeni.

(iv) Kubainisha makosa ya lugha kutoka magazetini na vyombo mbalimbali vya habari na kutoka katika vyanzo vingine na kutoa usahihi wake kwa jamii kupitia vyombo vya habari.

(v) Kutoa huduma za tafsiri na ukalimani serikalini, kwenye taasisi mbalimbali za umma na zisizo za umma na kwa watu binafsi.

(vi) Kupitia machapisho yanayoandikwa kwa Kiswahili kabla ya kuyatoa na kutoa ithibati ya lugha; mamlaka ambayo yanatokana na sheria iliyopitishwa na Bunge ya mwaka 1983.

(vii) Kutoa vitabu pamoja na kamusi za lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, *Mwongozo kwa Waandishi wa Kiswahili Sanifu, Kiswahili na Utandawazi, Istilahi za Kiswahili, Kamusi ya Diplomasia* na *Kamusi Kuu ya Kiswahili (KKK).*

(viii) Kutoa mafunzo maalumu ya awali kuhusu lugha ya Kiswahili kwa wageni. Mpango huu ulianza Oktoba, 2016.

(ix) Kuendesha semina, warsha na makongamano kuhusu taaluma mbalimbali za lugha ya Kiswahili. Ili kufanikisha suala hili, wawezeshaji hualikwa kutoka ndani au nje ya BAKITA kuendesha mafunzo hayo.


PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 85 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Changamoto za BAKITA**

BAKITA limekuwa likikabiliwa na changamoto zifuatazo katika kutekeleza majukumu yake:

(i) Ari ndogo ya watu kupokea na kukubali mabadiliko mbalimbali pamoja na marekebisho yanayotolewa na BAKITA kuhusu matumizi sahihi ya Kiswahili;

(ii) Baadhi ya waandishi kutokupeleka machapisho yao BAKITA kwa ajili ya kupata ithibati ya lugha; na

(iii) Uhaba wa fedha ambao unalifanya BAKITA lishindwe kutimiza mipango yake kama vile kuchapisha jarida la *Lugha Yetu* lililokuwa likitoa mwongozo wa matumizi sahihi ya Kiswahili.

**Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni Zanzibar (TAKILUKI)**

Taasisi hii ilianzishwa mwaka 1979. Makao yake makuu yako mjini Unguja, Zanzibar. Taasisi hii iko chini ya ofisi ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali.

**Madhumuni ya TAKILUKI**

TAKILUKI ilianzishwa kwa madhumuni yafuatayo:

(i) Kutoa mafunzo na kusimamia matumizi ya Kiswahili fasaha na sanifu kwa watumishi wa serikali na wananchi;

(ii) Kufanya tafiti za lahaja zote za Zanzibar na vipengele vya sarufi na fasihi;

(iii) Kufundisha Kiswahili kwa wageni na lugha za kigeni kwa wenyeji;

(iv) Kutayarisha na kuchapisha vitabu na majarida mbalimbali;

(v) Kutoa miongozo ya namna bora ya kutumia Kiswahili sanifu; na

(vi) Kufanya tafiti za tungo mbalimbali za kifasihi zenye asili ya Kiswahili na kuhifadhi taarifa zake.

**Mafanikio ya TAKILUKI**

Yafuatayo ni mafanikio ya TAKILUKI:

(i) Kukusanya taarifa anuwai kuhusu lugha ya Kiswahili na lahaja zake na kuzihifadhi;

(ii) Kutoa mafunzo ya lugha ya Kiswahili kwa wageni na lugha za kigeni kwa wenyeji;

(iii) Kufanya tafiti kuhusu sarufi ya Kiswahili na tamaduni za jamii zinazoendana na lugha ya Kiswahili;



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 86 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


(iv) Kuchapisha vitabu vya lugha ya Kiswahili, mathalani, *Diwani ya Malenga Wapya*; na

(v) Kutoa mafunzo mbalimbali kwa watumishi wa serikali na watangazaji wa Shirika la Utangazaji la Zanzibar kuhusu matumizi ya Kiswahili sanifu.

**Changamoto za TAKILUKI**

TAKILUKI inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

(i) Ugumu katika ukusanyaji wa data na taarifa za zamani za fasihi kutokana na jamii kutokuwa na utaratibu wa kuhifadhi taarifa za matukio ya zamani;

(ii) Uhaba wa vifaa vya kufanyia kazi kama vile vyombo vya usafiri ili kurahisisha safari za kitafiti; na

(iii) Uhaba wa fedha za uendeshaji wa shughuli za taasisi na kushindwa kutekeleza baadhi ya majukumu yake.

Kuanzia mwaka 2012 TAKILUKI ilibadilisha jina na majukumu na kuwa Skuli ya Kiswahili na Lugha za Kigeni (SKILUKI). Lengo kuu likiwa ni kutoa walimu bora wa taaluma za Kiswahili na lugha za kigeni kama vile Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kireno, na Kichina. Taasisi hii ina Idara kuu tatu ambazo ni Idara ya Kiswahili, Idara ya Kiswahili kwa Wageni na Idara ya Lugha za Kigeni.

**Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA)**

Baraza hili lilianzishwa mwaka 1983 likiwa na jukumu la kuratibu shughuli zote za kukuza na kueneza Kiswahili Zanzibar. Hatua hii ilikuja baada ya kuona umuhimu mkubwa wa kuhimiza matumizi ya lugha ya Kiswahili kwa wananchi wote. Baraza hili limeshirikiana na serikali kuwaunganisha watu kwa ajili ya kushiriki shughuli za maendeleo ya Kiswahili.

**Madhumuni ya BAKIZA**

BAKIZA liliundwa kwa madhumuni yafuatayo:

(i) Kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili visiwani Zanzibar;

(ii) Kusimamia matumizi ya Kiswahili sanifu ndani ya Baraza la Wawakilishi na vyombo vya habari kwa ujumla;

(iii) Kuandaa na kuchapisha kamusi na majarida mbalimbali;

(iv) Kupitia na kusanifu maandishi ya Kiswahili; na

(v) Kutafsiri na kukalimani kazi mbalimbali.


PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 87 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Mafanikio ya BAKIZA**

Baraza limefanikiwa katika vipengele vifuatavyo:

(i) Kusimamia matumizi ya Kiswahili sanifu katika vikao vya Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

(ii) Kutoa ushauri na kusimamia matumizi ya Kiswahili sanifu katika vyombo vya habari vya Zanzibar.

(iii) Kuendesha semina ya kuwakumbuka na kuwaenzi waandishi wakongwe wa Kiswahili Zanzibar kila mwaka. Kwa mfano, semina ya Machi, 2017, ilikuwa ya kumkumbuka na kumuenzi mwandishi maarufu wa riwaya pendwa Mohamed Said Abdullah (Bwana Msa).

(iv) Kuandaa na kuchapisha kamusi mbalimbali za lugha ya Kiswahili kama vile *Kamusi la Kiswahili Fasaha, Kamusi la Lahaja ya Kipemba* na *Kamusi la Lahaja ya Kimakunduchi.*

(v) Kutafsiri machapisho mbalimbali ya serikali na taasisi mbalimbali. Kwa mfano, BAKIZA limetafsiri miswada mbalimbali ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

(vi) Kuandaa makongamano ya wasanii wa lugha ya Kiswahili.

**Changamoto za BAKIZA**

BAKIZA limekuwa likikabiliwa na changamoto mbalimbali kama ifuatavyo:

(i) Uhaba wa fedha ambao unasababisha kushindwa kutimiza majukumu yake kama vile kuandaa miswada mbalimbali na kufanya tafiti.

(ii) Upungufu wa wataalamu wa lugha ya Kiswahili katika BAKIZA kwa sababu ya uhaba wa fedha za kuajiri wataalamu wengi.

**Umoja wa Waandishi wa Vitabu Tanzania (UWAVITA)**

Umoja huu ulianzishwa na waandishi wa vitabu vya Kiswahili mwaka 1978. Umoja huu ulianzishwa kwa lengo la kuwaunganisha waandishi ili wafanye kazi zao kwa ufanisi zaidi.

**Madhumuni ya UWAVITA**

Umoja huu ulianzishwa kwa madhumuni yafuatayo:

(i) Kutetea na kusimamia haki na masilahi ya waandishi wa vitabu vya Kiswahili;

(ii) Kuandaa warsha za kuwaelimisha waandishi kuhusu uandishi bora wa vitabu;

(iii) Kuandaa na kuwajulisha waandishi kuhusu mada mbalimbali zinazotakiwa kuandikiwa kulingana na mwelekeo na uhitaji wa jamii;



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 88 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



(iv) Kukitangaza Kiswahili kwa njia ya mijadala na semina kupitia vyombo vya habari; na
(v) Kuamsha ari ya kusoma vitabu vya lugha ya Kiswahili.

**Mafanikio ya UWAVITA**

Yafuatayo ni mafanikio ambayo UWAVITA umeyapata tangu kuanzishwa kwake:
(i) Kuendesha semina mbalimbali kwa waandishi wa vitabu vya Kiswahili;
(ii) Kuongeza vitabu vya fani mbalimbali za Kiswahili kama vile vitabu vya hadithi za watoto, riwaya, tamthiliya, ushairi, na tahakiki; na
(iii) Kuandaa na kushiriki maonesho ya vitabu na kuhamasisha usomaji wa vitabu.

**Changamoto za UWAVITA**

Changamoto zilizoikabili UWAVITA ni:
(i) Uhaba wa fedha kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Chanzo cha mapato ya UWAVITA ni michango ya wanaumoja ambayo haitoshelezi mahitaji ya chama.
(ii) Mwamko mdogo wa kusoma vitabu katika jamii ya Watanzania. Hali hii huwakatisha tamaa waandishi kuendelea kuandika vitabu.
(iii) Kutokuwepo kwa umoja na mshikamano miongoni mwa waandishi na wachapishaji. Baadhi ya waandishi hawakujiunga na UWAVITA, hali ambayo inadhoofisha nguvu ya umoja.

## Zoezi la 3.3

1. Tathmini mchango wa vyombo vya habari vya sasa katika maendeleo ya lugha ya Kiswahili.
2. Bainisha namna wamisionari walivyokuwa nyenzo ya kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili.
3. Kwa kutumia mifano, eleza changamoto zinazoyakabili maendeleo ya Kiswahili katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa sasa.
4. Jadili mafanikio na changamoto zinazozikumba asasi mbalimbali za kukuza na kueneza Kiswahili nchini Tanzania baada ya uhuru.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 89 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Maendeleo ya Kiswahili nchini Kenya baada ya uhuru**

Kenya ilipata uhuru mwaka 1963 kutoka kwa Waingereza. Mara baada ya uhuru, Kiswahili kilitangazwa kuwa lugha ya taifa nchini humo mwaka 1963, ingawa hakukuwa na sera na sheria iliyohalalisha Kiswahili kuwa lugha ya taifa. Wakenya walikubali Kiswahili kuwa lugha yao ya mawasiliano, biashara, na utawala.

Rais wa kwanza wa Kenya alikuwa na nia ya kukuza na kueneza Kiswahili. Hili lilidhihirika wazi alipohutubia kwa lugha ya Kiswahili wakati wa ufunguzi wa Bunge la Jamhuri tarehe 14.12.1964. Ingawa hapakuwa na sera na sheria ambazo zilihalalisha Kiswahili kuwa lugha ya taifa, Rais Jomo Kenyatta alitoa tangazo la kusisitiza kuwa Kiswahili ni lugha ya taifa mwaka 1974. Tamko hilo lilihimiza matumizi ya Kiswahili katika shughuli za kiserikali likiwamo Bunge. Mnamo Julai mwaka 1974, Bunge lilipitisha uamuzi wa kutumia lugha ya Kiswahili katika vikao vyake. Rais Jomo Kenyatta alitumia lugha ya Kiswahili kila alipofanya mikutano na wananchi mijini na vijijini. Kupitia hotuba zake kwa Wakenya, Rais alitia hamasa kwa watu wa Kenya kuendelea kujifunza lugha ya Kiswahili. Juhudi za kurasimisha Kiswahili kuwa lugha ya taifa zimeendelea kuzaa matunda ambapo mwaka 2010 katika mabadiliko ya katiba Kiswahili kilitambuliwa kuwa lugha ya taifa katika ibara ya saba ya katiba hiyo.

Hatua nyingine ya mafanikio ilikuwa ni matumizi ya lugha ya Kiswahili katika elimu. Mwaka 1963 serikali iliunda tume ya kutafiti lugha inayofaa kutumika katika elimu. Lengo kuu lilikuwa ni kukusanya maoni kutoka kwa wananchi kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili au lugha nyingine katika elimu. Tume hiyo, ilipeleka mapendekezo kuwa Kiswahili kifundishwe kama somo bila kutahiniwa. Mapendekezo mengine yalikuwa ni pamoja na kuanzishwa kwa Idara ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Nairobi, kuendesha mafunzo maalumu ya lugha ya Kiswahili kwa walimu wa shule za msingi, na kufundisha kozi maalumu za Kiswahili kwa wakufunzi wa vyuo vya ualimu.

Tume nyingine zilizoundwa ni ya Wamalwa mwaka 1970, Gachathi mwaka 1976 na Mackay mwaka 1981 - 1982. Tume ya Wamalwa ilipendekeza kozi za Kiswahili zianzishwe katika taasisi ya usimamizi wa watumishi, na taasisi ya kutoa mafunzo kwa watumishi wa umma. Tume ya Gachathi ilipendekeza Kiswahili kiwe somo la lazima na la kutahiniwa katika shule za msingi, upili na vyuo vikuu. Pia, ilipendekeza utoaji wa mafunzo ya Kiswahili kwa walimu



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 90 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


wa Kiswahili.Tume ya Mackay ilipendekeza Kiswahili kiwe somo la lazima katika shule za msingi na sekondari kote nchini, ambapo agizo hilo lilitekelezwa na matokeo yake Kiswahili kiliweza kukua na kuenea miongoni mwa Wakenya wengi. Hali kadhalika, tume hii ilipendekeza kuanzishwa kwa Chuo cha Upili na Kiswahili kifundishwe chuoni kama somo la lazima. Baadhi ya mapendekezo ya tume hizo yametekelezwa kwa ufanisi kuanzia mwaka 1985. Kiswahili kilifanywa kuwa somo la lazima la kutahiniwa katika shule za msingi na za upili. Kwa hiyo, mwanafunzi hutakiwa kupata alama za juu katika somo hilo ili aweze kujiunga na shule ya upili, vyuo vya mafunzo au vyuo vikuu.

Mafanikio mengine ya kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Kenya yalionekana kupitia vyombo vya habari. Baada ya uhuru, matangazo ya redio na televisheni yalianza kutolewa kwa Kiswahili. Kwa upande wa redio, Shirika la Utangazaji la Kenya (KBC) linalomiliki Radio ya KBC – Nairobi ambayo hutangaza kwa Kiswahili lilianzishwa. Radio ya KBC – Nairobi imekuwa na kipindi maalumu cha lugha ya Kiswahili kinachoitwa *Lugha Yetu*. Kipindi hiki hutoa elimu kuhusu matumizi sahihi ya lugha ya Kiswahili. Kituo kingine cha redio ambacho hutangaza kwa Kiswahili ni *Radio Citizen*.

Kwa upande wa televisheni, Shirika la Utangazaji Kenya lina vituo vya KBC Runinga 1 na KBC Runinga 2 ambavyo hurusha matangazo yake kwa lugha ya Kiswahili. Televisheni nyingine ambayo hurusha matangazo kwa Kiswahili ni televisheni ya Citizen na runinga ya K24. Televisheni nchini Kenya zimekuwa na vipindi mbalimbali vya mijadala ya Kiswahili, ambavyo vina watazamaji na wasikilizaji wengi. Kupitia televisheni, Kiswahili kimekua na kuenea kwa kiwango kikubwa.

Magazeti pia yamesaidia kukuza na kueneza Kiswahili nchini Kenya. Mwaka 1975 serikali iliasisi mradi mkubwa wa kuandaa gazeti linaloitwa *Kisomo* ambalo lilikuwa linaandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Gazeti hili lilichapishwa katika mji wa Mrunga na lilikuwa maalumu kwa ajili ya watu wa mashambani. Nakala elfu tano za gazeti hili zilitolewa kila mwezi. Mradi huu ulikua na kuendelea kiasi kwamba kufikia mwaka 1980 kukawa na magazeti zaidi ya 11 yaliyosomwa katika sehemu kubwa ya Kenya. Miongoni mwa magazeti hayo ni *Nyota ya Magharibi*, *Sauti ya Pwani*, *Sauti ya Gasi*, *Nyota ya Mashariki*, *Maarifa*, *Habari*,


PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 91 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*Sauti ya Kericho, Mwongozo, Jicho,* na *Nuru*. Magazeti mengine ambayo hutumia lugha ya Kiswahili ni *Taifa Leo, Kenya Leo, Taifa la Pili* na *Baraza*. Sambamba na hilo, kumekuwa na matumizi makubwa ya lugha ya Kiswahili katika mitandao ya kijamii. Kupitia magazeti na mitandao ya kijamii, watu wengi wamejifunza, na kuendeleza hadhi ya lugha ya Kiswahili nchini Kenya.

**Vyombo vya kukuza na kueneza Kiswahili Kenya**

Baada ya uhuru, serikali ya Kenya ilichukua hatua mbalimbali za kukuza na kueneza Kiswahili kwa kuunda vyombo mbalimbali. Vyombo hivyo vilianzishwa na serikali, watu binafsi, na taasisi mbalimbali. Vyombo hivyo ni kama vile *Chama cha Kiswahili cha Taifa (CHAKITA)* na Idara mbalimbali za Vyuo Vikuu nchini Kenya. Miongoni mwa idara hizo ni: *Idara ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Kenyatta, Idara ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Nairobi, Chama cha Walimu wa Kiswahili Mkoa wa Nairobi,* na *Chama cha Kiswahili Chuo Kikuu cha Mount Kenya.*

**Chama cha Walimu wa Kiswahili Mkoa wa Nairobi**

Chama hiki kilianzishwa mwaka 1975 mjini Nairobi kikijumuisha walimu wa somo la Kiswahili wa mkoa huo. Mpango wa kuanzisha chama hicho ulifanywa kwa lengo la kuhamasisha wanafunzi wengi kusoma somo la Kiswahili. Walimu hawa walijipa jukumu la kukikuza na kukitukuza Kiswahili. Malengo mengine ya chama hiki yalikuwa haya yafuatayo:

(i) Kuwakutanisha walimu wa Kiswahili ili kujadili na kutafuta njia za kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili;

(ii) Kutunga majaribio na mitihani ya somo la Kiswahili kwa shule za sekondari;

(iii) Kuwashirikisha wanafunzi katika shughuli za kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili; na

(iv) Kutoa mafunzo mbalimbali kwa walimu na wakufunzi ili kupata ujuzi wa kufundisha lugha ya Kiswahili.

**Mafanikio ya Chama**

Chama kilipata mafanikio yafuatayo:

(i) Chama kimefanikiwa kufundisha walimu lugha ya Kiswahili na kuwapa ujuzi wa juu katika kufundisha na kuzungumza. Kupitia mafunzo haya, walimu walipata moyo na maarifa zaidi katika lugha ya Kiswahili.

(ii) Chama kimeongeza ufaulu wa somo la Kiswahili kwa wanafunzi wa mkoa


PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 92 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


wa Nairobi ukilinganisha na masomo mengine. Hatua hii iliwahamasisha wanafunzi wengine kusoma Kiswahili.

(iii) Kuanzisha mashindano ya sanaa ya lugha ambayo hufanyika mwezi Juni kila mwaka. Mashindano haya huhusisha usomaji na mazungumzo ya papo kwa papo. Katika mashindano haya, tuzo maalumu hutolewa kwa wanafunzi wanaofanya vizuri.

**Changamoto za Chama**

Pamoja na mafanikio, Chama kilikabiliwa na changamoto zifuatazo:

(i) Kuhamishwa mara kwa mara kwa walimu wa Kiswahili kwenda nje ya Mkoa wa Nairobi;

(ii) Upungufu mkubwa wa walimu wa lugha ya Kiswahili kulinganisha na idadi za shule na wanafunzi wanaosoma lugha ya Kiswahili; na

(iii) Uhaba wa fedha kwa ajili ya kuendeshea shughuli za chama.

**Idara ya Kiswahili na Lugha za Kigeni Chuo Kikuu cha Kenyatta**

Idara hii ilianzishwa mwaka 1987 ambapo lengo mojawapo lilikuwa ni kufundisha lugha ya Kiswahili. Idara hii hutoa shahada za Kiswahili na kufanya tafiti mbalimbali kuhusu lugha ya Kiswahili na lahaja zake.

**Madhumuni ya Idara**

Madhumuni ya idara hii yalikuwa:

(i) Kufundisha na kuandaa wataalamu mbalimbali kwa ajili ya kufundisha somo la Kiswahili katika shule na vyuo nchini Kenya;

(ii) Kufanya tafiti mbalimbali kuhusu lugha ya Kiswahili na lahaja zake;

(iii) Kushirikiana na idara za serikali na za binafsi katika kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili; na

(iv) Kuchapisha vitabu vya lugha ya Kiswahili kwa ajili ya matumizi ya shule na wageni wanaojifunza Kiswahili.

**Mafanikio ya Idara**

Idara ilipata mafanikio yafuatayo:

(i) Kuanzisha maktaba maalumu ya vitabu na machapisho ya lugha ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Kenyatta ambayo yalitokana na tafiti mbalimbali;

(ii) Kufungua maabara ya lugha katika Chuo Kikuu cha Kenyatta kwa ajili ya mafunzo na tafiti kuhusu lugha ya Kiswahili;


PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
For Online Use Only
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 93 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(iii) Kuongeza idadi kubwa ya wataalamu wa lugha ya Kiswahili katika shahada mbalimbali; na

(iv) Kuendesha semina mbalimbali kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili kwa wabunge wa bunge la Kenya na maafisa wa serikali.

**Changamoto za Idara**

Idara inakabiliwa na changamoto mbalimbali. Changamoto hizo ni pamoja na:

(i) Mwamko mdogo wa wanafunzi wanaosoma lugha ya Kiswahili ambapo wengi hukimbilia taaluma nyingine na kuona lugha ya Kiswahili ni lugha ya kienyeji.

(ii) Uhaba wa fedha za kuendesha shughuli za idara kama vile semina, warsha, makongamano pamoja na tatifi mbalimbali.

(iii) Baadhi ya wataalamu wa lugha ya Kiswahili kuacha kufanya kazi za Kiswahili na kufanya kazi au shughuli nyingine, kama siasa na biashara.

**Chama cha Kiswahili cha Taifa Kenya (CHAKITA)**

Chama hiki kilianzishwa mwaka 1998 kama jukwaa la wapenzi wa Kiswahili wakiwamo wahadhiri na walimu kwa ajili ya kubadilishana maarifa kuhusu lugha ya Kiswahili kwa maendeleo ya taifa.

**Madhumuni ya Chama**

Madhumuni ya CHAKITA yalikuwa ni:

(i) Kuhakikisha Kiswahili kinakua na kuenea ndani na nje ya Kenya;

(ii) Kutoa vitabu na machapisho mbalimbali ya lugha ya Kiswahili;

(iii) Kushirikiana na serikali katika masuala ya kukuza na kueneza Kiswahili pamoja na kutoa msaada wa kitaaluma; na

(iv) Kuendesha semina, warsha na makongamano kuhusu lugha ya Kiswahili.

**Mafanikio ya Chama**

CHAKITA kilipata mafanikio yafuatayo:

(i) Kutafsiri na kutoa misaada mingine ya kitaaluma kwa serikali na taasisi nyingine za umma na binafsi; na

(ii) Kuendesha warsha na makongamano ya Kiswahili.

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 94 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



**Changamoto za CHAKITA**

CHAKITA kilipata changamoto zifuatazo:

(i) Kiswahili kutopewa hadhi kama ilivyo kwa lugha za jamii na Kiingereza.

(ii) Uhaba wa fedha za kuendesha shughuli mbalimbali za Chama.

**Changamoto za ukuzaji na uenezaji wa Kiswahili nchini Kenya**

Pamoja na juhudi zilizofanyika, kumekuwa na changamoto mbalimbali kuhusu maendeleo ya Kiswahili nchini Kenya. Kwanza, Kiingereza kimeendelea kutumika zaidi kuliko Kiswahili katika shule na taasisi mbalimbali za elimu, vyombo vya habari, shughuli za kiserikali, na katika mawasiliano ya kila siku. Pili, bado kuna upinzani kutoka katika lugha za jamii. Tatu, kutokuwepo kwa chombo maalumu cha kusimamia maendeleo ya Kiswahili.

## Zoezi la 3.4

1. Bainisha mambo yaliyosababisha kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Kenya baada ya uhuru.
2. Jadili changamoto zilizotokea wakati wa kukuza na kueneza Kiswahili nchini Kenya.
3. Eleza jinsi unavyoweza kutatua changamoto zinazokikabili Chama cha Kiswahili cha Kenya.
4. Ukipewa nafasi ya kuishauri serikali ya Kenya kuhusu kukuza na kueneza Kiswahili, utaishauri mambo gani? Toa hoja tano.

**Kukua na kuenea kwa lugha ya Kiswahili nchini Uganda baada ya uhuru**

Uganda ilipata uhuru tarehe 9/10/1962 kutoka kwa utawala wa Kiingereza. Tofauti na nchi zingine za Afrika Mashariki, matumizi ya Kiswahili nchini Uganda yalikuwa madogo sana. Hadhi ya lugha haikuwa dhahiri ingawa Kiswahili kilikuwa kikizungumzwa na baadhi ya watu kama Lugha ya pili (L2). Pia, Kiswahili kilikuwa hakifundishwi sana.

Mara baada ya uhuru, Uganda ilikabiliwa na tatizo la kuchagua lugha ya taifa, ambapo haikuwa rahisi kwani kulikuwa na mvutano baina ya makundi ya wananchi kuhusu lugha inayofaa. Rais Milton Obote wa Chama cha Uganda Peoples' Congress (UPC) alikusudia kukifanya Kiswahili kuwa lugha ya

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 95 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

taifa kama ilivyokuwa kwa Tanzania na Kenya. Hata hivyo, lengo la Rais Obote halikufanikiwa kutokana na upinzani kutoka kwa chama cha Kabaka Yekka kilichopendelea lugha ya Kiganda itumike. Lugha ya Kiganda ilikuwa ikifundishwa na kutumika zaidi katika vyombo vya habari, na mawasiliano ya kawaida kuliko Kiswahili na lugha nyingine za makabila ya Uganda. Katika kipindi hicho, Kiswahili kilibaki kuwa lugha ya askari polisi na wanajeshi.

Kutokana na kukosekana kwa mwafaka kati ya vyama vya UPC na Kabaka Yekka, utawala wa Milton Obote haukutambua lugha ya Kiswahili kama lugha rasmi. Kila kabila lilitumia lugha yake katika shughuli za kiutawala. Suala hili lilichangiwa zaidi na utawala wa machifu waliokuwa na nguvu za kukumbatia na kusimamia misingi ya tamaduni zao za jadi. Hata hivyo, Kiganda ndiyo lugha iliyokuwa na nafasi kubwa ya kutumika kuliko lugha nyingine za makabila. Aidha, Kiingereza kilitumika sambamba na Kiganda.

Hadhi ya Kiswahili ilianza kubadilika baada ya Idi Amini Dada kushika madaraka ya nchi mwaka 1971, ambapo alijaribu kutangaza Kiswahili kitumike kama lugha ya taifa kwa sababu aliona kuwa Kiswahili kingefaa kuwaunganisha Waganda wote. Pamoja na Kiswahili kupendwa na wananchi, serikali haikutunga sera kuhusu matumizi ya lugha hii. Hata hivyo, Kiswahili kiliendelea kutumiwa na askari pamoja na wanajeshi na kufundishwa katika shule chache kama somo. Hatua nyingine ilikuwa ni kuanzishwa kwa idhaa ya Kiswahili katika redio Uganda mwaka 1971. Idhaa hii ilikuwa chini ya Idara ya Matangazo ya Nje. Matangazo ya Kiswahili katika Idara ya Matangazo ya Ndani yaligawanywa kati ya Idhaa ya Taifa na Idhaa ya Mamboleo. Idhaa hizi zilitangaza vipindi kama vile *Hodi Hodi Mitaani, Darubini, Kwa Akina Mama, Burudikeni Shoo, Porojo za Mjomba, Dunia Wiki Hii, Jifunze na Uburudike, Usiku Mwema,* na *Michezo*.

Baada ya Rais Yoweri Museveni kuingia madarakani mwaka 1986, Kiswahili kilipata mwamko mpya na kasi ya kuenea hasa mijini. Rais Museveni amekuwa akitumia Kiswahili katika mikutano yake ya hadhara. Hadhi ya Kiswahili ilipanda zaidi kuanzia mwaka 2005 baada ya bunge kupiga kura na kuamua Kiswahili kuwa lugha rasmi sambamba na Kiingereza. Kiswahili kimekuwa kikitumika katika kampeni za uchaguzi na mawasiliano ya kiofisi na kibiashara. Kiswahili kimeingizwa katika mfumo wa elimu ambapo kinafundishwa katika shule zote za msingi, vyuo vya ualimu na vyuo vikuu. Vyuo vikuu vinavyofundisha Kiswahili nchini Uganda ni Chuo Kikuu cha Makerere, *Chuo Kikuu cha Kiislamu, Chuo Kikuu cha Kyambogo* na *Chuo Kikuu cha Kampala*. Aidha, Baraza la Mitihani la



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 96 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Taifa limekuwa likitahini somo la Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za msingi na za sekondari.

**Changamoto za kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Uganda**

Kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Uganda kumekumbwa na changamoto zifuatazo:

(i) Upinzani kati ya Kiganda na Kiswahili. Lugha hizi zimekuwa zikishindania hadhi ya kitaifa ambapo Kiganda kimekuwa kikipewa kipaumbele kwa sababu ni lugha ya wazawa na kabila kubwa miongoni mwa makabila ya Uganda;

(ii) Kukosekana kwa sera madhubuti kuhusu lugha ya Kiswahili kama ilivyo kwa nchi nyingine za Afrika Mashariki. Hali hii imedhoofisha hadhi ya Kiswahili;

(iii) Kutokuwepo kwa asasi au taasisi na vyombo maalumu vya kukuza na kueneza Kiswahili; na

(iv) Kutokuwepo kwa vyombo vya habari vingi vinavyotumia lugha ya Kiswahili.

Kwa ujumla, Kiswahili kinazidi kuwavutia wananchi wengi wa Uganda, hasa baada ya kuwa lugha ya pili rasmi. Vilevile, Kiswahili kinazidi kustawi na kuimarika nchini Uganda kwa kuwa Kiswahili ni lugha ya kikazi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo Uganda ni mwanachama. Kwa hiyo, Kiswahili kitazidi kukua na kusitawi nchini Uganda.

## Zoezi la 3.5

1. Jadili mambo yaliyosababisha kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Uganda.
2. Eleza changamoto zilizoikumba Uganda katika kukuza na kueneza Kiswahili.
3. Pendekeza hatua ambazo serikali ya Uganda inapaswa kuchukua ili kukuza na kueneza Kiswahili nchini humo.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 97 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kukua na kuenea kwa Kiswahili duniani**

Kutokana na kukua kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni, lugha ya Kiswahili imekuwa lugha muhimu ya mawasiliano. Hali hii imefanya Kiswahili kukua na kuenea kwa kiwango kikubwa duniani. Hapo awali, Kiswahili kilitumika sana Pwani ya Afrika ya Mashariki na baadaye kuenea ndani na nje ya Afrika ya Mashariki na kuvuka ng'ambo ya Afrika. Kukua na kuenea kwa Kiswahili duniani kunajidhihirisha katika mambo yafuatayo:

***1 K iswahili katika elimu***

Kiswahili kinafundishwa katika nchi nyingi duniani. Nchi mbalimbali barani Afrika na duniani zimeanzisha programu ya somo la Kiswahili katika vyuo vikuu na kwenye taasisi zake za lugha za kigeni. Nchi hizi ni pamoja na Sudani, Botswana, Namibia, Ghana, Afrika Kusini, Burundi, Rwanda, Comoro, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Zambia, Msumbiji, Somalia, Malawi, Zimbabwe, na Libya. Nchi nyingine zinazofundisha Kiswahili duniani ni Uingereza, Japan, Ujerumani, Korea Kusini, Marekani, Kanada, China na Saudi Arabia. Baadhi ya vyuo vikuu na taasisi zenye programu ya somo la Kiswahili duniani ni:

(i) Chuo Kikuu cha Rwanda (Rwanda);
(ii) Chuo Kikuu cha Bujumbura (Burundi);
(iii) Chuo cha Jeshi cha Bujumbura (Burundi);
(iv) Chuo Kikuu cha Ghana (Ghana);
(v) Taasisi ya Elimu ya Ghana (Ghana);
(vi) Chuo Kikuu cha Botswana (Botswana);
(vii) Chuo Kikuu cha Kwa-Zulu Natal (Afrika Kusini);
(viii) Chuo Kikuu cha Sebha (Libya);
(ix) Chuo Kikuu cha Wisconsin – Maddison (Marekani) – Idara ya Lugha za Kiafrika na Fasihi;
(x) Chuo Kikuu cha Havard (Marekani) - Idara ya Masomo ya Kiafrika na Kiafro – Amerika;
(xi) Chuo Kikuu cha Howard (Marekani) – Idara ya Masomo ya Kiafrika;
(xii) Chuo Kikuu cha Ohio (Marekani) – Idara ya Masomo ya Kiafrika - Amerika;
(xiii) Chuo Kikuu cha London (Uingereza) – Shule Kuu ya Taaluma za Mashariki ya Mbali na Kiafrika;



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 98 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



(xiv) Chuo Kikuu cha Lugha za Kigeni cha Beijing (China) – Idara ya Afrika;

(xv) Chuo Kikuu cha Lugha za Kigeni Hankuk (Korea Kusini) - Idara ya Kiswahili;

(xvi) Chuo Kikuu cha Lugha za Kigeni cha Tokyo (Japan) - Idara ya Lugha na Utamaduni wa Asia na Afrika;

(xvii) Chuo Kikuu cha Bayreuth (Ujerumani); na

(xviii) Chuo Kikuu cha Zimbabwe (Zimbabwe).

Mbali na Kiswahili kufundishwa katika taasisi mbalimbali duniani, vilevile kuna majarida ya kitaaluma ya kimataifa ambayo huchapisha makala zinazohusu Kiswahili na taaluma zake. Miongoni mwa majarida hayo ni *Swahili Forum* (Ujerumani), Nordic *Journal of African Studies* (Uswidi), *Mulika*, *Kioo cha Lugha na Kiswahili* (TATAKI - Chuo Kikuu cha Dar es Salaam) na *Journal of Humanities* (Shule Kuu ya Sanaa na Lugha – Chuo Kikuu cha Dodoma).

***2K iswahili katika vyomb v ya habr i***

Vyombo mbalimbali vya habari vinavyotangaza kwa Kiswahili vimesaidia kukuza na kueneza Kiswahili duniani. Vyombo hivyo vina vipindi vya redio na televisheni ambavyo husikika sehemu mbalimbali duniani. Vifuatavyo ni baadhi ya vyombo hivyo:

(i) Idhaa ya Kiswahili ya Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC);

(ii) Idhaa ya Kiswahili ya Sauti ya Amerika (VOA);

(iii) Idhaa ya Kiswahili ya Shirika la Utangazaji la Ufaransa (RFI);

(iv) Idhaa ya Kiswahili ya Shirika la Utangazaji la Ujerumani (DeutscheWelle-DW);

(v) Idhaa ya Kiswahili ya Radio Tehran (Iran);

(vi) Idhaa ya Kiswahili ya Radio Japan;

(vii) Idhaa ya Kiswahili ya Radio India;

(viii) Idhaa ya Kiswahili ya Radio China;

(ix) Idhaa ya Kiswahili ya Radio Vatican;

(x) Idhaa ya Kiswahili ya UN Radio;

(xi) Idhaa ya Kiswahili Radio Cairo; na

(xii) Radio Sudani.

Aidha, kuna vyombo vingine vya habari kama vile redio na televisheni katika nchi za Kiafrika ambazo ni *Radio Rwanda* ambayo imekuwa ikitangaza kwa

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kiswahili tangu mwaka 1961. Redio hii hutangaza taarifa ya habari, taarifa za mpira na salamu za wasikilizaji. Hali kadhalika, nchini Burundi kuna *Radio Burundi*, *Ibyizigiro* na *Isanganiro* na televisheni ambazo hutangaza vipindi kama vile *habari*, *utamaduni*, *mafunzo*, na *michezo*. Vilevile, nchini Comoro kuna *Radio Comoro* ambayo hutoa matangazo yake kwa Kiswahili.

### *3 K iswahili katika b ashara za kimataifa na utalii*

Kukua kwa utandawazi duniani kumesababisha kuwa na uhusiano mkubwa baina ya nchi nyingi duniani. Biashara ni jambo mojawapo linalosababisha uhusiano baina ya nchi. Nchi nyingi duniani zimesaini mikataba ya biashara za kimataifa. Mikataba hii huruhusu nchi hizo kuwa na vituo maalumu vya kibiashara. Vituo hivyo hukutanisha watu wa mataifa mbalimbali na miongoni mwa lugha ambazo hutumika kuwaunganisha ni Kiswahili. Baadhi ya vituo hivyo hupatikana katika miji ya Beijing (China), Dubai (Falme za Kiarabu), Moscow (Urusi), New York (Marekani), London (Uingereza), na Adis Ababa (Ethiopia).

Mbali na vituo hivyo, wafanyabiashara na watalii kutoka sehemu mbalimbali za dunia wamekuwa wakitembelea Tanzania, Kenya na Uganda ambapo hujifunza na kutumia Kiswahili. Watu hawa wanaporudi katika nchi zao hueneza Kiswahili. Kwa mfano, wafanyabiashara kutoka China hujifunza Kiswahili ili waweze kuwasiliana na wafanyabiashara wa Kitanzania. Pia, inawezekana kukutana na Mchina akiongea Kiswahili pindi akutanapo na mtumiaji wa Kiswahili nchini China.

### *4K iswahili katika uhusiano na ushirikiano wa kimataifa*

Kiswahili ni miongoni mwa lugha chache ambazo zimepata nafasi kutumika katika vikao na shughuli za kidiplomasia barani Afrika na duniani kote. Katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo hujumuisha nchi sita, Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi na Sudani Kusini, Kiswahili hutumika katika mikutano ya jumuiya hiyo likiwamo Bunge la Afrika Mashariki. Pia, Jumuiya ya Afrika Mashariki imeanzisha Kamisheni ya Kiswahili kwa lengo la kukuza Kiswahili kwa ajili ya maendeleo na ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika nyanja za kielimu, kisayansi, kijamii, kiutamaduni na kiteknolojia katika nchi wanachama. Makao makuu ya Kamisheni ya Kiswahili yako Zanzibar.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 100 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Katika Umoja wa Afrika ambao unajumuisha nchi wanachama zaidi ya 53 za Afrika, Kiswahili ni miongoni mwa lugha rasmi ambazo hutumika katika mikutano na vikao vya umoja huo tangu mwaka 2004. Vilevile, Kiswahili ni miongoni mwa lugha ambazo zimekuwa zikitumika katika shughuli za uliokuwa Umoja wa Nchi Huru za Afrika tangu miaka ya 1970.

Mashirika ya Umoja wa Mataifa kama vile UNESCO, UNHCR, na UNICEF hutumia Kiswahili kama lugha mojawapo ya kazi na katika kuchapisha habari mbalimbali. Kama tulivyoeleza katika sehemu iliyotangulia, Umoja wa Mataifa pia umeanzisha idhaa ya Kiswahili ya redio ya Umoja wa Mataifa ambayo imesaidia kukua na kuenea kwa Kiswahili. Matumizi ya Kiswahili katika mashirika haya, huipa lugha hii adhama na nafasi ya kufahamika katika nchi mbalimbali duniani.

***5K iswahili katika intaneti***

Katika zama hizi za utandawazi, kumekuwa na mapinduzi makubwa ya mawasiliano duniani. Mawasiliano hufanyika katika mifumo maalumu ya kompyuta na simu ambayo huwezeshwa na intaneti. Katika mfumo huu, watu huweza kupata na kusambaza habari popote duniani. Mapinduzi hayo yamesababisha kuibuka kwa mitandao mbalimbali duniani. Mitandao hiyo ni kama vile *Facebook*, *Twitter*, *Instagram*, *WhatsApp*, *Imo*, *Viber*, *Skype*, na *Simu ya Maandishi* (Telegramu). Mitandao mingine ni *tovuti* na *blogu*. Mitandao hii huunganisha watu duniani kote. Aidha, kuna programu za kompyuta zinazotumia lugha ya Kiswahili. Programu hizo ni *Linux Operating System, Jambo Open Office, Kiolesura Fungasha Kiswahili cha Windows XP,* na *Swahili Language Manager Program* (SALAMA). Hali kadhalika, mwaka 2005 kampuni ya *Microsoft* ilianzisha kamusi maalumu ya kutumia lugha ya Kiswahili katika kompyuta. Katika intaneti kuna programu za kutafsiri Kiswahili (*google translator*) ambazo huwezesha kutafsiri kutoka lugha ya Kiswahili kwenda lugha nyingine na kutoka lugha nyingine kwenda Kiswahili. Kupitia mitandao hii, watu huweza kusoma magazeti, kusikiliza redio na kutazama televisheni za Kiswahili popote pale duniani kwa msaada wa intaneti.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 101 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### *6K iswahili katika sanaa*

Lugha ya Kiswahili imepata umaarufu mkubwa duniani katika tasnia za muziki na filamu. Baadhi ya wanamuziki wa kimataifa wametumia maneno ya Kiswahili katika kutoa ujumbe wa nyimbo zao. Baadhi ya wanamuziki hao ni Harry Belafonte (Carribean), bendi ya Osibisa (Nijeria), Miriam Makeba (Afrika Kusini), Leon Bukasa, Luambo Makiadi, Ilunga wa Ilunga, Pepe Kale, Sam Mangwana (Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo), Michael Jackson (Marekani), Bonney M (Ujerumani na Swiden), Lionel Richie (Marekani), na Rocco Granata (Italia). Baadhi ya wanamuziki wa Afrika Mashariki wameweza kushirikiana na wanamuziki wa nchi nyingine duniani kuimba nyimbo za Kiswahili. Mwanamuziki Naseeb Abdul (Diamond Platinumz – Tanzania) ameshirikiana na Mafikizolo (Afrika Kusini) katika wimbo wa *Colours of Africa*; Davido (Nigeria) katika wimbo wa *Number One*; Peter na Paul Okoye (P-Square) katika wimbo wa *Kidogo;* na Ne-yo (Marekani) katika wimbo wa *Marry You*.

Aidha, mwanamuziki Ali Kiba (Tanzania) akiwa na kundi la Nyota wa Afrika, walishirikiana na Robert Kelly (R-Kelly – Marekani) kuimba wimbo wa pamoja unaojulikana kama *Hands Across the World*. Vilevile, Ali Kiba aliimba na Justine Bieber (Canada) wimbo unaoitwa *Collaboration*. Wanamuziki wengine ni Josee Chameleone (Uganda) na Jaguar na Prezzo (Kenya) ambao wameimba nyimbo za Kiswahili ambazo zimesikika nje ya mipaka ya Afrika. Baadhi ya nyimbo hizo ni *Walewale, Jamila, Tubonge na Naumia* (Josee Chameleone); *Ndoto, Kigeugeu* na *Huu Mwaka* (Jaguar) na *Nataka Tupendane* na *Mrembo* (Prezzo). Mwanamuziki mkongwe wa Afrika Kusini, Miriam Makeba (Mama Afrika) aliimba wimbo maarufu sana ulimwenguni kwa lugha ya Kiswahili ambao unaitwa *Malaika*.

Kwa upande wa filamu, baadhi ya wasanii wa Afrika Mashariki wameshirikiana na wasanii wengine duniani. Kwa mfano, marehemu Steven Kanumba alishirikiana na waigizaji wa Nijeria katika filamu za *Dar to Lagos, She is my Sister* na *Devil Kingdom*. Filamu nyingine yenye maneno ya Kiswahili ni *Disney* (The Lion King) ambayo iko katika mtindo wa vibonzo na hupendwa sana na watoto. Maneno ya Kiswahili katika filamu hii ni *simba*, *hakuna matata* na *rafiki*. Kwa ujumla, wasanii wamesaidia kukuza na kueneza Kiswahili duniani.

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 102 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


*7V yama na taasisi za kukuza na kueneza Kiswahili duniani*

Vyombo mbalimbali vimeanzishwa kwa ajili ya kutimiza azma ya kukuza na kueneza Kiswahili duniani. Baadhi ya vyombo hivyo ni Chama cha Kiswahili cha Afrika (CHAKA), Chama cha Kiswahili Afrika Mashariki (CHAKAMA), Chama cha Ukuzaji Kiswahili Duniani (CHAUKIDU), na Kamisheni ya Kiswahili ya Jumuiya Afrika ya Mashariki.

**Chama cha Kiswahili cha Afrika (CHAKA)**

Chama hiki kiliundwa mwezi Mei, mwaka 1980 baada ya semina ya pili ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili iliyofanyika katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Semina hizo zilifadhiliwa na UNESCO na SIDA. Mkutano wa kwanza wa kuzindua rasimu ya katiba ya chama hiki ulifanyika tarehe 19/05/1980 katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Chama hiki kiliundwa na wajumbe kutoka nchi zipatazo tisa zilizohudhuria katika semina zote mbili. Nchi hizo ni Tanzania, Burundi, Rwanda, Uganda, Kenya, Msumbiji, Madagaska, Sudani, na Somalia. Chama hiki kilikuwa na lengo la kukuza na kueneza Kiswahili ndani na nje ya Tanzania.

**Madhumuni ya CHAKA**

Yafuatayo yalikuwa ni madhumuni ya kuanzishwa kwa CHAKA:

(i) Kuanzisha vyama vya Kiswahili kwa kila taifa ambalo ni mwanachama wa Chama hiki;

(ii) Kuandaa vituo vya utafiti ili kuweza kukusanya data za lugha ya Kiswahili kadiri ya mahitaji ya jamii;

(iii) Kuendesha mikutano na semina za kimataifa kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa wakuzaji wa lugha ya Kiswahili na wadau wengine kama vile walimu, watangazaji na watumishi wa serikali; na

(iv) Kuchapisha nyaraka zenye taarifa za maendeleo ya chama na kijarida cha Kiswahili kinachoitwa CHAKA na kusambaza kwa wajumbe na nchi wanachama.

**Mafanikio ya CHAKA**

Chama hiki kilipata mafanikio yafuatayo:

(i) Kukutanisha wajumbe wengi kutoka nchi nyingi za Afrika katika mikutano na semina zake;

(ii) Kutoa jarida la CHAKA ambalo limekuwa na mchango mkubwa kuelezea maendeleo ya lugha ya Kiswahili katika nchi mbalimbali; na


PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

For Online Use Only

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 103 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(iii) Kutoa taarifa za Chama kwa wajumbe kupitia nyaraka mbalimbali zilizohusu Chama.

**Changamoto za CHAKA**

CHAKA kilikumbwa na changamoto zifuatazo:

(i) Ukosefu wa fedha za kuendeshea shughuli za chama na kugharimia vitendea kazi. Chanzo kikuu cha mapato ya CHAKA ilikuwa ni michango ya wanachama ambayo ni dola ishirini kwa mwanachama wa kawaida na dola kumi kwa wanachama ambao ni wanafunzi, ambayo ama haikutolewa kwa wakati, au haikutolewa kabisa.

(ii) Baadhi ya nchi wanachama zilijitoa katika chama. Hali hii ilizorotesha maendeleo ya chama kwa ujumla.

(iii) Kutokuwa na mikakati madhubuti wakati wa kuanzishwa kwa CHAKA.

(iv) Kuwa na wanachama ambao Kiswahili hakikuwa kipaumbele katika nchi zao. Hivyo, walishindwa kukiendeleza kutokana na kukosekana kwa sera na mwamko kuhusu Kiswahili katika nchi wanachama.

**Chama cha Kiswahili Afrika Mashariki (CHAKAMA)**

Chama hiki kiliundwa katika warsha ya walimu wa Kiswahili wa vyuo vikuu vya Afrika Mashariki ambao walikutana mwezi Julai mwaka 2002, Arusha Tanzania.

**Madhumuni ya CHAKAMA**

Yafuatayo ni madhumuni ya CHAKAMA:

(i) Kuratibu shughuli mbalimbali za tafiti zinazohusu Kiswahili;

(ii) Kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili;

(iii) Kuhamasisha ufundishaji na utumiaji wa lugha ya Kiswahili katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki;

(iv) Kuandaa makongamano, warsha na semina zinazowakutanisha walimu na watafiti ili kubadilishana maarifa na uzoefu;

(v) Kuchapisha jarida la CHAKAMA na machapisho mengine ya kusaidia kueneza taaluma ya Kiswahili;

(vi) Kuandaa machapisho mbalimbali yanayohusu maarifa ya isimu, fasihi na utamaduni kwa ajili ya wanafunzi na walimu; na

(vii) Kuandaa vifaa vya kufundishia na kujifunzia lugha ya Kiswahili kama vile kamusi, vitabu vya lugha na fasihi, kanda za sauti na za video, kanzidata, CD-Rom, na DVD.


PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 104 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



**Mafanikio ya CHAKAMA**

Yafuatayo ni mafanikio ya CHAKAMA katika kukuza na kueneza Kiswahili.

(i) Kuandaa na kuratibu makongamano ya Kiswahili kila mwaka;
(ii) Kuchapisha majarida ya CHAKAMA ambayo yana makala mbalimbali zinazohusu lugha ya Kiswahili;
(iii) Kuwahamasisha wataalamu kufanya tafiti mbalimbali zinazohusu lugha ya Kiswahili; na
(iv) Kuwaunganisha wadau wa lugha ya Kiswahili katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**Changamoto za CHAKAMA**

Zifuatazo ni changamoto ambazo CHAKAMA inakabiliana nazo:

(i) Uhaba wa fedha za kuendeshea shughuli mbalimbali za CHAKAMA kama vile kuratibu makongamano na kugharimia uchapishaji wa majarida;
(ii) Mwitiko mdogo wa wataalamu wa Kiswahili kujiunga na chama;
(iii) Kusuasua kwa michango ya wanachama ambayo ingesaidia katika kuendesha shughuli za chama; na
(iv) Kuwepo kwa utitiri wa vyama vingine vya Kiswahili kwa kila nchi mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo husababisha wanachama kushindwa kujiunga na CHAKAMA kwa kuwa tayari ni wanachama wa vyama vingine.

**Kamisheni ya Kiswahili ya Jumuiya ya Afrika Mashariki**

Kamisheni hii ilianzishwa mwaka 2014 ikiwa ni utekelezaji wa ibara ya 137 ya mkataba wa uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ibara hii imeweka wazi kuwa Kiswahili kitaendelezwa ili kuwa lugha ya mawasiliano katika jumuiya hiyo. Makao makuu ya Kamisheni yako Zanzibar. Jukumu la Kamisheni hii ni kuendeleza usanifishaji na kueneza lugha ya Kiswahili katika jumuiya.

**Madhumuni ya Kamisheni**

Kamisheni ina madhumuni yafuatayo:

(i) Kuishauri Jumuiya ya Afrika Mashariki katika masuala yote yanayohusu Kiswahili;
(ii) Kuratibu na kusimamia kazi za mabaraza ya Kiswahili ya taifa na asasi nyingine zinazohusiana na lugha ya Kiswahili katika nchi wanachama;
(iii) Kuimarisha ushirikiano katika utafiti wa kikanda na kusaidia nchi wanachama kuanzisha vituo vya masomo na tafiti kuhusu lugha ya Kiswahili;



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 105 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(iv) Kuanzisha uhusiano na taasisi na asasi zote zenye malengo ya kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili;

(v) Kuwezesha maendeleo ya sera za Kiswahili katika jumuiya kwa ajili ya ubadilishanaji wa wafanyakazi na wanafunzi katika asasi na taasisi za Kiswahili na kusimamia ufanisi wa sera hizo;

(vi) Kubainisha mahitaji ya mafunzo ya Kiswahili, kuhakiki mitaala na mbinu za ufundishaji, kuangalia zana za ufundishaji, na tafiti;

(vii) Kuhamasisha matumizi ya Kiswahili katika utekelezaji wa shughuli rasmi za umma ndani ya jumuiya; na

(viii) Kupokea na kutekeleza kazi zozote kwa ajili ya kutimiza malengo ya kamisheni kadiri itakavyoelekezwa na Baraza la mawaziri la jumuiya.

**Mafanikio ya Kamisheni**

Tangu kuanzishwa kwake, Kamisheni imepata mafanikio yafuatayo:

(i) Kukuza na kuendeleza Kiswahili katika nchi wanachama. Nchi hizi zinalazimika kutumia Kiswahili katika shughuli mbalimbali;

(ii) Kutoa ushauri kwa waandishi na kuwasaidia kuchapisha vitabu vyao;

(iii) Kuratibu na kuendesha vikao, semina na warsha kwa wanachama wake; na

(iv) Kutoa fursa kwa nchi wanachama kujifunza kuhusu mipango na mikakati ya kukuza na kueneza Kiswahili.

**Changamoto za Kamisheni**

Kamisheni imepata changamoto zifuatazo:

(i) Baadhi ya nchi wanachama kutokuwa na vyombo vya kukuza Kiswahili vinavyoweza kutoa uwakilishi wa kutosha katika kamisheni;

(ii) Mwamko mdogo kwa baadhi ya nchi wanachama kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili; jambo ambalo husababisha ugumu katika kutekeleza malengo ya kamisheni; na

(iii) Baadhi ya nchi wanachama hutoa kipaumbele kwa lugha nyingine katika shughuli za umma kinyume na malengo ya kamisheni.

**Chama cha Ukuzaji wa Kiswahili Duniani (CHAUKIDU)**

CHAUKIDU kilianzishwa mwaka 2012 na walimu wa Kiswahili kutoka maeneo mbalimbali duniani. Makao makuu ya Chama hiki yako nchini Marekani.


PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 106 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


**Madhumuni ya CHAUKIDU**

Yafuatayo ni madhumuni ya CHAUKIDU:

(i) Kuwajumuisha pamoja wakuzaji wa Kiswahili duniani kote kwa lengo la kuchochea ushirikiano miongoni mwao;

(ii) Kukuza matumizi ya Kiswahili katika nyanja zote ambamo lugha hii inatumika, au inaweza kutumika na kuongeza ufanisi wa mawasiliano katika ufundishaji na utafiti wa maarifa ya aina zote, uandishi au utangazaji wa habari, uandishi wa vitabu, uchapishaji vitabu na majarida, utayarishaji wa safari za mafunzo katika Afrika ya Mashariki na Kati, na kadhalika;

(iii) Kusambaza habari na matokeo ya utafiti kwa kutumia machapisho mbalimbali na teknolojia ya mtandao wa kompyuta juu ya vipengele mbalimbali vya Kiswahili na masuala yanayohusiana na Kiswahili;

(iv) Kuwajumuisha wanachama kwa ajili ya kubadilishana mawazo na tajiriba zao katika masuala mbalimbali yanayohusu Kiswahili (kama vile uboreshaji wa ufundishaji, utangazaji, utafiti, uandishi, na kadhalika) kwa njia ya mkutano wa kila mwaka, warsha au semina au kongamano maalumu, na hata kwa njia ya mtandao;

(v) Kuelimisha umma juu ya umuhimu wa kujivunia, kuendeleza, na kuheshimu Kiswahili; na

(vi) Kushauri au kushinikiza serikali za nchi ambamo Kiswahili kina zungumzwa, kutambua thamani iliyobebwa na rasilimali hii, ili kuunda sera mwafaka za kukiendeleza kadri ya uwezo wake kwa manufaa ya maendeleo ya serikali na watu wake kijamii, kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni, kielimu, na kadhalika.

**Mafanikio ya CHAUKIDU**

CHAUKIDU kimekuwa na mafanikio kadhaa tangu kuanzishwa kwake. Mafanikio hayo ni kama yafuatayo:

(i) Kuandaa na kuratibu makongamano na warsha za Kiswahili;

(ii) Kuwakutanisha wataalamu mbalimbali wa Kiswahili duniani;

(iii) Kutoa ufadhili kwa wanafunzi wa vyuo vikuu mbalimbali wa kuhudhuria makongamano ya CHAUKIDU; na

(iv) Kusambaza habari na matokeo ya utafiti kwa kutumia machapisho mbalimbali na teknolojia ya mtandao wa kompyuta juu ya vipengele mbalimbali vya Kiswahili na masuala yanayohusiana na Kiswahili.


PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 107 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Changamoto za CHAUKIDU**

Tangu kuanzishwa kwake, CHAUKIDU kimekuwa na changamoto kadhaa. Miongoni mwa changamoto hizo ni hizi zifuatazo:

(i) Uhaba wa fedha za kuratibu shughuli za umoja;

(ii) Ukosefu wa wanachama kutoka katika baadhi ya maeneo mengine ya ulimwengu ambako lugha ya Kiswahili inafundishwa; na

(iii) Mwitiko hafifu wa serikali za nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika kushirikiana na CHAUKIDU.

## Zoezi la 3.6

1. Eleza kwa mifano mchango wa sekta ya elimu katika kukuza na kueneza Kiswahili duniani.
2. Jadili shughuli za uhusiano wa kimataifa katika kukuza na kueneza Kiswahili duniani.
3. Fafanua mchango wa vyombo vya habari vya kimataifa katika kukuza na kueneza Kiswahili duniani.

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 108 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



## Tamrini

1. Eleza sababu za Kiswahili kuenea kwa haraka nchini Tanganyika kuliko Kenya na Uganda kabla ya uhuru.
2. Toa maoni yako kuhusu namna ya kuendesha Kamisheni ya Kiswahili ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa ufanisi.
3. Jadili mambo yaliyosaidia kukua na kuenea kwa Kiswahili katika nchi mbalimbali duniani.
4. Jadili changamoto za Kamisheni ya Kiswahili ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.
5. Kwa kutumia mifano, bainisha changamoto zilizokikumba Chama cha Kiswahili cha Afrika.
6. Kwa kutumia mifano dhahiri jadili mchango wa wasanii katika kukuza na kueneza Kiswahili duniani.
7. Kwa nini Kiswahili kinafaa kutumika katika elimu kuliko lugha nyingine za Kiafrika kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki?
8. Eleza namna Tanzania inavyonufaika kutokana na kukua na kuenea kwa Kiswahili duniani.

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 109 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Nne
# Sarufi ya Kiswahili

## Utangulizi

Sura hii inahusu mada ya sarufi ya Kiswahili. Katika mada hii utajifunza kuhusu dhana ya sarufi, matawi ya sarufi, dhana za mofimu na mofu, kauli za vitenzi vya Kiswahili, uainishaji wa maneno, uambishaji katika Kiswahili, uundaji wa maneno, na ngeli za nomino. Malengo ya kujifunza sarufi ya Kiswahili ni kukuwezesha kutumia kanuni za kisarufi kwa usahihi. Inatarajiwa kwamba malengo hayo yakifikiwa, utakuwa na ujuzi wa kutumia Kiswahili kwa ufasaha katika nyanja zote.

**Dhana ya sarufi**

Mara nyingi watu huwasiliana kwa kutumia lugha na kukosoana kutokana na makosa wanayoyafanya bila kujua kwa nini wanafanya hivyo. Makosa ya namna hiyo yanatokana na kushindwa kuzingatia kanuni za lugha. Usahihi wa matumizi ya lugha umejikita katika kanuni na taratibu ambazo hutawala matumizi ya lugha inayohusika, yaani sarufi. Hivyo, sarufi ni kanuni na sheria zinazotawala matumizi sahihi ya matamshi, maumbo ya maneno, miundo, na maana zake katika lugha.

**Matawi ya sarufi**

Sarufi imegawanyika katika matawi makuu manne ambayo ni *fonolojia* (sarufi matamshi), *mofolojia* (sarufi maumbo), *sintaksia* (sarufi miundo), na *semantiki* (sarufi maana).

**Fonolojia (sarufi matamshi)**

Fonolojia ni tawi la sarufi linalohusika na uchunguzi wa mfumo wa sauti za lugha mahususi katika kuunda maneno. Aidha, fonolojia ni tawi la isimu ambalo hujishughulisha na uchunguzi, uchambuzi, na uainishaji wa sauti pambanuzi ambazo hutumika katika mfumo wa lugha mahususi. Kipashio cha msingi katika fonolojia ni fonimu. Fonimu ni vitamkwa vinavyoweza kujenga maneno yenye



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 110 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



maana tofauti au vinavyoweza kubadili maana za maneno. Fonimu ni sauti mahususi za lugha fulani. Mathalani Kiswahili kina jumla ya sauti thelathini na mbili zilizogawanyika katika makundi matatu ambayo ni irabu, konsonanti na viyeyusho. Kwa mfano, katika Kiswahili kuna irabu tano ambazo ni: a, e, i, o, u, konsonanti ishirini na saba ambazo ni b, ch, $c^h$, d, dh, f, g, gh, h, j, k, $k^h$, l, m, n, ny, ng', p, $p^h$, r, s, sh, t, $t^h$, th, v, z, na viyeyusho viwili ambavyo ni w, na y. Katika matamshi ya Kiswahili sanifu, fonimu hizi huwakilishwa kwa alama zifuatazo: /p/, /b/, /t/, /d/, /f/, /v/, /θ/, /ð/, /s/, /z/, /č/, au /t ʃ /, /ɟ/, /k/, /g/, /γ/, /h/, /š/, /m/, /n/, /ň/, /ŋ/, /l/, /r/, /w/, /j/ mtawalia (Massamba *na wenzie*, 2004:39-45).

Sauti hizo wakati mwingine hurejelewa kama vitamkwa. Kwa hiyo fonimu (sauti) ni kitamkwa kinachoweza kuunganishwa na kitamkwa kingine ili kujenga maneno yenye maana. Kwa mfano neno *mama* limeundwa na konsonanti na irabu kama linavyoonekana.

Isitoshe, fonimu ndizo hutofautisha maana za maneno katika lugha mahususi. Tazama mifano ifuatayo:

Piga - /p/ /i/ /**g**/ /a/

Pika - /p/ /i/ /**k**/ /a/

Pita - /p/ /i/ /**t**/ /a/

Pisha - /p/ /i/ /**š**/ /a/

Fonimu zote katika maneno haya zinafanana isipokuwa /**g**/, /**k**/, /**t**/ na /**š**/. Fonimu hizi tofauti ndizo zinazotofautisha maana za maneno hayo.

Mbali na kuhusika na sauti pambanuzi za lugha, fonolojia huhusika pia na vipengele vingine vya matamshi vinavyohusiana na sauti na mpangilio wake katika uundaji wa maneno katika lugha mahususi. Vipengele hivyo ni *kiimbo, mkazo, lafudhi, silabi*, na *kidatu*.

**Kiimbo** ni upandishaji au ushushaji wa sauti unaofanywa na mzungumzaji.

M**kazo** ni kiwango cha nguvu anachokifanya mtamkaji katika maneno anayoyatamka. Kiwango hicho cha nguvu kinawekwa katika silabi ya pili kutoka mwisho wa neno. Mfano wa mkazo umewekwa katika silabi zilizopigiwa mstari kama ifuatavyo:



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 111 25/09/2019 13:57

For Online Use Only

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

ana<u>*pi*</u>ka

anafu<u>*ndi*</u>sha

**Silabi** ni kipashio kinachohusu utamkaji wa sauti kama fungu-tamko moja katika lugha fulani. Tazama mifano ifuatayo:

soma = so-ma

amachelewa = a-me-che-le-wa

**Lafudhi** ni namna mtu binafsi anavyotamka maneno ambapo huathiriwa na mazingira ya kijamii au kijiografia atokapo mtu huyo. Kwa mfano Mchaga, Mhaya, Msukuma wanaweza kuongea Kiswahili chenye lafudhi ya lugha hizo.

**Kidatu** ni kiwango cha juu, cha kati, au cha chini cha msikiko wa sauti katika usemaji.

**Mofolojia (sarufi maumbo)**

Mofolojia ni tawi la sarufi linaloshughulika na uundaji wa maneno ya lugha mahususi kwa kutumia vipashio na kuzingatia mpangilio wake. Vipashio hivyo vya lugha huitwa mofimu, ambavyo huwakilishwa na mofu. Kwa mfano, katika Kiswahili mofimu za umoja na wingi huwakilishwa na mofu kama katika mifano ifuatayo:

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| *m*-ti | *mi*-ti |
| *m*-toto | *wa*-toto |
| *ki*-ti | *vi*-ti |

Mofu *m*- na *ki*- huonesha dhana ya umoja, ilhali mofu *mi*-, *wa*- na *vi*- zinaonesha wingi.

Aidha, mofolojia huchunguza maumbo ya aina mbalimbali za maneno katika lugha mahususi.

**Sintaksia (sarufi miundo)**

Sintaksia ni tawi la sarufi linaloshughulika na uchanganuzi wa mpangilio wa maneno katika kuunda sentensi na uhusiano wa vipashio vyake. Mpangilio wa

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 112 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



maneno katika kuunda sentensi hutawaliwa na kanuni za lugha mahususi. Hii ina maana kwamba kila lugha ina mpangilio wa maneno tofauti na lugha nyingine. Kanuni hizo zisipozingatiwa husababisha tungo zisizokubalika katika lugha inayohusika. Tazama mifano ifuatayo:

(a) (i) Mwanafunzi hodari hujifunza kwa bidii.
(ii) Asha amejenga nyumba kubwa sana.

(b) (i) Hodari mwanafunzi kwa bidii hujifunza.
(ii) Amejenga nyumba Asha kubwa sana.

Sentensi za mfano (a) zinafuata kanuni za uundaji wa sentensi za Kiswahili na hivyo zinakubalika. Sentensi za mfano (b) hazikufuata kanuni za uundaji wa sentensi za Kiswahili. Sentensi b (i) haikubaliki kwa sababu kivumishi *hodari* kimetangulia nomino *mwanafunzi* badala ya kutanguliwa na nomino hiyo. Pia, kitenzi *hujifunza* kinapaswa kufuatiwa na kirai kielezi *kwa bidii*. Hali kadhalika, sentensi b (ii) haikubaliki kwa sababu kirai kitenzi *amejenga nyumba* kimetangulia kirai nomino *Asha* badala ya nomino *Asha* kutangulia kirai kitenzi hicho. Katika lugha ya Kiswahili sentensi huundwa na *kiima* + *kitenzi* + *yambwa* (K + T + (Yb)) katika muundo msingi. Hivyo basi, kanuni za uundaji wa sentensi za Kiswahili zinamtaka mtumiaji wa lugha kuunda sentensi zinazozingatia mpangilio huo.

Kwa ujumla, sintaksia hushughulikia mambo makuu mawili. Mambo hayo ni kanuni za miundo ya sentensi na uhusiano wa maneno katika sentensi hiyo. Aidha, ifahamike kuwa kipashio cha msingi cha kisintaksia ni neno.

**Semantiki (sarufi maana)**

Semantiki ni tawi la sarufi linalochunguza na kuchanganua maana za maneno na sentensi katika lugha. Maana ni kipengele muhimu sana katika mchakato wa uchuguzi na uchanganuzi wa lugha. Semantiki huchunguza maana katika viwango mbalimbali, mathalani kiwango cha neno, sentensi, na kadhalika. Katika kiwango cha neno, maana inayochunguzwa ni ya kileksika. Maana ya kileksika ni maana inayopatikana katika kamusi, yaani maana ya msingi ya neno. Mifano ifuatayo inaonesha maneno na maana zake za kileksika:



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 113 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**abiri** - safiri kwa chombo chochote cha majini, angani, au nchi kavu;
- bashiri au eleza jambo kwa ufasaha; na
- jifunze jambo kutokana na mfano fulani.

**chao** - kitu kama gogo kinachotumika kuvutia dau majini;
- sehemu ya wazi juu ya shimo la mmea, ya kuingizia mbolea na maji; na
- neno linalotambulisha umiliki/umilikishi wa kitu.

Miongoni mwa mambo yanayochunguzwa kwenye kiwango cha sentensi ni maana ya tungo nzima inayotokana na maana za maneno yanayounda sentensi hiyo na mpangilio wake. Jambo lingine linalochunguzwa ni utata unaotokana na viambishi au maumbo mahususi, kama inavyooneshwa katika mifano ifuatayo:

(a) Dogori alimwandik*i*a Ngavanga barua.

Kipashio -*i*- katika sentensi kinadokeza maana zaidi ya moja kama ifuatavyo:

(i) Dogori aliandika barua kwa niaba ya Ngavanga.
(ii) Dogori aliandika barua kumjulisha Ngavanga jambo fulani.

(b) Kalunde alikwenda nyumbani *kwake*.

Sentensi hii nayo inadokeza maana zaidi ya moja kutokana na kuwapo kwa kipashio *kwake*. Maana hizo ni kama zifuatazo:

(i) Kalunde alikwenda kwenye nyumba anayoishi au anayoimiliki yeye mwenyewe.
(ii) Kalunde alikwenda kwenye nyumba inayomilikiwa na mtu mwingine.

Hapo juu, tumefafanua matawi ya sarufi. Ifahamike kuwa matawi hayo huingiliana. Kielelezo kifuatacho kinaonesha mwingiliano baina ya tawi moja na jingine.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 114 25/09/2019 13:57




**Kielelezo 4.1** Matawi ya sarufi

**Uainishaji wa maneno**

Wanaisimu waliochunguza lugha ya Kiswahili wameainisha aina za maneno kwa idadi na istilahi tofauti tofauti. Baadhi ya wanaisimu kama vile Nkwera (1978), Kapinga (1983), Mohamed (1986), na Kihore *na wenzie* (2008) wanadai kuwa lugha ya Kiswahili ina aina saba za maneno kama ifuatavyo:

(i) Nomino au majina (N)
(ii) Kiwakilishi (W)
(iii) Kivumishi (V)
(iv) Kitenzi (T)
(v) Kielezi (E)
(vi) Kiunganishi (U)
(vii) Kiingizi au Kihisishi (I)

Kwa upande mwingine, kuna wanaisimu wanaodai kuwa lugha hii ina aina nane za maneno. Miongoni mwao ni Mdee (1999), Mgullu (1999), Habwe na Karanja (2004), na Matei (2008). Wanaisimu hawa wanabainisha aina za maneno zifuatazo:



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 115 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(i) Nomino au Majina (N)
(ii) Kiwakilishi (W)
(iii) Kivumishi (V)
(iv) Kitenzi (T)
(v) Kielezi (E)
(vi) Kiunganishi (U)
(vii) Kiingizi au Kihisishi (I)
(viii) Kihusishi (H)

Ukichunguza orodha hizo mbili za aina za maneno, utabaini kuwa zinatofautiana kwa jambo moja tu, nalo ni kuwa katika kundi la pili kuna aina ya ziada ya maneno ambayo ni kihusishi.

Aidha, wanaisimu wengine, kama vile Matinde (2012), wanabainisha aina tisa za maneno zifuatazo:

(i) Nomino (N)
(ii) Kitenzi (T)
(iii) Kivumishi (V)
(iv) Kiwakilishi (W)
(v) Kielezi (E)
(vi) Kihusishi (H)
(vii) Kiunganishi (U)
(viii) Kihisishi (I)
(ix) Kibainishi (B)

Uainishaji wa kundi la tatu umehusisha aina zote zilizoainishwa katika kundi la pili kisha ikaongezwa aina nyingine ya neno ambayo ni kibainishi (B). Maneno yanayotajwa kuwa ni vibainishi katika lugha ya Kiswahili ni yale ambayo yanarejelea idadi ya vitu kama vile *wawili*, *watatu*, *mmoja*, *wengi*, *wachache*, na kadhalika. Maneno mengine ni yale yanayorejelea umiliki wa vitu kama vile *changu*, *yako*, *yenu*, *wenu*, *wao* na *vyako*. Pia, kuna maneno yanayoonesha umbali kama vile *hapo*, *kule*, *humu*, *hapa*, *yule*, *hawa*, na kadhalika.

Pamoja na hayo, katika kiwango hiki hatutaingilia mjadala huo wa idadi ya aina za maneno. Mjadala huu bado unaendelea kupamba moto miongoni mwa



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 116 25/09/2019 13:57

For Online Use Only

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



wanazuoni. Kwa hiyo, katika vipengele vinavyofuata tutajadili aina saba za maneno zilizopo katika lugha ya Kiswahili. Aina hizo ni nomino, viwakilishi, vivumishi, vitenzi, vielezi, viunganishi, na vihisishi.

**Nomino (N)**

Nomino ni maneno yanayotaja au kubainisha viumbe, vitu, hali, mahali na dhana. Katika baadhi ya maandiko ya sarufi ya Kiswahili, hasa yale ya zamani, nomino huitwa pia majina (Kapinga 1983; Nkwera 1978). Aina hii ya maneno hujibu maswali ya nani na nini. Nomino zinaweza kugawanywa katika makundi mbalimbali kulingana na vigezo kadhaa. Vigezo hivyo ni kigezo cha upekee, udhahania, na idadi.

**Kigezo cha upekee**

Kwa kuzingatia kigezo hiki, nomino zinaweza kugawanywa katika makundi madogo mawili ambayo ni nomino za pekee na nomino za kawaida. Nomino za pekee hujulikana pia kama nomino mahususi. Hizi ni nomino zinazotaja au kubainisha watu na vitu maalumu. Nomino za pekee hazina maumbo ya umoja na wingi. Kwa kawaida, nomino hizi huanza kwa herufi kubwa hata kama nomino hiyo haitokei mwanzoni mwa sentensi. Nomino za pekee hujumuisha majina ya watu, siku za wiki, miezi, vijiji, miji, majiji, nchi, mabara, bahari, mito, maziwa, milima na majangwa. Kwa mfano, *Pendo, Shukuru, Jumatatu, Jumanne, Januari, Februari, Mtakuja, Majengo Mapya, Kasulu, Arusha, Tanzania, Uchina, Afrika, Marekani, Bahari ya Atlantiki, Bahari ya Hindi, Malagarasi, Wami, Nyanza, Tanganyika, Mlima Kilimanjaro, Mlima Meru, Jangwa la Kalahari,* na nyingine nyingi.

Kwa upande mwingine, nomino za kawaida ni aina ya nomino ambazo hutaja vitu, dhana au viumbe ambavyo si mahususi. Nomino za kawaida hujulikana pia kama nomino za jumla. Kwa mfano, *dawati, mbuzi, gari, samaki, embe*, na kadhalika. Tofauti na nomino za pekee, nomino za kawaida zinaweza kuwa na umbo la umoja na wingi, umbo la umoja tu au umbo la wingi tu. Nomino za kawaida huanza kwa herufi ndogo zinapoandikwa isipokuwa kama zinatokea mwanzoni mwa sentensi.

**Kigezo cha udhahania**

Kwa kuzingatia kigezo cha udhahania nomino zinaweza kugawanywa katika makundi mawili ambayo ni nomino dhahania na zisizo dhahania. Nomino dhahania ni zile zinazotaja vitu visivyoonekana kwa macho na kugusika. Dhana



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 117 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

zinazotajwa na nomino hizi huweza kufikirika au kuhisika tu. Mifano ya nomino dhahania ni kama vile *uzalendo, upendo, utamu, uchungu, njaa, afya, usingizi, maumivu* na *utaratibu.* Nomino zisizo dhahania ni nomino ambazo hutaja vitu au dhana za vitu vinavyoonekana na kugusika. Kwa mfano, *nguo, yai, ndoo, sukari, maji, punda,* na kadhalika.

**Kigezo cha idadi**

Katika kigezo hiki nomino zinaweza kugawanywa katika makundi mawili ambayo ni nomino zinazohesabika na zisizohesabika. Nomino zinazohesabika ni nomino zinazoonesha idadi ya vitu na viumbe mbalimbali. Kwa kawaida nomino hizi huhesabika. Nomino zinazohesabika zinaweza kuwa na maumbo ya umoja na wingi au umbo la umoja au wingi tu. Mifano ya nomino zinazohesabika ni kama vile *mgonjwa, msemo, kisiwa, nyumba, ungo, nchi, jeshi, suruali,* na *chupa*. Nomino zisizohesabika ni maneno yanayotaja vitu visivyoweza kuhesabika. Mfano wa nomino za kundi hili ni *maji, maziwa, mafuta, sukari, mchanga, mchele, chumvi, urefu,* na *upana.*

Kundi lingine la nomino zisizohesabika ni nomino za kitenzi–jina ambazo hutokana na vitenzi. Umbo la nomino hizo hufanana na kitenzi ambacho kimeambikwa kiambishi *ku*- mwanzoni. Nomino za aina hii hufanana na kitenzi asilia. Mifano ya nomino za vitenzi–jina ni kama vile *kucheza, kuimba, kulima, kujidai, kutembea,* na *kujitanua*. Mathalani, katika sentensi *Kucheka kwake kunanifurahisha*. Neno *kucheka* ni kitenzi–jina.

**Viwakilishi (W)**

Viwakilishi ni maneno yenye uhusiano wa karibu sana na nomino. Kama ambavyo mwakilishi hufanya kazi badala ya mtu mwingine, ndivyo viwakilishi hufanya kazi badala ya nomino au hukaa mahali pa nomino katika tungo. Kuwepo kwa viwakilishi katika lugha ya Kiswahili husaidia kutorudiarudia nomino katika tungo. Nomino na viwakilishi haviwezi kutokea kwa pamoja katika tungo. Kutokea kwa kimojawapo husababisha kingine kisitokee. Kuna aina tisa za viwakilishi. Aina hizo ni: viwakilishi vya nafsi, viwakilishi vimilikishi, viwakilishi vioneshi, viwakilishi viulizi, viwakilishi vya a-unganifu, viwakilishi virejeshi, viwakilishi vya sifa, viwakilishi vya idadi, na viwakilishi vya pekee.

**(a) Viwakilishi vya nafsi**

Viwakilishi vya nafsi ni maneno yanayosimama badala ya nomino inayorejelea mtu au watu. Viwakilishi vya nafsi hurejelea nafsi ya mtu



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 118 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



anayetenda, anayetendwa au anayetendewa jambo. Viwakilishi vya nafsi viko sita ambavyo vimegawanyika katika umoja na wingi kama inavyooneshwa katika jedwali lifuatalo.

**Jedwali 4.1** Viwakilishi vya nafsi

| Nafsi | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| 1 | Mimi | sisi |
| 2 | Wewe | ninyi |
| 3 | Yeye | wao |

Viwakilishi vya nafsi vimeundwa pasipo kuambikwa au kupachikwa viambishi. Maumbo yake ni huru na yanatofautiana na maumbo ya viwakilishi vya aina nyingine zinazofuata.

**(b) Viwakilishi vimilikishi**

Hii ni aina ya viwakilishi ambavyo huonesha umiliki wa kitu. Viwakilishi vimilikishi katika Kiswahili hubainishwa na mizizi *-angu*, *- etu*, *-ako*, *-enu*, *-ake* na *-ao*. Nafasi zinazowakilishwa na vistari hujazwa na viambishi vya upatanisho wa kisarufi vya umoja na wingi. Kwa mfano:

(i) *Yangu* imepotea.

(ii) *Wetu* ni mkali.

(iii) *Yako* ni nyeupe.

(iv) *Yenu* imeharibika.

(v) *Yake* imepatikana.

(vi) *Yao* imekuja.

**(c) Viwakilishi vioneshi**

Viwakilishi hivi huonesha umbali wa nomino inayowakilishwa. Kuna aina tatu za viwakilishi vioneshi. Aina ya kwanza ni viwakilishi vioneshi vya karibu na msemaji kama vile *hiki*, *hili*, *huu*, *huyu*, na *haya*. Aina ya pili ni viwakilishi vioneshi vya karibu na msikilizaji kama vile *hicho*, *hayo*, *hao*,



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 119 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*hivyo*, na *hizo*. Aina ya tatu ni viwakilishi vioneshi vya mbali na msemaji na msikilizaji kama vile *kile, wale, lile, vile* na *zile*. Jedwali lifuatalo linaonesha maumbo ya viwakilishi vioneshi vya Kiswahili.

**Jedwali 4.2** Maumbo ya viwakilishi vioneshi

| Viwakilishi vioneshi vya karibu na msemaji | | Viwakilishi vioneshi vya karibu na msikilizaji | | Viwakilishi vioneshi vya mbali na msemaji na msikilizaji | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Mfano wa matumizi** | | **Mfano wa matumizi** | | **Mfano wa matumizi** |
| Huyu | Anampenda huyu. | huyo | Anampenda huyo. | yule | Anampenda yule. |
| Hawa | Hawa wanacheza sana. | hao | Hao wanacheza sana. | wale | Wale wanacheza sana. |
| Huu | Huu ni wetu. | huo | Huo ni wetu. | ule | Ule ni wetu. |
| Hii | Hii inapendeza. | hiyo | Hiyo inapendeza. | ile | Ile inapendeza. |
| Hili | Hili lilijengwa lini? | hilo | Hilo lilijengwa lini? | lile | Lile lilijengwa lini? |
| Haya | Haya nitayanywa yote. | hayo | Hayo nitayanywa yote. | yale | Yale nitayanywa yote. |
| Hiki | Hiki ni nini? | hicho | Hicho ni nini? | kile | Kile ni nini? |
| Hivi | Hivi vinapelekwa wapi? | hivyo | Hivyo vinapelekwa wapi? | vile | Vile vinapelekwa wapi? |
| Hizi | Hizi ni zangu. | hizo | Hizo ni zangu. | zile | Zile ni zangu. |
| Hapa | Hapa panatufaa sote. | hapo | Hapo panatufaa sote. | pale | Pale panatufaa sote. |
| Huku | Huku kuna mambo! | huko | Huko kuna mambo! | kule | Kule kuna mambo! |
| Humu | Humu mna joto kali. | humo | Humo mna joto kali. | mle | Mle mna joto kali. |



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 120 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


**(d) Viwakilishi viulizi**

Haya ni maneno yanayowakilisha nomino inayouliziwa katika swali. Nomino hiyo inaweza kutokea kabla au baada ya kitenzi. Viwakilishi viulizi vya Kiswahili vinaweza kuwekwa katika makundi mawili kwa kuzingatia maumbo yake. Kundi la kwanza huundwa na viulizi ambavyo ni maneno huru na haviambikwi viambishi vyovyote. Mifano ya viwakilishi hivyo ni kama vile *nani*, *nini*, *lini*, na *gani*. Kundi la pili huundwa na viulizi vinavyotokana na kuambika viambishi katika mizizi ya viwakilishi hivyo. Mizizi hiyo ni *-pi* na *-ngapi*. Mwishoni mwa tungo au sentensi huwa na alama ya kuuliza. Chunguza mifano ifuatayo:

(i) *Nani* amekuja?

(ii) *Nini* kimejiri?

(iii) *Ipi* imeuzwa?

(iv) *Kipi* kimenunuliwa?

(v) *Ngapi* zimepotea?

(vi) *Wangapi* waje?

(vii) *Vingapi* vimevunjika?

(viii) Ataondoka *lini?*

(ix) Mtoto wa Ali anaitwa *nani*?

(x) Leo unataka *nini*?

(xi) Baba ameenda *wapi*?

(xii) Unasoma darasa la *ngapi*?

Maneno yaliyoandikwa kwa *hatimlalo* ni viwakilishi viulizi. Katika mifano ya (i) – (vii) viwakilishi viulizi vimejitokeza kabla ya kitenzi, ilhali katika mifano (viii) – (xii) vimejitokeza baada ya kitenzi.


PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 121 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**(e) Viwakilishi vya sifa**

Haya ni maneno yanayoonesha sifa ya nomino ambayo inawakilishwa. Matumizi ya viwakilishi hivi huendana na nomino inayowakilishwa. Tazama mifano ifuatayo:

(i) *Kizuri* chajiuza, *kibaya* chajitembeza.
(ii) *Wanene* wanacheza ngoma vizuri.
(iii) *Warefu* hukimbia kwa kasi.
(iv) *Vizuri* vimepotea.
(v) *Vibovu* vimetupwa.

**(f) Viwakilishi vya idadi**

Haya ni maneno yanayoonesha idadi dhahiri au isiyo dhahiri ya watu au vitu vinavyotajwa na nomino inayowakilishwa. Viwakilishi hivi hutumia maneno yanayobainisha tarakimu. Viambishi viwakilishi vya idadi isiyo dhahiri huambikwa katika mizizi *-ingi*, *-chache* na *-ote* kutegemeana na nomino inayowakilishwa. Chunguza mifano ifuatayo:

(i) *Wawili* waingie darasani.
(ii) *Kumi* watakuja kesho.
(iii) *Vingi* vimenunuliwa.
(iv) *Vichache* vimebaki.
(v) *Wote* wamefaulu.

**(g) Viwakilishi vya pekee**

Hivi ni viwakilishi vilivyoundwa na mzizi *-ingine* na *–enyewe*. Chunguza mifano ifuatayo:

(i) *Vingine* havijulikani.
(ii) *Lenyewe* limeiva.
(iii) *Wengine* waingie.
(iv) *Mwenyewe* haonekani.
(v) *Kingine* kimejitokeza.
(vi) *Lingine* limenunuliwa.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 122 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



**Vivumishi (V)**

Hii ni aina ya maneno ambayo hutoa maelezo zaidi au sifa kuhusu nomino au viwakilishi. Kwa kawaida, maelezo hayo huhusu namna au jinsi nomino ilivyo, inavyoonekana, inavyofikiriwa, idadi, na tabia yake. Aina hii ya maneno ina uhusiano na nomino au viwakilishi. Hii inamaanisha kuwa kutokea kwa kivumishi hutegemea kutokea kwa nomino au kiwakilishi. Vivumishi katika baadhi ya maandiko ya sarufi ya Kiswahili huitwa *sifa*. Zifuatazo ni aina za vivumishi katika Kiswahili.

**(a) Vivumishi vya sifa**

Hii ni aina ya vivumishi ambavyo hueleza namna kiumbe au kitu kilivyo. Vivumishi vya sifa katika lugha ya Kiswahili vinaweza kuwa na maumbo yenye viambishi au yasiyo na viambishi. Ifuatayo ni mifano ya vivumishi vya sifa katika Kiswahili.

(i) Bidhaa *adimu* zimenunuliwa.
(ii) Mtu *mzima* ameanguka.
(iii) Mkulima *bora* amepata tuzo.
(iv) Ile *michungu* ilitupwa.
(v) Huyu *jasiri* amefaulu.
(vi) Msichana *hodari* anaimba vizuri.

**(b) Vivumishi vya idadi**

Hivi ni vivumishi vinavyoonesha jumla au hesabu ya vitu. Hesabu hiyo inaweza kuwa dhahiri au isiyo dhahiri. Kwa hiyo, kuna aina mbili za vivumishi vya idadi ambazo ni vivumishi dhahiri na vivumishi visivyo dhahiri. Vivumishi dhahiri hutaja idadi ya nomino ilhali vivumishi visivyo dhahiri hutaja idadi ya nomino kwa namna isiyo wazi. Vivumishi vya lugha ya Kiswahili hutokea baada ya nomino inayovumishwa. Ifuatayo ni mifano ya vivumishi vya idadi.

(i) Kijiji *kimoja* kimepata mafunzo ya Elimu ya Afya.
(ii) Mito *mingi* imefurika.
(iii) Miaka *kumi na mitatu* inatosha.
(iv) Zile *chache* zimenunuliwa.
(v) Wengine *kadhaa* wameripotiwa.
(vi) Shilingi *elfu tano* zimechangwa.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

For Online Use Only

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**(c) Vivumishi vioneshi**

Hivi ni vivumishi ambavyo huonesha umbali wa mahali nomino ilipo. Umbali huo huweza kuwa wa karibu na msemaji, karibu na msikilizaji au mbali na msemaji na msikilizaji. Tazama mifano ifuatayo:

(i) Mtoto *huyu* ni mtukutu.
(ii) Nyasi *hizi* zimenyauka.
(iii) Ukuta *huo* umepinda.
(iv) Nyumba *hiyo* imejengwa vizuri.
(v) Kile *kile* ni kizuri.
(vi) Kompyuta *ile* ilikuwa inasumbua.

Katika mifano hapo juu, mfano wa (i) - (ii) ni vivumishi vya kuonesha karibu na msemaji, mfano wa (iii) - (iv) ni vivumishi vya kuonesha karibu na msikilizaji na mifano (v) - (vi) ni vivumishi vya kuonesha mbali na msemaji na msikilizaji.

**(d) Vivumishi viulizi**

Hivi ni vivumishi ambavyo vinauliza swali kuhusu nomino. Vivumishi viulizi vya Kiswahili vina maumbo ya namna mbili. Vivumishi viulizi vinaweza kuwa ni maneno huru, yaani maneno yasiyoambikwa viambishi au maneno yaliyotokana na kuambika viambishi katika mzizi wa kivumishi kinachohusika. Mwishoni mwa tungo huwa kuna alama ya kuuliza (?). Tazama mifano ifuatayo:

(i) Gari *gani* limepata pancha?
(ii) Watoto *wangapi* wamefaulu?
(iii) Bunduki *ngapi* zilipatikana?
(iv) Kingine *kipi* kimevunjika?
(v) Mwingine *yupi* amehamishwa?

**(e) Vivumishi vimilikishi**

Hivi ni vivumishi ambavyo huonesha umiliki wa mtu au kitu. Vivumishi vimilikishi vya Kiswahili huundwa kwa kuambika viambishi vya upatanisho wa kisarufi (kwa kuzingatia nomino inayovumishwa) katika mizizi. Mizizi hiyo ni *-angu, -etu, -ako, -enu, -ake,* na *-ao.* Tazama mifano ifuatayo:


PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 124 25/09/2019 13:57

(i) Wale *wangu* wamefaulu vizuri.
(ii) Hii *yetu* ina maua mengi.
(iii) Viatu *vyako* vinapendeza.
(iv) Kuimba *kwenu* kunavutia.
(v) Mke *wake* alinunua pikipiki mpya.
(vi) Mbuzi *wao* anatoa maziwa mengi.

**(f) Vivumishi vya pekee**

Hivi ni vivumishi ambavyo huundwa na mizizi *-enyewe*, na *-ingine*. Chunguza mifano ifuatayo:

(i) Kiti *kingine* kimevunjika.
(ii) Pori *lenyewe* halina miti mingi.
(iii) Jambo *lenyewe* lina utata.
(iv) Kile *chenyewe* ni butu.
(v) Huyu *mwingine* atakatiwa bima ya afya.
(vi) Kucheza *kwingine* kunashangaza.

**Vitenzi (T)**

Hii ni aina ya maneno ambayo hutoa taarifa kuhusu tendo linalofanyika, lililofanyika au litakalofanyika. Kitenzi kinapoondolewa, tungo hukosa maana. Kwa hiyo, kitenzi ni sehemu muhimu ya sentensi kwa sababu hubeba taarifa za msingi katika sentensi. Kitenzi katika Kiswahili huweza kusimama peke yake na kutoa taarifa kamili. Kwa hiyo, kitenzi kinaweza kuwa na sifa au hadhi ya sentensi. Vitenzi huweza kuainishwa katika aina mbalimbali kwa kutumia kigezo cha uamilifu. Kwa kuzingatia kigezo hicho tunaweza kuainisha vitenzi katika makundi matatu kama ifuatavyo:

**(a) Vitenzi vikuu (Tk)**

Hii ni aina ya vitenzi ambavyo hudokeza taarifa ya msingi ya tendo linaloelezwa katika tungo husika. Vitenzi vikuu hutoa taarifa kamili na huweza kusimama kama sentensi. Kwa mfano:

(i) Juma *anacheza* mpira.
(ii) *Analima*.
(iii) *Amewasili* salama.
(iv) Mwanakombo *ameondoka* haraka.


PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
For Online Use Only
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 125 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**(b) Vitenzi visaidizi (Ts)**

Hii ni aina ya vitenzi ambavyo hutumika sambamba na vitenzi vikuu katika kuvisaidia kukamilisha taarifa inayoelezwa katika sentensi. Aidha, vitenzi visaidizi hutumika kudokeza muda ambao tendo hufanyika. Vilevile, hudokeza hali ya ukanushi au uyakinifu. Kazi ya vitenzi visaidizi ni kusaidia vitenzi vikuu na hujitokeza katika tungo kabla ya kitenzi kikuu. Chunguza mifano ifuatayo:

(i) Mhe. Rais *alikuwa* anahutubia leo.
(ii) Kaka *alikuwa* anacheza mpira vizuri.
(iii) Vijana *watakuwa* wamepumzika.

**(c) Vitenzi vishirikishi (t)**

Hii ni aina ya vitenzi ambavyo hushirikisha kiima na vijalizo vyake katika tungo. Vitenzi vishirikishi huweza pia kudokeza kuwepo au kutokuwepo kwa hali au vitu fulani. Katika njeo iliyopita na ijayo vitenzi vishirikishi hutumia shina -*wa* (mzizi wa kitenzi *ku*-*wa*) ambao huambikwa viambishi vya nafsi, njeo na kiambishi kiso ukomo –*ku*- na katika njeo ya mazoea huambikwa kiambishi cha mazoea *hu*-. Tazama mifano ifuatayo:

(i) Kapemba *ni* mwalimu wa Jiografia.
(ii) Huyu *si* adui yangu.
(iii) Mama *alikuwa* hodari wa mapishi.
(iv) Kijana huyu *atakuwa* mwanariadha mzuri.
(v) Mungu *yu* mwema.
(vi) Mtu huyu *huwa* mpole
(vii) Huyu *ndiye* Mkuu wa Mkoa wa Simiyu.

**Dhima za viambishi katika vitenzi**

Vitenzi vya Kiswahili vina sifa ya kuambikwa viambishi ambavyo vina uamilifu mbalimbali. Zifuatazo ni dhima zinazooneshwa na viambishi katika vitenzi:

(i) Kuonesha nafsi. Kwa mfano, *ni*nasoma, *u*naimba, *a*talima, *a*naondoka, *tu*napika.

(ii) Kuonesha idadi. Kwa mfano, *i*melimwa, *ki*meoza, *u*meanguka, *tu*taondoka.

(iii) Kuonesha njeo. Kwa mfano, a*li*lima, a*na*cheza, a*ta*imba.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 126 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



(iv) Kuonesha yambwa au yambiwa. Kwa mfano, Ame*m*piga (yambwa), ame*m*pigia (yambiwa).

(v) Kuonesha urejeshi. Kwa mfano, wana*o*imba, wataka*vyo*ondoka, zili*zo*vunjika, kina*cho*vuja.

(vi) Kuonesha hali. Kwa mfano, *hu*cheza, a*me*maliza, a*ki*ja, *ha*takula, a*ka*lala.

(vii) Kuonesha kauli za vitenzi. Kwa mfano, pend*a*, teg*ek*a, pig*wa*, toza, some*a*, sem*ana*.

**Vielezi (E)**

Hii ni aina ya maneno yanayoeleza jinsi au namna, wakati, idadi, au mahali tendo linapotendeka. Vilevile, vielezi hutoa taarifa zaidi kuhusu kivumishi au kielezi kingine. Vielezi huweza kutokea mwanzoni, katikati au mwishoni mwa sentensi. Hata hivyo, baadhi ya vielezi vikiondolewa katika tungo maana ya msingi ya tungo haiwezi kupotea. Zifuatazo ni aina za vielezi katika lugha ya Kiswahili.

**(a) Vielezi vya namna (jinsi)**

Hivi ni vielezi ambavyo hutoa taarifa kuhusu namna au jinsi tendo lilivyotendeka, linavyotendeka au litakavyotendeka. Kwa mfano:

(i) Anaimba *vizuri*.

(ii) Anapika *taratibu.*

(iii) Unacheza *kizembe.*

(iv) Wanaandika *ovyoovyo.*

(v) Anakula *harakaharaka*

**(b) Vielezi vya wakati**

Hivi ni vielezi vinavyotoa taarifa kuhusu wakati ambao tendo lilitendeka, linatendeka au litakapotendeka. Kwa mfano:

(i) Hamisa alifika hapa *jana*.

(ii) Huruma atafika *alfajiri.*

(iii) Kasabila na Mugisha wanaondoka *sasa*.

(iv) *Asubuhi* Kadebi atapita hapa.

(v) Habari za kimataifa zitaletwa kwenu *punde*.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 127 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**(c) Vielezi vya idadi**

Hivi ni vielezi vinavyotoa taarifa kuhusu idadi au kiasi cha kufanyika kwa tendo. Aina hii ya vielezi huweza kudokeza idadi dhahiri au idadi isiyo dhahiri. Tazama mifano ifuatayo:

(i) Mvua imenyesha *mara mbili*.
(ii) Hamisi hupita hapa *mara chache*.
(iii) Wao hula nyama *mara tatu kwa wiki*.
(iv) Kuku hunywa maji *mara kwa mara*.
(v) *Kila siku* wanafunzi hujifunza.

**(d) Vielezi vya mahali**

Hivi ni vielezi ambavyo hutoa taarifa kuhusu mahali ambapo tendo au tukio lilifanyikia, linafanyikia au litakapofanyikia. Vielezi hivi huweza kubainishwa kwa neno linalotaja jina la mahali, nomino ya kawaida iliyoongezewa kipashio -*ni* au kifungu cha maneno kinachodokeza mahali. Tazama mifano ifuatayo:

(i) Mtoto anacheza *shuleni*.
(ii) Masanja amehamia *hapa*.
(iii) Fisi anaishi *mwituni*.
(iv) Juma alifika *kwetu*.
(v) Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania liko *Dodoma*.

**Viunganishi (U)**

Hii ni aina ya maneno ambayo huunganisha vipashio vyenye hadhi sawa na visivyo na hadhi sawa katika tungo. Vipashio hivyo huweza kuwa neno na neno, kirai na kirai, kishazi na kishazi, au sentensi na sentensi. Viunganishi vimeainishwa katika aina saba kwa kuzingatia kigezo cha dhima zinazobebwa na viunganishi hivyo katika sentensi. Aina hizo ni: viunganishi vya nyongeza, viunganishi vya sababu, viunganishi vya masharti, viunganishi vya wakati, viunganishi vya chaguo, viunganishi vya ulinganishi, na viunganishi vya ukanushi.

**(a) Viunganishi vya nyongeza**

Hivi ni viunganishi ambavyo hueleza dhana ya kuongeza kitu, taarifa, tendo, au idadi ya kitu. Kwa mfano:

(i) Rais *na* Makamu wake wanakuja leo.
(ii) Baba ni mwandishi *na* mtangazaji.


PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
For Online Use Only

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



(iii) Walimpiga *pamoja na* kumwibia.

(iv) Walimzomea *halafu* wakamshtaki.

**(b) Viunganishi vya sababu**

Hivi ni viunganishi ambavyo hudokeza au hueleza sababu ya kutokea kwa jambo au hali fulani. Ifuatayo ni mifano ya viunganishi vya sababu:

(i) Ngowi alilia sana *kwa sababu* hakufaulu mtihani wake.

(ii) Mimi nimefaulu *kwa kuwa* nilisoma kwa bidii.

(iii) Aliwahi mapema *ili* asichelewe basi.

(iv) Juma alipiga kelele *kusudi* asaidiwe.

(v) Alikasirika *kwa vile* aliibiwa pesa zake za vikoba.

**(c) Viunganishi vya masharti**

Hivi ni viunganishi ambavyo hudokeza masharti ya utokeaji wa kitu, tukio au hali fulani. Ifuatayo ni mifano ya viunganishi vya masharti:

(i) Dada atafaulu vizuri *endapo* atasoma kwa bidii.

(ii) Watawasili kesho *iwapo* mvua haitanyesha.

(iii) Zubeda ataenda mjini *kama* atapewa ruhusa.

(iv) Nitakuletea mzigo wako *ikiwa* utatuma pesa za kuagizia mzigo.

**(d) Viunganishi vya wakati**

Hivi ni viunganishi ambavyo hudokeza muda au wakati wa utokeaji wa tendo fulani. Tazama mifano ifuatayo:

(i) Wananchi walimsubiri mbunge *mpaka* Mkuu wa Wilaya aliposema hatakuja.

(ii) Hawajawahi kuwa washindi *tangu* waanze mashindano.

(iii) Dada alianza kusoma jioni *hadi* asubuhi.

**(e) Viunganishi vya chaguo**

Hivi ni viunganishi ambavyo huonesha hali ya kuchagua kitu kimoja dhidi ya kingine, jambo moja dhidi ya lingine, na kadhalika. Huonesha uhuru wa kuchagua kitu kimojawapo miongoni mwa vitu vingi vilivyopo. Tazama mifano ifuatayo:

(i) Jibu swali moja kutoka sehemu A *au* B.

(ii) Mimi nitasoma *ama* kwa Kiswahili *au* kwa Kiingereza.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 129 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**(f) Viunganishi vya ulinganishi**

Hivi ni viunganishi ambavyo hulinganisha vitu au hali mbili au zaidi. Hujulikana pia kama viunganishi linganishi. Viunganishi hivi huweza kulinganisha maumbile ya watu, mwonekano, hali, umri, au rangi za watu na vitu. Tazama mifano ifuatayo:

(i) Ninaipenda nyumba hii *kuliko* nyumba ile
(ii) Mbuga zetu ni nzuri *kushinda* mbuga zao.
(iii) Mimi ni mrefu *kumzidi* yeye.
(iv) Mwanahawa ni mrefu *zaidi ya* Furaha.
(v) Tanzania ina madini mengi *kupita* nchi zote za Afrika Mashariki.

**(g) Viunganishi vya ukanushi**

Hivi ni viunganishi ambavyo hudhihirisha au kudokeza hali ambayo haikutarajiwa. Hubainisha vitu visivyotarajiwa kulingana na hali halisi iliyopo au iliyokuwepo kama inavyooneshwa katika mifano ifuatayo:

(i) Alimpenda sana *lakini* hakumuoa.
(ii) Anacheza vizuri *ila* hafungi magoli.
(iii) Ana nguvu nyingi *ijapokuwa* ni mwembamba.
(iv) Alilima shamba kubwa *ingawa* hakuvuna mazao mengi.

**Vihisishi (I)**

Haya ni maneno ambayo hulenga kuonesha hisia za mtu. Aina hii ya maneno hujulikana pia kama viingizi. Hudokeza hisia mbalimbali za mzungumzaji kama vile huzuni, majuto, sikitiko, tahadhari, na furaha. Hata hivyo, maneno ya Kiswahili yanaweza yasiwe vihisishi kwa asili lakini yanapowekewa alama ya mshangao (!) katika tungo huwa vihisishi au viingizi. Zifuatazo ni aina za vihisishi:

**(a) Vihisishi vya mshangao**

Hivi ni vihisishi ambavyo hudokeza hisia za hali ya kushangaa. Hubainishwa kwa maneno kama vile *Mtume! Yesu wangu! salaale! mama we! mama yangu! kumbe!* na *aah!* Ifuatayo ni mifano ya vihisishi:

(i) *Aaah!* Umemaliza.
(ii) *Mama yangu!* Umekwisha.
(iii) *Alaa!* Kumbe wewe ndiye uliyeniibia?
(iv) *Mama we!* Amekamatwa tayari.

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



**(b) Vihisishi vya shukurani**

Hivi ni vihisishi ambavyo hudokeza hali ya kushukuru. Kwa mfano:

*Asanteni!*

**(c) Vihisishi vya mwitiko**

Hivi ni vihisishi ambavyo hudokeza hali au tendo la kuitika jambo fulani. Tazama mifano katika tungo zifuatazo:

(i) *Naam!* Ninakuja.

(ii) *Abee!* Nimesikia.

(iii) *Haaya!* Atakuja.

(iv) *Sawa!* Unasemaje?

(v) *Labeka!* Naja.

**(d) Vihisishi vya furaha**

Hivi ni vihisishi ambavyo hudokeza hali au hisia za furaha. Tazama mifano ifuatayo:

(i) Tanzania *oyee!*

(ii) *Oyaa!* Shangilieni.

(iii) Mkutano *hoyeee!*

(iv) *Waooo!* Nimekuona kwenye televisheni.

**(e) Vihisishi vya masikitiko**

Hivi ni vihisishi ambavyo hudokeza hali ya huzuni au simanzi kuhusu jambo fulani. Tazama mifano ifuatayo:

(i) *Daah!* Akinikamata nitamwambiaje?

(ii) *Masikini wee!* Ameachwa peke yake!

(iii) *Mamaaa!* Amesombwa na maji.

(iv) *Ayaa!* Maganga amemwaga maji kitandani.

**(f) Vihisishi vya tahadhari**

Hivi ni vihisishi ambavyo hudokeza hali ya kuwa na uangalifu au zingatio. Ifuatayo ni mifano ya vihisishi vya tahadhari:

(i) *Thubutu!* Atakupiga mpaka usahau kwenu.

(ii) *Ebo!* Ukileta masihara nitakushitaki.

(iii) *Kaa chonjo!* Saa mbaya.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 131 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 4.1

1. Eleza namna nomino za lugha ya Kiswahili zinavyoweza kujibainisha.
2. Kwa kutumia mifano, eleza tofauti kati ya kiwakilishi na kivumishi.
3. Fafanua kwa mifano anuai vipengele vya kisarufi ambavyo hujitokeza kwenye vitenzi vya Kiswahili.
4. Jadili dhima za vielezi katika lugha ya Kiswahili.
5. Eleza jinsi matawi ya sarufi yanavyotofautiana na kuhusiana.

### Mofimu

Mofimu ni kipashio kidogo cha kimofolojia kilichomo akilini mwa msemaji wa lugha, ambacho ni cha kidhahania. Mofimu hudhihirishwa na mofu. Mathalani, mofu *ma*- katika neno *mananasi* imebeba mofimu ya wingi ambayo imo akilini mwa mtumiaji wa lugha. Kwa hiyo, tunaweza kusema kuwa mofimu ni dhana ambayo haiwezi kudhihirika kimatamshi wala kimaandishi.

### Mofu

Mofu ni kipashio cha kimofolojia kinachodhihirika kimatamshi na kimaandishi, au kinaweza kuwa kapa ambacho hudhihirisha mofimu. Kwa mfano, katika neno *amefika*, kuna mofu na mofimu zifuatazo:

| Mofu | | Mofimu |
|---|---|---|
| a- | - | nafsi (ya tatu umoja), idadi (umoja) |
| -me- | - | hali timilifu |
| -fik- | - | mzizi |
| -a- | - | kiambishi tamati cha uyakinishi |



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 132 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



**Aina za mofu**

Mofu zinaweza kuainishwa kwa kutumia vigezo viwili ambavyo ni kigezo cha maana na kigezo cha maumbo.

**(a) Kigezo cha maana**

Katika kigezo hiki tunapata aina mbili za mofu: (i) mofu zinazowakilisha mofimu huru na (ii) mofu zinazowakilisha mofimu funge. Mofu huru ni zile ambazo husimama peke yake kama maneno yanayojitosheleza kimaana. Kwa mfano, *kaka, chupa, ndoo,* na *maji*. Aidha, mofu za aina hii huweza kuungana na kuunda maneno ambatani. Kwa mfano:

(i) askari+ kanzu - askarikanzu

(ii) pembe +tatu - pembetatu

(iii) kuku + maji - kukumaji

(iv) paka + shume - pakashume

Mofu za aina ya pili haziwezi kusimama peke yake kama neno mpaka ziungane na mofu nyingine ili kujenga neno. Kwa mfano, katika neno *anapika*, mofu *a-*, *-na-*, *-pik-*, *-a* haziwezi kusimama kila moja peke yake bila kutegemeana. Mofu hizo ni lazima ziungane ili kutoa dhana inayokusudiwa na msemaji. Kwa ujumla, tunaweza kusema kuwa dhana ya mofimu na mofu zina uhusiano mkubwa. Uhusiano huo tunaweza kuuita uhusiano wa umbo na maana yake.

**(b) Kigezo cha maumbo**

Kigezo hiki kinazingatia mofu dhahiri na mofu kapa. Mofu dhahiri ni zile zinazoonekana na zinaweza kutamkika na kuandikika. Mofu kapa ni zile ambazo hazina maumbo dhahiri. Mifano ifuatayo inaonesha mofu dhahiri na mofu kapa. Mofu kapa zimeoneshwa kwa alama ø.

(i) øjiko - majiko
(ii) øgari - magari
(iii) ukuta - økuta
(iv) ukucha - økucha

Alama ø katika mifano hapo juu inaonesha kutokuwepo kwa umbo linalobeba mofimu husika katika neno (umoja au wingi).



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 133 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Dhima za mofimu**

Mofimu zina dhima mbalimbali katika neno kama ifuatavyo:

(a) Kuonesha nafsi na mtenda wa jambo. Kwa mfano:

(i) *ni*nakula – mofu *ni*- huonesha mofimu ya nafsi ya kwanza umoja

(ii) *a*nakula – mofu *a*- huonesha mofimu ya nafsi ya tatu umoja

(iii) *wa*takula – mofu *wa*- huonesha mofimu ya nafsi ya tatu wingi

(b) Kuonesha idadi. Kwa mfano:

(i) *m*-ku-lima – mofu *m*- huonesha mofimu ya umoja

(ii) *wa*-li-m-saidia – mofu *wa*- huonesha mofimu ya wingi

(c) Kuonesha njeo (wakati). Inaweza kuwa wakati uliopo, uliopita au ujao. Kwa mfano:

(i) u-*li*-lima - mofu -*li*- huonesha mofimu ya wakati uliopita

(ii) u-*na*-lima - mofu -*na*- huonesha mofimu ya wakati uliopo

(iii) u-*ta*-lima - mofu -*ta*- huonesha mofimu ya wakati ujao

(d) Kuonesha hali mbalimbali za matendo kama vile hali timilifu, masharti, mazoea na mfuatano wa matukio. Kwa mfano:

(i) Amani a-*me*-kula.
Mofu -*me*- huonesha mofimu ya hali timilifu.

(ii) U-*ki*-ja nitakupa zawadi.
Mofu -*ki*- huonesha mofimu ya hali ya masharti.

(iii) Mimi *hu*-anza kazi saa mbili asubuhi.
Mofu *hu*- huonesha mofimu ya hali ya mazoea.

(iv) Mkurugenzi alikuja, a*ka*toa maagizo kisha a*ka*ondoka.
Mofu *ka*- huonesha mofimu ya hali ya mfuatano wa matukio.

(e) Kuonesha urejeshi. Mofu -o-, -ye-, -vyo-, na -zo- zinaonesha mofimu za urejeshi. Kwa mfano:

(i) Wanafunzi wali -*o*- faulu walipewa zawadi.

(ii) Ng'ombe ali -*ye*- vunjika mguu yumo zizini.

(iii) Vyombo vili -*vyo*- nunuliwa ni vizuri sana.

(iv) Nyumba zili -*zo*- jengwa vizuri zinavutia.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 134 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



(f) Kuonesha kauli mbalimbali za vitenzi kama vile utendeshi, utendea, utendeka, utendwa, utendani na utenda. Tazama mifano ifuatayo kwa kuzingatia mfuatano wa kauli kama zilivyoorodheshwa:

(i) Waziri Mkuu ameend-*esh*-a kampeni ya kuchangia damu.(utendeshi)
(ii) Kazimoto alimpik-*i*-a Subira chakula. (utendea)
(iii) Ardhi hii inalim-*ik*-a vizuri. (utendeka)
(iv) Mbuzi amechinj-*w*-a. (utendwa)
(v) Dingiswayo na Zwida wanashauri-*an*-a. (utendani)
(vi) Mama anapik-*a*. (utenda, kiambishi tamati – uyakinishi)
(vii) Mama hapik-*i*. (utenda, kiambishi tamati – ukanushi)

Katika mifano (vi) hapo juu mofu –*a* huonesha kauli ya utenda (uyakinishi) kwa upande wa vitenzi vyenye asili ya Kibantu. Kwa upande wa ukanushi vitenzi vyenye asili ya lugha za Kibantu mofu –*i* huonesha kauli ya utenda (ukanushi) kama inavyoonekana katika mfano (vii) hapo juu. Katika vitenzi vyenye asili ya Kiarabu kama vile *sahau*, *safari*, na *shukuru* shina zima linaonesha kauli ya kutenda uyakinishi. Ikiwa vitenzi hivyo vitaambikwa mofu za ukanushi basi shina hilo litaonesha kauli ya utenda – ukanushi. Kwa mfano, *usisahau*, *hasafiri,* na *sikushukuru*. Aidha, mofu hizo hufanya kazi kama viambishi tamati maana. Viambishi tamati maana ni mofu zinazotokea mwishoni mwa kitenzi ili kukamilisha maana ya kitenzi hicho.

**Alomofu**

Kietimolojia, neno *alomofu* limeundwa na maneno mawili yenye asili ya lugha ya Kigiriki. Maneno haya ni *allo*- lenye maana ya *mbalimbali* au *tofautitofauti* na *morph* (mofu) lenye maana ya *umbo*. Kwa hiyo, alomofu ni maumbo mbalimbali ya mofimu moja. Maumbo haya huwa na maana na dhima moja kisarufi na hujitokeza katika mazingira tofauti ya kimtoano katika neno. Hii inamaanisha kwamba linapotokea umbo fulani linaloiwakilisha mofimu fulani, umbo lingine la mofimu ileile haliwezi kujitokeza katika nafasi ileile ya neno hilo. Kila umbo linalowakilisha mofimu husababishwa na mazingira fulani tofauti na lingine. Chunguza mifano ifuatayo ya ngeli ya kwanza katika Kiswahili.

(i) *m*-tu
(ii) *mu*-ungwana
(iii) *mw*-alimu



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 135 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Mofimu ya ngeli ya kwanza katika umoja wa maneno hayo inawakilishwa na maumbo (mofu) matatu. Maumbo hayo ni *m-*, *mu-* na *mw-*. Kwa hiyo, maumbo hayo matatu ni alomofu za mofimu ya umoja katika ngeli ya kwanza.

Alomofu hujitokeza pia katika kauli mbalimbali za vitenzi. Kwa mfano, mofimu ya kauli ya utendeshi inaweza kudhihirishwa na alomofu zifuatazo kwa kutegemea irabu inayounda mzizi wa vitenzi husika. Mizizi ya vitenzi vyenye irabu /a/, /i/ au /u/ hutumia alomofu -*ish*- na ile yenye irabu /e/ na /o/ hutumia -*esh*- kuwakilisha mofimu ya kauli ya utendeshi. Chunguza mifano ifuatayo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| (i) | paka | pak-*ish*-a | (mzizi una irabu *a*) |
| (ii) | pika | pik-*ish*-a | (mzizi una irabu *i*) |
| (iii) | fuga | fug-i*sh*-a | (mzizi una irabu *u*) |
| (iv) | ona | on –*esh*-a | (mzizi una irabu *o*) |
| (v) | cheka | chek-*esh*-a | (mzizi una irabu *e*) |

Hata hivyo, ni vema ieleweke wazi kuwa kuna baadhi ya vitenzi havitumii alomofu hizo. Tazama mifano ifuatayo:

| | | |
|---|---|---|
| (i) | lia | li-*z*-a |
| (ii) | jaa | ja-*z*-a |
| (iii) | ogopa | ogo-*fy*-a |
| (iv) | lewa | le-*vy*-a |

Katika mifano hapo juu maumbo –*ish*-, -*esh*-, -*z*-, -*fy*- na –*vy*- ni alomofu za mofimu moja ya utendeshi.

**Dhana ya shina**

Shina ni sehemu ya neno ambayo kwa kawaida huwa na kiambishi tamati isipokuwa katika maneno yanayoweza kusimama kama mofimu huru. Shina haliwezi kuongezewa viambishi baada ya kiambishi tamati. Aidha, mofimu huru nayo huweza kurejelewa kama shina. Kwa hiyo, si mashina yote yana kiambishi tamati. Hii ndiyo sababu ya dhana ya mofimu huru na shina kuwa na uhusiano wa karibu. Chunguza mifano katika jedwali lifuatalo:

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 136 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


**Jedwali 4.3** Maumbo ya mofimu huru na shina katika Kiswahili

| Neno | Mofimu huru | Shina |
|---|---|---|
| chupa | chupa | chupa |
| kalamu | kalamu | kalamu |
| dada | dada | dada |
| kaka | kaka | kaka |
| paka | paka | paka |

Kuna aina mbili za mofimu ambazo ni mofimu huru na mofimu funge. Mofimu funge ni mofimu ambayo haiwezi kusimama peke yake na kuleta maana. Kwa mfano, mofimu inayowakilishwa na mzizi *-imb-* haiwezi kuleta maana bila kufungamanishwa na mofu nyingine funge. Kwa mfano:

(i) u-na -*imb* -a
(ii) w -*imb* -o
(iii) wa-*imb*-aji
(iv) u-*imb*-aji
(v) mw-*imb*-aji

## Dhana ya mzizi

Mzizi ni neno au sehemu ya neno ambayo haibadiliki baada ya kuondolewa viambishi. Mzizi ndiyo msingi wa kila neno. Hivyo, kila neno sharti liwe na mzizi wake. Mzizi hubeba maana ya msingi ya neno linalohusika. Mathalani, kwa kutumia mzizi -*let*- tunapata maneno kama vile:

(i) *let*a
(ii) wali*let*wa
(iii) ame*let*ewa
(iv) wata*let*eana

## Uambishaji katika Kiswahili

Kiswahili ni lugha ambishi, yaani maneno yake mengi hubeba viambishi mbalimbali. Kabla ya kufafanua dhana yenyewe ya uambishaji, ni vema kwanza tuelewe dhana ya viambishi.


PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 137 25/09/2019 13:57
For Online Use Only

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Dhana ya viambishi**

Viambishi ni mofu tegemezi zinazoambikwa kwenye mzizi wa neno ili kudokeza dhana fulani ya kisarufi au kuunda neno jipya. Katika muundo wa maneno ya Kiswahili viambishi hupachikwa kabla na baada ya mzizi wa neno. Viambishi huainishwa kwa kigezo cha nafasi ambapo viambishi hivyo hutokea. Kwa hiyo, kuna viambishi vinavyotokea kabla ya mzizi wa neno ambavyo huitwa viambishi awali na vile vinavyotokea baada ya mzizi wa neno huitwa viambishi tamati. Tazama mifano ifuatayo:

(a) (i) *a-na*-pik-a
(ii) *wa-ta*-kimbi-a
(iii) *u-me*-ruk-a
(iv) *ha-tu-ku-m*-som-e-a

(b) (i) a-ta-ni-pig-*i-a*
(ii) a-me-m-som-*esh-a*
(iii) m-chez-*o*

Viambishi vilivyoandikwa kwa hatimlalo katika (a) hapo juu ni viambishi awali na katika (b) ni viambishi tamati.

**Dhana ya uambishaji**

Uambishaji ni mchakato wa uundaji wa maneno kwa kuongeza viambishi awali, kati au tamati kwenye mzizi wa neno. Hata hivyo, lugha ya Kiswahili haina viambishi kati. Kwa hiyo, lugha ya Kiswahili ina uambishaji ambao hufanyika kabla na baada ya mzizi. Kwa mfano, mzizi *som-* unaweza kuwekewa viambishi kama ifuatavyo: *u*-som-*i*, som-*o*, *a-na*-som-*a*, som-*e-a*, som-*esh-a*, *ki*-som-*o*, na *m*-som-*i*.

**Aina za uambishaji**

Kuna aina mbili za uambishaji ambazo ni uambishaji nyambulishi au unyambulishaji na uambishaji wa kisarufi au uambatizi.

**(a) Uambishaji nyambulishi (unyambulishaji)**

Huu ni uambishaji wenye uamilifu wa kuunda maneno mapya. Matokeo ya uambishaji huu hubadili aina ya neno au kupanua maana ya neno. Angalia mifano ifuatayo:

(i) piga (T) - pi*go*, *ki*pigo, *m*piga*ji*, mpig*anaji*, pig*ano* (N)



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 138 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



(ii) safi(V)- safi*sha* (T) *u*safi (N)

(iii) taifa (N) –taifi*sha* (T)

Katika mifano hiyo hapo juu, viambishi vilivyoandikwa kwa hatimlalo ndivyo vilivyobadilisha aina za maneno hayo. Hata hivyo uambishaji huu unajitokeza tena kwenye kipengele cha uundaji wa maneno katika aya zinazofuata.

**(b) Uambishaji wa kisarufi (uambatizi)**

Huu ni uambishaji ambao uamilifu wake ni kupachika viambishi vyenye kazi za kisarufi kwenye mzizi. Uambishaji huu haubadilishi kategoria za maneno bali huongeza maana za kisarufi katika neno. Hii ndiyo sababu inayofanya uambishaji wa aina hii uitwe uambishaji wa kisarufi. Viambishi vyenye dhima ya kisarufi ni kama vile viambishi vya ngeli, nafsi, njeo, urejeshi, au yambwa. Wakati mwingine, uambishaji wa namna hii huitwa *uambatizi*. Viambishi vilivyoandikwa kwa hatimlalo katika mifano ifuatayo ni mifano ya viambishi vyenye dhima ya kisarufi:

-pig- *a*-*na*-pig-a

*a*-*na*-*ye*-pig-a

*a*-*na*-*ye*-*m*-pig-a

## Zoezi la 4.2

1. Kwa kutumia mifano jadili dhana ya mofu, mofimu na viambishi.
2. Tofautisha kwa mifano dhana za uambishaji nyambulishi na uambishaji wa kisarufi.
3. Bainisha viambishi katika maneno yafuatayo:
   (a) lililonikera
   (b) tutafahamiana
   (c) walikikimbilia
   (d) sababu
   (e) magazeti
   (f) hawajajadiliana
4. Kwa kutumia mifano ya vitenzi vya lugha ya Kiswahili, onesha alomofu za kauli ya utendea na kauli ya utendeka.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 139 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Uundaji wa maneno**

Uundaji wa maneno ni mchakato wa uongezaji wa msamiati wa lugha kwa njia mbalimbali kwa lengo la kukidhi mahitaji ya lugha. Kutokana na maendeleo ya jamii katika nyanja mbalimbali, mahitaji ya matumizi ya lugha huongezeka siku hadi siku. Kutokana na kuongezeka kwa mahitaji hayo, taratibu mbalimbali hutumika katika kupata msamiati mpya ili kuziba pengo la msamiati linalojitokeza.

**Sababu za uundaji wa maneno**

Kuna sababu mbalimbali za msingi ambazo huwalazimu watumiaji wa lugha kuunda msamiati. Sababu hizi ni kama zifuatazo:

(i) Kuibuka kwa mambo mapya katika jamii na shughuli mbalimbali kama vile za kiuchumi, kisayansi, kiafya, kisiasa, na kiutamaduni. Kuongezeka na kupanuka kwa shughuli nyingi kumesababisha vitu vipya ambavyo hapo mwanzo havikuwepo katika jamii. Kwa mfano, maendeleo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano yamekuja kwa kasi kubwa na kuingiza istilahi nyingi ambazo hazikuwepo katika lugha ya Kiswahili. Kuna istilahi mpya zinazotokana na maendeleo haya kama vile *mtandao, kikokotozi, tovuti, simumtelezo, nukushi*, na *muamala*.

(ii) Kukidhi haja ya mawasiliano ya kila siku katika nyanja mbalimbali. Haja ya mawasiliano katika taaluma mbalimbali hulazimu kuundwa kwa istilahi mpya ili kutosheleza mahitaji hayo. Katika uhitaji huu tunapata maneno kama *muamala* (benki–uchumi), *mrabaha* (uhasibu), *kirai na kishazi* (isimu), na *makinikia* (madini). Istilahi hizi zinatumika katika uwanja mahususi wa kitaaluma kama inavyoonyeshwa.

(iii) Kukuza lugha ili kukidhi mahitaji ya jamii katika maeneo mbalimbali. Sababu nyingine ya kuunda maneno ni kukuza lugha na kuifanya ikidhi mahitaji ya kimawasiliano. Lugha inapokuzwa, huweza kuendelea na kujitosheleza kimawasiliano na hivyo kuiwezesha kutumika katika nyanja mbalimbali.

**Njia za uundaji wa maneno**

Kuna njia mbalimbali ambazo hutumika kuunda maneno mapya katika lugha ya Kiswahili. Njia hizi ni kukopa na kutohoa msamiati, kufupisha maneno, uambatanishaji, uradidi, unyambulishaji, kupanua maana za maneno, na ufananisho.

**(a) Kukopa na kutohoa msamiati**

Kukopa ni mbinu ya kuchukua msamiati kutoka katika lugha moja na



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

For Online Use Only

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 140 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



kuuingiza katika matumizi ya lugha nyingine. Katika mchakato wa ukopaji, maneno hufanyiwa marekebisho kulingana na taratibu za lugha inayokopa. Urekebishaji huo huitwa utohoaji. Mbinu hii ya kukopa hutumiwa na watumiaji wa lugha zote duniani. Ukopaji na utohoaji wa msamiati hutokana na sababu zifuatazo:

(i) Mwingiliano baina ya watumiaji wa lugha zaidi ya moja
Jamiilugha mbili au zaidi zinapokaribiana huweza kuathiriana katika matumizi ya lugha na hata utamaduni wake. Kwa njia hii, kila jamiilugha huweza kukopa msamiati wa jamiilugha nyingine. Kwa mfano, mwingiliano wa jamii za Waarabu na Waswahili katika upwa wa Afrika Mashariki umesababisha Kiswahili kikope maneno mengi ya Kiarabu. Maneno hayo ni kama vile *adabu, ghadhabu,* na *shikamoo*. Vilevile, kutokana na Kiswahili kutumika pamoja na Kiingereza, Kiswahili kimetohoa maneno mengi ya Kiingereza kama vile *shati*, *baiskeli*, *soksi*, *kemia*, *na lori*. Aidha, Kiswahili kimekopa maneno kutoka lugha nyingine za jamii za Kibantu. Mifano ya maneno hayo ni *ikulu* (Kinyamwezi/Kigogo), *kitivo* (Kipare), *ngalemu* (Kimasai), *ngeli* (Kihaya), na *ng'atuka* (Kizanaki).

(ii) Tofauti za uchumi na teknolojia
Jamii mbalimbali zinatofautiana kisayansi, kiuchumi na kiteknolojia. Jamii ambayo imeendelea katika nyanja hizo itavumbua vitu vingi. Hivyo, jamii nyingine ambazo hutumia vitu hivyo hulazimika kukopa majina ya vitu hivyo kutoka katika jamii zilizoendelea. Kwa mfano, Kiswahili kimekopa kutoka katika Kiingereza maneno kama vile *data*, *stigma* na *video*. Maneno yaliyotoholewa ni kama vile *kompyuta*, *kamera*, *redio*, *televisheni*, na *fotokopi*.

(iii) Kuibuka kwa shughuli ambazo hazikuwepo mwanzoni
Ukopaji na utohoaji wa maneno huweza kutokea panapokuwa na shughuli ambazo hazikuwepo katika jamii. Mifano ya shughuli hizo ni kama vile *dini, vyombo vya usafiri, michezo,* na *mawasiliano* ambazo zimeingiza maneno kama vile *soka*, *vuvuzela*, *treni*, *katekista*, *mhashamu*, *shehe*, *ustadhi*, *helikopta*, *basi*, *boti*, na *netiboli* katika Kiswahili.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 141 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**(b) Kufupisha maneno**

Kufupisha maneno ni kitendo cha kuchukua herufi za mwanzo za maneno au sehemu za maneno na kuziweka pamoja ili kupata neno jipya. Kuna aina mbili za ufupishaji wa maneno. Njia hizo ni akronimu na uhulutishaji.

(i) Akronimu ni njia ya ufupishaji ambapo herufi za mwanzo katika kila neno katika jina ambalo linaundwa na maneno mengi huunganishwa ili kuunda neno moja. Aghalabu, maneno ya namna hii huwa ni majina ya taasisi, vyama na mashirika. Mfano wa maneno haya ni:

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET)

Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI)

Baraza la Mitihani la Taifa (BAMITA)

Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI)

(ii) Uhulutishaji ni njia ya ufupishaji ambapo sehemu ya neno au maneno huunganishwa na sehemu ya neno jingine kuunda neno jipya. Tazama mifano ifuatayo:

| | | |
|---|---|---|
| chakula cha jioni | - | chajio |
| chakula cha mchana | - | chamcha |
| hati za kukataza | - | hatazo |
| biolojia na kemia | - | biokemia |
| fupa la paja | - | fupaja |
| hati ya kumiliki | - | hatimiliki |

**(c) Uambatanishaji**

Huu ni mchakato wa kuunganisha maneno mawili au zaidi ili kupata neno moja ambalo huwa na maana tofauti na maneno ya awali. Tazama mifano ifuatayo:

| | | |
|---|---|---|
| bata + mzinga | - | batamzinga |
| mwana + hewa | - | mwanahewa |
| mwana + maji | - | mwanamaji |
| bongo + lala | - | bongolala |



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 142 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


| | | |
|---|---|---|
| jungu + kuu | - | jungukuu |
| pembe + tatu | - | pembetatu |
| mwana + isimu + jamii | - | mwanaisimujamii |

**(d) Uradidi**

Uradidi ni njia ya kurudia neno zima au sehemu ya neno ili kuunda neno jipya. Tazama mifano ifuatayo:

| | | |
|---|---|---|
| mbali | - | mbalimbali |
| pole | - | polepole |
| haraka | - | harakaharaka |
| taka | - | takataka |
| kata | - | katakata |

**(e) Unyambulishaji**

Uambishaji nyambulishi ni njia ambayo inahusu kuongeza viambishi katika mzizi wa neno na kupata maneno mapya. Uongezaji wa viambishi katika mzizi wa neno, hususani ule unaolenga kuhamisha neno kutoka aina moja kwenda aina nyingine, ndiyo unaohusika katika uundaji wa maneno. Chunguza mifano ifuatayo:

| | | |
|---|---|---|
| imba (T) | - | wimbo, mwimbaji na uimbaji (N) |
| cheza (T) | - | mchezo, mchezaji na mchezeshaji (N) |
| zuri (V) | - | uzuri (N) |
| taifa (N) | - | taifisha (T) |

**(f) Ufananisho**

Hii ni njia ya kuunda maneno kwa kuhusianisha na milio, umbile, tabia au matumizi ya kitu kinachohusika. Maneno yanayoundwa kwa kutumia njia hii hutumia vigezo vifuatavyo:

(i) Kufananisha sauti (onomatopeia au tanakali sauti). Katika kigezo hiki, uundaji wa maneno huiga sauti au mlio wa kitu kinachopewa jina hilo. Kwa njia hii tunapata maneno kama vile *pikipiki*, *nyau*, *mtutu*, *malapa*, *kuku*, *vuma*, *mvumo*, na *cherehani*.


PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 143 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(ii) Kuangalia umbo au maumbile ya kitu. Njia hii huunda maneno kwa kuangalia mwonekano wa kitu kinachopewa jina. Hapa tunapata maneno mapya kama vile *kifaru* (gari la kivita la kijeshi ambalo linafanana na mnyama anayeitwa kifaru) na *kidoletumbo* (ni sehemu ya utumbo mpana ambayo inafanana na umbile la kidole).

(iii) Kukipa kifaa jina kutokana na matumizi yake. Kwa mfano, *kipimajoto*, *ufagio*, *kifuniko*, na *kibanio*.

## Zoezi la 4.3

1. Kwa kutumia mifano, elezea umuhimu wa kuunda maneno mapya katika lugha ya Kiswahili.
2. Kuna tofauti gani kati ya utohoaji na ukopaji wa maneno?
3. Taja njia zilizotumika kuunda maneno yafuatayo:
   (a) pundamilia
   (b) jotoridi
   (c) kilimo
   (d) TAKILUKI
   (e) kitivo
   (f) tangatanga
4. Tathmini jinsi maendeleo ya sayansi na teknolojia yanavyosababisha ukuaji wa msamiati wa lugha ya Kiswahili.
5. Kwa kutumia mifano dhahiri, jadili mbinu tano za uundaji wa maneno.

### Kauli za vitenzi vya Kiswahili

Kauli za vitenzi vya Kiswahili hubebwa katika viambishi tamati vya vitenzi. Viambishi hivi huwekwa kabla ya irabu tamati. Miongoni mwa kauli za vitenzi vya Kiswahili ni kauli ya *utenda*, *utendwa*, *utendeka*, *utendani*, *utendea*, na *utendeshi*.

**(a) Kauli ya utenda**

Katika kauli hii kitenzi hubainisha mtendaji wa tendo. Kitenzi huwa hakina kiambishi tamati chochote isipokuwa irabu tamati. Kwa mfano, tukisema, *Mwalimu anafundisha*, mtenda ni *mwalimu* na kauli ni ya utenda. Chunguza mifano ifuatayo:

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 144 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



(i) Amani *anacheza*.

(ii) Rehema *anaandika*.

(iii) Ali *atalima* bustani.

(iv) Wanafunzi *walifanya* mtihani.

**(b) Kauli ya utendwa**

Hii ni kauli inayoonesha mwathiriwa wa tendo linalotajwa na kitenzi. Katika kauli hii, mtenda wa jambo sio lazima atambulike. Ikiwa italazimika kutambuliwa basi kitaongezeka kihusishi *na* kikiambatana na jina au kiwakilishi cha mtenda. Mofu ya utendwa ni -*w*-. Mifano ifuatayo inaonesha kauli ya utendwa katika Kiswahili:

(i) Chakula kimepik*w*a.

(ii) Mwizi amekamat*w*a.

(iii) Nyumba imejeng*w*a na mwashi.

(iv) Uchafu umetup*w*a na mama.

**(c) Kauli ya utendeka**

Hii ni kauli inayoonesha uwezekano wa jambo kufanyika au kuwa na hali ya kufanyika. Katika kauli hii tendo haliwekwi wazi kuwa linatendwa na nani bali huonesha uwezekano wa kutendeka kwa tendo hilo. Mofu za kauli ya utendeka ni -*ek*-, -*ik*-, -*lik*- na -*lek*-. Tazama mifano ifuatayo:

(i) Kitabu kinasom*ek*a.

(ii) Kuta zinajeng*ek*a.

(iii) Wavivu wanafaham*ik*a.

(iv) Pori linaingi*lik*a.

(v) Mazoezi yanafany*ik*a.

(vi) Udongo unazo*lek*a.

Mofu za kauli ya utendeka hujitokeza kama -*ik*- ikiwa mzizi wa kitenzi una irabu *a*, *i* au *u* na huwa -*ek*- ikiwa mzizi una irabu *e* au *o*. Ikiwa kitenzi kina irabu *a*, *i* au *u* katika mzizi na kuishia na irabu mbili basi mofu ya utendeka itakuwa -*lik*- na ikiwa mzizi una irabu *e* au *o* na kuishia na irabu mbili basi mofu ya utendeka itakuwa -*lek*-.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 145 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**(d) Kauli ya utendani**

Katika kauli hii, watendaji hufanyiana tendo hilo hilo kwa wakati mmoja. Mofu ya kauli ya utendani ni -*an*-. Mofu zilizoandikwa kwa hatimlalo katika mifano ifuatayo zinaonesha kauli ya utendani.

(i) Juma na Paulo wanatembele*ana*.

(ii) Watoto wanape*ana* zawadi.

(iii) Mabasi yamepish*ana* vizuri.

(iv) Walimu wanasaidi*ana* kazi.

**(e) Kauli ya utendea**

Katika kauli hii mtendaji hufanya tendo fulani badala au kwa niaba ya mhusika mwenyewe. Mofu za kauli hii ni -*i*-, -*e*-, -*li*- na -*le*-. Tazama mifano ifuatayo:

(i) Mwanahamisi amempik*i*a mtoto chakula.

(ii) Zabibu atamsom*e*a mama yake kitabu.

(iii) Wanafunzi walimkimbi*li*a mwalimu wao.

(iv) Kalimanzila alimzo*le*a bibi yake takataka.

Mofu za kauli ya utendea hujitokeza kama -*i*- ikiwa mzizi wa kitenzi una irabu *a*, *i* au *u* na huwa -*e*- ikiwa mzizi una irabu *e* au *o*. Ikiwa kitenzi kina irabu *a*, *i* au *u* katika mzizi na kuishia na irabu mbili basi mofu ya utendea itakuwa -*li*- na ikiwa mzizi una irabu *e* au *o* na kuishia na irabu mbili basi mofu ya utendea itakuwa -*le*-.

**(f) Kauli ya utendeshi au usababishi**

Hii ni kauli ambayo inaonesha hali ya kusababisha kutokea kwa tendo fulani. Mofu za kauli hii ni -*esh*-, -*ish*-, -*z*-, -*lish*-, -*lesh*-, -*fy*-, na -*vy*-. Mifano ifuatayo inaonesha utokeaji wa kauli hii katika Kiswahili:

(i) Bibi alimbeb*esh*a mjukuu mzigo wake.

(ii) Pit*ish*a kamba hii kwenye miti.

(iii) Kombo alimwoza bintiye mwezi uliopita.

(iv) Sisi tutamka*lish*a mtuhumiwa kikao.

(v) Mama amemzo*lesh*a Pili uchafu.

(vi) Matukio ya mauaji yanaogo*fy*a.

(vii) Sanga alimeza dawa za malaria zikamle*vy*a.

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 146 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


Katika kauli hii kuna maumbo mbalimbali yanayoonesha kauli ya utendeshi. Mofu ya kauli ya utendeshi huwa -*ish*- ikiwa mzizi wa kitenzi una irabu *a*, *i* au *u* na huwa -*esh*- ikiwa mzizi una irabu *e* au *o*. Ikiwa kitenzi kina irabu *a*, *i* au *u* katika mzizi na kuishia na irabu mbili basi mofu ya utendeshi itakuwa -*lish*- na ikiwa mzizi una irabu *e* au *o* na kuishia na irabu mbili basi mofu ya utendeshi itakuwa -*lesh*-. Vitenzi vingine vichache kama vile *lia*, *lala*, *jua*, *toa*, na *oa* hutumia mofu -*z*-. Vilevile, kuna vitenzi vichache ambavyo hutumia mofu -*vy*- na -*fy*-. Kwa mfano, *levya* katika neno *lewa* na *ogofya* katika neno *ogopa*. Hata hivyo, maneno haya huweza kutumia -*esh*- kama ilivyo katika maneno *lewesha* na *ogopesha*.

Kutokana na mifano hiyo hapo juu ni dhahiri kuwa viambishi vya kauli za vitenzi hutokea baada ya mzizi. Viambishi hivi ndivyo huwakilisha kauli mbalimbali za vitenzi katika lugha ya Kiswahili. Aidha, imebainika kuwa viambishi vya kauli moja huweza kuwa na maumbo tofautitofauti lakini yakibeba dhana ile ile ya kisarufi. Dhana au maana hiyo ya kisarufi huitwa mofimu. Kwa hiyo, maumbo hayo ni alomofu za mofimu moja. Kwa mfano, -*esh*-, -*ish*-, -*z*-, -*lish*-, -*lesh*-, -*vy*-, na -*fy* - ni alomofu za mofimu ya usababishi

## Zoezi 4.4

1. Badilisha vitenzi vifuatavyo viwe katika kauli ya utendeka, kisha bainisha alomofu zinazojikeza katika kauli hiyo:
   (a) fua
   (b) chukua
   (c) toa
   (d) pita
   (e) hesabu
   (f) soma
2. Orodhesha vitenzi katika kauli ya utendeshi kwa kuzingatia maumbo mbalimbali.


PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 147 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Ngeli za nomino**

Ngeli ni neno lenye asili ya lugha ya Kihaya likiwa na maana ya aina ya kitu au vitu. TUKI (2004) inasema kuwa neno ngeli katika taaluma ya sarufi lina maana ya kundi la nomino zenye sifa zinazofanana kisarufi. Hivyo, ngeli za nomino ni makundi ya majina yaliyopangwa kwa kuzingatia sifa za majina hayo kama vile maumbo ya umoja na wingi au upatanisho wa kisarufi. Ngeli za nomino husaidia kuzipanga nomino katika makundi na kurahisisha ujifunzaji na utumiaji wa lugha ya Kiswahili.

**Mitazamo ya uainishaji wa ngeli za nomino**

Ngeli za nomino katika lugha ya Kiswahili zimeainishwa kwa mitazamo mikuu miwili, ambayo ni mtazamo wa kimapokeo na mtazamo wa kisasa.

***Mtazamo wa kimapke o***

Uainishaji wa ngeli za nomino katika mtazamo huu huzingatia viambishi awali vya umoja na wingi. Mtazamo huu hujulikana pia kama mtazamo wa kimofolojia au maumbo. Katika mtazamo huu, maumbo ya viambishi awali vya nomino katika umoja na wingi hutumika kuainisha ngeli. Nomino zenye viambishi awali vinavyofanana hupangwa pamoja na kuwa kundi moja la ngeli, kama inavyodhihirika katika jedwali 4.4 hapa chini.

**Jedwali 4.4** Ngeli za nomino kwa mtazamo wa kimapokeo (kimaumbo) (Guthrie, 1948; Polomé 1967).

| Ngeli | Viambishi | Mifano |
|---|---|---|
| 1 | m-, mu-, mw- | mtu, muuguzi, mwanafunzi (hujumuisha majina yote ya viumbe hai isipokuwa mimea |
| 2 | wa- | watu, wauguzi, wanafunzi |
| 3 | m-, mu-, mw- | mti, muwa, mwiba |
| 4 | mi- | miti, miwa, miba |
| 5 | ji-, ø- | jiwe, jicho, sikio, gome |
| 6 | ma- | mawe, macho, masikio, magome |
| 7 | ki- | kiti, kisu, kikombe |
| 8 | vi- | viti, visu, vikombe |
| 9 | n-, ø- | nguo, ndoo, nchi, mboga, meza |
| 10 | n-, ø- | nguo, ndoo, nchi, mboga, meza |



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 148 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



| Ngeli | Viambishi | Mifano |
|---|---|---|
| 11 | u- | ulimi, ukuta, ukucha |
| 12 | *ka, | kalimi, katoto |
| 13 | *tu- | tulimi, tutoto |
| 14 | u- | uzuri, ubaya, uovu, uasi, ugonjwa |
| 15 | ku- | kuogelea, kukimbia, kuimbia |
| 16 | pa- | pale |
| 17 | mu- | mule |
| 18 | ku- | kule |

*ka- na *tu- zilitoweka; sasa zimeanza kutumika.
Alama ø imetumika kuonesha kwamba nomino za kundi hilo hazina viambishi awali vya umoja au wingi.

Uainishaji huu unatofautiana na uainishaji wa mwanaisimu mwingine, Broomfield ambaye aliweka majina ya umoja na wingi katika kundi moja la ngeli. Uainishaji wa Broomfield ulipunguza idadi ya makundi na kupata ngeli nane kama ifuatavyo:

**Jedwali 4.5** Ngeli za nomino kwa mtazamo wa kimapokeo (Broomfield, 1935)

| Ngeli | Viambishi (umoja/wingi) | Mifano ya maneno |
|---|---|---|
| 1 | mu-/wa- | msomi-wasomi mtu- watu |
| 2 | m-/mi- | mti -miti mto - mito |
| 3 | ki-/vi- | kijiti - vijiti kijiko - vijiko |
| 4 | n-n | nguo – nguo |
| 5 | ji-/ma- | jicho - macho jiwe - mawe |
| 6 | u-/ny-<br>u-/ma- | uso – nyuso<br>ugonjwa – magonjwa |
| 7 | pa-<br>mu-<br>ku- | pale<br>mule<br>kule |
| 8 | ku- | kuimba, kuruka, kucheza |



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 149 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Ubora wa mtazamo wa kimapokeo**

Mtazamo huu una ubora ufuatao:

(i) Ni rahisi kuzipanga nomino katika ngeli kwa kuangalia viambishi awali vinavyofanana katika maumbo ya umoja na wingi.

(ii) Kwa kupanga nomino katika umoja na wingi, ni rahisi kujua nomino zisizo na umoja na wingi.

(iii) Husaidia katika kuthibitisha Ubantu wa Kiswahili kwa kuangalia viambishi vya umoja na wingi.

(iv) Mtazamo huu ndiyo msingi mkuu wa kuainisha ngeli za nomino za Kiswahili.

**Udhaifu wa mtazamo wa kimapokeo**

(i) Baadhi ya nomino hazina maumbo ya umoja na wingi. Kwa mfano, *kalamu, karatasi,* na *barabara*.

(ii) Nomino za viumbe hai zilichanganywa na vitu visivyo na uhai kwa kuwekwa katika ngeli ya KI-/VI-. Nomino hizi ni kama vile *kiongozi – viongozi, kiti-viti* na *kiranja–viranja.*

(iii) Wanaisimu walioainisha kwa mtazamo huu wanatofautiana katika idadi. Ni vigumu kutambua idadi sahihi ya ngeli za nomino. Guthrie na Polomé walibainisha makundi 18, Broomfield alibainisha makundi 8.

(iv) Kuna mwingiliano wa viambishi katika baadhi ya ngeli. Kwa mfano, viambishi vya ngeli ya kwanza umoja vinafanana na vya ngeli ya tatu umoja kwa mtazamo wa Guthrie na Polomé.

(v) Uainishaji wa ngeli ya 16, 17 na ya 18 unajikita katika vielezi vya mahali na si katika nomino.

***Mtazamo wa kisasa***

Uainishaji wa ngeli za nomino kwa mtazamo huu huzingatia viambishi vya upatanisho wa kisarufi. Mtazamo huu hujulikana pia kama mtazamo wa kimamboleo au mtazamo wa upatanisho wa kisarufi (kisintaksia). Upatanisho wa kisarufi ni hali ya nomino au kiwakilishi kupatana au kuendana na kiambishi chake kiwakilishi katika maneno yanayoandamana nayo. Chunguza mifano ifuatayo:

(i) Kitabu hi*ki ki*navutia - Vitabu hi*vi vi*navutia.

(ii) Meza hi*i i*napendeza - Meza hi*zi zi*napendeza.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 150 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Viambishi vilivyoandikwa kwa hatimlalo katika mifano (i) – (ii) hapo juu vinaonesha upatanisho wa kisarufi.

Uainishaji wa ngeli za nomino kwa mtazamo huu huzingatia kiambishi awali cha kitenzi katika umoja na wingi. Miongoni mwa wataalamu walioainisha ngeli za nomino kwa mtazamo huu ni Nkwera (1978), Kapinga (1983) na TUMI (1988). Mtazamo wa kisasa umejikita katika upatanisho wa kisarufi kwa kuzingatia nomino za ngeli zilizobainishwa na wanamapokeo. Uainishaji huu umezigawa ngeli katika makundi tisa kama ifuatavyo:

**Jedwali 4.6** Ngeli za nomino kwa mtazamo wa kisasa

| Ngeli | Viambishi | Mifano |
|---|---|---|
| 1 | YU/A - WA | Mtoto *a*nakuja/ mtoto *yu*aja<br>Watoto *wa*nakuja/ watoto *wa*ja |
| 2 | U – I | Mti *u*mekatwa<br>Miti *i*mekatwa |
| 3 | LI – YA | Jicho *li*mevimba<br>Macho *ya*mevimba |
| 4 | KI – VI | Kiti *ki*mevunjika<br>Viti *vi*mevunjika |
| 5 | I – ZI | Nguo *i*meshonwa<br>Nguo *zi*meshonwa |
| 6 | U – ZI | Ukuta *u*mejengwa<br>Kuta *zi*mejengwa |
| 7 | U – YA | Uasi *u*mezidi<br>Maasi *ya*mezidi |
| 8 | Ku | Kucheza *ku*nachangamsha |
| 9 | PA<br>MU<br>KU | Pale *pa*napendeza<br>Mule *mu*napendeza<br>Kule *ku*napendeza |



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 151 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Ubora wa mtazamo wa kisasa**

Mtazamo wa kisasa una faida zifuatazo:

(a) Husaidia kuondoa utata kwenye nomino zenye maana zaidi ya moja. Tazama mifano ifuatayo:

(i) Paa *a*naruka - Paa *wa*naruka.

(ii) Paa *li*meezekwa - Mapaa *ya*meezekwa.

Katika mfano (i) neno *paa* lipo katika ngeli ya YU-A-WA ambalo linamaanisha *aina ya mnyama*. Katika mfano (ii) neno *paa* lipo katika ngeli ya LI –YA ambalo linamaanisha *sehemu ya juu ya nyumba*.

(b) Husaidia kuweka nomino za viumbe hai katika ngeli inayohusika ambayo ni ngeli ya YU/A - WA. Mfano wa nomino hizo ni:

(i) Kiongozi *a*naimba - Viongozi *wa*naimba

(ii) Mbuzi *a*mechinjwa - Mbuzi *wa*mechinjwa.

(c) Husaidia kutumia lugha kwa usahihi kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi.

(d) Mtazamo huu hautatanishi kwa vile viambishi awali katika kitenzi huwa bayana kwa kuwa hurejelea kitajwa. Kwa mfano, mtu akisema, *Ameanguka*, ina maana ya *mtu au mnyama* lakini akisema, *Umeanguka* ina maana ya *mti* kama vile *mpera*, *mpapai*, na kadhalika.

(e) Husaidia kuthibitisha Ubantu wa Kiswahili kwa kutumia kigezo cha kisintaksia.

**Udhaifu wa mtazamo wa kisasa**

Mtazamo wa kisasa una mapungufu yafuatayo:

(i) Baadhi ya nomino zinakosa ngeli. Nomino hizo ni kama vile *uji*, *njaa* na *maji*.

(ii) Kuna mwingiliano wa viambishi katika ngeli. Kwa mfano, ngeli ya 2, 6 na ya 7 zina kiambishi cha umoja ambacho ni U-, ngeli ya 5 na ya 6 zina kiambishi cha wingi ZI-. Pia, ngeli ya 3 na ya 7 zina kiambishi cha wingi YA-.

(iii) Kiambishi YU- cha ngeli ya kwanza umoja ni cha kilahaja na si Kiswahili sanifu.

(iv) Uainishaji wa ngeli katika mtazamo huu umejikita katika viambishi awali vya vitenzi badala ya nomino ambazo ndizo msingi wa uainishaji wa ngeli.

(v) Uainishaji huu umetumia viwakilishi vya mahali katika ngeli ya tisa badala ya nomino.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 152 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



## Zoezi la 4.5

1. Eleza kwa mifano dhana ya ngeli za nomino.
2. Eleza tofauti ya uainishaji wa ngeli kwa mtazamo wa kimapokeo na wa kisasa.
3. Ainisha ngeli za nomino zifuatazo kwa mtazamo wa kisasa na wa kimapokeo; soko, kalamu, kitabu, kiti, kifaranga na majani.

## Tamrini

1. Fafanua namna nonimo za Kiswahili zinavyoweza kujibainisha katika mtazamo wa kimapokeo wa ngeli za nomino.
2. Eleza maana ya kiwakilishi kisha bainisha aina za viwakilishi.
3. Fafanua kwa mifano jinsi vivumishi vya Kiswahili vinavyoweza kuainishwa.
4. Jadili maana ya kitenzi na aina zake.
5. Eleza maana ya kielezi, kisha bainisha aina zake.
6. Ainisha vihisishi katika Kiswahili.
7. Fafanua aina za viunganishi.
8. Fafanua kwa mifano vipengele vya kisarufi ambavyo huweza kujitokeza kwenye vitenzi vya Kiswahili.

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 153 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Tano Tungo za Kiswahili

## Utangulizi

Sura hii inahusu tungo za Kiswahili. Katika sura hii, utajifunza dhana na aina za tungo. Vilevile, utajifunza uchanganuzi wa sentensi na urejeshi katika tungo za Kiswahili. Lengo la sura hii ni kukuwezesha kupata maarifa na ujuzi kuhusu tungo na uchanganuzi wa sentensi.

**Dhana ya tungo**

Tungo ni kipashio cha kimuundo kinachotokana na uwekaji pamoja wa vipashio vidogovidogo ili kujenga kipashio kikubwa zaidi. Uwekaji pamoja wa vipashio huongozwa na kanuni za kisarufi za lugha inayohusika. Tungo huweza kuwa neno au kifungu cha maneno chenye kutoa taarifa fulani. Tazama mifano ifuatayo:

(i) Anayecheza.

(ii) Wanafunzi waliosajiliwa.

(iii) Kijana mzuri.

(iv) Sara alisafiri jana.

Mifano yote iliyotolewa katika (i) - (iv) ni tungo lakini viwango vya kukamilika kwa taarifa zake ni tofauti. Tofauti hiyo inajitokeza katika maana na mpangilio wa maneno uliojenga tungo hizo. Kwa mfano (i) - (ii) ni tungo ambazo zinatoa taarifa lakini taarifa zake hazijakamilika kimaana. Tungo ya (iii) - (iv) ndizo zinazotoa taarifa kamili. Tungo hizi zimegawanyika katika viwango vinne. Viwango hivyo ni tungo neno, tungo kirai, tungo kishazi na tungo sentensi. Kwa hiyo, kuna aina nne za tungo katika lugha ya Kiswahili. Mchoro ufuatao unaonesha mpangilio wa viwango hivyo vya tungo. Alama ya mshale inaonesha uhusiano wa kidarajia.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

For Online Use Only

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 154 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE






**Kielelezo 5.1** Aina za tungo

**Tungo neno**

Neno katika lugha ya Kiswahili linaweza kusimama peke yake kama tungo na likatoa taarifa fulani. Neno hilo linaweza kuwa shina kama vile *cheza* na *soma* au muunganiko wa shina na viambishi kama vile *analima na nitakuja* . Neno ndilo kipashio cha msingi cha kisintaksia na ndilo pia huwa msingi wa uundaji wa tungo nyingine kubwa zaidi yake.

**Tungo virai**

Kirai ni aina ya tungo yenye neno moja au zaidi ambayo uhusiano wake umekitwa katika neno kuu. Neno kuu katika kirai hutokana na aina za maneno. Aina hizo za maneno zinaweza kusimama peke yake kama kirai au kuandamana na maneno mengine kwa kuzingatia uhusiano maalumu baina ya maneno hayo na neno kuu. Kwa hiyo, katika Kiswahili, jina la aina ya kirai hutokana na neno kuu lililopo katika kirai hicho. Kwa mfano kama neno kuu ni nomino, kirai kitaitwa kirai nomino na kama neno kuu ni kielezi, basi kirai kitaitwa kirai kielezi.

**Aina za virai**

Virai vinaweza kugawanywa katika aina mbalimbali kwa kuzingatia neno kuu. Aina za maneno zinazotupatia aina za virai ni nomino, vivumishi, vitenzi, na vielezi. Viwakilishi huingia katika kundi la kirai nomino, hivyo viwakilishi na maneno mengine kama vile viunganishi na vihisishi hayaundi kirai. Viunganishi hutumika kuunganisha virai. Aidha, vihisishi havifungamani au kushikana na

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 155 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

maneno mengine katika tungo za Kiswahili. Hivyo basi, aina hizi za maneno haziwezi kuunda virai. Kwa hiyo, tutaangalia aina nne za virai katika lugha ya Kiswahili. Virai hivyo ni *kirai nomino, kirai kivumishi, kirai kitenzi,* na *kirai kielezi*.

**Kirai nomino (KN)**

Hiki ni kirai ambacho neno lake kuu ni nomino au kiwakilishi. Hii ina maana kwamba nomino au kiwakilishi hutawala upatanisho wa kisarufi wa neno au maneno yanayoandamana nalo katika tungo inayohusika. Tazama mifano ifuatayo:

(i) *Gari kubwa* limerudishwa.

(ii) *Gari kubwa kuliko yote* limerudishwa.

(iii) *Gari kubwa lililokuwa juu ya mlima* limerudishwa.

(iv) *Gari lililogongwa* limerudishwa.

**Miundo ya kirai nomino**

Kirai nomino huwa na miundo mbalimbali ambayo imeoneshwa kwa hatimlalo katika mifano. Kwa mfano:

(a) Nomino moja peke yake. Tazama mifano ifuatayo:

(i) *Mwanamichezo* amependeza.
(ii) *Mtoto* anacheza vizuri.
(iii) *Shule* imefunguliwa leo.

(b) Nomino mbili au zaidi zilizounganishwa na kiunganishi. Kwa mfano:

(i) *Baba, mama na kaka* wamesafiri leo.
(ii) *Juma na Roza* wanapendeza sana.
(iii) *Mjomba, shangazi na binamu* watawasili kesho.

(c) Kiwakilishi kimoja au zaidi. Kwa mfano:

(i) *Wao* walifika mapema sana.
(ii) *Sisi* tunasisitiza kwamba tutakuja.
(iii) *Huyu na yule* wanalima vizuri.
(iv) *Vyake na vyangu* mtavikuta nyumbani.

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 156 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



(d) Kiwakilishi na kivumishi. Kwa mfano:
- (i) *Sisi sote* ni ndugu.
- (ii) *Yule mrembo* amefaulu mtihani.
- (iii) *Wale warefu* watakuja kesho.
- (iv) *Kile kizuri* kimevunjika.

(e) Nomino na kivumishi kimoja au zaidi. Kwa mfano :
- (i) *Mtoto mzuri* anacheza.
- (ii) *Mbwa mnene mweupe* amepotea.
- (iii) *Meza ndogo fupi* imefunikwa vizuri.
- (iv) *Magari mawili makubwa* yanakuja.

(f) Nomino na kishazi rejeshi. Kwa mfano :
- (i) *Wanafunzi waliokuja jana* wameitwa.
- (ii) *Kalamu inayovuja* ni yangu.
- (iii) *Redio iliyonunuliwa* imeibwa.
- (iv) *Karatasi zilizoletwa leo* ni nzuri sana.

(g) Kitenzi-jina na kivumishi au bila kivumishi. Kwa mfano:
- (i) *Kucheza kwao* kutaleta balaa.
- (ii) *Kulima kule* kunapendeza.
- (iii) *Kula kuzuri* kumeshamiri kijijini kwetu.
- (iv) *Kusoma* kunaburudisha.

**Kirai kivumishi (KV)**

Hiki ni kirai ambacho neno lake kuu ni kivumishi. Kirai hiki kina miundo ifuatayo:

(a) Kivumishi peke yake. Kwa mfano:
- (i) Wanafunzi *wazuri* wanahudhuria darasani.
- (ii) Mtu *mnene* anakimbia taratibu.
- (iii) Mwalimu *hodari* huwahimiza wanafunzi wasome.
- (iv) Mbuzi *mweusi* amepelekwa mnadani.

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 157 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(b) Kivumishi na kielezi. Kwa mfano:
   (i) Chakula ni *kitamu mno*.
   (ii) Mboga ni *nzuri sana*.
   (iii) Mtoto *mweupe sana* amekuja.
   (iv) Mvulana *mrefu zaidi* aanike nguo.

(c) Kivumishi na kivumishi. Kwa mfano:
   (i) Mtoto *wetu mwerevu* atafaulu masomo.
   (ii) Watoto *kumi warefu* walifika shuleni.
   (iii) Mbuzi *mmoja mnene* atachinjwa kesho.
   (iv) Mtoto *wangu mfupi* anapenda kucheza mpira.

**Kirai kitenzi (KT)**

Hii ni aina ya kirai ambacho neno lake kuu ni kitenzi. Hii ina maana kwamba muundo wake umeegemea katika uhusiano wa kitenzi na neno au mafungu mengine ya maneno katika tungo. Kirai hiki hutawaliwa na kitenzi kwa sababu hilo ndilo neno kuu. Kirai kitenzi kina miundo ifuatayo:

(a) Kitenzi kimoja au zaidi. Kwa mfano:
   (i) Watoto *wanasoma*.
   (ii) Watalii *walikuwa wamepumzika*.
   (iii) Mwenyekiti *atakuwa anakuja*.
   (vi) Mwalimu *anafundisha*.

(b) Kitenzi na nomino moja au zaidi (na kivumishi). Kwa mfano:
   (i) Malima *anapenda maua*.
   (ii) Dada *alimpa mgeni zawadi*.
   (iii) Anna *alimnunulia mgonjwa matunda*.
   (iv) Waziri Mkuu *alisoma hotuba*.
   (v) Dada *anapika chakula kitamu*.

(c) Kitenzi na kielezi. Kwa mfano:
   (i) Baba *anatembea polepole*.
   (ii) Mbuzi *anakula harakaharaka*.
   (iii) Mama *amekwenda sokoni*.


PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 158 25/09/2019 13:57

For Online Use Only

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



(d) Kitenzi na kivumishi. Kwa mfano:
   (i) Walimu *ni wabunifu.*
   (ii) Jadia *ni mpole.*
   (iii) Antonio *hapendi wazembe.*
   (iv) Mti huu *sio mrefu.*

**Kirai kielezi (KE)**

Hiki ni kirai ambacho neno lake kuu ni kielezi. Kielezi huweza kukaa peke yake au kuambatana na kielezi kingine. Aidha, kielezi katika tungo huweza kuelezea kitenzi, kivumishi au kielezi kingine. Tazama mifano ifuatayo:

(i) Ntekaniwa anatembea *polepole sana*.
(ii) Mwalimu atakuja *kesho asubuhi*.
(iii) Alijigonga *mbele ya gari*.
(iv) Dada amechoka *sana*.
(v) *Kesho asubuhi* tukutane *katika ukumbi huu*.

## Zoezi la 5.1

1. Unaelewa nini kuhusu neno kuu katika muundo wa kirai?
2. Eleza maana ya kirai nomino huku ukibainisha miundo yake.
3. Kwa kutumia mifano, fafanua miundo mbalimbali ya kirai kitenzi.
4. Eleza tofauti kati ya tungo neno na tungo kirai.

**Kishazi**

Kishazi ni tungo ya ngazi ya juu kuliko kirai na ya chini kuliko sentensi. Kishazi kinaweza ama kuwa na maana kamili au maana isiyo kamili kutegemeana na kitenzi kilichomo katika kishazi hicho. Kitenzi ni kipashio cha msingi katika kishazi. Kitenzi kinaweza kujitosheleza, yaani kuwa na maana kamili au kutojitosheleza na hutegemea kitenzi cha kishazi kingine ili kukamilisha maana. Kwa msingi huo, tunaweza kupata aina mbili za vishazi. Aina hizo ni kishazi huru na kishazi tegemezi.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 159 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kishazi huru**

Hiki ni kishazi kinachoweza kujitosheleza kimaana na kusimama peke yake kama sentensi. Hutambulishwa kwa alama *KHr au* $\alpha$. Ifuatayo ni mifano ya vishazi huru:

(i) Tanzania inapendeza.

(ii) Anafundisha.

(iii) Wimbo wa taifa huimbwa katika shughuli maalumu.

(iv) Dada anapika chakula.

**Miundo ya kishazi huru**

Kishazi huru kina miundo mbalimbali kama ifuatavyo:

(a) Kitenzi kikuu pekee yake. Kwa mfano:
   (i) Alicheza.
   (ii) Tunalima.
   (iii) Wanakimbizana.
   (vi) Wataondoka.

(b) Nomino, kitenzi kikuu na nomino. Kwa mfano:
   (i) Mama anapika ugali.
   (ii) Mtoto anacheza mpira.
   (iii) Diririja anatengeneza kinyago.
   (iv) Manase anapiga gitaa.

(c) Nomino na kitenzi kikuu. Kwa mfano:
   (i) Baba anasoma.
   (ii) Redio imeharibika.
   (iii) Kiswahili kinakua.
   (iv) Ng'ombe amezaa.

(d) Nomino, kitenzi kisaidizi na kitenzi kikuu. Kwa mfano:
   (i) Mama alikuwa anapika.
   (ii) Mgonjwa atakuwa amelala.
   (iii) Mwalimu alikuwa anafundisha.

For Online Use Only


PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 160 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


(e) Nomino/kiwakilishi, kitenzi kishirikishi na nomino na (au kivumishi). Kwa mfano:
   (i) Joel ni mtoto mzuri.
   (ii) Hii ni nchi kubwa.
   (iii) Manka ni mama yangu.
   (iv) Twiga ndiye mnyama mrefu.

**Sifa za kishazi huru**

Kishazi huru, kama kipashio cha msingi katika tungo, kina sifa mbalimbali ambazo huweza kutumika kukibainisha. Sifa hizo ni kama zifuatazo:
   (a) Hujitosheleza kimuundo na kimaana.
   (b) Kina sifa ya kuwa sentensi sahili.
   (c) Hukamilisha taarifa ya kishazi tegemezi.

**Kishazi tegemezi**

Hiki ni kishazi ambacho hakiwezi kutoa maana kamili mpaka kikamilishwe na kishazi huru. Kwa hiyo, kishazi tegemezi huacha maswali kwa msomaji kutokana na kutokamilika kwake. Hivyo, huhitaji kukamilishwa ili kuondoa maswali hayo. Tazama mifano ifuatayo:
Maswali yaliyosahihishwa…
Samaki waliovuliwa…
Alivyoingia…
Kwa sababu alikuwa mchangamfu…
Kishazi tegemezi hutambulishwa kwa alama *KTg* au *ß*.

**Miundo ya vishazi tegemezi vya Kiswahili**

Lugha ya Kiswahili ina miundo minne ya vishazi tegemezi. Miundo hiyo ni vishazi tegemezi vyenye viunganishi tegemezi, vyenye mofu za masharti, mofu za utegemezi wa urejeshi, na vyenye maneno *kwamba* au *kuwa*.

**(a) Vishazi tegemezi vyenye muundo wa viunganishi tegemezi**

Vishazi tegemezi hivi hutokana na kuwapo kwa viunganishi tegemezi kama vile *ingawa, ijapokuwa, isipokuwa, ikiwa, kwa kuwa*, na *kwa vile*. Ifuatayo ni mifano ya vishazi tegemezi vya aina hiyo:
   (i) *Kwa kuwa wanafunzi wanajisomea kwa bidii,* watafaulu mitihani yao.
   (ii) Hakuruka juu sana, *ijapokuwa alikuwa mwepesi.*


PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 161 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(iii) *Ingawa alikuwa mrefu*, hakuweza kuudaka mpira.

(iv) *Ikiwa wananchi tutashirikiana kuwalinda tembo*, vizazi vyetu vitanufaika kwa utalii.

(v) Mlifaulu vizuri, *kwa vile mlikuwa mnasoma kwa bidii*.

**(b) Vishazi tegemezi vyenye muundo wa mofu za masharti**

Hizi ni mofu zinazodokeza hali ya masharti. Mfano wa mofu hizo ni -*ki*-, -*nge*-,-*ngeli*- na –*ngali*- Chunguza mifano ifuatayo:

(i) A*ki*nipa pesa zangu, nitanunua vitabu.

(ii) Utaadhibiwa na mwalimu, u*ki*shindwa kufuata taratibu za shule.

(iii) Wa*nge*ondoka mapema, wa*nge*wahi kufika ukumbini.

(iv) U*ngeli*kuwa na pesa u*ngeli*nunua gari.

(v) A*ngali*kuwa mwaminifu a*ngali*pewa mtaji mkubwa.

**(c) Vishazi tegemezi vyenye kwamba na kuwa.** Kwa mfano:

(i) *Kusema kwamba hatupendi wali* ni kusema uongo.

(ii) *Kudai kuwa chakula hakitoshi* kutasababisha matatizo.

**(d) Vishazi tegemezi vyenye mofu za urejeshi**

Aina hii ya muundo wa vishazi tegemezi hutokana na kupachika mofu za urejeshi katika vitenzi au baada ya neno *amba*-. Kwa mfano:

(i) *Walimu wanaofundisha kwa juhudi* watapewa zawadi.

(ii) *Daraja lililobomoka* limejengwa.

(iii) *Kitabu ambacho kimeletwa* ni kizuri.

(iv) *Mwanafunzi aliyefaulu mitihani* atajiunga na chuo kikuu.

(v) *Michezo ambayo itafanyika mwaka huu* itawavutia wengi.

Kitenzi cha kishazi tegemezi kinachotokana na mofu za urejeshi hushushwa hadhi na kufanya kazi ya kivumishi au kielezi. Kwa hiyo, kutokana na mofu za urejeshi, tunapata aina anuai za vishazi rejeshi.

**Vishazi rejeshi**

Vishazi rejeshi ni vishazi tegemezi ambavyo hufafanua zaidi nomino au kiwakilishi chake, na huonesha wakati, mahali, au namna.

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 162 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Jedwali lifuatalo linaonesha muhtasari wa maumbo ya urejeshi katika ngeli za nomino za Kiswahili.

**Jedwali 5.1** Maumbo ya urejeshi kwa kila ngeli

| Ngeli | Viambishi vya ngeli | Viambishi vya o-rejeshi | Mifano |
|---|---|---|---|
| 1 | YU/A – WA | YE – O | Mtoto ana*ye*cheza ni mpole. |
| | | | Watoto wana*o*cheza ni wapole. |
| 2 | U – I | O – YO | Mkoba uli*o*nunua una rangi nzuri. |
| | | | Mikoba uli*yo*nunua ina rangi nzuri. |
| 3 | LI – YA | LO - YO | Embe lili*lo*iva limemenywa. |
| | | | Maembe yali*yo*iva yamemenywa. |
| 4 | KI – VI | CHO – VYO | Kisu kili*cho*potea kimepatikana. |
| | | | Visu vili*vyo*potea vimepatikana. |
| 5 | I – ZI | YO – ZO | Njia ili*yo*tengenezwa ni hii. |
| | | | Njia zili*zo*tengenezwa ni hizi. |
| 6 | U – ZI | O – ZO | Ubao uli*o*letwa umewekwa juani. |
| | | | Mbao zili*zo*letwa zimewekwa juani. |
| 7 | U – YA | O – YO | Ugonjwa uli*o*enea ni hatari. |
| | | | Magonjwa yali*yo*enea ni hatari. |
| 8 | KU | KO | Kucheza kuna*ko*furahisha kuna faida. |
| 9 | PA | PO | Mahali pana*po*pendeza ni hapa. |
| | MU | MO | Mahali mli*mo*ingia ni salama. |
| | KU | KO | Kule kuna*ko*pendeza hakuna wadudu. |

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**(a) Vishazi rejeshi vinavyorejelea nomino/viwakilishi.** Kwa mfano:

(i) Wao w*alioumia* wamepona.

(ii) Miti *ambayo imekatwa* ilikuwa barabarani.

(iii) Wanafunzi *waliosimama mstari wa mbele* wasogee mbele hatua moja.

(iv) Mkulima *alimaye kwa bidii* hupata mazao mengi.

**(b) Vishazi rejeshi vinavyoonesha wakati.** Kwa mfano:

(i) Mwanahawa alifurahi sana *alipofaulu mtihani wa kidato cha sita.*

(ii) Sisi tulimlimia sehemu yake *alipoumia*.

(iii) Baba *alipokuja* tulifurahi sana.

(iv) Wakati *alipokuwa kijana* nilimfahamu vyema.

**(c) Vishazi rejeshi vinavyoonesha mahali.** Kwa mfano:

(i) Mahali *panapopendeza* ni hapa.

(ii) Mahali *mlimoingia* ni salama.

(iii) Kule *kunakopendeza* hakuna wadudu.

**(d) Vishazi rejeshi vinavyoonesha namna/jinsi.** Kwa mfano:

(i) Watu walishangaa *alivyoingia*.

(ii) Kabula hakuelewa *alivyoachwa na basi*.

(iii) *Tulivyoondoka* tuliwashangaza.

**Sifa za vishazi tegemezi**

(i) Havijitoshelezi kimaana. Hivyo, huhitaji vishazi huru ili kukamilisha maana.

(ii) Huundwa na:

(a) Viambishi rejeshi;



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 164 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



(b) Mofu za mashariti;

(c) Viunganishi tegemezi; na

(d) Maneno *kwamba* au *kuwa*.

(iii) Huweza kuondolewa katika sentensi bila kupoteza maana ya msingi ya sentensi hiyo.

(iv) Huweza kutanguliwa au kufuatwa na kishazi huru.

(v) Kishazi tegemezi kinaweza kufanya kazi kama ifanywayo na kielezi au kivumishi.

## Zoezi la 5.2

1. Fafanuna aina za vishazi kwa kutumia mifano mbalimbali.
2. Kwa kutumia mifano, bainisha miundo ya vishazi tegemezi.
3. Eleza tofauti kati ya kishazi tegemezi na kishazi huru.
4. Onesha vishazi tegemezi na vishazi huru kwa kutumia alama maalumu katika sentensi zifuatazo:

   (a) Hakutaka kabisa kumsikiliza Madebe kwa sababu ni mwongo.

   (b) Nitamwelewesha vizuri akinifuata.

   (c) Kaka alichukia alipochekwa.

   (d) Miwani yangu ilipovunjika nilishindwa kusoma.

   (e) Aombaye hupewa.

**Sentensi**

Sentensi ni neno au kifungu cha maneno chenye kiima na kiarifu na hutoa taarifa iliyokamilika. Hiki ndicho kipashio kikubwa kabisa cha kimuundo katika tungo. Sentensi huwa na muundo uliokamilika ambao hutoa taarifa kamili. Aidha, sifa ya kikazi au kiuamilifu inayotofautisha sentensi na vipashio vingine vya lugha ni kuwa na kiima (K), na kiarifu (A). Sentensi huundwa na vipashio vingine vidogo ambavyo ni neno, virai na vishazi.

**Aina za sentensi**

Uainishaji wa sentensi hufanywa kwa kutumia vigezo viwili ambavyo ni kigezo



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 165 25/09/2019 13:57

For Online Use Only

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

cha kimuundo na kigezo cha kidhima. Kigezo cha kimuundo huzingatia mjengo au mpangilio wa vipashio katika sentensi, ilhali kigezo cha kidhima huzingatia uamilifu wa vipashio vya sentensi.

**Uainishaji wa sentensi kwa kigezo cha kimuundo**

Katika kigezo hiki, sentensi huainishwa kwa kuangalia vipashio vilivyounda sentensi na uhusiano uliopo baina ya kipashio kimoja na kingine. Uhusiano wa vipashio katika sentensi hurejelea namna vipashio vya sentensi vinavyoshikana, vinavyotegemeana na kutawalana katika kuunda sentensi. Kuna aina tatu za sentensi kwa kuzingatia kigezo cha kimuuundo ambazo ni sentensi sahili, sentensi ambatani na sentensi changamani.

***1 S entensi sahili***

Hizi ni sentensi ambazo huundwa na kishazi huru kimoja. Sentensi za aina hii huwa na wazo kuu moja. Kimsingi, usahili wa sentensi sahili hutokana na sentensi kuwa na taarifa moja, ambayo hubebwa na kitenzi kamili. Ikiwa sentensi ina vitenzi zaidi ya kimoja vyenye taarifa tofauti, basi sentensi hiyo haitakuwa sahili. Sentensi sahili ndiyo msingi wa uundaji wa sentensi nyingine. Ifuatayo ni mifano ya sentensi sahili.

(i) Doto ana watoto wawili.
(ii) Mwalimu anaandika ubaoni.
(iii) Baba yangu alikuwa mkali.
(iv) Kaka alikuwa anaimba.
(v) Rais anahutubia wananchi wake.

**Miundo ya sentensi sahili**

Tunapozungumzia miundo ya sentensi sahili, tunaangalia vipashio vinavyozijenga sentensi hizo. Sentensi sahili huundwa na kitenzi kimoja au zaidi vinavyodokeza wazo kuu moja. Kwa kuzingatia ujitokezaji wa kitenzi katika tungo, sentensi sahili zinaweza kugawanywa katika miundo ya aina tatu ambayo ni kitenzi kikuu peke yake, kitenzi kisaidizi na kitenzi kikuu, na kitenzi kishirikishi.

**(a) Kitenzi kikuu peke yake**

Katika lugha ya Kiswahili, kitenzi kikuu kinaweza kusimama peke yake na kuunda sentensi sahili. Aidha, kitenzi kikuu kinaweza kuambatana na aina nyingine za maneno. Tazama mifano ya sentensi zifuatazo:

(i) Anaimba.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

For Online Use Only

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 166 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



(ii) Anatembea polepole.

(iii) Tunasoma kitabu.

(iv) Anaogelea kwenye bwawa.

**(b) Kitenzi kisaidizi na kitenzi kikuu**

Muundo huu unajengwa na kitenzi kisaidizi kimoja au zaidi na kitenzi kikuu. Vilevile, vitenzi hivyo vinaweza kuandamana na maneno mengine katika sentensi. Tazama mifano hapa chini:

(i) Dereva *atakuwa amegonga* mti.

*Ts* *Tk*

(ii) Dada *alikuwa anapenda* nyimbo.

*Ts* *Tk*

(iii) Baba *alikuwa analima*.

*Ts* *Tk*

**(c) Kitenzi kishirikishi**

Muundo huu huwa na kitenzi kishirikishi ambacho huandamana na maneno mengine kuunda sentensi.Tazama mifano ifuatayo:

(i) Mtoto *angali* mgonjwa.

(ii) Juma na Paulo *ni* watoto wetu.

(iii) Maua *yalikuwa* machanga.

(iv) Maji safi *yamo* mtungini.

(v) Wao *si* wanafunzi.

***2 S entensi changamani***

Hizi ni sentensi ambazo huundwa na kishazi tegemezi kimoja au zaidi na kishazi huru au vishazi tegemezi viwili vinavyokamilishana. Vishazi hivi viwili au zaidi haviunganishwi kwa kutumia viunganishi. Chunguza mifano ifuatayo:

(i) Mchezaji aliyecheza vizuri amepata zawadi.

(ii) Mgeni rasmi alipofika, sherehe ilianza rasmi.

(iii) Akifika tu, nitaarifu.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 167 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(iv) Kwa sababu alikuwa na adabu, watu wengi walimpenda.

(v) Angekuwa mwaminifu, angekabidhiwa duka la baba yake.

**Miundo ya sentensi changamani**

Sentensi changamani zina miundo miwili kama ifuatavyo:

(a) Kishazi tegemezi kimoja au zaidi na kishazi huru. Kwa mfano:

(i) Kiti kilichoharibika, kimetengenezwa.

(ii) Kila nilipokuwa nikitaka kumpiga, roho ilikataa.

(iii) Msichana aliyekuja juzi, akiwa amesuka nywele, ameondoka na begi langu.

(iv) Babu aliyewasili leo, tulipokuwa tunakula ugali, anaitwa mzee Kidimo.

(b) Vishazi tegemezi viwili vinavyokamilishana. Kwa mfano:

(i) Angesoma kwa bidii, angefaulu vizuri.

(ii) Angalianza matibabu mapema, angalipona.

(iii) Angelikuwa na sauti nzuri, angelijiunga na kwaya ya shule.

***3 S entensi ambt ani***

Hizi ni sentensi ambazo huundwa na sentensi mbili au zaidi ambazo huunganishwa kwa kutumia kiunganishi. Kwa hiyo, aina hii ya sentensi ina taarifa zaidi ya moja. Kwa mfano:

(i) Mwalimu anafundisha na mwanafunzi anasikiliza.

(ii) Mtoto analia, mama anambembeleza, na baba anamsaidia.

(iii) Dada anakuja leo na kaka atakuja kesho, lakini mjomba hatafika kabisa.

(iv) Mwanafunzi aliyeumia amepelekwa hospitalini, na kijana aliyempiga ameadhibiwa.

(v) Kwa sababu hakuwa mwadilifu alifukuzwa shule mara moja, lakini wenzake waliendelea na masomo kama kawaida.

For Online Use Only


PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 168 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



**Miundo ya sentensi ambatani**

Sentensi ambatani ina miundo mitatu kama inavyooneshwa hapa chini.

(a) Vishazi huru au sentensi sahili mbili au zaidi. Kwa mfano:

(i) Mtoto anacheza na mama anafua nguo.

(ii) Dada ameenda kuchota maji na kaka ameenda mjini.

(iii) Mwalimu anafundisha lakini wanafunzi hawazingatii.

(iv) Gawile anafanya kazi ila Elimboto anategea.

(v) Tulicheza vizuri lakini hatukufunga magoli wala hatukufungwa.

(c) Sentensi changamani na sentensi sahili. Kwa mfano:

(i) Watoto waliosafiri wamerudi, ila wamesahau mizigo yao.

(ii) Mtoto aliyefanya vizuri amekuja, lakini hajafika na mitihani yake.

(iii) Ingawa leo ni siku ya mnada, hakuchinja ng'ombe, bali amechinja mbuzi.

(iv) Akifika nitampa chakula isipokuwa sitampa kinywaji.

(d) Sentensi changamani mbili au zaidi. Kwa mfano:

(i) Kijana aliyevaa shati jekundu ni mwanafunzi, lakini yule aliyevaa shati jeupe ni kaka yangu.

(ii) Akija kwangu nitamsikiliza, lakini asipokuja sitamtafuta.

(iii) Kwa sababu alikuwa anaimba harakaharaka, sikupenda uimbaji wake, ila kucheza kwake kulinivutia.

(iv) Iwapo atakuuliza maswali, mwelekeze kwangu, lakini asipokuuliza usimwelekeze.

**Uainishaji wa sentensi kwa kutumia kigezo cha kidhima**

Kigezo hiki cha uainishaji wa sentensi hujikita katika uamilifu ambao umebebwa na sentensi inayohusika. Katika uainishaji huu, tunaangalia kama sentensi inatoa taarifa, amri, inauliza swali, au inadokeza hali ya mshangao. Kwa hiyo sentensi zinazoainishwa kwa kutumia kigezo hiki ni: sentensi agizi, sentensi arifu, sentensi ombi, sentensi ulizi, na sentensi mshangao.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 169 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**1. *Sentensi amrishi***

Hizi ni sentensi ambazo hutoa maelekezo ya kutendeka kwa jambo fulani. Katika aina hii ya sentensi, msemaji ndiye mwamuzi, na mtendaji hutarajiwa atekeleze agizo. Katika sentensi amrishi, kitenzi huwa na umbo la shina na katika wingi hubeba kiambishi tamati *–ni* katika uyakinishi. Katika ukanushi hubeba kiambishi cha nafsi na kiambishi cha ukanushi na irabu tamati ya kitenzi hubadilika na kuwa *-e*. Tazama mifano ifuatayo:

(i) Nendeni.

(ii) Ondoka.

(iii) Nenda darasani.

(iv) Dai risiti.

(v) Zima redio.

(vi) Msikae hapa.

**2. *Sentensi omb***

Hizi ni sentensi ambazo humsihi mtu mwingine akubali kutenda jambo fulani.Sentensi za ombi hutumia sauti ya upole. Katika sentensi za ombi, kitenzi huanza kwa nafsi ya pili umoja au wingi, na irabu tamati hubadilika na kuwa *–e* katika vitenzi vyenye asili ya Kibantu. Tazama mifano ifuatayo:

(i) Unisaidie chenji.

(ii) Mniombee.

(iii) Unifikirie vizuri.

**3. *Sentensi arifu***

Hizi ni sentensi ambazo hutoa taarifa kuhusu jambo fulani. Sentensi hizi huishia na nukta. Tazama mifano ifuatayo:

(i) Mheshimiwa Rais atawasili kesho asubuhi.

(ii) Baba yao ameteuliwa kuwa mkuu wa wilaya.

(iii) Uandishi wa kitabu hiki utakamilika mwaka ujao.

(iv) Nchi yetu inapendeza sana.


PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 170 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



4. ***Sentensi ulizi***

Hizi ni sentensi ambazo msingi au ujumbe wake huwa katika swali. Hivyo ni sentensi ambazo huwa na pengo linalohitaji jibu la taarifa fulani. Sentensi hizi huishia kwa alama ya kuuliza. Kwa mfano:

(i) Mama atarudi lini?

(ii) Mmeelewa?

(iii) Hata wewe unacheza mpira?

(iv) Kwa nini umepita hapa?

5. ***Sentensi mshango***

Hizi ni sentensi ambazo huonesha kustaajabu, au kushikwa na butwaa. Sentensi hizi huishia kwa alama ya mshangao. Kwa mfano:

(i) Hee! Hata yeye amechaguliwa!

(ii) Kumbe! Halipi kodi!

(iii) Maskini! Wamefungwa!

(iv) Aaaah! Mjomba anajua kusoma!

**Uchanganuzi wa sentensi**

Uchanganuzi wa sentensi ni uchambuzi wa sentensi kwa kubainisha vipashio vyake vya kimuundo au kidhima katika sentensi. Katika kubainisha vipashio, tunaanza na kipashio kikubwa hadi vidogo katika sentensi. Uchanganuzi wa sentensi za Kiswahili huongozwa na mikabala miwili ambayo ni mkabala wa kidhima, na mkabala wa kimuundo. Hatua za uchanganuzi wa sentensi zinafanana kwa mikabala yote miwili, isipokuwa istilahi za vipashio vinavyounda sentensi. Aidha, mikabala hii haipaswi kuchanganuliwa kwa kuchanganywa. Mkabala wa kidhima hutumia vipashio vya kidhima pekee, ilhali mkabala wa kimuundo hutumia vipashio vya kimuundo pekee.

**Mkabala wa kidhima**

Mkabala huu huzingatia uamilifu wa vipashio vinavyounda sentensi. Kwa hiyo, unatumia istilahi za kidhima zifuatazo:

**Kiima**

Kiima ni kipashio cha kiuamilifu cha sentensi ambacho hufafanuliwa na kitenzi. Sehemu ya kiima huweza kukaliwa na nomino, kiwakilishi, au kifungu kingine cha maneno kinachofanya kazi kama nomino. Katika sentensi za kauli ya kutenda



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 171 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kiima huwa mtenda wa jambo, ilhali katika sentensi za kauli ya kutendwa kiima huwa mtendwa wa jambo. Kiima hutambulishwa kwa alama *K*. Chunguza maneno yaliyoandikwa kwa hatimlalo katika mifano ifuatayo:

(i) *Mtoto mdogo* analia.

(ii) *Juma* amefaulu vizuri.

(iii) *Mbwa* amecharazwa viboko.

(iv) *Nguo* zimefuliwa vizuri.

**Vipashio vya kiima**

Kiima huundwa na vipashio mbalimbali kama inavyooneshwa na maneno yaliyoandikwa kwa hatimlalo katika vipengele vifuatavyo:

(a) Nomino moja au zaidi au nomino na kivumishi. Kwa mfano:

(i) *Paka* amekamata panya.

(ii) *Mariamu na Hamida* walialikwa kwenye sherehe.

(iii) *Kaka mkubwa* anacheza mpira.

(iv) *Mtoto mzuri* amefaulu mtihani.

(v) *Mwalimu mweledi* anafundisha.

(b) Kiwakilishi peke yake au kiwakilishi na kivumishi. Kwa mfano:

(i) *Yule* analima sana.

(ii) *Wao* watakuja kesho.

(iii) *Yule mrefu* ni kaka yetu.

(iv) *Wale wanene* walikuja jana.

(c) Nomino na kishazi rejeshi. Kwa mfano:

(i) *Mtoto aliyekuja leo* amefaulu.

(ii) *Kiatu kilichopotea* kimeonekana.

(iii) *Msichana aliyevaa vizuri* ni rafiki yangu.

(iv) *Kicheko ambacho alicheka* kilinishtua.

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 172 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



(d) Kitenzi–jina na kivumishi. Kwa mfano:

(i) *Kucheka kwao* kuliwafurahisha wote.

(ii) *Kupotea kwake* kuliwaumiza wengi.

(iii) *Kukimbia kule* hakukuwa kwa kawaida.

**Kiarifu**

Hiki ni kipashio cha kiuamilifu katika sentensi ambacho kina kitenzi ndani yake na kinafafanua kiima. Kipashio kikuu cha kiarifu ni kitenzi. Kiarifu hutokea upande wa kulia mwa kiima cha sentensi za Kiswahili. Kiarifu hutambulishwa kwa alama *A*. Chunguza maneno yaliyoandikwa kwa hatimlalo katika mifano ifuatayo:

(i) Mtoto *anacheza.*

(ii) Mwalimu *alikuwa anacheza vizuri.*

(iii) Juma *aliimba vizuri.*

(iv) Batu *anacheza muziki*.

**Vipashio vya kiarifu**

Kiarifu huundwa na vipashio mbalimbali kama inavyooneshwa na maneno yaliyoandikwa kwa hatimlalo katika mifano kwenye vipengele vifuatavyo:

**Kitenzi (T)**

Hii ni sehemu muhimu ambayo hutoa taarifa kuhusu tendo katika sentensi. Kwa mfano:

(i) Mtoto *anacheza* vizuri.

(ii) Juma *ni* mrefu.

(iii) *Anacheza.*

(iv) Yeye *hucheza* kila jioni.

(v) Mwanamwema *alikuwa anaumwa*.

**Shamirisho (SH) au kijalizo**

Shamirisho ni sehemu ya kiarifu ambayo hukaliwa na mtendwa au mtendewa. Mtendwa hujulikana pia kama *yambwa* na mtendewa hujulikana pia kama *yambiwa*. Yambwa ni kipashio ambacho huathiriwa na tendo, ilhali yambiwa ni mnufaika wa tendo linaloelezwa na kitenzi. Dhima ya shamirisho ni kukamilisha taarifa inayoelezwa na kitenzi elekezi. Vitenzi elekezi ni vitenzi vinavyobeba yambwa au yambiwa. Kwa mfano:



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 173 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(i) Jana tulichinja *mbuzi wawili*.

(ii) Kaka amemjengea *baba nyumba kubwa*.

(iii) Mwalimu amewaonesha *wanafunzi vitabu vipya.*

(iv) Raina amempa *Ndola ukwaju mtamu sana.*

(v) Baba amemnunulia *dada nguo nzuri*.

Katika lugha ya Kiswahili kitenzi kikiwa kinahitaji kukamilishwa kwa nomino mbili basi nomino ya kwanza ni yambiwa na nomino ya pili ndiyo yambwa.

**Chagizo (CH)**

Chagizo ni sehemu ya kiarifu ambayo hukaliwa na kielezi. Kielezi kinaweza kuhamahama katika sentensi bila kuathiri maana. Kwa mfano:

(i) Mwalimu aliwaambia wanafunzi waondoke *upesi*.

(ii) Ngoswe alikimbia *mapema*.

(iii) Unapenda kula *polepole*.

(iv) Abel anachora *ubaoni*.

Aidha, vielezi vinaweza kuhamahama katika sentensi. Kwa mfano:

(i) *Leo* nitakula ugali.

(ii) Nitakula ugali *leo*.

**Uchanganuzi wa sentensi kidhima**

Uchanganuzi wa sentensi kidhima hufuata hatua mbalimbali ambazo huanzia katika kipashio kikubwa kabisa kwenda kipashio kidogo. Hatua hizo ni hizi zifuatazo:

(i) Kubainisha aina ya sentensi ili kujua vipashio vinavyounda sentensi hiyo. Aina za sentensi katika mkabala wa kidhima ni sentensi arifu, amrishi, ulizi na mshangao.

(ii) Kubainisha vipashio vinavyounda sehemu kuu mbili za sentensi. Katika mkabala wa kidhima vipashio hivyo ni kiima (K) na kiarifu (A).

(iii) Kubainisha vipashio vinavyounda kiima na kiarifu ambavyo kwa upande wa mkabala wa kidhima, ni nomino (N) au kiwakilishi (W) na kivumishi (V) katika kiima, na kitenzi (T), shamirisho (SH) na chagizo (CH) katika kiarifu.

For Online Use Only


PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 174 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



(iv) Kuandika aina za maneno zilizomo katika sentensi inayohusika. Aina hizo huandikwa kwa kutumia vifupisho vya aina za maneno kama vile N, T, V, E, W, H, na U. Hii hutumika sawia katika mikabala yote ya uchanganuzi.

Kwa kawaida uchanganuzi huu hufuata njia ya majedwali na maelezo. Chunguza mifano ifuatayo:

**Njia ya Jedwali**

(i) Sentensi sahili

Maziwa ni lishe bora.

<table>
<tr><th colspan="4">S</th></tr>
<tr><th>K</th><th colspan="3">A</th></tr>
<tr><th rowspan="2">N</th><th>T</th><th colspan="2">SH</th></tr>
<tr><th>t</th><th>N</th><th>V</th></tr>
<tr><td>Maziwa</td><td>ni</td><td>lishe</td><td>bora</td></tr>
</table>

(ii) Sentensi ambatani

Wanafunzi wanafagia darasani na wengine wanapanga viti.

<table>
<tr><th colspan="7">S</th></tr>
<tr><th colspan="3">$S_1$</th><th rowspan="4">U</th><th colspan="3">$S_2$</th></tr>
<tr><th>K</th><th colspan="2">A</th><th>K</th><th colspan="2">A</th></tr>
<tr><th rowspan="2">N</th><th rowspan="2">T</th><th>CH</th><th rowspan="2">W</th><th rowspan="2">T</th><th>SH</th></tr>
<tr><th>E</th><th>N</th></tr>
<tr><td>Wanafunzi</td><td>wanafagia</td><td>darasani</td><td>na</td><td>wengine</td><td>wanapanga</td><td>viti</td></tr>
</table>

(iii) Sentensi changamani

Mtoto aliyepotea amepatikana leo.

<table>
<tr><th colspan="4">S</th></tr>
<tr><th colspan="2">K</th><th colspan="2">A</th></tr>
<tr><th rowspan="2">N</th><th rowspan="2">KR*</th><th rowspan="2">T</th><th>CH</th></tr>
<tr><th>E</th></tr>
<tr><td>Mtoto</td><td>aliyepotea</td><td>amepatikana</td><td>leo</td></tr>
</table>

***KR = kishazi kirejeshi**



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 175 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Njia ya maelezo**

(i) Sentensi sahili

Maziwa ni lishe bora.

- Hii ni sentensi arifu.
- Sentensi hii imeundwa na kiima na kiarifu.
- Kiima kimeundwa na nomino.
- Nomino ni *maziwa.*
- Kiarifu kimeundwa na kitenzi kishirikishi na shamirisho.
- Kitenzi kishirikishi ni *ni*.
- Shamirisho imeundwa na nomino na kivumishi.
- Nomino ni *lishe* .
- Kivumishi ni *bora*.

(ii) Sentensi ambatani

Wanafunzi wanafagia darasani na wengine wanapanga viti.

- Hii ni sentensi arifu.
- Sentensi arifu imeundwa na sentensi mbili.
- Sentensi ya kwanza imeundwa na kiima, na kiarifu.
- Kiima kimeundwa na nomino.
- Nomino ni *wanafunzi*.
- Kiarifu kimeundwa na kitenzi na chagizo.
- Kitenzi ni *wanafagia*.
- Chagizo imeundwa na kielezi.
- Kielezi ni *darasani*.
- Kuna kiunganishi *na*.
- Sentensi ya pili imeundwa na kiima na kiarifu.
- Kiima kimeundwa na kiwakilishi.
- Kiwakilishi ni *wengine*.
- Kiarifu kimeundwa na kitenzi na shamirisho.
- Kitenzi ni *wanapanga.*
- Shamirisho imeundwa na nomino.
- Nomino ni *viti*.


PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 176 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



(iii) Sentensi changamani

Mtoto aliyepotea amepatikana leo.

- Hii ni sentensi arifu.
- Sentensi hii imeundwa na kiima na kiarifu.
- Kiima kimeundwa na nomino na kishazi rejeshi.
- Nomino ni *mtoto*.
- Kishazi rejeshi kimeundwa na kiambishi rejeshi.
- Kishazi rejeshi ni *aliyepotea*.
- Kiarifu kimeundwa na kitenzi na chagizo.
- Kitenzi ni *amepatikana*.
- Chagizo imeundwa na kielezi.
- Kielezi ni *leo*.

**Mkabala wa kimuundo**

Mkabala huu hutumika kuchanganulia sentensi kwa kuzingatia muundo wa vipashio vya sentensi. Kwa hiyo, istilahi za kimuundo kama vile kirai nomino (KN), kirai kitenzi (KT), kirai kivumishi (KV), kirai kielezi (KE), na kirai kihusishi (KH) ndizo hutumika katika uchanganuzi wa sentensi.

**Uchanganuzi wa sentensi kimuundo**

Uchanganuzi wa sentensi kimuundo hufuata hatua mbalimbali ambazo huanzia katika kipashio kikubwa kabisa kwenda kipashio kidogo. Hatua hizo ni hizi zifuatazo:

(i) Kubainisha aina ya sentensi ili kujua vipashio vinavyounda sentensi hiyo. Katika mkabala wa kimuundo kuna sentensi sahili, ambatani na changamani.

(ii) Kubainisha vipashio vinavyounda sehemu kuu mbili za sentensi, ambavyo ni kirai nomino (KN) na kirai kitenzi (KT).

(iii) Kubainisha vipashio vinavyounda kirai nomino (KN) na kirai kitenzi (KT). Vipashio vinavyounda kirai nomino (KN) ni nomino (N) au kiwakilishi (W) vikifuatwa na kirai kivumishi (KV) au kishazi rejeshi (KR). Vipashio vinavyounda kirai kitenzi (KT) ni kitenzi (T) ambacho kinaweza kuambatana na kirai nomino (KN), kirai kivumishi (KV), kirai kielezi (KE), au vyote kwa pamoja.

(iv) Kubainisha vipashio vyote vinavyounda virai katika sentensi inayohusika. Vipashio hivyo ni aina za maneno zinazowakilishwa kwa vifupisho N, T, V, E, W, H, U, na kadhalika.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 177 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Mkabala huu huzingatia njia zote za uchanganuzi wa sentensi kama ifuatavyo:

**Njia ya matawi**

(i) Sentensi sahili

Mtoto yule alikuwa anacheza mpira uwanjani.




For Online Use Only


PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 178 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


(ii) Sentensi ambatani

Wanafunzi hawa wanasoma vitabu lakini wale watatu wanaandika.




For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(iii) Sentensi changamani

Kiti kilichovunjika kimetengenezwa.




**Njia ya Jedwali**

(i) Sentensi sahili

Maziwa ni lishe bora

<table>
<tr><td colspan="4">S</td></tr>
<tr><td>KN</td><td colspan="3">KT</td></tr>
<tr><td rowspan="3">N</td><td>T</td><td colspan="2">KN</td></tr>
<tr><td rowspan="2">t</td><td rowspan="2">N</td><td>KV</td></tr>
<tr><td>V</td></tr>
<tr><td>Maziwa</td><td>ni</td><td>lishe</td><td>bora</td></tr>
</table>

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 180 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



(ii) Sentensi ambatani

Wanafunzi wanafagia darasani na wengine wanapanga viti.

<table>
<tr><th colspan="7">S</th></tr>
<tr><td colspan="3">$S_1$</td><td rowspan="4">U</td><td colspan="3">$S_2$</td></tr>
<tr><td>KN</td><td colspan="2">KT</td><td>KN</td><td colspan="2">KT</td></tr>
<tr><td rowspan="2">N</td><td rowspan="2">T</td><td>KE</td><td rowspan="2">W</td><td rowspan="2">T</td><td>KN</td></tr>
<tr><td>E</td><td>N</td></tr>
<tr><td>Wanafunzi</td><td>wanafagia</td><td>darasani</td><td>na</td><td>wengine</td><td>wanapanga</td><td>viti</td></tr>
</table>

(iii) Sentensi changamani

Mtoto aliyepotea amepatikana leo.

<table>
<tr><th colspan="5">S</th></tr>
<tr><td colspan="3">KN</td><td colspan="2">KT</td></tr>
<tr><td rowspan="3">N</td><td colspan="2">$S_2$</td><td rowspan="3">T</td><td>KE</td></tr>
<tr><td>KN</td><td>KT</td><td rowspan="2">E</td></tr>
<tr><td>N</td><td>T</td></tr>
<tr><td>Mtoto</td><td>Ø</td><td>aliyepotea</td><td>amepatikana</td><td>leo</td></tr>
</table>

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 181 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Njia ya kanuni**

(i) Sentensi sahili

Maziwa ni lishe bora.

**S**

| | | |
|---|---|---|
| **S** | → | **KN + KT** |
| **KT** | → | **t + KN** |
| **KN** | → | **N + KV** |
| **KV** | → | **V** |
| **T** | → | **t** |
| **t** | → | **ni** |
| **N** | → | **maziwa, lishe** |
| **V** | → | **bora** |

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



(ii) Sentensi ambatani

Wanafunzi wanafagia darasani na wengine wanapanga viti.

**S**

**S** → $S_1 + S_2$

$S_1$ → **KN + KT**

$S_2$ → **KN + KT**

**KT** → **T** { **KT** / **KE** }

**KN** → { **N** / **W** }

**KE** → **E**

**N** → **wanafunzi, viti**

**W** → **wengine**

**T** → **wanafagia,wanapanga**

**E** → **darasani**

**U** → **na**

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(iii) Sentensi changamani

Mtoto aliyepotea amepatikana leo.

**S**

| | | |
|---|---|---|
| **S** | → | **KN + KT** |
| **$S_2$** | → | **KN + KT** |
| **KT** | → | **T + KE** |
| **KN** | → | **N** |
| **KE** | → | **E** |
| **E** | → | **leo** |
| **N** | → | **mtoto** |
| **T** | → | **aliyepotea, amepatikana** |

**Njia ya maelezo**

Njia ya maelezo hutumia maneno katika kuchanganua sentensi.

(i) Sentensi sahili

Maziwa ni lishe bora.

- Hii ni sentensi sahili.
- Sentensi hii imeundwa na kirai nomino na kirai kitenzi.
- Kirai nomino kimeundwa na nomino.
- Nomino ni *maziwa*.
- Kirai kitenzi kimeundwa na kitenzi kishirikishi na kirai nomino.
- Kitenzi kishirikishi ni *ni*.
- Kirai nomino kimeundwa na nomino na kirai kivumishi.
- Nomino ni *lishe*.
- Kirai kivumishi kimeundwa na kivumishi.
- Kivumishi ni *bora*.

For Online Use Only


PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 184 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



(ii) Sentensi ambatani

Wanafunzi wanafagia darasani na wengine wanapanga viti.

- Hii ni sentensi ambatani.
- Sentensi hii imeundwa na sentensi mbili.
- Sentensi ya kwanza imeundwa na kirai nomino na kirai kitenzi.
- Kirai nomino kimeundwa na nomino.
- Nomino ni *wanafunzi*.
- Kirai kitenzi kimeundwa na kitenzi na kirai kielezi.
- Kitenzi ni *wanafagia*.
- Kirai kielezi kimeundwa na kielezi.
- Kielezi ni *darasani*.
- Kuna kiunganishi *na*.
- Sentensi ya pili imeundwa na kirai nomino na kirai kitenzi.
- Kirai nomino kimeundwa na kiwakilishi.
- Kiwakilishi ni *wengine*.
- Kirai kitenzi kimeundwa na kitenzi na kirai nomino.
- Kitenzi ni *wanapanga*.
- Kirai nomino kimeundwa na nomino.
- Nomino ni *viti*.

(iii) Sentensi changamani

Mtoto aliyepotea amepatikana leo.

- Hii ni sentensi changamani.
- Sentensi hii imeundwa na kirai nomino na kirai kitenzi.
- Kirai nomino kimeundwa na nomino na sentensi ya pili.
- Nomino ni *mtoto*.
- Sentensi ya pili imeundwa na kirai nomino na kirai kitenzi.
- Kirai nomino kimeundwa na nomino.
- Nomino ni *kapa*.
- Kirai kitenzi kimeundwa na kitenzi.
- Kitenzi ni *aliyepotea*.
- Kirai kitenzi kimeundwa na kitenzi na kirai kielezi
- Kitenzi ni *amepatikana*.
- Kirai kielezi kimeundwa na kielezi.
- Kielezi ni *leo*.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 185 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi 5.3

1. Fasili dhana ya sentensi kwa kutumia mifano ya Kiswahili.
2. Bainisha aina za sentensi za Kiswahili kwa mkabala wa kiuamilifu.
3. Jadili kwa mifano hatua za uchanganuzi wa sentensi.
4. Changanua sentensi zifuatazo kwa njia ya maelezo na majedwali kwa kutumia mikabala yote:
   (a) Gobosi amempa Kambona karatasi.
   (b) Msichana aliyekuja jana ameondoka leo.
   (c) Mama anapika na baba anaosha vyombo.
   (d) Sisi tulikubali kukosolewa ila wao walikataa.
   (e) Tuliondoka asubuhi sana.

**Urejeshi katika Kiswahili**

Miongoni mwa sifa za vitenzi vya lugha ya Kiswahili ni kubeba dhana ya urejeshi. Urejeshi huu hubainishwa kwa kutumia kiambishi cha o–rejeshi. Urejeshi katika Kiswahili hurejea nomino au kiwakilishi ambacho kilikwishatajwa au kinajulikana kulingana na muktadha. Aidha, kiambishi cha o–rejeshi hufuata mfumo wa upatanisho wa kisarufi kwa kuzingatia ngeli ya nomino iliyotajwa. Tazama mifano ifuatayo:

(i) Kitambaa kili*cho*nunuliwa kimefuliwa.

(ii) Mikoba iliy*o*haribika imetupwa.

(iii) Mhogo uli*o*nipa ni mchungu.

(iv) Mtoto aliy*e*faulu amekwenda chuo kikuu

**Utokeaji wa maumbo ya o–rejeshi**

Kama ilivyobainishwa katika vipengele mbalimbali vya sarufi, kila umbo lina kanuni au utaratibu maalumu wa utokeaji wake. Hivyo, maumbo ya o–rejeshi katika lugha ya Kiswahili hujitokeza katika mazingira yafuatayo:

(i) Hupachikwa mwishoni mwa shina *amba*-. Kwa mfano, amba*ye*, amba*cho*, amba*lo*, na amba*ko*.

(ii) Hutokea katikati ya kitenzi baada ya kiambishi cha wakati na kabla ya mzizi wa neno. Kwa mfano, ali*ye*ingia, tuna*cho*taka na ana*vyo*lima.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 186 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



(iii) Hutokea mwishoni mwa mzizi wa vitenzi vishirikishi. Kwa mfano, ndi*ye*, ndi*yo*, ndi*ko*, ndi*cho*, si*yo*, si*mo*, yu*mo*, na li*ko*.

(iv) Hutokea mwishoni mwa mizizi ya vioneshi vya karibu na msikilizaji. Hata hivyo, urejeshi huo hutegemea nomino iliyotangulia. Tazama mifano ifuatayo: Mti hu*o*, kiti hi*cho*, watoto ha*o*, nyumba hi*zo*, mahali hu*mo*, na kadhalika.

(v) Hupachikwa mwishoni mwa neno *kwa* kurejelea kilichotajwa. Kwa mfano, kwa*lo*, kwa*zo*, kwa*o* kama ilivyo katika sentensi, "Jambo amba*lo* kwa*lo* nimesikitika ni ulevi."

(vi) Hutokea mwishoni mwa vitenzi. Kwa mfano, aomba*ye*, kifuata*cho*, liliza*lo*, na aenda*ko*.

(vii) Hutokea mwishoni mwa kitenzi cha *kuwa na*. Kwa mfano, nina*cho*, ana*lo*, tuna*vyo*, na kadhalika.

**Dhima za urejeshi**

Urejeshi una dhima mbalimbali katika tungo za Kiswahili. Miongoni mwa dhima hizo ni hizi zifuatazo:

(a) Kurejelea mtenda au mtendwa wa jambo. Kwa mfano:

(i) Mwalimu ana*ye*fundisha aliajiriwa mwaka jana.

(ii) Walimu wana*o*fundisha waliajiriwa mwaka jana.

(iii) Mbuzi ali*ye*chinjwa alikuwa wa Mzee Kiki.

(iv) Kitabu kili*cho*potea kimepatikana kwenye begi la Majivuno.

Viambishi vya urejeshi -*ye*- na -*o*- vinamrejelea mtenda ambaye ni *mwalimu* katika sentensi (i) na *walimu* katika (ii). Katika mifano (iii) na (iv) viambishi vya urejeshi –*ye*- na –*cho*- vimetumika kurejelea mtendwa.

(b) Kushusha hadhi ya vishazi huru kuwa vishazi tegemezi. Kwa mfano:

| **Kishazi huru** | - | **Kishazi tegemezi** |
|---|---|---|
| Kiti kilivunjika | - | Kiti kilichovunjika |
| Mama alinunua nguo | - | Mama aliyenunua nguo |
| Gari linavuja mafuta | - | Gari ambalo linavuja mafuta |
| Jambo linatusumbua | - | Jambo litusumbualo |



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 187 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(c) Kutambulisha ngeli za nomino. Kila ngeli ina kiambishi chake cha urejeshi kama mfano unavyoonesha katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali 5.2** Urejeshi wa ngeli

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| (a) Mti uli*o*anguka | Miti ili*y*oanguka |
| (b) Sikio lili*lo*katwa | Masikio yali*yo*katwa |

Nomino katika (a) iko katika ngeli ya U - I, ambapo -*o*- na -*yo*- ndivyo viambishi vya urejeshi na mfano (b) ni ngeli ya LI - YA, ambapo viambishi vya urejeshi ni -*lo*- na -*yo*-.

(d) Kuunganisha sentensi mbili zinazohusiana katika kuunda sentensi changamani. Kwa mfano:
   (i) Mwizi amekamatwa.
   (ii) Mwizi amepelekwa polisi.

   Sentensi hizi mbili zikiunganishwa zitakuwa:

   (i) Mwizi amba*ye* amekamatwa amepelekwa polisi.
   (ii) Mwizi ali*ye*kamatwa amepelekwa polisi.

(e) Kueleza namna au jinsi tendo linavyotendeka. Kwa mfano:
   (i) Tunafurahia ana*vyo*imba nyimbo zake.
   (ii) Ninapenda ana*vyo*fanya kazi zake.

   Kuwapo kwa kiambishi cha urejeshi {-*vyo*-} katika mifano (i) na (ii) kunaonesha jinsi tendo linavyotendeka.

(f) Kuonesha mahali au sehemu ambapo jambo au tukio fulani linatendeka na mahali kitu au mtu alipo au anapopatikana. Kwa mfano:
   (i) Kule ana*ko*ishi ni mbali sana.
   (ii) Chumbani wana*mo*lala mna kitanda cha mbao.
   (iii) Wana*po*elekea ni ofisini kwangu.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 188 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Viambishi virejeshi -*ko*-, -*mo*-, na -*po*- vinaonesha mahali. Kiambishi -*ko*- hudokeza mahali kokote (sehemu ambayo si mahususi), -*po*- hudokeza sehemu mahususi na -*mo*- hudokeza sehemu ambayo ni ndani ya kitu.

## Zoezi la 5.4

1. Fafanua dhana ya urejeshi katika lugha ya Kiswahili.
2. Tunga sentensi kumi kuonesha dhima tofautitofauti za urejeshi.
3. Bainisha mazingira mbalimbali ya utokeaji wa viambishi vya O-rejeshi katika lugha ya Kiswahili.

## Tamrini

1. Eleza tofauti kati ya kirai na tungo nyingine.
2. Fafanua kwa mifano aina mbalimbali za virai.
3. Bainisha sifa za kishazi tegemezi na kishazi huru.
4. Eleza kwa mifano vigezo vinavyotumika kubainisha aina za sentensi.
5. Weka bayana tofauti zilizopo baina ya uchanganuzi wa kimuundo na uchanganuzi wa kidhima.
6. Kwa kutumia mifano fafanua njia zinazotumika kuchanganua sentensi.
7. Changanua sentensi zifuatazo kwa njia ya matawi kwa mkabala wa kimuundo.
   (a) Mwalimu hodari sana amehamishwa.
   (b) Mkuu wa shule anatoa nasaha ingawa wanafunzi hawamsikilizi kabisa.
   (c) Wakulima wamevuna maharage mengi sana mwaka huu.
   (d) Baridi ilipozidi walijifunika mashuka mazito.
   (e) Wezi waliokamatwa kwa kuvunja nyumba tatu wamepandishwa kizimbani.

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Sura ya Sita

# Utungaji

## Utangulizi

Sura hii inahusu utungaji. Katika sura hii utajifunza dhana ya utungaji, dhana ya insha, uandishi wa barua, kadi za mialiko, risala, hotuba, matangazo, na wasifukazi. Baada ya kumaliza kujifunza sura hii, utaweza kufafanua mambo muhimu ya kuzingatia katika uandishi wa insha na kuandika insha kwa kutumia mitindo mbalimbali. Pia, utaweza kuandika barua, kadi za mialiko, risala, hotuba, matangazo, na wasifukazi kwa kufuata taratibu za uandishi wa kazi hizo.

**Dhana ya utungaji**

Mrikaria (2009) anafafanua kwamba utungaji ni neno lenye kumaanisha namna au tendo la kutunga na kuyaweka maneno katika muundo wa kusikika au kusomeka. Pia anaendelea kufafanua kuwa ni utengenezaji wa mawazo ubongoni na kuyatoa kwa hadhira (msikilizaji/ msomaji) kwa njia ya mdomo au maandishi. Hivyo, kutunga ni kuweka pamoja mawazo au fikira ya dhana au wazo fulani katika mtiririko maalumu kwa maandishi au masimulizi ili kutoa picha halisi iliyokusudiwa kwa wasomaji au wasikilizaji.

**Dhana ya insha**

Insha ni utungo wenye mtiririko wa mawazo kuhusu jambo fulani. Kutunga insha ni kutoa mawazo kutoka kichwani, kuyakusanya kisha kuyaweka katika maandishi. Katika uandishi wa insha inampasa mwandishi kuzingatia taratibu za uandishi na matumizi ya lugha fasaha, sanifu na inayovutia hadhira.

**Aina za insha**

Kuna aina mbalimbali za insha mathalani insha za ufafanuzi, usimulizi, utoaji hoja, na uelezaji. Hata hivyo kwenye kiwango hiki tutahusika na insha za hoja, insha za wasifu, na insha za kisanaa kama zinavyofafanuliwa hapa chini.

***1 I nsha za hoja***

Insha za hoja ni insha ambazo hutetea mawazo ya aina fulani na kupinga mengine kwa ushahidi dhahiri. Insha hizi huwa na lugha ya kawaida ambayo si ya kisanaa.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 190 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



### *2 I nsha za wasifu*

Insha za wasifu ni insha zinazoeleza sifa za mtu binafsi. Sifa hizo zinaweza kuhusu maisha, uzuri, ubaya, au tabia zake kwa ujumla. Pia, insha za wasifu zinaweza kueleza sifa za mahali au za kitu.

### *3 I nsha za kisanaa*

Insha za kisanaa ni zile zilizoandikwa kwa kutumia vipengele vya kisanaa kama vile lugha ya picha na wahusika wa kubuni. Insha za kisanaa huwa na lugha yenye mvuto kama nahau, misemo, methali, tamathali za semi, picha, na ishara.

## Mambo muhimu ya kuzingatia katika uandishi wa insha

Kuna mambo muhimu ya kuzingatia katika uandishi wa insha. Mambo hayo ni kama vile:

(i) Kuelewa vyema mada inayozungumziwa.
(ii) Kuzingatia mpangilio mzuri wa mawazo wenye mantiki kutoka mwanzo hadi mwisho.
(iii) Kuwa na msamiati wa kutosha kuwezesha utumiaji mzuri wa lugha, sanifu na fasaha.
(iv) Kuzingatia matumizi mazuri ya alama za kiuakifishaji.
(v) Kuhusisha yanayoelezwa na hali halisi ilivyo katika jamii kwa kutoa mifano.
(vi) Kuwa na utangulizi unaofafanua mambo muhimu na hitimisho linaloendana na insha.
(vii) Kujua na kuzingatia sarufi ya lugha.

## Mitindo ya uandishi wa insha

Mitindo ya uandishi wa insha ni taratibu au namna za uandishi zinazotofautiana kati ya mwandishi mmoja na mwingine kulingana na aina ya insha inayoandikwa. Uchaguzi wa mtindo wa uandishi unategemea sana aina ya insha inayotungwa. Insha inaweza kuwa ya wasifu, hoja , matukio, visa vya kubuni, majadiliano (mjadala), au maelezo ya ufafanuzi wa kitaalamu kuhusu jambo au kitu fulani. Kwa mfano, insha inaweza kuhusu maisha ya mtu binafsi miaka 20 iliyopita, ukomeshaji wa dawa za kulevya, ajali, uvuvi, ugonjwa wa UKIMWI, na kadhalika. Aina ya mada ndiyo humwongoza mwandishi wa insha kuchagua mtindo wa uandishi utakaomsaidia kufafanua kwa ufasaha zaidi dhana aliyoikusudia ili kueleweka kwa hadhira yake.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 191 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Uandishi wa insha unaweza kutumia nafsi ya kwanza au ya tatu. Aidha, insha inaweza kutumia uandishi usiorejelea nafsi yoyote. Mitindo hii ya uandishi wa insha, inahusu insha za kisanaa na zisizo za kisanaa. Chunguza mifano ya insha ifuatayo:

**Insha ya kisanaa**

*Ilikuwa usiku wa manane, siku nisiyoweza kuisahau. Usingizi ulinipaa, mawazo yakaingia kichwani mwangu. Nje kulikuwa na giza nene lililotanda angani. Kwa mbali, nilisikia bundi wakilia na wadudu wakitoa milio inayovutia. Macho yangu yalielekea juu ingawa hakuna nilichokiona.*

*Nilizama katika dimbwi la mawazo kiasi cha kuhama nilipokuwa. Ooh! Masikini, kwa nini hakusikiliza ushauri? Ama kweli, asiyesikia la mkuu huvunjika guu. Mh! lakini kwa nini? Anhaa! Wahenga walisema, "Mkataa pema pabaya panamwita". Dimbwi hili la mawazo liliwahusu Gobosi na Simosa, vijana waliokuwa maarufu katika kijiji chetu. Gobosi alikuwa mvulana jamali wa miaka 19 na Simosa alikuwa msichana mrembo wa miaka 20. Vijana hawa walikuwa viongozi wa wanafunzi katika Shule ya Sekondari Jitambueni. Simosa alikuwa kidato cha sita na Gobosi kidato cha tano.*

*Gobosi na Simosa walipendana sana. Walisaidiana mambo mengi na kushikamana kama pete na kidole. Waliporudi kijijini kwetu walitukusanya vijana wenzao na kutufundisha mbinu za kilimo bora na ufugaji bora. Mimi nilijifunza kufuga kuku na kulima nyanya. Hakika nilijifunza mengi. Gobosi alieleza ndoto za maisha yake. Vijana wote tulimpenda sana. Wengi tulimtazamia kuwa kiongozi mzuri katika taifa letu.*

*Baada ya kuhitimu kidato cha sita, Simosa alifaulu na kujiunga na Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine kilichopo Morogoro. Yeye alipenda kilimo na ufugaji. Gobosi alichaguliwa katika Chuo Kikuu cha Mzumbe kusomea shahada ya uongozi. Wanakijiji tulifurahi sana. Tulikuwa na matarajio makubwa kwa wasomi hawa.*



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 192 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



*Siku moja majira ya asubuhi nilipata fununu iliyokuwa ikisambaa kijijini kumhusu Gobosi. Moyo ulienda mbio na macho ya wengi yalibaki yakitiririka machozi na kukodolewa. Ooh! Masikini Gobosi! Mzee mmoja alisikitika. Kumbe alipofika Mzumbe alijiunga na makundi ya vijana wa mitaani wanaotumia dawa za kulevya. Ni mwaka mmoja sasa umepita tangu alipojiunga na Chuo Kikuu cha Mzumbe. Sasa, akili zimemruka na amekuwa kama teja! Hawezi tena kusoma. Wazazi wake walimpeleka Hospitali ya Taifa Muhimbili kupatiwa matibabu, lakini bado hali haikuwa nzuri. Baada ya kuanza kutumia dawa za kulevya alianza kuwa mgomvi. Siku moja alipigana na mwenzake ambaye alimpiga jiwe kichwani na kuharibu sehemu ya ubongo wake. Ndoto zake zote zimepotea. Wazazi na jamii tumepoteza nguvu kazi ya taifa. Alishauriwa sana aachane na vikundi hivyo lakini hakusikia; hakika mkaidi hafaidi mpaka siku ya Idi. Ghafla nilianza kusinzia kwa huzuni ya moyo na kutokomea katika ulimwengu wa njozi.*

**Insha ya hoja**

*Sanaa ni namna ya mtu kutumia vitendo kujieleza. Sanaa inaweza kuwa ya kutengeneza kitu au kuchora picha yenye ujumbe fulani. Watu wengi huwa na kipaji cha sanaa wanapokuwa wadogo. Wanapenda kuchorachora picha za watu, picha za wanyama au za magari. Pia, hutengeneza vitu kama magari kwa kutumia matete, mabua, maboksi na vipande vya madebe, na kujaribu kuyaendesha. Hujenga vijumba vya udongo, hutengeneza vyungu na kusuka vikapu. Tanzania inatambua umuhimu wa sanaa kwa kuwa ujuzi huu hufundishwa katika elimu ya jadi. Kwa hiyo, ni lazima taifa litoe nafasi kwa watoto kujifunza sanaa. Mahali pazuri pa kujifunzia elimu hii ni shuleni.*

*Watoto wetu wakipata nafasi ya kujifunza aina mbalimbali za sanaa wataweza kufanya shughuli mbalimbali za ufundi kama ujenzi, useremala, ufundi rangi na uchoraji, ambazo zitawawezesha kuishi kwa kujitegemea na kuinua uchumi wa taifa. Vilevile, sanaa itawaongezea moyo wa kuthubutu au kujaribu kutengeneza vitu bila kuogopa na itainua upeo wa utendaji wao na uwezo wao wa kubuni vitu.*



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 193 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*Ujuzi watakaopata kwenye sanaa utawasaidia watoto kutumia muda wao vizuri. Kwa hiyo, ni muhimu kuifundisha na kuiendeleza sanaa kwa watoto kwa sababu itawasaidia kujitegemea, kuwapatia riziki na ajira.*

## Insha ya wasifu

*Katika historia ya nchi yetu, tuliwahi kuwa na Waziri Mkuu aliyekuwa akiitwa Edward Moringe Sokoine. Yeye alizaliwa mwaka 1938 katika wilaya ya Maasai land (kwa sasa Monduli), mkoani Arusha na kufariki mwaka 1984 kwa ajali ya gari. Edward Moringe Sokoine alikuwa miongoni mwa viongozi wazalendo waliowahi kupata nafasi za kuiongoza nchi yetu. Sokoine alikuwa Waziri Mkuu kwa miaka tofautitofauti tangu 1977 hadi mwaka 1981 alipomuomba ruhusa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ili aende nje ya nchi kujifunza kuhusu ujamaa. Alirudi nchini mwaka 1983 ambapo alirejea katika nafasi yake ya Waziri Mkuu mpaka mwaka 1984 alipofariki.*

*Katika uongozi wake, hayati Sokoine aliamini katika haki na usawa kwa watu wote. Pamoja na kusimamia hayo, alisisitiza pia uwajibikaji kwa kila mwananchi katika kufanya kazi. Kiongozi huyu alikuwa mfuasi wa falsafa ya hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, baba wa taifa la Tanzania, ambayo ilikuwa ikisisitiza uhuru, umoja na kazi. Katika falsafa hii, iliaminika kuwa matunda ya uhuru tulioupata kutoka kwa wakoloni yanapaswa kuendana na watu kuwajibika katika kufanya kazi viwandani, kazi za kilimo, uvuvi na ufugaji. Aidha, watumishi wa umma walitakiwa kuwajibika kutoa huduma kwa wananchi bila kuomba wala kupokea rushwa.*

*Kutokana na msimamo huo, Edward Moringe Sokoine alianzisha vita dhidi ya uhujumu uchumi, biashara za magendo na ulanguzi vilivyokuwa vimeanza kushamiri katika kipindi hicho. Akiwa kama kiongozi wa serikali, alipambana na hali hiyo kwa mafanikio makubwa. Aidha, Sokoine alikuwa ni kiongozi aliyeichukia rushwa kwa vitendo. Katika mapambano yake dhidi ya rushwa aliwahi*



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 194 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



*kusema kuwa, "Ole wao wale wanaotumia nafasi zao za umma na serikali kuiba, kuhujumu uchumi na kupokea rushwa kwa maana salama yao ni kudra za Mwenyezi Mungu; labda nisiwajue."*

*Kwa hakika, yapo mengi yanayostahili kusemwa kuhusiana na hayati Sokoine kutokana na uzalendo wake katika taifa hili. Hata hivyo, itoshe tu kwa sasa kusema kuwa hayati Edward Moringe Sokoine ni miongoni mwa viongozi waliowahi kutokea katika taifa hili la Tanzania ambao wanaendelea kuwa mfano wa kuigwa.*

## Zoezi la 6.1

1. Je, ni vipengele gani vinavyobainisha sanaa katika insha za kisanaa?
2. Pendekeza kichwa cha insha kinachofaa kwa kila insha.
3. Utafanya nini ili kujiepusha na hali iliyomkuta Gobosi katika insha ya maelezo ya kisanaa?
4. Tunga insha moja ya wasifu wa kiongozi mashuhuri unayemfahamu katika bara la Afrika.
5. Tunga insha moja ya kisanaa.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 195 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Uandishi wa barua**

Barua ni maandishi yenye ujumbe unaopelekwa kwa mtu mwingine kwa njia ya mkono au posta. Kuna aina mbalimbali za barua, ambazo tofauti zake hutokana na dhima za barua hizo. Aina hizo ni:

(i) Barua za kirafiki
(ii) Barua rasmi
(iii) Barua na kadi za mialiko
(iv) Barua za magazetini

**Barua za kirafiki**

Hizi ni barua ambazo huandikwa kwa ndugu na jamaa kama vile rafiki, baba, shangazi, mama, mjomba, dada, na kaka. Vilevile hujulikana kama barua za kindugu. Maudhui ya barua za aina hii yanaweza kuwa kusalimiana, kupeana taarifa juu ya maisha ya kila siku, kushukuru, kuomba kusaidiwa, na hata kutoa pongezi au rambirambi. Barua ya kirafiki ina muundo ufuatao:

(a) Anwani ya mwandishi

Anwani ya mwandishi huandikwa juu upande wa kulia pembeni mwa karatasi. Anwani hii hutumiwa na mwandikiwa pindi anapojibu barua aliyopelekewa.

(b) Tarehe

Tarehe huandikwa mara tu baada ya anwani ya anayeandika barua. Lengo ni kumjulisha mwandikiwa muda au wakati ambao barua hiyo imeandikwa. Kuna namna mbalimbali za uandishi wa tarehe kama ifuatavyo:

(i) 12.3.2016
(ii) 12/3/2016
(iii) 12-3-2016
(iv) 12 Machi, 2016

(c) Mwanzo wa barua

Mwanzo wa barua za kirafiki huwa na salamu ya awali. Salamu ni maneno yanayoonesha uhusiano alionao mwandishi na mtu anayemwandikia. Pia, maneno haya humweka tayari aliyeandikiwa barua kujua kuwa anawasiliana na nani; hivyo, kujenga hamasa ya kuisoma barua. Mfano wa salamu za awali ni kama ifuatavyo:



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 196 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



(i) Mpendwa mama, shikamoo!
(ii) Baba mpendwa, shikamoo!
(iii) Dada mpendwa, salamu!
(iv) Mpendwa mwanangu, salamu!

(d) Kiini cha barua
Sehemu hii ndiyo inayoeleza madhumuni ya kuandika barua. Hivyo, mwandishi anapaswa kubainisha kusudi la barua. Sehemu hii isipoandikwa vizuri, lengo zima la kuandika barua linaweza kupotea. Pia, huonesha kama barua iliyoandikwa inahitaji kujibiwa.

(e) Mwisho wa barua
Sehemu hii inaonesha mwisho wa barua kwa namna mbalimbali. Namna hizi hutegemea uhusiano wa aliyeandika na anayeandikiwa barua. Miisho ya barua za kindugu au kirafiki inaweza kuwa:

(i) Wasalamu,
(ii) Mwanenu mpendwa,
(iii) Mwanao mpendwa,
(iv) Rafiki yako wa moyo,
(v) Wako akupendaye,

(f) Jina la mwandishi
Sehemu hii inaonesha jina la mtu aliyeandika barua. Jina la mwandishi huandikwa mwishoni kabisa mwa barua. Mwandishi anaweza kuweka saini yake sambamba na jina au asiweke saini.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 197 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Muundo wa barua za kirafiki






PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 198 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



**Mfano wa barua ya kirafiki**

Shule ya Sekondari Chang'ombe,
S.L.P. 2329,
Dar es salaam.
4. 4. 2016.

Wazazi wapendwa, shikamooni!

Ni wiki moja sasa tangu niondoke nyumbani kurejea masomoni. Ninapenda kukujulisheni kuwa, safari yangu ilikuwa nzuri na kuwa mimi na marafiki zangu wote tulifika salama. Pia, sote tu wazima na tunaendelea vema na masomo. Ninaomba mzidi kutuombea afya njema, ili tuweze kuendelea na masomo yetu bila kikwazo na hatimaye tufaulu vizuri katika mitihani yetu ya muhula mwezi wa sita. Binafsi, ninakuahidini kuwa nitajitahidi kufanya vizuri katika masomo yangu. Salamu zangu ziwafikie bibi, babu, na mjomba Lukas na familia yake.

Mwanenu,



Kidinga Kadunga.

## Zoezi la 6.2

1. Fafanua kwa mifano mambo muhimu ya kuzingatia katika uandishi wa barua za kindugu au kirafiki.
2. Andika barua kwa baba ukimweleza kuwa likizo imekaribia akutumie nauli ya kurudi nyumbani.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 199 25/09/2019 13:57
For Online Use Only

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Barua rasmi**

Barua rasmi, ambazo pia hujulikana kama barua za kikazi au kiofisi, huandikwa kutoa taarifa za mikutano, vikao, kuomba huduma, kuomba kazi, kufanya manunuzi kwa kuagiza, kualika kiongozi na kutoa taarifa ya kutohudhuria kikao au mkutano (shughuli rasmi). Kuna aina mbalimbali za barua rasmi. Barua hizo zinaweza kuwa barua za kuomba kazi au huduma, kuagiza na kupokea vifaa, kutoa taarifa, utambulisho, au kuomba ruhusa. Barua hizi huwa ni fupi na zenye kueleza ujumbe maalumu kwa lugha nyepesi na ya wazi. Hivyo, sentensi zake huwa fupi, chache na zenye kulenga dhamira kuu ya barua.

**Muundo wa barua rasmi**

Barua rasmi zinajengwa na anwani ya mwandishi, tarehe, namba ya kumbukumbu, anwani ya mwandikiwa, mwanzo wa barua, kichwa cha barua, kiini cha barua, hitimisho, saini, jina la mwandishi, na cheo cha mwandishi wa barua.

(a) Anwani ya mwandishi
Anwani ya mwandishi huandikwa juu, kulia mwa karatasi. Anwani ya mwandishi inatakiwa kuandikwa kwa usahihi kwa sababu anwani hii hutumika kutuma majibu au taarifa kwa mwandishi wa barua husika.

(b) Tarehe
Tarehe huandikwa chini ya anwani ya mwandishi katika mstari wa kumbukumbu ya barua.

(c) Namba ya kumbukumbu
Namba ya kumbukumbu huandikwa sambamba na tarehe upande wa kushoto. Namba ya kumbukumbu husaidia katika kutunza barua kwa utaratibu katika jalada la mhusika. Vilevile, husaidia katika urejeleaji wa barua husika kwa urahisi. Kwa kawaida, namba ya kumbukumbu huandikwa kwa ufupi kama *Kumb.Na*.

(d) Anwani ya mwandikiwa
Anwani ya mwandikiwa huandikwa kushoto baada ya namba ya kumbukumbu. Anwani hiyo hutanguliwa na cheo cha anayeandikiwa barua.

(e) Mwanzo wa barua
Mwanzo wa barua huandikwa chini ya anwani ya mwandikiwa. Mifano ya mwanzo wa barua ya kikazi ni kama vile *Ndugu*, *Mheshimiwa*, *Shekh*, *Mstahiki*, na *Askofu*.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

For Online Use Only

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 200 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



(f) Kichwa cha barua

Kichwa cha barua lazima kitaje wazi jambo au dhamira ya barua. Kichwa cha barua kinaandikwa kwa ufupi. Huandikwa ama kwa herufi kubwa bila kupigiwa mstari au kwa herufi ndogo na kupigiwa mstari. Katika uandishi wa kuchapa si lazima kupigia mstari kichwa cha habari badala yake hukolezwa wino.

(g) Barua yenyewe

Kiini cha barua huandikwa kwa ufupi na kwa uwazi ili ujumbe ueleweke. Vilevile, ni lazima kiini kitoe taarifa zote za lazima zinazohusiana na lengo la barua.

(h) Mwisho wa barua

Hii ni sehemu ambayo huhitimisha barua yenyewe. Mara nyingi, huwa na maneno kama vile *wako mtiifu*, *wako kazini*, *wako katika ujenzi wa taifa*, *wako katika imani*, *wako katika utume*, *wako katika utumishi*, na *wasalaam*.

(i) Saini na jina

Hii ni sehemu ambayo mwandishi wa barua anatakiwa kutia saini na chini ya saini hiyo huandikwa jina lake kamili.

(j) Cheo cha mwandishi

Cheo cha mwandishi huandikwa chini ya jina la mwandishi. Kipengele hiki kinawahusu waandishi wenye vyeo vya kiofisi. Kielelezo kifuatacho kinaonesha mfano wa muundo wa barua rasmi.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 201 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Muundo wa barua rasmi**






PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 202 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



**Mfano wa barua ya maombi ya kazi**

Kijiji cha Ujamaa Simakweni,
S.L.P. 235,
**Arusha.**
02.04.2016

Kumb. Na.2018/KPF/01.

Mkurugenzi Mtendaji,
Kampuni ya Viatu,
S.L.P. 458,
**Bahi.**

Ndugu,

**YAH: MAOMBI YA KAZI YA UHANDISI**

Tafadhali husika na somo lililotajwa hapo juu.
Rejea tangazo la tarehe 12.3.2016 lililotolewa kwenye gazeti la Mwananchi likihitaji mhandisi mitambo katika Kampuni ya Viatu Bahi.

Ninayo heshima kubwa kuomba kazi ya Uhandisi wa Mitambo katika kampuni yako. Mimi ni Mtanzania mwenye umri wa miaka 25. Nilihitimu elimu yangu ya shahada ya awali ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika masomo ya uhandisi mwaka 2015 na kufaulu kwa kupata daraja la kwanza. Katika kipindi cha masomo, nilifanya kazi hiyo katika kampuni mbili wakati wa mazoezi ya mafunzo kwa vitendo. Hivyo, nina imani kwamba elimu na uzoefu nilionao katika kazi hiyo vitanisaidia kuleta ufanisi wa kazi kama nitakubaliwa kufanya kazi katika kampuni yako.

Pamoja na barua hii, ninaambatisha nakala za vyeti na wasifukazi wangu kwa uthibitisho. Ninatanguliza shukurani zangu za dhati.

Wako mwaminifu,



Athumani Makame,
Mwombaji.

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 6.3

1. Chunguza barua hiyo ya maombi ya kazi kisha bainisha vipengele muhimu vilivyomo katika barua.
2. Jifanye wewe ndiye Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Viatu Bahi. Mwandikie ndugu Athuman Makame barua ya kumtaarifu kuwa anatakiwa kuhudhuria kwenye usaili utakaofanyika tarehe mliyoipanga.

**Barua na kadi za mwaliko**

Taarifa za mwaliko huweza kutolewa kwa njia ya barua au kadi.

**Barua za mwaliko**

Barua za aina hii zinatoa taarifa kuhusu kufanyika kwa shughuli fulani na kualika. Shughuli hii inaweza kuwa mkutano, semina, tukio la kutoa elimu kuhusu jambo fulani, ufunguzi wa shughuli fulani maalumu, mahafali au utoaji wa vyeti. Ikiwa ni mwaliko wa kiofisi barua hizi hufuata muundo wa barua rasmi. Mwaliko huwa na vipengele mbalimbali kama vile jina la mwandishi na anwani yake, jina la mwalikwa, lengo la mwaliko, siku, tarehe, mahali, na muda wa tukio. Vilevile, iwapo anayealikwa anatakiwa kuja na vifaa au vitu maalumu vitakavyotumika basi hupewa taarifa hiyo siku kadhaa kabla ya tukio.

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 204 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



**Mfano wa barua ya mwaliko**

Tunza Mazingira,
S.L.P. 2121,
**Newala.**

Kumb. Na. AY/P3/20/015. 02/09/2016.

Allen Isango,
Meneja wa Soko la Majengo,
S. L.P. 51,
**Mtwara.**

Ndugu,

**YAH: MWALIKO WA KUWA MGENI RASMI KATIKA MAADHIMISHO YA MIAKA KUMI YA KIKUNDI CHA KUTUNZA MAZINGIRA**

Tafadhali husika na kichwa cha barua hapo juu.
Kikundi cha Tunza Mazingira (TM) kinaadhimisha miaka kumi tangu kianzishwe. Sherehe ya maadhimisho hayo itafanyika tarehe 20/10/2016 saa 10:00 jioni, katika ukumbi wa Changamkeni.

Katika sherehe hiyo, unaalikwa uwe mgeni rasmi. Vilevile, tutakuomba uwatunuku vyeti wanachama walioshiriki kikamilifu katika kuyatunza mazingira tangu kikundi kilipoanzishwa.

Tunategemea maombi yetu yatakubaliwa.
Wako,



Akilimali Bichuro.
**Mwenyekiti.**

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 205 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kadi ya mwaliko**

Kama ilivyo kwa barua za mialiko, kadi ya mwaliko hutumia maneno machache kutoa taarifa inayokusudiwa. Tofauti kati ya barua ya mwaliko na kadi ya mwaliko iko katika muundo. Tazama mfano ufuatao wa kadi ya mwaliko:

> **Mwaliko**
>
> *Familia ya Bw. na Bi. Hatto Bito wa Namtumbo, Songea inayo furaha kukualika/kuwaalika Mhe./Prof./Dkt./Shk./Mch./Pdr./Bw./Bi./Bw.&Bi.*
>
> *……………………………………………………*
>
> *Kwenye tafrija ya ndoa ya kijana wao Mbeki anayemwoa Umu Muru siku ya Jumamosi, tarehe 27 Julai, 2017 katika ukumbi wa Kumbikumbi uliopo Chanji, Sumbawanga kuanzia saa 12:00 jioni hadi saa 06:00 usiku.*
>
> *Tafadhali fika na kadi hii.*
>
> *Majibu (kwa wasiofika)*
> *Dugilo Dami; Simu: 0977-0909909*

## Zoezi la 6.4

1. Andika kadi ya mwaliko wa harusi ya kijana wako Julius Mapembe na kuomba michango kwa ndugu, marafiki na majirani ili kufanikisha shughuli hiyo.
2. Andika barua kujibu mwaliko wa harusi ya Julius Mapembe ulioalikwa ukiitaarifu familia hiyo kuwa hutahudhuria.

**Barua ya uagizaji na upokeaji wa vifaa**

Hii ni barua inayohitaji maelezo maalumu na ya kutosha ya vitu au bidhaa zinazoagizwa au kupokelewa. Barua ya kuagiza bidhaa ni lazima imtaje mwagizaji au kampuni ambako bidhaa zinatakiwa kupelekwa, aina ya bidhaa, kiasi cha bidhaa, kiasi cha fedha zinazolipwa, njia ya malipo, siku ya kutuma mzigo, na njia ya usafirishaji. Njia ya usafirishaji inaweza kuchaguliwa na anayeagiza bidhaa au ikafanywa kwa makubaliano kati ya mtumaji na mwagizaji. Taarifa hizi zote



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 206 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



za uagizaji na upokeaji wa mzigo zinatakiwa kuwa wazi kwa pande zote mbili. Baada ya kupokea bidhaa, anayeagiza lazima aandike barua ya kukiri kupokea bidhaa hizo. Barua hiyo itaonesha pia iwapo bidhaa zote zimefika salama au kuna upungufu au uharibifu wowote uliotokea ambao unahitaji kufidiwa. Aidha, aliyetuma bidhaa ni lazima aandike barua ya kukiri kupokea fedha za malipo kwa ajili ya bidhaa alizotuma. Wakati mwingine fedha za malipo hutumwa kabla ya mwagizaji kutumiwa bidhaa. Ikiwa fedha hizo zitatumwa kabla ya kutumwa kwa bidhaa basi stakabadhi ya malipo itatumwa pamoja na bidhaa.

**Mfano wa barua ya uagizaji wa bidhaa**

Shirika la Ufugaji wa Kuku,
S.L.P. 1,
**Tarime.**

Kumb. Na. AF/P1/15/1. 20/03/2016.

Meneja Masoko,
Kampuni ya Mifugo Nianjema,
S.L.P. 9540,
**Ukerewe.**

Ndugu,

**YAH: AGIZO LA BIDHAA ZA KUKU**

Tafadhali husika na kichwa cha habari hapo juu. Nitumie bidhaa zifuatazo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mifuko ya chakula cha kwanza cha vifaranga 20 @ sh. 40,000 | 800,000/= |
| 2. | Mifuko ya chakula cha kukuzia vifaranga 20 @ sh. 40,000 | 800,000/= |
| 3. | Vyombo vya chakula 25 @ sh. 5000 | 125,000/= |
| 4. | Vyombo vya kunyweshea maji 15 @ sh. 10,000 | 150,000/= |
| 5 . | Chanjo ya kideri chupa 3 @ sh. 50,000 | 150,000 /= |
| 6. | Gharama za usafiri | 125,000/= |
| JUMLA | | 2,150,000/= |



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 207 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Ninakutumia shilingi milioni mbili, laki moja na elfu hamsini tu (**2,150,000/=** kwa njia ya simu ikiwa ni fedha ya kulipia bidhaa hizo, na gharama ya usafiri. Tafadhali tumia gari la mizigo kusafirisha bidhaa hizo. Iwapo gharama zitaongezeka, ninaomba uniarifu.

Ni mimi,



Simbila Kibukile,
**Afisa Manunuzi.**

## Zoezi la 6.5

Ukiwa kama Meneja Masoko wa Kampuni ya Mifugo ya Nianjema, jibu barua hii ukikiri kupokea bidhaa.

**Barua za taarifa**

Hizi ni barua zinazoandikwa kutoa taarifa fulani. Taarifa hizo zinaweza kuwa wizi, uchomaji ovyo misitu, tahadhari kuhusu hali ya hewa, matukio mbalimbali yanayotokea ofisini, kijijini na ziara mbalimbali za viongozi. Barua hizi zina muundo sawa na barua nyingine za kiofisi. Tazama mfano ufuatao wa barua ya taarifa:

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 208 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Mwenyekiti Serikali ya Mtaa,
Mtaa wa Ilongero,
S.L.P. 1001,
**Singida.**

Kumb.Na.IL/PL.03. 21.04.2001.

Mkuu wa Kituo cha Polisi,
Kata ya Ilongero,
S.L.P. 36,
**Singida**.

Ndugu,

**YAH: KUKITHIRI KWA MATUKIO YA WIZI WA MIFUGO**

Kichwa cha habari kinahusika.
Ninakutaarifu kwamba kumekuwa na wizi wa mifugo katika maeneo mbalimbali ya kijiji cha Ilongero kwa takribani majuma mawili sasa, hasa nyakati za usiku. Kama kijiji, tumeanzisha ulinzi shirikishi lakini wezi wanatumia silaha za moto. Kwa hiyo, tumeshindwa kupambana nao. Tafadhali tunaomba msaada wa polisi ili kukomesha matukio haya.

Wako katika utumishi,



Irunde Mawazo,
**Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa.**

**Barua ya utambulisho**

Hii ni barua ambayo huandikwa na afisa mwenye mamlaka kwa ajili ya kumtambulisha mtu katika ofisi au taasisi fulani. Mtu anayetambulishwa anaweza kuwa ni mfanyakazi, muumini wa dini, mwanafunzi au mkazi wa eneo fulani. Mara nyingi, barua za utambulisho huwa na picha ya anayetambulishwa. Picha hii hugongwa muhuri wa mamlaka inayomtambulisha. Tazama mfano ufuatao:

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 209 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Picha iliyogongwa mhuri

Serikali ya Mtaa wa Migombani,
S.L.P. 41,
Buhigwe.

22.08.2018.

Meneja wa Benki,
NMB,
Tawi la Buhigwe,
S.L.P. 1617,
**Buhigwe**.

Ndugu,

**Yah: Utambulisho wa Bw. Kenasi Ukweli**

Mtajwa hapo juu ni mkazi wa mtaa wa Migombani. Ni mjasiriamali wa biashara ndogondogo katika soko la Kumusenga. Kutokana na biashara anazozifanya, ana kipato cha uhakika. Tafadhali akubaliwe kufungua akaunti ya akiba katika tawi lako.

Wako katika utendaji,



Petro Gasore,
**Afisa Mtendaji wa Mtaa wa Migombani.**

**Barua za magazetini**

Hizi ni barua zinazoandikwa kwa mhariri. Barua hizi zinaweza kuwa na lengo la kutoa pongezi, kutoa maoni, kushauri, au kufichua maovu. Barua hizi ni fupi na za wazi. Hutumia lugha rahisi na yenye kueleweka. Barua hizi hutumwa kwa mhariri na kuandikwa gazetini ili jamii iweze kuzisoma. Hata hivyo, kuchapishwa kwa barua hizi kwenye gazeti kunategemea uzito wa hoja na kupatikana kwa nafasi katika gazeti zinakotumwa. Barua za magazetini huwa zina muundo ufuatao:



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

For Online Use Only

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 210 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


(a) Kichwa cha barua

Huandikwa mwanzoni kwa herufi kubwa zilizokolezwa wino ikiwa kimechapwa, au kwa herufi ndogo na kupigiwa mstari.

(b) Mwanzo wa barua

Huandikwa upande wa kushoto baada ya kichwa cha barua. Huanza kwa kumtaja mhariri, kwa mfano, *Ndugu Mhariri*.

(c) Kiini cha barua

Katika sehemu hii hutolewa sababu za kuandika barua (hoja) ambazo hutolewa kwa mantiki na mtiririko unaofaa.

(d) Mwisho wa barua

Katika sehemu hii mwandishi husisitiza kiini cha barua ambacho huendana na lengo la barua. Kwa mfano, kama ni barua ya maombi itaishia na maombi.

(e) Jina la mwandishi, anwani na tarehe

Taarifa hizi huandikwa mwishoni mwa barua upande wa kushoto. Namba ya simu ya mwandishi pia inaweza kuandikwa.

For Online Use Only

**Muundo wa barua za magazetini**

KICHWA CHA BARUA

MWANZO WA BARUA

KIINI CHA BARUA

MWISHO WA BARUA

JINA, ANWANI YA MWANDISHI NA TAREHE


PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 211 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Mfano wa barua ya gazetini**

**UMUHIMU WA TEKNOLOJIA KATIKA ELIMU**

Ndugu Mhariri,

Ninaomba kutumia fursa hii kuwasilisha maoni yangu kupitia ukurasa wa gazeti lako. Maoni yangu yanaelekezwa katika mfumo wa elimu, hususani mchango wa teknolojia katika kuboresha utoaji na upataji wa elimu. Ili kuboresha mfumo wa utoaji na upataji wa elimu kuna mambo mengi ambayo teknolojia inaweza kutumika kuyafanya.

Mosi, teknolojia inaweza kutumika kama chanzo cha maarifa mbalimbali. Mathalani, wanafunzi na walimu wanaweza kupakua vitabu, majarida na machapisho mbalimbali ambayo yatatumika kuimarisha maarifa yanayopatikana katika somo linalofundishwa.

Pili, teknolojia inaweza kutumika katika uwasilishaji wa somo darasani. Katika hili mwalimu anaweza kutumia kompyuta na projekta ambavyo vitamrahisishia kuwa na uwezo wa kufundisha mambo mengi kwa muda mfupi na kwa ufanisi. Aidha, mwalimu anaweza kuonesha mambo mbalimbali kwa kuyatengeneza kwa programu za kompyuta au kuyapakua kwenye mtandao na kuyaonesha darasani kwa kutumia projekta kama mifano.

Tatu, teknolojia inaweza kutumika kufundishia darasa kubwa kwa wakati mmoja. Vilevile, inaweza kutumika katika kuweka usawa kwa wanafunzi wote ambapo mwalimu mmoja wa somo fulani anaweza kufundisha nchi nzima na walimu wengine wakawa wanatumika katika kuwawezesha wanafunzi kuelewa somo lililofundishwa na kusimamia ufanyaji wa mazoezi kama ilivyo nchini China.

Kwa hiyo, ninapenda kutoa maoni haya kupitia ukurasa huu ili jamii ione umuhimu wa kutumia teknolojia katika kuboresha elimu nchini mwetu.

Ni mimi,
Mkereketwa wa Teknolojia,
S.L.P. 2013,
Mpanda, Katavi.
Simu: 0141-010209.
21/12/2018.

For Online Use Only


PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 212 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



## Zoezi la 6.6

Andika barua kwa mhariri wa gazeti lolote ukionesha masikitiko yako kuhusu jambo lolote linalokukera.

**Uandishi wa risala**

Risala ni aina ya utungaji wa kuandikwa ambao huandaliwa na kundi la watu na kusomwa kwa kiongozi au mgeni rasmi. Kundi la watu linaweza kuwa la wanafunzi, wafanyakazi, wafanyabishara, wanakijiji na kadhalika. Risala husomwa kwa lengo la kupata majibu au ufafanuzi wa changamoto kutoka kwa mgeni rasmi. Kupitia risala, mgeni rasmi pamoja na wageni wengine hupata fursa ya kujua mambo mbalimbali kuhusu kundi lililoandaa risala.

**Mambo ya kuzingatia wakati wa kuandika risala**

Mwandishi wa risala anapaswa kuzingatia mambo yafuatayo:

(i) Kuzingatia sheria na kanuni za sarufi ya lugha inayohusika ili iweze kueleweka kwa mgeni rasmi na kwa hadhira iliyopo;

(ii) Kutumia alama sahihi za kiuakifishaji kwa sababu ndizo zinazobainisha na kujenga maana katika habari;

(iii) Kueleza wazo moja katika aya inayojitegemea, mathalani, kama anaeleza hoja tano, kila aya iwe na hoja moja;

(iv) Kuzingatia muundo wa risala. Risala inatakiwa iwe na sehemu nne: kichwa cha risala, utangulizi, kiini cha risala na hitimisho ili iwe na mtiririko wa kimantiki;

(v) Kutumia lugha fasaha na sanifu inayoeleweka kwa jamii inayohusika; na

(vi) Kufahamu mamlaka na uwezo wa mgeni rasmi ili kumweleza mambo ambayo yapo ndani ya uwezo wake ili mgeni rasmi aweze kuijibu risala hiyo.

**Sifa za msomaji wa risala**

Msomaji wa risala anatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:

(i) Awe na sauti ya kusikika vizuri kwa mgeni rasmi na hadhira.

(ii) Aweze kutamka maneno kwa usahihi ili aeleweke kwa mgeni rasmi na hadhira.

(iii) Aweze kusoma kwa kuzingatia alama za kiuakifishaji.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 213 25/09/2019 13:57

For Online Use Only

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(iv) Aweze kuisoma na kuimudu hadhira na wasikilizaji wake kwa kuangalia mwitikio wao. Kwa mfano, kama wanashangilia ni vyema aache kusoma mpaka watakapoacha kushangilia ili kuhakikisha hadhira inasikiliza na kuelewa kila kitu kinachosomwa.

(v) Kujiamini na kuwa na utashi wa kutosha ili uwasilishaji uwe mzuri na kuepuka kuathiri ujumbe kwa namna yoyote.

**Muundo wa risala**

Muundo wa risala una sehemu nne zifuatazo:

(a) Kichwa cha risala

Kichwa cha risala ni lazima kibebe mambo muhimu matano ambayo ni mwandishi au waandishi, mahali, mwandikiwa, tukio na tarehe. Kichwa cha risala lazima kiandikwe kwa herufi kubwa. Tazama mfano ufuatao:

RISALA YA WAHITIMU WA KIDATO CHA SITA KATIKA SHULE YA SEKONDARI MSALATO KWA MGENI RASMI, NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA, KATIKA MAHAFALI YA NANE TAREHE 22/04/2016

(b) Utangulizi wa risala

Utangulizi wa risala hujumuisha vipengele vifuatavyo:

(i) Kuwatambua viongozi waliopo kwa kutaja vyeo na majina yao.

Ili kipengele hiki kiandikwe vizuri ni lazima mwandishi wa risala awajue wageni watakaohudhuria katika tukio linalohusika. Mpangilio huanza na mgeni rasmi na kufuatiwa na wageni wengine kwa kuzingatia vyeo vyao, yaani kuanza na mwenye cheo cha juu zaidi na kuishia na mwenye cheo cha chini. Angalia mfano ufuatao:

*Ndugu mgeni rasmi, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia,*

*Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo,*

*Mheshimiwa Afisa Elimu wa Mkoa wa Dodoma,*

*Waheshimiwa Maafisa Elimu wa Wilaya zote za Mkoa wa Dodoma,*
*Ndugu viongozi wote mliopo hapa,*

*Ndugu wageni waalikwa,*



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 214 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



*Mabibi na mabwana,*

*Itifaki imezingatiwa.*

(ii) Kumkaribisha mgeni rasmi sambamba na shukurani kwa kuja kwake. Katika sehemu hii ya utangulizi mgeni rasmi hukaribishwa kwa maneno maalumu ya ukarimu sambamba na kumshukuru kwa kukubali kuhudhuria na kuwa mgeni rasmi. Tazama mfano ufuatao:

*Ndugu mgeni rasmi, kwa moyo wa unyenyekevu tunakukaribisha katika sherehe hii. Awali ya yote, tunakushukuru kwa kukubali kuwa mgeni rasmi na kuhudhuria siku ya leo. Pili, tunapenda kuwakaribisha wageni wote katika sherehe hii ya mahafali. Karibuni sana.*

(c) Kiini cha risala

Kiini cha risala ni sehemu ambapo malengo, mafanikio, changamoto au mapendekezo huandikwa kulingana na aina ya kundi la wahusika. Hoja hupangwa kwa mtiririko wenye kuleta mantiki kwa kuzingatia vipengele hivyo.

(d) Hitimisho la risala

Katika kipengele hiki shukurani hutolewa kwa mgeni rasmi kwa kusikiliza risala. Vilevile, mgeni rasmi huombwa kufanyia kazi changamoto zilizobainishwa katika risala. Msomaji wa risala huaga hadhira yake kwa kutumia maneno maalumu kulingana na dhima ya risala kama vile:

*Udumu muungano!*

*Asante kwa kunisikiliza!*

*Tanzania yenye amani inawezekana.*

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 215 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Ufuatao ni mfano wa risala:

RISALA YA KIKUNDI CHA WAKULIMA WA MBOGAMBOGA MKOANI IRINGA KWA MGENI RASMI, WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI KATIKA SIKU YA UFUNGUZI WA MAONESHO YA NANENANE 2018.

Ndugu mgeni rasmi, Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi,
Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa,
Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya,
Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa Vijijini,
Ndugu viongozi mbalimbali,
Mabibi na mabwana,
Karibuni sana.

Ndugu mgeni rasmi, Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, awali ya yote tunayo furaha kubwa sana kukukaribisha katika hafla hii fupi ya ufunguzi wa maonesho ya Nanenane 2018 hapa Iringa. Tunakushukuru sana kwa kuitikia wito wetu na kushirikiana nasi. Aidha, tunapenda kuwakaribisha viongozi wote, wageni waalikwa na watu wote katika hafla hii fupi ya ufunguzi wa maonesho haya.

Ndugu mgeni rasmi, kikundi hiki cha Wakulima wa Mbogamboga-Iringa kilianzishwa rasmi mwaka 2000. Kikundi hiki kilianza na wakulima wa mbogamboga 50 walioko katika maeneo ya Ilula kikiwa na malengo yafuatayo:

(i) Kukuza kilimo cha mbogamboga na kuongeza uzalishaji wa mbogamboga nchini;
(ii) Kuongeza tija kwa wakulima wa mbogamboga katika mkoa wa Iringa ili waweze kuyamudu maisha na kukuza maendeleo ya mkulima mmoja mmoja, mkoa na taifa kwa ujumla;
(iii) Kuunganisha juhudi za kutafuta soko zuri la mbogamboga;
(iv) Kurahisisha utoaji wa elimu ya kilimo kwa ujumla, hususani kuhusiana na kilimo cha mbogamboga;
(v) Kurahisisha usambazaji wa pembejeo za kilimo; na
(vi) Kurahisisha utoaji wa elimu ya utunzaji wa vyanzo vya maji na umwagiliaji.

Ndugu mgeni rasmi, mpaka kufikia mwaka 2018 kikundi hiki kimepata mafanikio yafuatayo:

(i) Kuongeza wanachama wengine wapya 1000 na kufikia jumla ya wanachama 1050 katika wilaya zote za Mkoa wa Iringa;


PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 216 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



(ii) Kuongeza uzalishaji wa mbogamboga kwa asilimia 80;

(iii) Kutafuta masoko nje ya mkoa wa Iringa;

(iv) Kutoa mafunzo ya kilimo cha mbogamboga na umwagiliaji;

(v) Kurahisisha usambazaji wa pembejeo za kilimo kiasi kwamba kila mkulima anapata fursa sawa na wengine katika mgao wa pembejeo zilizopo; na

(vi) Kutoa elimu ya utunzaji wa vyanzo vya maji.

Ndugu mgeni rasmi, pamoja na mafanikio hayo kikundi hiki kinakabiliwa na changamoto zifuatazo:

(i) Uhaba wa pembejeo na vifaa vya kilimo.

(ii) Kukosekana kwa soko la uhakika la mbogamboga ambako kunatokana na mwamko mdogo wa Watanzania wa kula mbogamboga.

Ndugu mgeni rasmi, kwa kuhitimisha tunapenda kusema kuwa tuna imani kwako na kwa wizara unayoiongoza, kuwa utatusaidia katika kukabiliana na changamoto tulizozieleza zinazokikabili kikundi chetu na wakulima kwa ujumla. Pembejeo na soko la uhakika ni kilio, si tu kwa Kikundi cha Wakulima wa Mbogamboga – Iringa, bali kwa wakulima wengi nchini Tanzania.

Ndugu mgeni rasmi, tunakushukuru kwa utulivu na umakini wako katika kusikiliza risala yetu na tunakutakia afya njema na utekelezaji mwema wa majukumu yako. Kilimo oyeeee!

## Zoezi la 6.7

1. Eleza mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa uandishi wa risala.
2. Kwa niaba ya wahitimu wenzako, andika risala itakayosomwa mbele ya mgeni rasmi Mh. Mkuu wa Mkoa katika mahafali ya kidato cha sita.

**Uandishi wa hotuba**

Hotuba ni mazungumzo yaliyoandaliwa ili kutolewa mbele ya watu kwa malengo maalumu. Hotuba huweza kuandaliwa kwa muda mfupi au mrefu kabla ya kutolewa. Hotuba hutolewa mbele za watu kwa malengo mbalimbali kama vile kuhamasisha, kutoa maelekezo maalumu, kutoa pongezi, kutoa shukurani, pamoja na malengo mengine. Hotuba hutolewa na mtu mmoja mbele za watu, mathalani, anaweza kuwa kiongozi, au mwakilishi wa jumuiya fulani. Hotuba



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
For Online Use Only

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

huweza kuwa na wahutubiaji zaidi ya mmoja katika tukio moja. Aidha, kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia hotuba huweza pia kutolewa kupitia vyombo vya habari.

**Sifa za hotuba**

Ili hotuba iwe na ubora inatakiwa izingatie vigezo vitano kama ifuatavyo:

(a) Ukweli wa habari na taarifa

Mhutubiaji anapaswa kujiridhisha na usahihi au ukweli wa habari anazozizungumzia mbele za watu. Kama hotuba itahusisha takwimu, ni vyema takwimu hizo zikawa sahihi na kukumbuka matukio na miaka au muda sahihi. Hotuba isipokuwa na taarifa zenye ukweli huweza kupotosha umma na mhutubiaji huweza kudharauliwa na kubezwa.

(b) Matumizi ya lugha fasaha na sanifu yanayozingatia hadhira na muktadha.

Ni vyema mwaandaaji wa hotuba akazingatia uteuzi wa msamiati kulingana na watu wanaohutubiwa.

(c) Mpangilio mzuri wa mawazo wenye kuleta mantiki.

Hotuba nzuri ni ile ambayo maelezo yake yamepangiliwa vizuri kwa mfuatano wenye kujenga mantiki. Hii husaidia hotuba kueleweka kwa urahisi na kutowachosha wasikilizaji.

**Sifa za msomaji wa hotuba**

(a) Awe na nidhamu anapozungumza mbele za watu.
Msomaji wa hotuba anapaswa kufuata nidhamu, maadili na taratibu zinazozingatiwa katika tukio husika. Hii ni pamoja na kuwa na mwonekano nadhifu kwani mwonekano wa mtu huweza kuathiri uwasilishaji wa hotuba.

(b) Awe na sauti inayosikika vyema.
Mhutubiaji anapaswa kuwa na sauti inayosikika na awe na matumizi mazuri ya ishara za mwili. Ni vyema matumizi ya ishara kama mikono na mwonekano wa sura viendane na maudhui ya hotuba, ili hotuba iweze kueleweka na kuvutia.

**Aina za hotuba**

Hotuba huainishwa kwa kuzingatia maudhui yaliyomo katika hotuba inayohusika. Kutokana na maudhui tunaweza kupata aina tano za hotuba; hotuba za kiserikali, hotuba za kisiasa, hotuba za mahubiri au mawaidha, mihadhara ya masomo na hotuba za mambo ya kijamii.

For Online Use Only


PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



(a) Hotuba za kiserikali

Hotuba za kiserikali ni aina za hotuba ambazo hutolewa na viongozi wa kiserikali kama vile, Rais, Makamu wa Rais, Mawaziri, Viongozi wa Wizara, Mikoa, Wilaya, Tarafa, Kata, Mitaa na Vitongoji. Katika hotuba hizi ufafanuzi, maelekezo au mipango na taarifa za utendaji wa serikali hutolewa. Taarifa hizo ni kama vile, bajeti za wizara, ripoti za tume maalumu, maelekezo na hatua za utekelezaji.

(b) Hotuba za kisiasa

Hotuba za kisiasa ni aina ya hotuba ambazo hutolewa kwenye majukwaa ya kisiasa, hususani, katika vikao, na mikutano ya vyama vya siasa. Hotuba hizi hulenga kushawishi watu kuendelea kujenga imani na kueleza sera, mipango, na mikakati ya vyama. Aghalabu, hotuba hizi hutolewa wakati wa kampeni za chaguzi.

(c) Hotuba za mahubiri au mawaidha

Hotuba za mahubiri au mawaidha ni aina za hotuba zenye mafundisho ya kidini ambazo hutolewa makanisani, misikitini au maeneo ya ibada. Katika hotuba hizi, viongozi wa kidini hutoa mafundisho mbalimbali na maelekezo ya kiimani.

(d) Hotuba za mihadhara ya kimasomo

Hotuba za mihadhara ya kimasomo ni hotuba au mafundisho maalumu ambayo hutolewa darasani au mahali popote katika mazingira ya kitaaluma. Hotuba za namna hii hutolewa hasa na wahadhiri, wakufunzi au walimu wanapofundisha kundi kubwa la wanafunzi.

(e) Hotuba za shughuli za kijamii

Hizi ni aina za hotuba ambazo hutolewa katika mikusanyiko ya kijamii kama misiba na sherehe mbalimbali. Hotuba hizi hulenga kufariji, kuusia, kupongeza, au kushukuru.

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 219 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Muundo wa hotuba**

Hotuba huundwa kwa vipengele vinne vifuatavyo:

(a) Kichwa cha hotuba

Kichwa cha hotuba hujumuisha mambo matano. Mambo hayo ni mwandishi wa hotuba au mhutubiaji, hadhira, tukio, mahali, na tarehe. Kichwa cha hotuba lazima kiandikwe kwa herufi kubwa. Ikumbukwe kuwa kichwa cha hotuba huweza kutumiwa kama jina la hotuba au rejea pale inaporejelewa katika kumbukumbu au vyombo vya habari. Ufuatao ni mfano wa kichwa cha hotuba:

HOTUBA YA MKUU WA SHULE KATIKA UZINDUZI WA CHAMA CHA KISWAHILI CHA WANAFUNZI WA SHULE YA SEKONDARI MILAMBO TAREHE 11/1/2018

(b) Utangulizi wa hotuba

Utangulizi wa hotuba huwa na salamu, kuwatambua wageni, pamoja na shukurani. Salamu katika hotuba hujulikana pia kama miito ya hamasa ambapo mhutubiaji huanza na kauli za hamasa kulingana na muktadha au lengo la hotuba. Kauli hizi hulenga kuvuta hisia au kuandaa usikivu kwa hadhira ili ikae tayari kupokea hotuba. Mfano wa kauli hizo ni:

*Elimu juu!*

*Kiswahili juu!*

Kipengele kingine cha utangulizi wa hotuba ni kuwatambua viongozi pamoja na wageni wote waalikwa kulingana na vyeo vyao. Kwa mfano:

*Makamu Mkuu wa Shule,*

*Mwalimu wa Taaluma,*

*Ndugu Walimu,*

*Viongozi wa Serikali ya Wanafunzi,*

*Wanafunzi wote.*

Baada ya kutambua wageni, mgeni rasmi hutoa salamu zake kwa wageni na wenyeji sambamba na kutoa shukurani zake za dhati kwa kupewa nafasi ya kuwa mgeni rasmi.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 220 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



(c) Kiini cha hotuba

Kiini cha hotuba hubeba maudhui na ujumbe wa hotuba. Kipengele hiki hutofautisha hotuba moja na nyingine. Hoja za msingi za hotuba hutolewa kwa mpangilio wa aya zenye kuzingatia mantiki.

(d) Hitimisho la hotuba

Katika hatua hii, mhutubiaji hutoa maneno ya kuhitimisha hotuba yake. Mhutubiaji huweza kutoa shukurani kwa mara nyingine, kwa kualikwa na kusikilizwa pamoja na kutoa nasaha, au maagizo kulingana na muktadha wa hotuba. Kwa kawaida, mhutubiaji humalizia kwa neno la hamasa, au shukurani kama vile:

*Asanteni sana!*

Ufuatao ni mfano wa hotuba:

HOTUBA YA MGENI RASMI KATIKA MAHAFALI YA KUHITIMU KIDATO CHA SITA KATIKA SHULE YA SEKONDARI RUVU TAREHE 10 MEI, 2018

Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Pwani,
Mwenyekiti wa Bodi ya Shule,
Mkuu wa Shule ya Sekondari Ruvu,
Wajumbe wa Bodi ya Shule,
Walimu wa Sekondari Ruvu,
Wazazi na walezi wa wanafunzi,
Wahitimu wa kidato cha sita,
Wanafunzi wote,
Mabibi na mabwana,
Habari za mchana!

Ndugu Mkuu wa Shule, kwanza ninapenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa uongozi wa shule kwa kunialika kujumuika nanyi katika mahafali haya kama mgeni rasmi. Aidha, ninatumia nafasi hii kukupongeza wewe na walimu wote wa shule ya sekondari Ruvu kwa kuwaandaa wanafunzi hawa wanaohitimu leo. Mmefanya kazi kubwa, na hivyo, mnastahili pongezi nyingi.

Ndugu Mkuu wa Shule, nawapongeza pia wajumbe wa Bodi ya Shule ambao wameshirikiana na wazazi, na walezi katika kuisimamia shule hii na kufanikiwa



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 221 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kujenga maabara kubwa na ya kisasa. Napenda kukuhakikishia kuwa serikali inawaunga mkono na ninawataarifu kuwa tayari tumetenga fedha za kutosha kununua vifaa vya maabara hii.

Ndugu Mkuu wa Shule, naomba sasa nitoe nasaha kwa wahitimu wetu. Vijana mnaohitimu leo, ninapenda mfahamu kwamba mnategemewa sana na serikali kuwa chachu ya maendeleo ya taifa letu katika nyanja mbalimbali. Kwa hiyo, kila mmoja wenu ajiandae kutumia maarifa aliyoyapata kwa manufaa ya taifa letu. Tumieni nguvu na uwezo wenu wote wa kitaaluma mlioupata kwa miaka hii kulijenga taifa lenu hili, lenye amani na utulivu. Muuvae uzalendo kamili wa taifa letu, ambalo lina rasilimali za kutosha ambazo mkizilinda na kuzisimamia vizuri zina uwezo wa kuwaletea mafanikio makubwa, ninyi binafsi na taifa letu kwa ujumla.
Aidha, ninapenda kuwakumbusha kujiepusha na vitendo ambavyo vinaweza kuzima ndoto zenu za maisha ya baadaye. Ninafahamu kuwa walimu wamewafundisha mambo mengi kama vile kujiepusha na vikundi vya watu wanaotumia dawa za kulevya, ujambazi, na kadhalika. Vilevile, ninapenda kuwakumbusha kujiepusha na vitendo vinavyochochea maambukizi ya virusi vya UKIMWI. Hili ni jukumu la kila mmoja kujilinda na kujiepusha na vitendo vinavyoweza kumtumbukiza katika hatari ya kuambukizwa VVU na kujikuta anafupisha maisha yake. Kwa hiyo, ninawasihi mzingatie hayo yote ili ninyi wenyewe, familia zenu, na taifa kwa ujumla linufaike na elimu mliyoipata.

Ndugu mkuu wa shule, nimalizie kwa kuwaomba wanafunzi wanaobaki hapa shuleni kuendelea kuwa na nidhamu, na kutia bidii katika masomo. Vilevile, ninazidi kuwaomba walimu, wazazi, na walezi muendelee kushirikiana katika kuwalea na kuwasaidia vijana hawa ili wapate elimu bora kwa mustakabali wa maisha yao na taifa letu.

Nawatakieni mafanikio mema katika kujenga nchi yetu nzuri ya Tanzania.

Asanteni kwa kunisikiliza.

For Online Use Only


PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



## Zoezi la 6.8

1. Eleza mambo ya kuzingatia wakati wa kuandika hotuba.
2. Fafanua kwa kutumia mifano muundo wa hotuba.
3. Umealikwa kuwa Mgeni Rasmi katika uzinduzi wa harakati za kupambana na maambukizi mapya ya VVU. Andika hotuba utakayoisoma.

**Uandishi wa matangazo**

Tangazo ni taarifa au habari fupi inayoandikwa kwa lengo la kufikisha ujumbe au jambo fulani lililotokea au litakalotokea. Tangazo huhitaji umakini na ustadi mkubwa katika kuliandika ili taarifa muhimu na za msingi ziweze kuwafikia walengwa kwa usahihi. Tangazo huweza kubeba ujumbe wa kisiasa, kibiashara, kielimu, na kijamii.

**Malengo ya matangazo**

Matangazo huwa na malengo mbalimbali kama ifuatavyo:

(i) Kutoa taarifa kuhusu matukio, au huduma mbalimbali kama vile upimaji wa afya na tiba, biashara, mkutano, kikao, mafunzo, mnada, mahafali, msiba, ugonjwa, ajali, uhamisho, na mashindano.

(ii) Kutoa tahadhari kuhusu mambo ambayo yanatarajiwa kutokea kama vile upepo mkali, mvua kali au joto kali, tetemeko la ardhi, magonjwa ya mlipuko, kukatika kwa umeme, au maji. Tahadhari husaidia watu kuepuka hatari au madhara yoyote yanayoweza kutokea endapo watu hawatachukua tahadhari. Mara nyingi, taarifa hizi hutolewa na mamlaka inayohusika.

(iii) Kutoa onyo kuhusu mambo ambayo ni kinyume cha utaratibu wa jamii. Mambo hayo ni kama vile kukwepa kulipa kodi, kuchakachua mafuta, kufanya biashara haramu au katika maeneo ambayo hayaruhusiwi, kutupa taka mahali pasipohusika, kuharibu vyanzo vya maji, na kukata miti ovyo. Maonyo yanayotolewa hujumuisha na hatua zitakazochukuliwa endapo maonyo yaliyotolewa yatakiukwa.

**Sifa za matangazo**

Ili tangazo liwe bora ni lazima lijumuishe mambo yafuatayo:

(a) Kichwa cha Tangazo.
Kichwa cha tangazo lazima kieleze kuwa tangazo linahusu nini. Mwandishi wa tangazo anaweza kutumia lengo kuu la tangazo kama kichwa cha



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 223 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

tangazo. Kichwa cha tangazo kinatakiwa kiandikwe kwa herufi kubwa au kwa maneno makubwa. Mifano ya vichwa vya matangazo ni kama vile; MNADA, TANZIA, na KATIZO LA UMEME.

(b) Cheo au/na jina la mtoa tangazo
Lengo la kuweka jina ni kuwapa watu nafasi ya kujua watapata wapi taarifa za ziada au kutoa mwitikio au kuwajibika kuhusu tangazo. Kwa mfano, kama tangazo linahusu mnada, watamfahamu anayetangaza mnada huo. Anaweza kuwa mtu binafsi, shirika, au taasisi ya umma au serikali.

(c) Lugha nyepesi na yenye kueleweka kwa urahisi
Lengo la tangazo ni kufikisha ujumbe muhimu kwa jamii husika. Kwa hiyo, matumizi ya lugha inayoeleweka kwa urahisi hufanya ujumbe uifikie jamii bila kuwa na utata au ugumu.

(d) Matumizi ya michoro na picha zenye mvuto kwa walengwa
Tangazo bora huwa na picha na michoro yenye rangi za kuvutia. Hii huwasaidia walengwa kuvutiwa nayo na kupata ujumbe kwa urahisi. Ni muhimu kuchagua picha nzuri kwa sababu si kila picha inafaa kuwekwa.

(e) Kueleza jambo kwa ufupi
Ujumbe wa tangazo unapaswa kutolewa kwa ufupi bila kupoteza taarifa muhimu. Hii husaidia walengwa kulisoma, kulielewa, na kuweka kumbukumbu. Hivyo basi, tangazo linapaswa kubeba taarifa moja ili kuondoa mkanganyiko kwa walengwa.

(f) Walengwa wa tangazo wabainishwe wazi.
Hii husaidia walengwa kuwa makini pamoja na kupata ujumbe kwa urahisi.

(g) Ubunifu katika uwasilishaji
Tangazo lazima liwe na lugha ya mvuto na mwonekano wa kuvutia. Litumie michoro au picha zinazoendana na maudhui yake. Hata kama ni tangazo la msiba liwe na lugha au mwonekano wenye kutoa faraja kwa wafiwa.

**Muundo wa matangazo**

Matangazo huwa na miundo mbalimbali kulingana na ubunifu na mahitaji ya tangazo. Pamoja na miundo hiyo kuwa mingi, upo muundo wa msingi ambao lazima uzingatiwe hata kama tangazo litakuwa na ubunifu kwa kiwango cha juu.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 224 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Muundo huo hujumuisha sehemu zifuatazo:

(a) Jina la mtoa tangazo

Jina la mtoa tangazo huweza kuwa la mtu binafsi, shirika la umma, taasisi binafsi, au serikali. Mwandishi wa tangazo anaweza kutumia hata nembo maalumu yenye utambulisho. Ifuatayo ni mifano ya jina au majina ya mtoa tangazo:

- SHIRIKA LA UMEME TANZANIA –TANESCO
- NDUGU JAMAAL KARATA
- HALMASHAURI YA WILAYA YA LIWALE
- CHUO KIKUU CHA DODOMA
- BODI YA UTALII TANZANIA

(b) Kichwa cha tangazo

Huandikwa kwa kifupi kama inavyoonekana katika mifano ifuatayo:

- MNADA! MNADA!
- KUPOTELEWA NA CHETI
- TANZIA
- BIDHAA MPYA
- MALI MPYA WAHI

(c) Lengo la tangazo. Taarifa zote za msingi kuhusu tangazo huelezwa kwa ufupi. Taarifa hizi hutokana na kile kinachotangazwa. Kwa mfano, tangazo kuhusu huduma ya afya hujumuisha walengwa, mahali, tarehe, muda, na gharama. Tazama mfano ufuatao:

**TAASISI YA MOYO YA JAKAYA KIKWETE, INAWATANGAZIA WANANCHI WOTE WA MKOA WA DAR ES SALAAM NA MIKOA YA JIRANI KWAMBA KUTAKUWA NA ZOEZI LA UPIMAJI WA AFYA YA MOYO KWA WATOTO WENYE UMRI CHINI YA MIAKA MITANO.**

**MAHALI: TAASISI YA MOYO YA JAKAYA KIKWETE (MUHIMBILI)**
**TAREHE: 02-10/10/2018**
**MUDA: SAA 2:00 - 8:00 MCHANA**
**GHARAMA: BURE.**



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 225 25/09/2019 13:57

For Online Use Only

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(d) Cheo au wadhifa

Katika matangazo ya taasisi au kampuni fulani, cheo cha mtoa tangazo huandikwa kwenye tangazo, ili kumtambulisha aliyetoa tangazo na kurahisisha mawasiliano endapo yatahitajika. Tazama mifano ifuatayo:

- Mwenyekiti wa Kijiji
- Mkurugenzi wa Halmashauri
- Afisa Uhusiano wa Taasisi

**Ifuatayo ni mifano ya matangazo:**

**TANGAZO**
**NAFASI ZA MASOMO**
**CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM**

*Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam anapenda kuutangazia umma nafasi za masomo kwa mwaka wa masomo 2017/2018 katika programu mbalimbali kwa Shahada za Awali, Umahiri na Uzamivu. Wenye sifa wanashauriwa kufanya maombi kwenye mtandao kupitia tovuti ya chuo; www.udsm.ac.tz na waambatishe nakalatepe za vyeti vyao vya taaluma.*

*Mwisho wa kupokea maombi hayo ni tarehe **31/07/2017**. Kwa maelezo zaidi tembelea tovuti ya chuo; www.udsm.ac.tz.*

***Tangazo hili limetolewa na:***
*Kitengo cha Mawasiliano kwa Umma*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

**TANGAZO**





**MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA**

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) inawatangazia wakazi wa mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Lindi, Mtwara pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba kuwa kutakuwa na mvua kubwa zitakazoambatana na upepo mkali. Mvua hizo zinatarajiwa kunyesha kwa siku tatu mfululizo kati ya tarehe 12 - 14/9/2016. Hivyo wakazi wote waishio maeneo ya mabondeni wanashauriwa kuchukua tahadhari.

Utabiri huu umetolewa leo tarehe 6/9/2016

Mkurugenzi Mkuu
Mamlaka ya hali ya Hewa

**TANGAZO**

**NI MARUFUKU KUTUPA TAKA KATIKA ENEO HILI. HATUA KALI ZA KISHERIA ZITACHUKULIWA KWA ATAKAYEKAIDI.**

**UTAWALA**

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 227 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**DUKA LA VITABU - TAASISI YA ELIMU TANZANIA**

Uongozi wa Taasisi ya Elimu Tanzania Unawatangazia wanafunzi na umma kwa ujumla kuwa vile vitabu vya Kiswahili Sarufi na Fasihi vinapatikana dukani kwetu kwa bei nafuu.

Ili kujipatia kitabu chako fika katika duka Letu lililoko jirani na kituo cha mabasi cha Bamaga – Mwenge, Dar es Salaam.

Karibuni sana.

**Uongozi**
**Taasisi ya Elimu Tanzania**




## Zoezi la 6.9

1. Bainisha mambo ya msingi ya kuzingatia wakati wa uandishi wa tangazo.
2. Eleza sifa za msingi za tangazo.
3. Ukiwa Mkuu wa Shule ya Sekondari Janda, andika tangazo la nafasi ya kazi kwa mwalimu wa somo la Kiswahili Kidato cha Tano.
4. Eleza tofauti kati ya tangazo la biashara na tangazo la kazi.

### Wasifukazi

Haya ni maelezo yanayotoa taarifa za mtu binafsi zinazojumuisha mahali anapoishi, tarehe ya kuzaliwa, usuli wa elimu, uzoefu wa kazi, raghba, ujuzi, wadhamini na mawasiliano yake ambayo huambatanishwa na barua ya kuomba ajira au kujitambulisha mahali fulani. Wasifukazi hutumika kwa malengo maalumu kama vile kuomba ajira, au nafasi ya masomo.

### Muundo wa wasifukazi

Muundo wa wasifukazi huwa na vipengele vifuatavyo:

(a) Taarifa binafsi

Sehemu hii hujumuisha taarifa muhimu za awali zinazomtambulisha mhusika. Katika sehemu hii, wasifukazi hudokeza sifa bainifu za mtu

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 228 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


ambazo ni jina au majina, anwani, tarehe ya kuzaliwa, jinsia, uraia, lugha, na hali ya ndoa.

Ufuatao ni mfano wa taarifa binafsi:

| | |
|---|---|
| Jina la Ukoo: | Malimji |
| Majina mengine: | Midosi Gado |
| Tarehe ya kuzaliwa: | 23.05.1983 |
| Jinsi: | Me |
| Makazi: | Chakechake |
| Uraia: | Mtanzania |
| Hali ya ndoa: | Sijaoa |
| Anwani: | S.L.P. 16, Kusini Unguja. |
| Simu: | 0116 – 000 000 |
| Baruapepe: | kjkmimi.yeye@gmail.com |
| Lugha: | Kiswahili na Kiingereza |

(b) Usuli wa elimu

Katika sehemu hii, mwandishi huandika au kuorodhesha taasisi za elimu alizopitia pamoja na kiwango cha elimu ambacho alihitimu katika taasisi inayohusika. Taarifa hizi hujumuisha mwaka, kiwango cha elimu, programu, na aina ya cheti ambacho mhusika alipata baada ya kuhitimu. Usuli wa elimu huandikwa kwa kuanzia kiwango cha elimu kilichofikiwa hivi karibuni. Tazama mfano ufuatao:

| Mwaka | Kiwango cha Elimu | Taasisi | Tuzo |
|---|---|---|---|
| 2017- hadi sasa | Shahada ya awali katika kilimo | Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine | - |
| 2014 – 2016 | Kidato cha 5 – 6 | Shule ya Sekondari Kishoju | Cheti cha kuhitimu kidato cha sita |

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 229 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

| | | | |
|---|---|---|---|
| 2010 – 2013 | Kidato cha 1 – 4 | Shule ya Sekondari Munanila | Cheti cha kuhitimu kidato cha nne |
| 2003 – 2009 | Darasa la 1 – 7 | Shule ya Msingi Nzega A | Cheti cha kuhitimu darasa la saba |

(c) Uzoefu wa kazi

Katika sehemu hii mwandishi huandika uzoefu wa kazi alionao. Uzoefu ni lazima uendane na kazi inayoombwa. Kwa mfano, kama mwombaji wa kazi anaomba kazi ya kusimamia mradi kama meneja inabidi aeleze uzoefu alionao katika kazi hiyo ikiwa ni pamoja na muda alioutumia kuupata na mahali alipopatia uzoefu huo. Tazama mfano ufuatao:

| Mwaka | Shule | Wadhifa | Mahali |
|---|---|---|---|
| Januari 2011 – Juni 2012 | Shule ya Sekondari Dodoma | Mwalimu wa somo la Historia na Kiingereza | Dodoma |
| Julai 2002 - Novemba 2006 | Shule ya Sekondari Kantalamba | Mkuu wa Idara ya Historia na Mwalimu wa somo la Historia na Kiingereza | Sumbawanga |

(d) Majina ya wadhamini

Majina kamili na anwani za wadhamini huandikwa katika sehemu hii. Wadhamini ni lazima wawe watu wanaomfahamu vizuri mhusika. Hii huwasaidia kutoa taarifa sahihi kuhusu mhusika. Taarifa hizi humsaidia mwajiri wakati wa kufanya tathmini ya watu atakaowaajiri. Aidha, wadhamini wanatakiwa kuwa watu wanaoaminika. Wadhamini wanaweza kuwa walimu wa mhusika, wakuu wa idara au vitengo katika kituo chake cha kazi, viongozi wa dini au serikali, hasa serikali za mitaa. Wadhamini hawapaswi kuwa ndugu au wanafamilia kwa sababu wanaweza kuwa na upendeleo na hivyo kutoa taarifa ambazo si za ukweli kuhusu mhusika. Chunguza mifano ifuatayo:



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 230 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Bw. Ndola Kidura,
Mkuu wa Shule ya Sekondari Munanila,
S.L.P. 210,
Kigoma.
Simu: 0702 000000
Baruapepe: p.k.22.apemba@yahoo.com

Bi. Katani Mkonge,
Ofisa Utumishi (Wilaya),
Wilaya ya Bahi,
S.L.P. 35110,
Dodoma.
Simu: 0748 000000
Baruapepe: ninalimamkonge@gmail.com

Mfano wa wasifukazi

**WASIFUKAZI**

**1.0 Taarifa Binafsi**

| | |
|---|---|
| Jina la ukoo: | Mendi |
| Majina mengine: | Choto Wajua |
| Tarehe ya kuzaliwa: | 01/04/1990 |
| Uraia: | Mtanzania |
| Jinsi: | Ke |
| Hali ya ndoa: | Sijaolewa |
| Lugha: | Kinyakyusa, Kiswahili na Kiingereza |
| Anwani: | S.L.P. 10000, Tarime. |
| Simu: | 0475077722 |
| Baruapepe: | cmkyusa.kweli@gmail.com |



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 231 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## 2.0 Usuli wa elimu

| Mwaka | Kiwango cha Elimu | Shule | Tuzo |
|---|---|---|---|
| 2013 – 2015 | Elimu ya Juu ya Sekondari | Shule ya Sekondari Mtua | Cheti cha kuhitimu kidato cha sita |
| 2009 – 2012 | Elimu ya Sekondari | Shule ya Sekondari Matumaini | Cheti cha kuhitimu kidato cha nne |
| 2002 – 2008 | Elimu ya Msingi | Shule ya Msingi Mayego | Cheti cha kuhitimu darasa la saba |

## 3.0 Uzoefu wa kazi

| Mwaka | Kazi/Shughuli | Wadhifa | Mahali |
|---|---|---|---|
| 2016 – 2017 | Kuuza vitenge katika duka la KTM | Meneja msaidizi | Kitumbini |
| 2015 – 2016 | Kuuza kanga za Urafiki | Muuzaji wa Kawaida | Kitumbini |

## 4.0 Wadhamini

1. Bw. Karibu Mchapakazi
   Mwenyekiti wa Umoja wa Wauza Vitenge,
   S.L.P. 21211,
   **Tarime.**
   Simu: 010822110
   Baruapepe: taifa.leoasubuhi@yahoo.com

2. Bi. Mwangaza Mwelekeo,
   Katibu wa Umoja wa Wauza Vitenge,
   S.L.P. 333333,
   **Tarime.**
   Simu: 0705303090
   Baruapepe: vitenge.badovipo@hotmail.com



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 232 25/09/2019 13:57

For Online Use Only

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



## Zoezi la 6.10

1. Nini matumizi ya wasifukazi?
2. Fafanua mambo ya msingi ya kuzingatia katika uandishi wa wasifukazi.

## Tamrini

1. Eleza maana ya risala na mambo ya msingi ya kuzingatia katika kuandika risala.
2. Andika risala utakayoisoma siku ya mazingira duniani ukiwakilisha wanafunzi wa Tanzania.
3. Ni mambo gani ya msingi yanayotakiwa kuzingatiwa katika uandishi wa tangazo la biashara?
4. Meneja wa Kiwanda cha Vyandarua Arusha ametangaza nafasi za kazi katika kiwanda hicho. Ukiwa mhitimu wa Kidato cha VI, andika wasifukazi utakaoambatanishwa na barua ya kuomba kazi.
5. Bainisha faida za kuandika wadhamini kwenye wasifukazi.
6. Wewe ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Same na Halmashauri yako inataka kuuza magari na vifaa vya ofisi. Andaa tangazo la mnada.
7. Umechaguliwa kuwa mwanafunzi bora shuleni kwako na umetakiwa kutoa hotuba kwa wanafunzi wenzako baada ya kupokea zawadi. Andika hotuba hiyo.

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 233 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Saba: Ufahamu na ufupisho

## Utangulizi

Sura hii inahusu ufahamu na ufupisho. Kwa hiyo, utajifunza aina za ufahamu na ufupisho. Lengo kuu la kujifunza mada hii ni kukuwezesha kupata ujuzi na maarifa ya kuweza kusoma, au kusikiliza kwa ufahamu na kujibu maswali yanayotokana na habari uliyoisikiliza au kuisoma. Pia, utapata maarifa ya kufupisha habari mbalimbali.

**Dhana ya ufahamu**

Ufahamu ni neno linalotokana na kitenzi *fahamu*. Kufahamu ni kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu jambo fulani. Kwa hiyo, ufahamu ni uwezo wa kutambua na kuelewa mambo kutokana na kusikiliza, kusoma, na kufikiri kwa makini. Hii ina maana kwamba uwezo huo hutokana na usikilizaji, usomaji, utazamaji wa makini, na kutafakari mambo uliyoyasikia, uliyoyaona na kuyasoma. Ufahamu humwezesha mtu kufafanua, au kutoa taarifa kuhusiana na jambo au habari aliyoisikiliza, kuisoma, au kuiona. Kuna ufahamu wa aina tatu kama inavyofafanuliwa katika sehemu zinazofuata:

***1. Ufahamu wa kusikiliza***

Ni uwezo wa kutambua na kuelewa mambo kutokana na kusikiliza. Msikilizaji hupata habari kwa kusimuliwa, au kusomewa na mtu au kusikiliza kupitia kifaa kilichorekodiwa ili kujua jambo linalosisitizwa.

Kwa msingi huo, mzungumzaji anatakiwa kutamka maneno kwa ufasaha. Maneno yanatakiwa kuwa katika mpangilio wa kueleweka ili msikilizaji aelewe na kutoa mwitiko. Kwa mfano, mzazi anaweza kumtuma mtoto kusikiliza taarifa ya habari. Mtoto huyu atalazimika kuwa mtulivu na kusikiliza kwa makini kile anachokisema mtangazaji na baadaye atawajibika kueleza mambo muhimu aliyoyasikia. Kwa hiyo, msikilizaji anapaswa kuwa na utayari wa kusikiliza, usikivu, umakini, ufasiri, na uchanganuzi wa mambo anayoyasikia.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 234 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


**Mambo ya kuzingatia katika ufahamu wa kusikiliza**

(i) Kumtazama usoni yule anayesimulia (iwapo anaonekana).

(ii) Kuwa makini na mtulivu wakati wa kusikiliza masimulizi.

(iii) Kubainisha mawazo makuu kwa mtiririko mzuri.

(iv) Kuhusisha mazingira halisi na habari inayosimuliwa.

(v) Kuwa makini na matumizi ya lugha ya msimuliaji.

***2U fahamu wa kusoma***

Ufahamu wa kusoma ni uwezo wa kutambua na kuelewa jambo kutokana na kusoma maandishi. Mtu anaposoma habari anatakiwa kuyatafakari na kuyafafanua yale aliyoyasoma. Kuna namna mbalimbali za kusoma ambazo ni kusoma kwa sauti na kusoma kimya.

Kusoma kwa sauti hutokea pale msomaji anaposoma kwa kusikika. Usomaji huu humfanya msomaji ajisikilize na kujipima uwezo wake wa kutamka maneno kwa usahihi na kupima kasi na uwezo wa kuelewa yale anayoyasoma. Aidha, kusoma kwa sauti humfanya msomaji kuweka mawazo yake yote kwa kila anachokisoma.

Kusoma kimya ni kitendo cha msomaji kusoma habari bila kutoa sauti au bila kusikika. Usomaji wa namna hii, aghalabu, hutumiwa na mtu anapojisomea. Usomaji wa kimya humsaidia msomaji wa habari, hususani habari ndefu, kusoma kwa muda mfupi. Msomaji analazimika kuzingatia alama za kiuakifishaji. Kwa upande mwingine, usomaji huu siyo usomaji wenye ufanisi kwa sababu wakati mwingine msomaji huweza kuhamisha mawazo kutoka kwenye kile anachosoma.

Hivyo basi usomaji wa sauti na usomaji wa kimya unahitaji umakini mkubwa, ambapo msomaji huvuta fikira zake zote kwa kile anachokisoma. Katika usomaji huu, msomaji huzingatia maana ya kila neno, sentensi, na aya kwa makini. Lengo la usomaji huu ni kupata uelewa wa kina. Usomaji huu huhitaji muda, utulivu wa mawazo na mazingira tulivu.

**Hatua za kusoma habari**

Usomaji mzuri wa habari hufuata hatua tatu muhimu zifuatazo:

(a) Kabla ya kusoma

Kabla ya kusoma msomaji hana budi kujiuliza maswali yafuatayo:

(i) Je, kifungu cha habari kina mawazo gani makuu? Je, mawazo hayo yanahusianaje?


PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 235 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(ii) Je, kifungu hicho kimejengwa kwa muundo gani? Kwa mfano, ni muundo wa maelezo, majibizano au ushairi?

(iii) Je, kifungu cha habari kimejengwa na maneno mapya? Kama yapo, ni yapi? Yametumikaje katika sentensi?

(b) Wakati wa kusoma

Wakati wa kusoma msomaji anatakiwa kuzingatia yafuatayo:

(i) Kusoma kwa sauti inayosikika vizuri, kama anawasomea watu wengine.

(ii) Kuzingatia alama za uakifishaji katika usomaji.

(iii) Kusoma kwa kasi ya wastani.

(iv) Kuvuta umakini kwa kile anachokisoma bila kuruhusu kuingiliwa na mawazo mengine.

(c) Baada ya kusoma

Hatua hii ndiyo inayopima uelewa wa msomaji kulingana na kifungu cha habari alichosoma kwa kumuuliza maswali mbalimbali. Maswali hayo humfanya msomaji kutafakari, kueleza na kufafanua mambo aliyoyasoma. Iwapo atashindwa kujibu baadhi ya maswali, basi itamlazimu kurudia kusoma kifungu cha habari. Hatua hii ndiyo humwezesha msomaji kueleza mambo ya msingi aliyoyasoma kwa muhtasari.

***3. Ufahamu wa kuona***

Huu ni ufahamu unaotokana na kuchunguza tukio halisi, picha, video na michoro kisha, huliweka jambo hilo akilini ili kulichanganua na kulitafakari kwa kina. Baada ya kuchunguza kwa makini, mchunguzaji huweza kusimulia kwa ufupi alichokiona au kukihisi kupitia masimulizi ya mdomo au maandishi. Ufahamu huu huhusisha kushiriki katika mikusanyiko kama vile sherehe, ziara, na misiba. Pia, huhusisha kutazama picha mbalimbali zinazohusu matukio hayo. Maswali yanayotokana na ufahamu wa aina hii, humsaidia mtu kuwa mwepesi wa kufikiri, kuhusisha na kuumba kitu kinachoeleweka katika akili yake. Aidha, hupima uwezo wa mtu kuwa makini katika kuchunguza na kufuatilia matukio na uwezo wa kuchambua mambo.

For Online Use Only


PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 236 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



## Zoezi la 7.1

1. Iwapo msomaji wa ufahamu hakujiandaa kabla ya kusoma, unafikiri atapata changamoto gani? Fafanua.
2. Bainisha mambo ya kuzingatia wakati wa kusikiliza habari.
3. Linganisha na kulinganua changamoto zinazojitokeza katika aina tatu za ufahamu ulizojifunza.

**Ufupisho**

Kufupisha ni kutoa muhtasari wa maelezo kwa kuzingatia mawazo makuu au hoja muhimu kuhusu taarifa uliyoisikia, uliyoisoma au kuiona. Maelezo hayo yanatakiwa kutolewa kwa maneno tofauti na yale yaliyotumika katika habari bila kupoteza maana ya msingi. Hivyo, ufupisho huweza kufanyika kwa kuzingatia hatua zifuatazo:

(i) Kusoma au kusikiliza habari.

(ii) Kubaini mawazo makuu yote utakayosikiliza au kuyasoma katika kifungu cha habari.

(iii) Kuandika ufupisho kwa kutumia maneno yako mwenyewe bila kupoteza maana ya msingi.

(iv) Kusoma ufupisho wako kwa mara ya mwisho. Hatua hii husaidia kugundua kama kuna makosa madogo yanayohitaji kurekebishwa na kuyarekebisha.

Wakati wa kuandika ufupisho mwandishi anapaswa kuzingatia taratibu na alama za kiuakifishaji kwa usahihi na idadi ya maneno aliyopewa.

**Dhima za ufupisho**

Ufupisho hutumika katika kufanya mambo yafuatayo:

(i) Kutayarisha ripoti na kumbukumbu za mkutano.

(ii) Kudondoa hoja kutokana na mihadhara au hotuba.

(iii) Kuandaa shajara au kumbukumbu za kila siku.

(iv) Kuhariri habari.

(v) Kuwasilisha taarifa au ripoti.

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kwa ujumla, tunaweza kuhitimisha kwamba kufupisha habari iliyosikilizwa, kusomwa au kutazamwa kunahitaji uwezo wa kubaini mawazo makuu ya kilichozungumzwa, kilichoandikwa au kilichotazamwa ili kujua ukubwa wa ufupisho wake.

## Zoezi la 7.2

1. Soma habari ifuatayo kisha jibu maswali yatakayofuata:

   *Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazozalisha muhogo. Muhogo ni muhimu kwa biashara na ni kinga ya njaa. Pia, hutumika kutengeneza chakula cha mifugo na hutumika kama malighafi kwa viwanda. Hata hivyo, kwa muda mrefu, wakulima wamekuwa wakishindwa kupata mazao ya kutosha kutokana na magonjwa, hali ya hewa na uelewa mdogo wa mbinu za kilimo cha zao la muhogo.*

   *Uzalishaji wa zao la muhogo hapa Tanzania uko chini ya kiwango cha kimataifa. Wakulima hupata kati ya tani tano hadi saba kwa ekari ukilinganisha na wastani wa kimataifa ambao ni tani kumi kwa ekari. Utafiti unaonesha kuwa muhogo unaweza kutoa mazao kuanzia tani ishirini hadi hamsini kwa ekari kama kanuni za kilimo bora zitafuatwa na wakulima wakatumia mbegu bora za mihogo.*

   *Kwa kuzingatia changamoto hizo, wataalamu kutoka kituo cha utafiti wa kilimo cha Mikocheni (Mari) wamefanya tafiti za uzalishaji wa muhogo zilizoleta matokeo mazuri na kusambaza matokeo ya tafiti hizo katika baadhi ya nchi za Afrika. Mkuu wa kituo hicho na mratibu wa tafiti za bayoteknolojia nchini, Dkt. Joseph Ndunguru, anasema kuwa kuna tafiti zilizokamilika na zimeonesha mafanikio makubwa ndani na nje ya nchi. Utafiti wa uzalishaji wa muhogo kwa kutumia teknolojia ya uhandisijeni (GMO), unaendelea kwa sasa.*

   (Msuya - Mwananchi, Agosti 26, 2017).
2. Andika kichwa cha habari hiyo kisichozidi maneno matano.
3. Andika ufupisho wa habari hiyo kwa maneno yasiyozidi 100.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 238 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



## Tamrini

1. Linganisha na kulinganua dhana ya ufahamu na dhana ya ufupisho.
2. Unafikiri kwa nini ni muhimu kujifunza ufupishaji wa habari?
3. Soma habari ifuatayo kisha jibu maswali yanayofuata:

*Mchezo wa mpira wa miguu ni miongoni mwa michezo inayopendwa na watu wengi duniani. Mchezo huu unahusisha wachezaji wa timu mbili tofauti ambao ni mlinda mlango, walinzi wanne ambapo wawili huwa pembeni na wawili wengine huwa katikati. Vilevile, kuna wachezaji wawili wanaocheza nafasi ya kiungo ambapo mmoja akiwa mkabaji na mwingine mshambuliaji. Wachezaji wengine wanaokamilisha timu ya mpira wa miguu ni washambuliaji ambapo huwa kuna wawili katikati na wawili pembeni. Wachezaji wengine wa muhimu ni waamuzi watatu ambao si wa upande wowote. Mwamuzi mmoja huwa mwamuzi mkuu ambaye huwa uwanjani na wasaidizi wawili ambao huwa nje ya uwanja, kila mmoja upande wake.*

*Mchezo huu huchezwa kwa jumla ya dakika tisini ambazo hugawanywa katika vipindi viwili vya dakika arobaini na tano kwa kila kipindi. Hata hivyo, mwamuzi anaweza kuongeza dakika kadhaa kufidia muda ambao ulipotea wakati wa mchezo baada ya dakika tisini za mchezo kuisha. Wakati mchezo unaendelea, wachezaji wanaweza kuumia na kusababisha mchezo usimame kwa muda ili kutoa nafasi ya mchezaji aliyeumia kutibiwa. Iwapo mchezaji huyo atachelewa kupata nafuu, mwamuzi atawaita watoa huduma ya kwanza wamtoe nje mchezaji huyo ili akatibiwe zaidi. Katika mchezo huu ushindi unapatikana kwa wachezaji kufanikiwa kuingiza mpira kwenye goli la wapinzani, yaani kufunga goli. Timu inayofanikiwa kufunga magoli mengi ndiyo hupewa ushindi.*

*Mchezo huu unaongozwa na sheria mbalimbali. Kwa mfano, mchezaji hatakiwi kucheza mpira kwa kutumia mikono au kumchezea vibaya mwenzake. Mchezaji anayekiuka sheria hizo huwa anapewa onyo na mwamuzi na mpira hupigwa*



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 239 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*kuelekea kwenye goli la mchezaji huyo aliyekiuka sheria kama adhabu kwa timu yake. Mchezaji akiendelea kuvunja sheria, mwamuzi humwonya kwa kumwonesha kadi ya njano. Kadi hiyo humtahadharisha mchezaji huyo kuwa akiendelea kukiuka sheria ataondolewa uwanjani kwa kuonyeshwa kadi nyekundu.*

## Maswali

(i) Andika kichwa cha habari kisichozidi maneno matano.

(ii) Kwa nini dakika tisini za mchezo wa mpira wa miguu huwa zinagawanywa katika vipindi viwili?

(iii) Elezea taratibu za uchezaji wa michezo mingine ya mpira unayoijua.

(iv) Andika ufupisho wa habari hii kwa maneno yasiyozidi 120.

For Online Use Only


PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 240 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Sura ya Nane

# Tafsiri na ukalimani

## Utangulizi

Sura hii inahusu tafsiri na ukalimani. Tafsiri na ukalimani huwaunganisha watu wanaotumia lugha tofauti ili kukamilisha mawasiliano. Kwa hiyo, ni daraja la mawasiliano baina ya jamii zinazotumia lugha tofauti. Katika sura hii utajifunza dhana, aina na mbinu za tafsiri, na ukalimani. Lengo la kujifunza mada hii ni kukuwezesha kupata ujuzi wa kutafsiri matini na kukalimani mazungumzo ya lugha mbalimbali. Kwa mfano, tafsiri na ukalimani unaweza kutoka katika lugha ya Kiingereza kwenda Kiswahili au kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza.

**Dhana ya tafsiri**

Catford (1965) anasema kufasiri ni kuchukua mawazo yaliyo katika maandishi kutoka lugha moja (lugha chanzi) na kuyaandika mawazo hayo katika lugha nyingine (lugha lengwa). Kwa upande mwingine, TUKI (1990) wanafasili tafsiri kama kitendo cha kuhamisha habari kutoka kwenye lugha moja kwenda lugha nyingine bila kupoteza maana ya awali. Aidha, Mwansoko *na wenzie* (2006) wanasema kuwa tafsiri ni zoezi la uhawilishaji wa mawazo katika maandishi kutoka lugha moja hadi nyingine. Hivyo, tafsiri ni matokeo ya kuhamisha habari, taarifa, maarifa, au ujumbe kutoka lugha moja kwenda lugha nyingine kwa njia ya maandishi bila kupoteza maana. Ukichunguza fasili hizi utabaini kuwa tafsiri inahusisha mambo kadhaa kama yanavyofafanuliwa hapa chini.

**Uhawilishaji wa taarifa**

Uhawilishaji ni uhamishaji wa ujumbe au mawazo kutoka katika lugha moja kwenda lugha nyingine kwa njia ya maandishi au mazungumzo. Uhawilishaji huo hauathiri mabadiliko katika maudhui yake (Longhorn, 2016).

**Matini chanzi (MC)**

Hii ni matini ambayo iko katika lugha ya awali ambayo ujumbe wake huhawilishwa kwenda katika lugha nyingine. Wakati mwingine huitwa matini chasili au matini asilia. Matini chanzi inaweza kuwa katika lugha ya maandishi au alama.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 241 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Matini lengwa (ML)**
Matini lengwa ni matini yenye ujumbe uliohawilishwa kutoka matini chanzi. Kama ilivyo kwa matini chanzi, matini lengwa pia huweza kuwa katika lugha ya maandishi au alama.

**Lugha chanzi (LC)**
Hii ni lugha inayotumiwa katika matini chanzi. Lugha hii ndiyo inayobeba ujumbe kuhawilishwa kwenda katika lugha lengwa.

**Lugha lengwa (LL)**
Hii ni lugha inayotumiwa katika matini lengwa inayopokea ujumbe kutoka katika matini chanzi. Ni lugha ya jamii inayoelekezewa matini lengwa.

**Mfasiri**
Huyu ni mtaalamu anayehawilisha ujumbe au taarifa kutoka lugha moja kwenda lugha nyingine. Kazi ya kutafsiri ina changamoto nyingi sana. Hivyo, inahitaji mfasiri mwenye sifa mahususi ili tafsiri isipotoshe maana iliyokusudiwa katika matini chanzi. Sifa hizo ni:

(i) Azifahamu vizuri lugha mbili au zaidi, hasa zile anazoshughulika nazo (lugha chanzi na lugha lengwa).

(ii) Awe na taaluma ya tafsiri, yaani awe amesomea tafsiri, ili atumie ujuzi wa nadharia, mbinu na kanuni za tafsiri ambazo ndizo mwongozo wa tafsiri.

(iii) Afahamu vyema mada mbalimbali, hasa zile za matini anazozishughulikia.

(iv) Ajue na kujali mitindo ya uandishi. Hivyo, anapaswa kuwa makini katika kuhawilisha mitindo ya lugha chanzi kwenda lugha lengwa, kama kuna ulazima wa kufanya hivyo.

(v) Awe na umakini katika kuhawilisha ujumbe wa mwandishi wa matini chanzi kwenda kwa hadhira inayolengwa.

(vi) Aelewe vema utamaduni wa lugha chanzi na lugha lengwa ili aweze kutoa tafsiri bora.

(vii) Aelewe harakati mbalimbali za mabadiliko ya kijamii pamoja na masuala mtambuka.

(viii) Aendane na mabadiliko, mathalani ya kisayansi, kiteknolojia, kitamaduni, na kadhalika.


PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 242 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



**Aina za matini**

Kuna aina mbalimbali za matini kwa kigezo cha dhima ya lugha. Lugha ina dhima elezi, arifu, na amili. Kutokana na dhima hizi tunapata matini elezi, matini arifu, na matini amili.

**(a) Matini elezi**

Hizi ni matini zinazomwegemea mwandishi ambazo hueleza hisia za mwandishi. Mfasiri hufasiri hisia za mwandishi pasipo kujali athari zake kwa hadhira lengwa. Matini hizi zinakuwa zimebinafsishwa zaidi kwa maana kwamba anayeelewa vizuri taarifa za matini ni mwandishi. Mfasiri hatakiwi kuweka hisia zake na kuifafanua matini hiyo vinginevyo. Mifano ya matini elezi ni kama vile *kazi za fasihi*, *matamko ya kimamlaka* kama vile *hotuba, nyaraka za serikali, amri, nyaraka za kisheria, maandishi ya kisayansi*, na *kazi za kitaaluma*. Katika matini za aina hii, mwandishi huzingatia matakwa yake na kujiona yuko sahihi zaidi.

**(b) Matini arifu**

Hizi ni matini zinazotoa taarifa kuhusu jambo au mada fulani kama vile mada zenye maarifa ya kitaalamu. Mfano wa mada hizo ni kama vile sayansi, teknolojia, biashara, hesabu, historia, na mengineyo. Kwa kawaida matini za namna hii huwa katika mfumo wa ripoti kama vile ripoti za kiufundi, makala, vitabu, muhtasari wa ajenda za kikao, makala za magazetini, na tasinifu. Ni matini zinazojikita zaidi katika mada za kitaaluma.

**(c) Matini amili**

Hizi ni matini ambazo hulenga kuibua hisia za hadhira ili atende kama ilivyokusudiwa na mwandishi. Katika kufasiri matini hizi, dhana ya muktadha haina budi kuzingatiwa kwa sababu inaendana na utamaduni wa jamii fulani. Mifano ya matini za namna hii ni matini za matangazo ya biashara, maelekezo, propaganda, maombi mbalimbali, hasa ya kazi na michango, mialiko, fasihi pendwa, na vitabu vya watoto.

Hata hivyo, ni nadra sana kukutana na matini yenye sifa ya aina moja tu. Matini zilizo nyingi ni mchanganyiko, yaani ndani yake unaweza kukuta sehemu zenye matini elezi, arifu, au amili katika matini fulani. Kinachotokea ni kwamba, aina moja ya matini ndiyo inayochomoza zaidi kuliko aina nyingine za matini.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 243 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Aina za tafsiri**

Wataalamu wengi wanataja aina nyingi za tafsiri. Hata hivyo, wanaelekea kukubaliana juu ya aina kuu tatu za tafsiri. Baadhi ya wataalamu huzirejelea aina hizo kama mbinu za tafsiri. Zifuatazo ni aina au mbinu za tafsiri:

(a) **Tafsiri sisisi au ya neno kwa neno**

Hii ni aina au mbinu ya tafsiri ambayo maneno yake hutafsiriwa kiupwekeupweke kwa kuzingatia maana za msingi za lugha chanzi lakini kwa kufuata sarufi, hasa sintaksia, ya lugha lengwa. Chunguza mifano ifuatayo:

(i) Pull up your socks.
*Vuta soksi zako juu* badala ya *Ongeza juhudi*.

(ii) She bought me a book.
*Yeye alininunua mimi kitabu* badala ya *Alininunulia kitabu*.

(iii) Usinisumbuesumbue.
*Don't disturb disturb me* badala ya *Don't bother me.*

(iv) Mtoto wa nyoka ni nyoka.
*A child of a snake is a snake* badala ya *Like father like son*.

Udhaifu wa mbinu hii ya tafsiri ni kwamba inashindwa kufikisha ujumbe wa lugha chanzi katika lugha lengwa kwa ufanisi kwa sababu kunakuwa na upotoshaji wa maana ya lugha chanzi katika matini lengwa. Pia, misemo hutafsiriwa kwa makosa.

(b) **Tafsiri ya kisemantiki**

Hii ni aina au mbinu ya tafsiri ambayo huegemea zaidi kwa mwandishi wa matini chanzi ambapo maana na vipengele vidogovidogo hutiliwa maanani. Aina hii ya tafsiri huifanya kazi ya tafsiri iwe na taarifa nyingi. Mara nyingi tafsiri ya kisemantiki hujali zaidi maana na muundo wa matini chanzi. Chunguza mifano ifuatayo:

(i) Tanzania Electric Supply Company Ltd.
*Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania.*



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 244 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



(ii) Where there is a purpose, there is no failure.
*Palipo na nia, hapana kushindwa.*

(iii) Hapa kazi tu.
*Here job only.*

(iv) How are you doing?
*Je, wewe unafanyaje?*

Mifano hiyo hapo juu inaonesha kwamba kila neno katika matini chanzi limetafsiriwa katika lugha lengwa. Kutokana na hali hii, matini lengwa zimekuwa na taarifa nyingi ambazo siyo sahihi.

Mbinu hii ina uwezo mkubwa wa kuendeleza lugha lengwa kwa kuiingizia miundo na misemo kutoka katika lugha chanzi kama inavyoonekana katika mifano ifuatayo:

(i) Ladies and gentlemen - *mabibi na mabwana*
(ii) At the end of the day - *mwisho wa siku*
(iii) Weekend - *mwisho wa wiki (wikendi)*
(iv) Under the chairmanship of …- *chini ya uenyekiti* wa …

Tafsiri ya kisemantiki hutafsiri misemo ya kiutamaduni kisisisi. Tafsiri na muundo wa matini chanzi huwa haviendani na muundo wa lugha lengwa na huonekana kuwa ni ngeni. Tafsiri ya kisemantiki hutumika zaidi katika matini elezi kama vile wasifu binafsi, nyaraka za kisheria na kisiasa na fasihi iliyobuniwa kwa umakini.

(c) **Tafsiri ya kimawasiliano**

Hii ni tafsiri ambayo huzingatia kueleweka kwa ujumbe kwa hadhira lengwa. Huzingatia pia historia, muktadha, utamaduni, na itikadi ya mzungumzaji wa lugha lengwa. Kwa hiyo, ni tafsiri inayoilenga hadhira kwa vile humjali zaidi msomaji wa matini lengwa. Ni tafsiri iliyo wazi, huru na inayoeleweka kwa urahisi. Wakati mwingine hujulikana pia kama tafsiri huru. Hii ndiyo aina ya tafsiri au mbinu ambayo inaonekana kuwa na mashiko zaidi kwa sababu haina utata wowote kwa hadhira ya lugha lengwa. Mfasiri hapaswi kufungwa na miundo ya lugha chanzi kwani kinacholengwa ni kueleweka kwa ujumbe kwa hadhira. Mfasiri hufuata sarufi ya lugha lengwa na yuko huru kutafuta maneno au mafungu ya maneno yanayolingana na nahau,



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 245 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

misemo, methali, tamaduni, na mazingira ya lugha lengwa katika kuelezea ujumbe unaotolewa na matini chanzi. Angalia mifano ifuatayo:

(i) Tanzania Electric Supply Company Limited
*Shirika la Umeme Tanzania*

(ii) Where there is a purpose, there is no failure.
*Penye nia, pana njia.*

(iii) At the end of the day
*Hatimaye*

(iv) Kawia ufike
*Better late than never*

Tafsiri zilizotolewa katika mifano hapo juu zimefanyika kwa kuzingatia miundo na maana zake katika lugha lengwa. Hii ndiyo sababu hatuoni kila neno likiwa limetafsiriwa kipwekepweke. Aidha, msemo katika mfano (ii) umetafutiwa msemo unaofanana nao katika lugha lengwa badala ya kutafsiriwa kisisisi.

Tafsiri ya kimawasiliano hutumika zaidi kufasiri matini arifu kama vile za sayansi na teknolojia, kibiashara, ripoti za mikutano, na kazi za kifasihi. Tafsiri ya kimawasiliano ndiyo inayotumika zaidi katika tafsiri kuliko mbinu nyingine. Ikumbukwe kuwa wakati mwingine tafsiri ya kimawasiliano na ya kisemantiki hutokea pamoja au hufanana. Hii hutokana na kufanana kwa mahitaji na matarajio ya hadhira ya lugha chanzi na lugha lengwa kimuktadha, kiitikadi, kidini, kisiasa, kifalsafa, na kisayansi. Chunguza mifano ifuatayo:

(i) Big Results Now
*Matokeo Makubwa Sasa*

(ii) Propaganda
*Propaganda*

(iii) Animal Farm
*Shamba la Wanyama*

(i) Demonstration farm
*Shamba darasa*

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 246 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Mifano hii inaonesha kufanana kwa matini chanzi na matini lengwa, hususani kimaana kwa sababu mahitaji ya hadhira chanzi na lengwa yanafanana.

**Hatua za kutafsiri**

Ili kupata matini lengwa inayoeleweka na kukubalika kwa hadhira ni lazima mfasiri apitie hatua mbalimbali katika kutafsiri. Hatua hizo zinafafanuliwa kama ifuatavyo:

(a) Maandalizi

Katika hatua hii, mfasiri anapaswa kuisoma matini chanzi mara kadhaa ili kujiridhisha kuhusu maudhui yake, mtindo wake na kuziwekea alama maalumu sehemu au vipengele vinavyopaswa kupewa kipaumbele.Vilevile, huchunguza usuli wa matini chanzi, historia ya mwandishi, utamaduni wake, mazingira ya uandishi, malengo yake, na hadhira ya matini hiyo. Kama mfasiri ni mgeni zaidi katika utamaduni huo, inampasa kujisomea zaidi kuhusu utamaduni huo. Usuli huendana na uchambuzi wa vipengele vya kiisimu ambapo mfasiri huandika msamiati na istilahi maalumu, maneno ya kiutamaduni na sehemu ngumu kueleweka ili azifanyie kazi.

(b) Uchambuzi

Katika hatua hii, mfasiri huyafanyia kazi yale aliyoyabaini katika hatua ya maandalizi. Hutafuta visawe vya msamiati na istilahi ngumu au ngeni kwa kutumia marejeo mbalimbali kama ensaiklopidia na kamusi. Inashauriwa kuwa mfasiri awe na kompyuta au daftari au faili kwa ajili ya kutunzia msamiati au istilahi zitakazotumika.

(c) Uhawilishaji

Katika hatua ya uhawilishaji, mfasiri huhawilisha taarifa kutoka kwenye matini chanzi kwenda kwenye matini lengwa. Mfasiri anatakiwa kuzingatia sarufi ya lugha lengwa isipokuwa anapotumia tafsiri ya neno kwa neno.

(d) Kusawidi rasimu ya kwanza

Kazi ya tafsiri inayopatikana baada ya uhawilishaji wa visawe kutoka lugha chanzi kwenda lugha lengwa kukamilika ni rasimu ya kwanza ya tafsiri. Rasimu ya kwanza ya tafsiri iliyosawidiwa inaweza kuwa na dosari kadhaa. Kwa hiyo, haifai kupelekwa kwa mteja au hadhira lengwa kama ilivyo. Hivyo basi, mfasiri hulazimika kuidurusu rasimu hiyo ili kuondoa dosari.

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 247 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(e) Udurusu wa rasimu ya kwanza

Rasimu ya kwanza lazima ipitiwe tena na kurekebishwa au kudurusiwa. Mfasiri hupata fursa ya kwanza ya kuitathimini na kuifanyia marekebisho tafsiri yake mwenyewe. Kazi ya kudurusu haipaswi kufanywa haraka. Kwa mujibu wa Mwansoko *na wenzie* (2006) hatua hii huhusisha shughuli zifuatazo:

(i) Kusahihisha makosa ya kisarufi na miundo isiyoeleweka vizuri.

(ii) Kunyoosha sehemu zenye tafsiri ya mzunguko na zenye matumizi potofu ya visawe.

(iii) Kurekebisha sehemu zenye muunganiko mbaya ambazo zinazuia mtiririko mzuri wa matini.

(iv) Kuhakiki usahihi na kukubalika kwa maana zinazowasilishwa katika matini lengwa. Katika shughuli hii tunaangalia kama kuna mambo yameongezwa, yamepunguzwa, yamepotoshwa, au kubadilishwa.

(v) Kuhakiki kukubalika kwa lugha iliyotumika katika tafsiri kwa kuzingatia umbo lililotumika kuwasilisha matini lengwa na mada ya matini chanzi.

(vi) Kuona iwapo mada au ujumbe mkuu wa matini chanzi unajitokeza waziwazi katika matini lengwa.

(f) Kusomwa kwa rasimu ya pili na mtu mwingine

Msomaji wa rasimu ya pili anaweza kuwa mfasiri mwingine au mhakiki au mhariri wa tafsiri. Pia, anaweza kuwa mteja wa tafsiri inayohusika au mtu mwingine yeyote mwenye utaalamu wa uwanja uliotafsiriwa.

(g) Kusawidi rasimu ya mwisho

Katika hatua hii, mfasiri hufanyia kazi maoni na mapendekezo ya msomaji ambaye alimpa kazi yake. Matokeo ya kufanyia kazi maoni hayo humwezesha kuandika rasimu nzuri ya mwisho ambayo ndiyo humfikia hadhira.

**Dhima za tafsiri**

Tafsiri ina umuhimu mkubwa katika maendeleo ya binadamu kwa sababu husaidia kuunganisha jamii zinazotumia lugha tofauti ili ziweze kuelewana. Zifuatazo ni dhima za tafsiri:

(a) Chombo cha mawasiliano

Tafsiri hutumika kama njia ya kutolea ujumbe katika shughuli za biashara, nyaraka rasmi kama vile ripoti, mikataba ya kimataifa, makala za kitaaluma,



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 248 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



na vitabu vya kiada na ziada. Husaidia kuzikutanisha pamoja jamii zenye lugha tofauti. Hivyo, tafsiri tenge hukwamisha mawasiliano.

(b) Chombo cha kueneza utamaduni
Lugha ni kipengele cha utamaduni. Tafsiri inapofanyika, vipengele vya utamaduni wa lugha inayohusika pia hutafsiriwa. Kwa mfano, tafsiri ya Biblia kutoka Kilatini na Kiyunani imesababisha kuenea kwa utamaduni wa Kilatini na Kiyunani katika mataifa mengine ya Ulaya hadi mwanzoni mwa karne ya 19. Aidha, kuna tafsiri za kazi nyingi za fasihi za Ulaya ambazo zimesababisha kuenea kwa utamaduni wa Ulaya kama vile uvaaji, uongeaji na kadhalika.

(c) Chombo cha kujifunza na kufundishia lugha
Wakati wa kutafsiri, mfasiri hujikuta akilazimika kupekua marejeo mbalimbali ili apate maarifa anuwai kuhusu lugha anazoshughulikia. Vipengele vinavyosomwa vinaweza kuwa vya kiisimu kama vile msamiati, miundo ya tungo, mitindo, maumbo, na miktadha mbalimbali ya matumizi ya lugha ambayo husaidia kujifunza lugha anayoitafsiri kwa undani. Vilevile, tafsiri hutumika kufundishia lugha, hususani lugha ya kigeni ambapo vipashio mbalimbali vya lugha hutafsiriwa kutoka lugha chanzi kwenda lugha lengwa.

(d) Kiliwazo cha nafsi ya mfasiri
Zoezi la kufasiri ni gumu na lina changamoto nyingi, hasa kutafuta visawe, miundo, na mitindo sahihi katika lugha lengwa. Kwa hiyo, mfasiri anapopata ufumbuzi wa matatizo yaliyomkuta katika kufasiri, hufarijika sana. Faraja hii humpa moyo zaidi na kumfanya azidi kuipenda kazi ya kufasiri; hivyo, hujisikia kuliwazika.

## Zoezi la 8.1

1. Katika aina za matini ulizojifunza, unafikiri ni aina gani ya tafsiri inafaa kutumika katika kila moja ya aina za matini hizo? Toa sababu za kushadidia jibu lako.
2. Tafsiri sentensi ifuatayo kutoka lugha ya Kiswahili kwenda Kiingereza:

"Kwanza ninatoa shukurani zangu nyingi kwa kunikaribisha kuhudhuria sherehe hii ya kutoa zawadi kwa washindi wa mashindano ya insha yaliyoandaliwa na Baraza la Kiswahili la Taifa."



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 249 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Ukalimani

Neno ukalimani limefasiliwa na wataalamu mbalimbali duniani. Mathalani, TUKI (2004) wanasema ukalimani ni mchakato wa kufasiri mazungumzo papo kwa papo kutoka lugha moja kwenda lugha nyingine. Naye Nolan (2005) anafasili ukalimani kuwa ni mchakato wa kuhawilisha taarifa za mazungumzo kutoka lugha chanzi kwenda lugha lengwa kwa njia ya ufuatizi au usambamba. Ukichunguza fasili hizo mbili utaona kuwa fasili ya Nolan inafungamana na ile ya TUKI. Wote wanaonesha kuafikiana kuwa ukalimani hufanyika papo kwa papo na kwamba ukalimani huhusu lugha ya mazungumzo.

## Mambo ya msingi katika ukalimani

Kuna mambo mbalimbali ya msingi ya kuelewa kuhusu ukalimani. Baadhi ya mambo hayo ni:

(i) Ukalimani ni mchakato wa uhawilishaji wa ujumbe wa mazungumzo ya papo kwa papo.
(ii) Ukalimani unahusu lugha ya mazungumzo au alama.
(iii) Katika ukalimani, kuna wahusika watatu ambao ni mzungumzaji, mkalimani na msikilizaji.
(iv) Ukalimani huzingatia sarufi, utamaduni, muktadha wa tukio, na mada.
(v) Ukalimani unahusu lugha mbili tofauti. (Wanjala, 2011 na Nolan, 2005)

**Mkalimani** ni mtu afasiriye mazungumzo kutoka lugha moja kwenda nyingine.

## Sifa za mkalimani

Mkalimani anatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:

(i) Azijue lugha zote mbili kwa ufasaha ili kuepusha ukakasi katika ukalimani na awe na uwezo wa kuendana na wakati kulingana na mfumo wa lugha unavyobadilika katika jamii kisiasa, kiuchumi, na kiutamaduni kwa wakati huo.
(ii) Awe anayezingatia utamaduni wa lugha zote mbili wakati wa kukalimani.
(iii) Awe na uwezo wa kuutawala muktadha wa mazungumzo. Mkalimani anatakiwa kutawala jukwaa ambapo kazi ya ukalimani inafanyikia kwa kutoa sauti inayosikika kwa hadhira. Vilevile, anatakiwa kubadilika kadiri mzungumzaji anavyobadilika na kufuata ishara za mzungumzaji.
(iv) Awe na ujuzi wa kuhawilisha ujumbe kama ulivyo katika lugha chanzi.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 250 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



(v) Aelewe vema mada husika anayoikalimani pamoja na istilahi zake.

(vi) Ajue historia ya jamii lengwa ili imsaidie kuijua vyema lugha na utamaduni wake.

(vii) Awe na uwezo mkubwa wa kufikiri na kupambanua mambo kwa haraka na usahihi kwa sababu mzungumzaji anaweza kuibua mambo mapya ambayo mkalimani hakuyafanyia maandalizi.

(viii) Awe mtunza siri. Mkalimani anapaswa kuwa na uwezo wa kutunza siri kuhusu yale aliyohawilisha kwa kutegemea malengo ya ukalimani alioufanya.

(ix) Awe mvumilivu na mdadisi.

(x) Awe anazimudu vizuri stadi za kuzungumza na kusikiliza kwa lugha husika.

(xi) Awe na uwezo wa kubainisha hoja za msingi katika mazungumzo.

**Aina za ukalimani**

Kuna aina mbili za ukalimani ambazo ni *ukalimani fuatizi* na *ukalimani sawia au sambamba*.

**Ukalimani fuatizi**

Ukalimani fuatizi ni ukalimani wa mwanzo kabisa. Katika ukalimani huu, mzungumzaji huzungumza kisha humpa nafasi mkalimani ili akalimani. Mkalimani akimaliza, humpisha mzungumzaji na zoezi hili huendelea hivyo hadi mwisho. Ukalimani wa aina hii hufaa katika mijadala kunapokuwa na mazungumzo ya maswali na majibu kwa vile mkalimani atahitaji kuchukua nukuu na kumbukumbu. Vilevile, ukalimani huu hufanyika katika mikutano ya wanahabari, makubaliano ya kisheria ya pande mbili na kwenye kundi dogo la watu, mikutano ya kidini, na hospitalini.

Njia hii hutumika zaidi kwa vile haina gharama kubwa kutokana na gharama za vifaa vinavyotumika kuwa ndogo na rahisi kuvimudu. Hata hivyo, mkalimani anatakiwa kufanya maandalizi ya kutosha. Udhaifu wa njia hii ni kuwa hutumia muda mrefu zaidi kwani hoja moja husemwa mara mbili kwa lugha mbili tofauti na kwa kusubiriana.

**Ukalimani sawia (sambamba)**

Ukalimani sawia ni aina ya ukalimani unaoshughulika na uhawilishaji wa ujumbe kutoka lugha chanzi kwenda lugha lengwa; ambao hufanyika papo kwa papo wakati mzungumzaji anaendelea kuzungumza. Mzungumzaji na mkalimani huwasilisha ujumbe kwa pamoja bila kusubiriana. Wakati mwingine, mzungumzaji



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 251 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

humwacha mkalimani nyuma kwa sekunde mbili au tatu. Mzungumzaji hasitishi mazungumzo kumpisha mkalimani na mkalimani hamsubiri mzungumzaji kama ilivyo katika ukalimani fuatizi.

Ukalimani wa aina hii unahitaji umahiri wa kiwango cha juu wa lugha zote mbili, uwezo wa kutunza kumbukumbu na uwezo mkubwa wa kukumbuka istilahi, na kuzichagua. Njia hii hutumika katika matukio ambapo kunakuwa na vyombo vya kielektroniki ambavyo huvaliwa na wakalimani kwa ajili ya kuhawilishia ujumbe. Wakalimani hao hukaa katika vyumba maalumu ambavyo huitwa *vituturi* (vyumba maalumu vya wakalimani). Aina hii ya ukalimani hutumika katika mikutano ya kimataifa ambayo, aghalabu hujumuisha washiriki kutoka mataifa mbalimbali.

Aidha, katika ukalimani huu, wakalimani hufanya kazi kwa timu ya watu wawili au zaidi katika kila kituturi kwa sababu ukalimani sawia ni shughuli ya kuchosha. Hivyo, huachiana zamu kila baada ya dakika kumi na tano kila mmoja kwa ukomo wa juu wa saa moja kwa siku. Wakalimani wanatakiwa kuhawilisha taarifa kwenda katika lugha wanazozifahamu vizuri, hususani lugha za kwanza. Hadhira lengwa huwa wamevaa vifaa maalumu vya kusikilizia ambavyo huwa vimeunganishwa na mitambo iliyomo katika kituturi cha wakalimani.

Njia hii ina gharama kubwa sana ingawa inaokoa muda. Gharama zinatokana na maandalizi kabla ya ukalimani kuanza, vifaa na hata malipo ya wakalimani ni ya juu kutokana na idadi yao kuwa kubwa na ujuzi unaohitajika.

**Zana za ukalimani**

Maendeleo ya sayansi na teknolojia yameibua zana mbalimbali ambazo husaidia katika zoezi zima la ukalimani. Hata hivyo, zana za ukalimani hutegemea aina ya ukalimani wenyewe na muktadha unaohusika katika ukalimani huo. Kwa mfano, mtu anapokalimani mazungumzo ya kawaida baina ya watu wawili au watatu, hahitaji kutumia zana yoyote. Endapo ni ukalimani unaohusu mikutano mikubwa ya kitaifa, kimataifa, au kusanyiko kubwa la hadhira, mkalimani huhitaji kuwa katika kituturi chenye zana ambazo zinaweza kumsaidia katika kufanikisha shughuli nzima ya kukalimani. Zifuatazo ni baadhi ya zana ambazo huweza kutumika:

(i) Kituturi
(ii) Paneli pokezi na tolezi ya sauti



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 252 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



(iii) Maikrofoni

(iv) Kompyuta

(v) Jozi ya visikizio

Vilevile, kituturi huwa kinapaswa kuwa kisichoruhusu sauti nyingine kusikika ndani zaidi ya ile ya mzungumzaji. Hii humsaidia mkalimani kusikiliza sauti ya lugha chanzi kwa utulivu mkubwa. Mkalimani humwona mzungumzaji wa lugha chanzi kupitia dirisha lenye kioo angavu la chumba hicho. Wakati mwingine mkalimani huweza kumwona mzungumzaji wa matini chanzi kupitia kompyuta. Kwa uelewa zaidi angalia kielelezo namba 8.1.




**Kielelezo 8.1** Mkalimani akiwa katika kituturi cha ukalimani

**Mambo ya kuzingatia wakati wa ukalimani**

Mkalimani anatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo wakati wa mchakato wa kukalimani:

(a) Lugha

Mkalimani anatakiwa aijue lugha chanzi na lugha lengwa ikiwa ni pamoja na lafudhi ya mzungumzaji ili ayasikie vizuri mazungumzo na kuielewa habari inayozungumzwa kisha aihawilishe bila tatizo lolote.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 253 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(b) Mazungumzo

Mkalimani anatakiwa ajue aina ya mazungumzo atakayokalimani ili aweze kuteua msamiati mwafaka katika mada na mazungumzo hayo. Mazungumzo hayo yanaweza kuwa ya kitaaluma, kidini, au kisiasa.

(c) Hadhira

Mkalimani lazima aijue hadhira inayopokea ujumbe. Aidha, hana budi kuifanya hadhira iwe na ari na utayari wa kumsikiliza, ili iweze kupata ujumbe. Kuijua hadhira kunamsaidia mkalimani kuchagua maneno na mtindo wa mazungumzo, ili kuiwezesha kuelewa kinachosemwa.

(d) Muktadha

Muktadha ni muhimu wakati wa ukalimani. Mkalimani anatakiwa azingatie muktadha husika wa tukio.

(e) Ujumbe

Mkalimani azingatie ujumbe unaowasilishwa na mzungumzaji. Katika kukalimani ni muhimu kuzingatia zaidi ujumbe na kuuvaa uhusika zaidi kuliko muundo na mtindo wa lugha chanzi.

(f) Lengo la mazungumzo

Mkalimani anatakiwa kuzingatia lengo la mazungumzo na aoneshe hisia za mzungumzaji.

**Dhima za ukalimani**

Ukalimani una dhima zifuatazo:

(i) Ni kiungo cha mawasiliano kati ya jamiilugha moja na nyingine. Mawasiliano hayo yanaweza kuwa ya kitaaluma, kidini, kisiasa, na kadhalika.
(ii) Husaidia kueneza utamaduni katika jamii tofauti. Kupitia ukalimani jamii hupata kujua tamaduni za jamii nyingine, hususani mazungumzo yanayohusu utamaduni, vyakula, michezo, na kadhalika.
(iii) Husaidia katika shughuli za kidiplomasia ambapo kunakuwa na watumiaji wa lugha tofauti.
(iv) Husaidia kukuza lugha. Hadhira au wasikilizaji wa mazungumzo huweza kujifunza lugha nyingine kwa kujua maana ya maneno na hata miundo ya lugha ngeni.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 254 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



## Zoezi la 8.2

1. Jadili mambo ya kuzingatia wakati wa ukalimani.

2. Fikiria kuwa wewe ni mkalimani, umealikwa katika Shule ya Sekondari Matumaini kukalimani katika warsha ya UKIMWI inayoendeshwa na shirika la PASADA. Kalimani mazungumzo yafuatayo yanayotolewa na mzungumzaji wa PASADA, kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza:

   Wapendwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Matumaini, leo nimekuja na ujumbe mzuri ambao utawasaidia katika maisha yenu na vizazi vijavyo. Sote tunatambua kuwa duniani kote kuna vilio vya kusaga meno, kwa kuingiliwa na ugonjwa hatari wa UKIMWI.

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 255 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Tamrini

1. Kwa kutumia mifano, jadili kutofautiana na kufanana kwa tafsiri na ukalimani.
2. Jadili mambo ya kuzingatia katika tafsiri na ukalimani.
3. Tafsiri vifungu vifuatavyo:

   (a) Kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza

   *Mbwamwitu ni miongoni mwa makundi ya wanyama walio hatarini kutoweka duniani. Kutoweka kwa wanyama hao kunatokana na sababu mbalimbali zikiwamo magonjwa na kushambuliwa na binadamu. Eneo la ikolojia la Serengeti ni miongoni mwa maeneo ambayo miaka ya nyuma yalikuwa na idadi kubwa ya mbwamwitu. Hata hivyo, kufikia mwaka 1994, mbwamwitu wote walikuwa wametoweka eneo la ikolojia ya Serengeti.*

   (Mwananchi, 21 Machi, 2016)

   (b) Kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili

   *Phonology is the branch of linguistics that deals with the study of sound system of (natural) languages. This implies that each natural language has its own sound system upon which the words of that language are built. In fact, phonology deals with the way sounds are used in words of a language in order to convey meaning. In other words, it deals with the structure and function of sounds within natural languages.*

   (Massamba, 2010)



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 256 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



# Sura ya Tisa
# Makosa katika matumizi ya lugha

## Utangulizi

Sura hii inahusu makosa katika matumizi ya lugha. Katika sura hii utajifunza kuhusu makosa yanayojitokeza katika uandishi, usomaji na uzungumzaji. Utajifunza makosa yaliyogawanyika katika makundi matatu: makosa ya kisarufi, kimantiki, na kiuakifishaji. Hali kadhalika, utajifunza kuhusu vyanzo mbalimbali vya makosa hayo.

**Makosa ya kisarufi**

Makosa ya kisarufi hujumuisha makosa ya kimuundo, makosa ya kimsamiati na makosa ya kimatamshi.

***1 Makosa ya kimuundo***

Makosa ya kimuundo yamegawanyika katika makundi manne ambayo ni makosa ya upatanisho wa kisarufi, makosa katika mpangilio wa maneno, matumizi ya vipande vya sentensi na matumizi ya sentensi bebanifu.

(a) **Makosa ya upatanisho wa kisarufi**

Makosa ya upatanisho wa kisarufi ni makosa yanayofanywa kutokana na kukiuka utaratibu wa neno kuu katika sentensi kupatana na viambishi vya maneno yanayofuata. Tazama mifano ifuatayo:

(i) Jeshi *wa*meshiriki kikamilifu katika ujenzi wa taifa.

(ii) Mmoja miongoni mwa kaka zangu *wa*nazungumza lugha tano.

(iii) Gari *ya*ngu *i*meharibika.

Viambishi vilivyoandikwa kwa hatimlalo katika mifano (i) – (iii) vimekosewa. Hivyo, vimeathiri upatanisho wa kisarufi katika lugha ya



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 257 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kiswahili. Katika mfano (i) neno *jeshi* liko katika ngeli ya *LI – YA*. Kwa hiyo, kiambishi cha upatanisho wa kisarufi cha neno hili katika kitenzi kilipaswa kiwe *li*- badala ya *wa*-. Katika mfano (ii) neno kuu ni *mmoja* ambalo liko katika ngeli ya *YU/A - WA- umoja*. Kwa hiyo, kiambishi cha upatanisho wa kisarufi katika kitenzi kilipaswa kuwa *a*- badala ya *wa*-. Katika mfano (iii) nomino *gari* iko katika ngeli ya *LI –YA*. Kwa hiyo, kiambishi chake cha upatanisho wa kisarufi katika kitenzi kilitakiwa kiwe *li*- badala ya *i*-. Kwa hiyo, sentensi hizo zilitakiwa kuandikwa kwa usahihi kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi kama ifuatavyo:

(i) Jeshi *li*meshiriki kikamilifu katika ujenzi wa taifa.

(ii) Mmoja miongoni mwa kaka zangu *a*nazungumza lugha tano.

(iii) Gari *l*angu *li*meharibika.

(b) **Makosa katika mpangilio wa maneno**

Kila lugha ina mpangilio wake wa maneno katika sentensi zake. Kwa mfano, sentensi za Kiswahili zina muundo wa *Kiima+Kitenzi+Yambwa* ambao ni muundo wa msingi. Kwa hiyo, sentensi inakuwa siyo sahihi kisarufi iwapo itakiuka muundo huo wa msingi. Tazama mifano ifuatayo:

(i) Mwanafunzi mwenye bidii anasoma kitabu.

(ii) Mwenye bidii mwanafunzi anasoma kitabu.

(iii) Mtoto amekunywa uji.

(iv) Amekunywa uji mtoto.

Miundo ya sentensi (i) na (iii) imefuata kanuni za uundaji wa sentensi za Kiswahili. Kwa hiyo, sentensi hizo hazina makosa. Kwa upande mwingine, miundo ya sentensi (ii) na (iv) siyo sahihi kwa sababu imekiuka kanuni za mpangilio wa maneno katika sentensi za Kiswahili. Katika sentensi (ii) kirai kivumishi *mwenye bidii* kimetangulia nomino *mwanafunzi* badala ya kutanguliwa na nomino hiyo. Sentensi (iv) nayo si sahihi kwa sababu kitenzi *amekunywa* kimetangulia nomino *mtoto* ambaye ni mtenda wa jambo (kiima) badala ya kiima kutangulia kitenzi.

(c) **Makosa ya matumizi ya vipande sentensi**

Haya ni makosa ambayo hufanywa kwa kuandika sentensi isiyo kamili. Wakati mwingine sentensi hizo, ambazo hazikamiliki, huwekewa nukta, alama ya kuuliza au mshangao mwishoni kana kwamba ni sentensi kamili. Tazama mifano ifuatayo:



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 258 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



(i) Msichana aliyekuwa anasuka katika saluni iliyopo karibu na soko kuu la Majengo, barabara iendayo Nkuhungu.

(ii) Wanafunzi wengi kutokupenda kusoma kwa bidii. Je, ni tatizo la mazingira?

Mfano (i) una kipande sentensi kinachoundwa na kishazi tegemezi pekee. Mfano (ii) una sentensi mbili ambazo hazijakamilika kisarufi. Kwa hiyo, sentensi hizo zilitakiwa kukamilishwa kwa kuunganishwa pamoja ili kupata sentensi moja iliyokamilika. Hivyo, sentensi kamili zilitakiwa ziwe kama ifuatavyo:

(i) Msichana aliyekuwa anasuka katika saluni iliyopo karibu na soko kuu la Majengo, barabara iendayo Nkuhungu, amehitimu kidato cha nne mwaka huu.

(ii) Je, wanafunzi wengi kutokupenda kusoma kwa bidii ni tatizo la mazingira?

(d) **Makosa ya kuandika sentensi bebanifu**

Haya ni makosa ya kuandika sentensi kamili zaidi ya moja bila kutumia viunganishi au kuzitenganisha kwa alama sahihi zinazotumika mwishoni mwa sentensi. Wakati mwingine, sentensi hizo hukosewa kwa kutenganishwa kwa mkato. Tazama mifano ifuatayo:

(i) Mama alinunua mkate, baba alinunua siagi.

(ii) Asha ni mtoto wa Mohamed, alimaliza darasa la saba katika Shule ya Msingi Uhuru.

Ukichunguza mifano (i) - (ii) hapo juu utagundua kwamba kila mfano una sentensi mbili kamili. Katika mfano (i) sentensi ya kwanza ni *Mama alinunua mkate* na sentensi ya pili ni *Baba alinunua siagi*. Sentensi hizi zilipaswa kuunganishwa kwa kiunganishi *na, lakini* au kutenganishwa kwa nukta (.) kama ifuatavyo:

(i) Mama alinunua mkate na baba alinunua siagi.

(ii) Mama alinunua mkate lakini baba alinunua siagi.

(iii) Mama alinunua mkate. Baba alinunua siagi.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 259 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Katika mfano (ii) sentensi ya kwanza ni *Asha ni mtoto wa Mohamed* na sentensi ya pili ni *Alimaliza darasa la saba katika Shule ya Msingi Uhuru*. Sentensi hizi zilipaswa kutenganishwa kwa kutumia nukta na si mkato. Unaweza kutumia neno *ambaye* ili kuziunganisha sentensi hizo. Kwa hiyo, zilitakiwa kuandikwa kwa usahihi kama ifuatavyo:

(i) Asha ni mtoto wa Mohamed. Alimaliza darasa la saba katika Shule ya Msingi Uhuru.

(ii) Asha ni mtoto wa Mohamed ambaye alimaliza darasa la saba katika Shule ya Msingi Uhuru.

### *2 M akosa ya kimsamiati*

Haya ni makosa yanayohusu uteuzi wa msamiati usio sahihi. Watumiaji wa lugha hukosea kuteua maneno katika kuzungumza au kuandika. Makosa haya yanaweza kujitokeza kama inavyoonekana katika mifano ifuatayo:

(i) Matumizi ya neno *mwenyewe* badala ya *peke yake (yangu, yao)*
Katika lugha ya Kiswahili ni makosa kusema *Nimemkuta mwenyewe* kwa maana ya *kumkuta akiwa peke yake*. Mzungumzaji anapaswa kusema *Nimemkuta mwenyewe* ili kumaanisha *amemkuta mmiliki wa mali fulani* au *amemkuta mtu yule aliyetarajiwa na si mwingine*. Ili maana iwe *amemkuta bila kuwapo mtu mwingine*, basi mzungumzaji anapaswa kusema *Nimemkuta peke yake.*

(ii) Matumizi ya maneno *weka* na *tia*
Ni kosa kusema *niwekee chai katika kikombe hiki*, ambapo msemaji anataka atiliwe chai katika kikombe. Ni sahihi kusema *nitilie chai katika kikombe*. Hii ni kwa sababu kuweka kitu maana yake ni kuhifadhi au kutua kitu mahali fulani, wakati kutia kitu ni kukiingiza kitu hicho ndani ya kitu kingine. Hali kadhalika tunapaswa kusema, *tia sukari kwenye chai* au *tia chumvi kwenye mboga* na siyo *weka sukari kwenye chai* au *weka chumvi kwenye mboga*.

### *3 M akosa ya kimatamshi*

Haya ni makosa ambayo hutokana na mzungumzaji au mwandishi kushindwa kufuata taratibu za kifonolojia katika matumizi ya lugha. Makosa haya hujumuisha makosa ya kuongeza au kudondosha vipashio vya kifonolojia na kukosea kuviweka mahali panapotakiwa katika neno kwa mujibu wa kanuni za matamshi ya Kiswahili. Kwa mfano:



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 260 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



(i) *U*sisha badala ya *hu*sisha

(ii) Mhadhi*li* badala ya mhadhi*ri*

(iii) M*u*rembo badala ya *m*rembo

(iv) Nakwenda*ga* badala ya *hu*enda

(v) Ku*a* badala ya ku*wa*

Katika mifano hii tunaona makosa ya kudondosha sauti kama vile */h/* kwenye mfano wa (i) na */w/* katika mfano wa (v). Aidha, katika mfano wa (ii) kuna kosa la kutumia sauti */l/* badala ya */r/* na katika mfano wa (iii) na (iv) kuna kosa la kuongeza sauti */u/* na silabi *ga* mtawalia.

**Makosa ya kimantiki**

Mantiki ni mpangilio au mtiririko wa fikira wenye hoja zinazokubalika katika muktadha husika. Makosa ya kimantiki yanasababishwa na kukosekana kwa fikira sahihi katika kutoa hoja au maelezo. Watumiaji wa lugha hufanya makosa ya kimantiki pale wanapotoa hoja zisizo sahihi na zisizokubalika katika lugha inayohusika. Kwa msingi huo, makosa ya kimantiki huweza kuathiri mawasiliano, hasa kwa watumiaji ambao sio wazawa wa lugha husika. Hii ni kwa sababu watumiaji ambao sio wazawa hawawezi kubashiri maana. Hivyo, wanashindwa kuelewa ujumbe uliokusudiwa. Mifano ifuatayo inaonesha makosa ya kimantiki yanayofanywa na watumiaji wa lugha ya Kiswahili.

(i) Maji yana vumbi.

(ii) Ukuta umenigonga.

(iii) Anashona cherehani.

Katika mfano (i) kuna kosa la kimantiki kwa sababu *vumbi* likishachanganyika na *maji* linakuwa *tope*. Kwa hiyo, ni sahihi kusema *maji yana tope* ambalo aghalabu, hutuama chini ya chombo chenye maji. Kosa la kimantiki katika mfano (ii) linajitokeza kwa sababu ukuta haujongei. Hivyo, katika hali ya kawaida, ukuta hauwezi kumfuata mtu na kumgonga. Kwa hiyo, ni sahihi kusema *nimejigonga kwenye ukuta*. Kosa la kimantiki katika mfano (iii) linatokea kwa sababu cherehani ni mashine inayotumika kushonea vitu kama nguo, viatu, mikoba, na mifuko. Kwa hiyo, cherehani haishonwi. Hivyo, ni sahihi kusema *fulani ni fundi cherehani*.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 261 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Makosa ya kiuakifishaji**

Haya ni makosa yanayotokana na kutokuzingatiwa kwa kanuni, taratibu, na mbinu za uandishi. Makosa hayo yanajumuisha matumizi yasiyo sahihi ya alama za kiuakifishaji. Uakifishaji ni uwekaji wa alama zinazotenganisha na kuunganisha vipashio vya kisintaksia na kisemantiki katika sentensi. Dhima za alama za uakifishaji ni kuonesha jinsi sehemu moja ya sentensi inavyohusiana na sehemu nyingine. Alama ya uakifishaji ikibadilishwa, huweza kuathiri maana iliyokusudiwa. Kutokuweka alama sahihi au kutokuweka alama yoyote ya uandishi kulingana na nafasi au sehemu inayohusika ni miongoni mwa makosa yanayojitokeza katika matumizi ya lugha. Alama za uakifishaji ni kama vile *nukta* (kituo kikuu), *mkato* (kituo kidogo) *mshangao*, *kiulizo* (alama ya kuuliza), *nuktapacha*, na *nuktamkato*. Kwa mfano:

(i) Anna John amekuja.

(ii) Mshahara umetoka.

Ikiwa mzungumzaji katika mfano (i) amekusudia kumtaarifu *Anna* kwamba *John* amekuja basi sentensi hiyo itakuwa na utata. Mpokeaji wa ujumbe anaweza kuelewa kwamba aliyekuja anaitwa *Anna John*. Ili ujumbe uliokusudiwa umfikie mpokeaji, alama ya mkato inatakiwa kuwekwa baada ya jina *Anna* kama vile *Anna, John amekuja*.

Katika mfano (ii) tunaweza kusema kwamba, ikiwa mtumiaji wa lugha amekusudia kumwuliza mpokeaji wa ujumbe kama mshahara umetoka, mpokeaji wa ujumbe anaweza kuelewa kwamba, anapewa taarifa kuwa mshahara tayari umelipwa. Kwa hiyo, mtumiaji wa lugha anatakiwa kuweka alama ya kuuliza mwishoni mwa sentensi, ili mawasiliano sahihi yaweze kufanikiwa. Inatakiwa iwe *Mshahara umetoka?* Na kama anakusudia kutoa taarifa, basi anatakiwa kuweka nukta.

**Chanzo cha makosa katika matumizi ya lugha**

Makosa katika matumizi ya lugha husababishwa na mambo anuwai. Mambo hayo ni athari ya lugha mama (ya kwanza), ujumuishaji wa kanuni za lugha, na ujuzi wa lugha zaidi ya moja.

***1 Athari ya lugha mama***

Watumiaji wa lugha hufanya makosa kutokana na kuathiriwa na lugha zao za kwanza. Watumiaji hawa huhamisha vipashio vya lugha zao na kuvitumia katika lugha nyingine. Aghalabu, makosa haya hujitokeza katika matumizi



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 262 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



ya vitamkwa kama vile [l/r], [f/v], [h/a], [th(Ø)/s], na [dh(ð)/z] kama yanavyojitokeza katika mifano ifuatayo:

| **Utamkaji sahihi** | | | **Utamkaji wenye makosa** |
|---|---|---|---|
| (i) | ku*l*a*l*a | - | ku*r*a*r*a (Kikurya) |
| (ii) | *v*iatu | - | *f*iatu (Kinyakyusa) |
| (iii) | *dh*ambi | - | *s*ambi (Kichaga) |
| (iv) | *s*asa | - | *th*atha (Kipare) |
| (v) | *h*ana | - | *a*na (Kihaya) |
| (vi) | *a*inisha | - | *h*ainisha (Kihaya) |

### *2 U jumuishaji wa kanuni*

Kila lugha hutawaliwa na kanuni mbalimbali katika maumbo ya maneno na miundo ya sentensi. Kanuni hizi ndizo humwongoza mtumiaji wa lugha kuunda maneno na tungo zinazokubalika. Watumiaji wa lugha wanaweza kufanya makosa kwa kujumuisha kanuni ambazo zinatawala maumbo ya maneno au miundo ya tungo fulani wanaposhindwa kuzingatia upekee wa maumbo au miundo hiyo. Kwa mfano, Kiswahili kina kanuni ya kuongeza kiangama -*ni* katika nomino ili kurejelea mahali. Kiangama -*ni* kikiongezwa kwenye nomino, nomino hiyo hubadilika na kuwa kielezi. Tazama mifano ifuatayo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| (i) | nyumba | - | nyumba*ni* |
| (ii) | soko | - | soko*ni* |
| (iii) | ghorofa | - | ghorofa*ni* |
| (iv) | bustani | - | bustani*ni* |

Hata hivyo, si kila nomino hukubali utaratibu huu. Ni kawaida kusema *bustanini* lakini si kawaida kusema *machozini*. Kiangama hiki huunda kielezi cha mahali. Ni kosa kuiambika mofu hiyo katika maneno yasiyodokeza umahali.

Kanuni nyingine ni ya kuongeza kipashio -*ni* ili kuonesha wingi, mathalani:

| | | | |
|---|---|---|---|
| (i) | kaa | - | kae*ni* |
| (ii) | karibu | - | karibu*ni* |



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 263 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

| | | | |
|---|---|---|---|
| (iii) | asante | - | asante*ni* |
| (iv) | hamjambo | - | hamjambo*ni* |
| (v) | habari | - | habari*ni* |

Angalia kwa umakini mifano kama ilivyooneshwa katika kipengele hiki cha ujumuishaji wa kanuni. Mathalani mifano (i) – (iii) ni sahihi lakini (iv) - (v) si sahihi. Kuwepo kwa mofu *-ni* katika (iv) – (v) kunatokana na makosa ya kujumuisha kanuni. Vilevile, makosa ya ujumuishaji wa kanuni yanaweza kujitokeza katika kauli ya utendeshi. Chunguza mifano ifuatayo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| (i) | vaa | - | valisha |
| (ii) | kaa | - | kalisha |
| (iii) | zoa | - | zolesha |
| (iv) | toa | - | tolesha |
| (v) | poa | - | pozesha |

Mifano (i) - (iii) ni sahihi kulingana na kanuni ya utokeaji wa maumbo ya kutendesha. Mifano (iv) - (v) siyo sahihi ingawa watumiaji wanaweza kuona kuwa maumbo ya utendeshi ni sawa kutokana na makosa ya kujumuisha kanuni. Kutokana na makosa haya, watumiaji wanaweza kujumuisha matumizi ya *–esh–* na *–ish–* hata katika vitenzi ambavyo hutumia *-z-* katika utendeshi kama vile *toa (toza)* na *poa (poza).*

### *3 U juzi wa lugh a zaidi ya moja*

Mtumiaji wa lugha anapokuwa na ujuzi wa lugha zaidi ya moja anaweza kupata athari katika matumizi ya lugha hizo. Kwa mfano, watumiaji wa lugha ya Kiswahili wenye ujuzi wa lugha ya Kiingereza wanaweza kufanya makosa kama ya kimuundo au ya kimsamiati endapo hawatakuwa makini katika matumizi ya lugha mojawapo. Chunguza mifano ifuatayo:

(i) Baba amekwenda *aidha* sokoni *au* kazini.

(ii) Baba amekwenda *ama* sokoni *au* kazini.

Sentensi ya (i) si sahihi kwa sababu ya kukosea matumizi ya neno *aidha* ambalo limefananishwa na neno la Kiingereza *either* ambalo huambatana na *or (au)* katika lugha hiyo. Katika Kiswahili, *aidha* inamaanisha *isitoshe*


PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 264 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



au *zaidi ya hayo*. Kwa hiyo, haipaswi kutumiwa pamoja na *au* kama ilivyo *either* katika Kiingereza. Katika Kiswahili, kisawe cha *either* ... *or* ni *ama* ... *au* kama ilivyo katika mfano (ii) hapo juu.

**Jinsi ya kuondoa makosa katika matumizi ya lugha**

Kuna makosa mbalimbali ambayo hujitokeza katika matumizi ya lugha. Makosa hayo, mara nyingi, husababisha watumiaji wa lugha kutoelewana. Ili kupunguza au kuyaondoa makosa hayo, ni vyema kuzingatia mapendekezo yafuatayo:

(i) Kutilia mkazo ufundishaji na ujifunzaji wa matumizi sahihi ya lugha kuanzia elimu ya awali ili kujenga umahiri katika lugha inayohusika.
(ii) Watumiaji wa lugha kuwa makini na kuzingatia kanuni na taratibu za matumizi sahihi ya lugha.
(iii) Wataalamu wa lugha ya Kiswahili kuandika vitabu vya kuelimisha watumiaji wa lugha wa ngazi mbalimbali kuhusu matumizi sahihi ya Kiswahili.

## Zoezi la 9.1

1. Tofautisha makosa ya kisarufi na ya kimantiki kwa kutumia mifano.
2. Taja makosa manne (4) ya kimuundo na eleza sababu za utokeaji wa makosa hayo.
3. Eleza mambo yanayosababisha watumiaji wa lugha kufanya makosa ya kisarufi.

## Tamrini

1. Je, makosa ya ukiukaji wa mbinu za uandishi yanaathirije mawasiliano katika uandishi?

2. Jadili sababu za makosa ya kisarufi na jinsi ya kukabiliana nayo.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 265 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Faharasa

**Adhama** Jambo kubwa la heshima na fahari

**Durusu** Soma au pitia kwa makini kilichoandikwa

**Fundimchundo** Mtu anayefanya shughuli za ufundi chini ya usimamizi wa fundi mkuu

**Kanzidata** Mkusanyiko mkuu wa habari zinazoweza kutafutwa haraka hususani kwa njia ya kompyuta

**Kasida** Tungo za sifa zinazoghaniwa

**Kitelaoto** Mashine ya benki ya kutolea na kuwekea fedha

**Kisimbuzi** Kifaa kinachofichua alama za kieletroniki zilizofichwa ili ziweze kusikika na kuonekana kwenye simu, au televisheni kwa kutumia mfumo wa dijiti

**Kiswahili** Lugha kuu Afrika Mashariki na Kati inayojumuisha lahaja mbalimbali

**Kiswahili sanifu** Lahaja rasmi iliyosanifishwa na kupitishwa na Kamati ya Lugha (Kiswahili) ya Afrika Mashariki. Lahaja hii ndiyo inayotumika katika elimu na mawasiliano yote rasmi

**Malele** Majani yanayotumika kutengenezea rangi nyekundu

**Manamba** Mfanyakazi anayetoka maeneo ya mbali kwa ajili ya kufanya kazi katika mashamba makubwa kama kibarua

**Medani** Eneo ambalo askari hupigania vita au eneo maalumu la kitaaluma

**Mnasaba** Uhusiano baina ya pande mbili au zaidi



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 266 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



**Mnyapara** Mtu anayewasimamia watu wanaofanya kazi

**Mujarabu** -enye kufaa; -liojaribiwa

**Pweke** Bila ya -ingine

**Raghba** Hali inayompa mtu hamu au kuvutika na jambo fulani

**Sawidi** Andika au nakili makala au maandishi kama hatua ya mwanzo kabla ya kufanya uhariri wa mwisho

**Shajara** Kitabu kiandikwacho kumbukumbu za matukio ya mambo ya kila siku

**Simufifi** Simu zilizopigwa kwa mtu ambazo hazikupokelewa na mwenye simu

**Tamrini** Kazi inayotolewa na mwalimu darasani kwa wanafunzi baada ya kufundisha somo fulani

**Tasinifu** Maandiko ya kitaaluma yanayochanganua mada maalumu aghalabu kwa ajili ya kupata shahada ya juu

**Uakifishaji** Utumiaji wa alama za kiuandishi katika maandishi kama vile: nukta, koma, alama ya kuuliza, kufunga na kufungua usemi, na nyinginezo

**Ulumbi** Uwezo wa mtu au jamii ya watu fulani kuweza kutumia lugha nyingi katika mawasiliano

**Umahiri** Ujuzi mkubwa wa kufanya jambo fulani

**Usuli** Taarifa ambayo ni muhimu katika kuelewa tatizo au hali

**Waswahili** Watu watumiao Kiswahili katika mawasiliano (maana pana)

For Online Use Only



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 267 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Marejeleo teule

Ashton, E.O. (1944). *Swahili grammar.* London: Longman, Green & Co.

BAKITA (2015). *Kamusi kuu ya Kiswahili.* Nairobi: Longhorn Publishers Limited.

Broomfield, G.W. (1935). *Sarufi ya Kiswahili.* London: Oxford University Press.

Catford, J.C. (1965). *A linguistic theory of translation.* London: Oxford University Press.

Chiraghdin, S., & Mnyampala, M.E. (1977), *Historia ya Kiswahili*. Nairobi: Oxford University Press.

Crystal, D. (1992). *An encyclopedic dictionary of language and languages*. Blackwell: Oxford University Press.

Greenberg, J.H. (1955). *Studies in african linguistic classification*. Connectcut. New Haven.

Guthrie, M. (1948). *The classification of the Bantu languages.* London: IAI.

Guthrie, M. (1970). *Comparative bantu*. Vol. 2 and 3 Farnborough: Gregg International Publisher.

Habwe, J., & Karanja, P. (2004). *Misingi ya sarufi ya Kiswahili.* Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Iliffe, J. (1979). *A modern History of Tanganyika*. Cambridge: Cambridge University Press.

Johnson, F. (1939). *A standard English-Swahili dictionary.* London: Oxford University Press.

Johnson, F. (1939). *A standard Swahili-English dictionary.* London: Oxford University Press.

Johnston, H.H. (1919). *A comparative study of Bantu and semi-bantu languages* Vol. 2 Oxford: The Clarendon Press.

Kapinga, M.C. (1983). *Sarufi maumbo ya Kiswahili sanifu*. Dar es Salaam: TUKI.

Kihore, Y.M., Massamba, D.P.B., & Msanjila, Y.P. (2008). *Sarufi maumbo ya Kiswahili sanifu (SAMAKISA): Sekondari na vyuo*. Dar es Salaam: TUKI.

King'ei, K. (2010). *Misingi ya Isimujamii*. Dar es Salaam: TUKI.

Krumm, B. (1940). *Words of oriental origin in swahili*. London: The Sheldon Press.

Maganga, C. (1997). *Historia ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 268 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Massamba, D.P.B., Kihore, Y.M., & Hokororo, J.I. (1999). *Sarufi miundo ya Kiswahili sanifu (SAMIKISA)*: Sekondari na Vyuo. Dar es Salaam: TUKI.

Massamba, D.P.B., Kihore, Y.M., & Hokororo, J.I. (2001). *Sarufi miundo ya Kiswahili sanifu (SAMIKISA)*: Sekondari na Vyuo. Dar es Salaam: TUKI.

Massamba, D.P.B. (2002). *Historia ya Kiswahili: 50 BK hadi 1500 BK*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Massamba, D.P.B. (2004). *Kamusi ya isimu na falsafa ya lugha*. Dar es Salaam: TUKI.

Massamba, D.P.B., Kihore, Y.M., & Msanjila, Y.P. (2004). *Fonolojia ya Kiswahili Sanifu (FOKISA): Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: TUKI.

Massamba, D.P.B. (2007). *Kiswahili origins and the bantu divergence – convergence theory: Professorial inagural lecture serial No*. 48. Dar es Salaam: Institute of Kiswahili Research.

Massamba, D.P.B. (2010). *Phonological theory: History and development* (Toleo la pili). Dar es Salaam: TUKI.

Massamba, D.P.B. (2017). *Historia ya Kiswahili:* Mtazamo Mpya. Dar es Salaam: Development Limited.

Matei, A.K. (2008). *Darubini ya sarufi: Ufafanuzi kamili wa sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Matinde, R.S. (2012). *Dafina ya lugha: Isimu na nadharia*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers Limited.

Mazrui, A.M. & Shariff I.N. (1994). *The swahili: Idiom and identity of an African people.* Trenton. New Jersy: Africa Word Press.

Mbaabu, I. (2007). *Historia ya usanifishaji wa Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.

Mdee, J.S. (1999). "Faharasa za Shaaban Robert na Mchango katika Leksikografia ya Kiswahili". *Mulika.* Na. 24,14 - 31.

Mgullu, R.S. (2002). *Mtalaa wa isimu: fonetiki, fonolojia na mofolojia ya Kiswahili* Nairobi: Longhorn Publishers.

Mohammed, M.A. (1986). *Modern swahili grammar.* Nairobi: East African Educational Publishers.

Mrikaria, S.E. (2009). *Stadi za lugha ya Kiswahili: Utungaji 1*. Dar es Salaam: TUKI.

Msanjila, Y.P. (2009). *Stadi za lugha ya Kiswahili: Ufahamu na ufupisho 1*. Dar es Salaam: TUKI.



PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology

KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 269 25/09/2019 13:57

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Msanjila, Y. P., Kihore, Y. M., & Massamba D.P.B. (2009). *Isimujamii. Sekondari na vyuo*. Dar es Salaam: TUKI.

Msuya, E. (2017). *Tanzania kinara wa uzalishaji wa muhogo kiteknolojia Afrika*. Dar es Salaam: Mwananchi: Agosti, 26. 2017.

Mwansoko, H.J.M., Mekacha, R.D.K., Masoko, V.L.W., & Mtesigwa, P.C.K. (2006). *Kitangulizi cha tafsiri: Nadharia na mbinu*. Dar es Salaam: TUKI.

Nkwera, F. M.V. (1978). *Sarufi na fasihi sekondari na vyuo*. Dar es Salaam: TPH.

Nkwera, F.M.V. (1989). *Sarufi, fasihi na uandishi wa vitabu: sekondari na vyuo*. Dar es Salaam: TPH.

Nolan, J. (2005). "Interpretation Techniques and Exercises", katika *Linguistic service*. Clevadon: Multilingual Matters LTD.

Polomé, E. (1967). *Kiswahili language handbook*. Washington, D.C: Center for Applied Linguistists.

Rubanza, Y.I. (1996). *Mofolojia ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Rweyemamu, C. (2004). "Somo la Kiswahili katika Chuo cha Uandishi wa Habari", katika Mlacha, S.A.K (Mh). *Kiswahili na vyombo vya habari*. Dar es Salaam: TUKI.

Sassoon, H. (1980). "The Coastal Town of Jumba la Mtwana", katika *Kenya past and present, Juz.12,2-14.*

Steere, E. (1870). *A handbook of the Swahili language as spoken at Zanzibar*. London: S.P.C.K.

TUKI (1990). *Kamusi sanifu ya isimu na lugha*: Dar es Salaam: TUKI.

TUKI (2004). *Kamusi ya Kiswahili sanifu*. Nairobi: OUP.

TUKI (2010). *Makala za semina ya Kimataifa ya waandishi wa Kiswahili 1*. (Lugha ya Kiswahili). Dar es Salaam: TUKI.

Tuli, R.S.K. (1985). *Chimbuko la Kiswahili: Kukua na kuenea kwake Afrika ya Mashariki*. Arusha: Utalii Explorers & Publications.

TUMI (1988). *Kiswahili sekondari*. Dar es Salaam: TUMI

Turton, E.R. (1975). Bantu, Galla and Somali Migration in the Horn of Africa: A Reassesment of the Juba/Tana Area, katika *Journal of African History Vol. XVI No. 4:519-537.*

Wanjala, S.F. (2011). *Misingi ya ukalimani na tafsiri kwa shule, vyuo na ndaki*. Mwanza: Serengeti Educatinal Publishers (T) Ltd.


PROPERTY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA GOBVERNMENT
Ministry of Education, Science and Technology
KISWAHILI LUGHA 5 NA 6 (Kiwandani final).indd 270 25/09/2019 13:57

ISBN 978-9987-09-025-9